# MISINGI YA ITIKADI KWA VIJANA

أصول العقائد للشباب

**Kimetungwa na:**
Sheikh Nasir Makarim Shirazi

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui

ترجمة

# أصول العقائد للشباب

تأليف
ناصر مكارم الشيرازي

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

12_16_Misingi_13_January_2017.indd 2 1/13/2017 3:33:18 PM

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

**ISBN:** 978 - 9987 – 17 – 041 – 8

**Kimetungwa na:**
Sheikh Nasir Makarim Shirazi

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul-Karim Juma Nkusui
Barua pepe: abdulkarimjuma@yahoo.com

**Kimehaririwa na:**
Al-Haji Hemedi Lubumba

**Kimesomwa-Prufu na:**
Al-Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimepitiwa na:**
Al-Haji Mujahid Rashid

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Mei, 2017
**Nakala:** 2000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation

S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Utangulizi........................................................................viii

Neno la Mchapishaji ........................................................................ 1

**1. Masomo Kumi Katika Kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu**

**– Somo la Kwanza:**

Utafiti kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu................................ 3

**– Somo la Pili:**

Athari za Kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu
Katika Maisha Yetu .................................................................... 6

**– Somo la Tatu:**

Kumjua Mwenyezi Mungu Kwa Njia Mbili
Zenye Matumaini ...................................................................... 10

**– Somo la Nne**

Kujibu Swali Muhimu................................................................ 14

**– Somo la Tano:**

Kisa cha Uhalisia........................................................................ 18

**– Somo la Sita:**

Njia ya pili ya kumjua Mwenyezi Mungu................................ 20

**– Somo la Saba:**

Mifano kuhusu mfumo wa uumbaji ......................................... 23

**– Somo la Nane:**

Ulimwengu wa ajabu katika ndege mdogo .............................. 28

**– Somo la Tisa:**

Urafiki baina ya wadudu na maua............................................ 30

**– Somo la Kumi:**

Katika ulimwengu usio na kikomo katika viumbe vidogo...... 34

Utafiti wa ukamilisho wa somo la kumi: ................................. 39

**2. Masomo Kumi Katika Uadilifu wa Mwenyezi Mungu**

**– Somo la Kwanza:**

Uadilifu nini ?............................................................................. 44

**– Somo la Pili:**

Dalili za Uadlifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.................. 49
**– Somo la Tatu:**
Falsafa ya majanga na shari .................................................. 54
**– Somo la Nne:**
Falsafa ya matukio yenye kusikitisha katika maisha ............. 58
**– Somo la Tano:**
Falsafa ya majanga na shari kwa mara nyingine.................... 62
**– Somo la Sita:**
Mas'ala ya jaala na hiyari..................................................... 67
**– Somo la Saba:**
Dalili wazi zaidi juu ya uhuru wa matakwa ya hiyari............ 72
**– Somo la Nane:**
Nini maana ya jambo baina ya mambo mawili....................... 76
**– Somo la Tisa:**
Je, uongofu na upotovu uko mikononi
mwa Mwenyezi Mungu.......................................................... 80
**– Somo la Kumi:**
Uadilifu wa Mwenyezi Mungu na mas'ala ya kudumu milele...85
**3. Masomo kumi katika Unabii:**
**– Somo la Kwanza:**
Haja yetu kwa viongozi wa kiungu........................................ 90
**– Somo la Pili:**
Kuweka kanuni na haja ya kuwepo Manabii .......................... 95
**– Somo la Tatu:**
Kwa nini Manabii ni Maasumina......................................... 100
**– Somo la Nne:**
Njia bora zaidi ya kumjua Nabii .......................................... 104
**– Somo la Tano:**
Muujiza mkubwa zaidi wa Nabii wa Uislamu ...................... 109
**– Somo la Sita:**
Dirisha la muujiza wa Qur'ani ............................................. 114
**– Somo la Saba:**

Mtazamo wa Ulimwengu katika Qur'aniTukufu .................. 118
**– Somo la Nane:**
Qur'aniTukufu na uvumbuzi wa kielimu leo hii .................. 123
**– Somo la Tisa:**
Waraka mwingine juu ya haki ya Nabii wa Uislamu ............ 128
**– Somo la Kumi:**
Hitimisho la Unabii .................................................................. 133
**4. Masomo Kumi Katika Uimamu:**
**– Somo la Kwanza:**
Utafiti wa Uimamu umeanzia wapi? ...................................... 140
**– Somo la Pili:**
Falsafa ya kuwepo Imamu....................................................... 145
**– Somo la Tatu:**
Masharti na mazingira maalum kwa Imamu ......................... 149
**– Somo la Nne:**
Nani anayemteua Imamu? ...................................................... 153
**– Somo la Tano:**
Qur'ani na Uimamu.................................................................. 159
**– Somo la Sita:**
Uimamu katika Sunnah ya Nabii ......................................... 166
**– Somo la Saba:**
Hadithi ya Cheo na hadithi Karama ya jamaa wa karibu...... 171
**– Somo la Nane:**
Hadthi ya Vizito Viwili na Safina ya Nuhu عليه السلام ..................... 175
**– Somo la Tisa:**
Maimamu kumi na mbili ......................................................... 179
**– Somo la Kumi:**
Mahdi Imam wa kumi na mbili na mrekebishaji
mkuu wa Ulimwengu ............................................................. 185

**5. Masomo kumi kuhusu Marejeo:**

**– Somo la Kwanza:**
Swali muhimu: Je, mauti ni mwanzo au mwisho?................ 195

**– Somo la Pili:**
Marejeo yanatoa maana katika maisha.................................. 199

**– Somo la Tatu:**
Mfano wa mahakama ya Akhera ndani ya nafsi zenu........... 203

**– Somo la Nne:**
Marejeo yanapodhihirika katika maumbile ........................... 208

**– Somo la Tano:**
Ufufuo katika kipimo cha uadilifu ........................................ 212

**– Somo la Sita:**
Tumeshaona Siku ya Kiyama mara nyingi katika dunia hii............................................................ 215

**– Somo la Saba:**
Marejeo na falsafa ya kuumba .............................................. 219

**– Somo la Nane:**
Kubakia roho ni dalili ya siku ya Kiyama............................. 223

**– Somo la Tisa:**
Marejeo ya mwili na roho .................................................... 229

**– Somo la Kumi:**
Pepo, Jahanam na umbo la vitendo ....................................... 234

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji ya kiroho ya zama hizi pamoja na Ubongo na fikra zinazokuwa za Muislam. Jitihada kubwa zimefanywa na Taasisi kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia Unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an: (Surat Saba' 34:46).

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam
Al Itrah Foundation
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 8 1/13/2017 3:33:19 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako asili yake ni cha lugha ya Kiarabu kwa jina la, *Usulu 'l-'Aqaid li 'sh-Shabab* kilichoandikwa na Sheikh Nasir Makarim Shirazi. Sisi tumekiita, *Misingi ya Itikadi kwa Vijana.*

Mwandishi katika kitabu hiki ameshughulikia kwa upeo zaidi suala la itikadi ambalo kwalo baadhi ya wanazuoni na madhehebu za Kiislamu wamehitilafiana. Kwa mfano, suala kuonekana kwa Mungu hapa duniani na Akhera. Wako wanaosema ataonekana Akhera kwa waumini tu, wengine wanasema ataonekana hapa duniani na Akhera pia, lakini wengine wanasema kwa uhakika kabisa kwamba kamwe hataonekana si hapa duniani wala Akhera. Sasa ili kuyaelewa yote hayo fuatana na mwandishi wa kitabu hiki.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa makubwa hususan wakati huu wa sayansi na tekinolojia kubwa ambapo ngano, hadithi za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi kwa watu wa sasa.

Taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa makubwa kwao. Tunamshukuru ndugu yetu Ustadh Abdul Karim Juma Nkusui kwa kufanikisha tarjuma ya kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili, pia na wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha

kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na Akhera pia. Amin!

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**Dar es Salaam**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 2 1/13/2017 3:33:19 PM

# 1

# MASOMO KUMI KATIKA KUMJUA MWENYEZI MUNGU (SWT)

بسم الله الرحمن الرحيم

## SOMO LA KWANZA:

**Utafiti juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa nini tumjue Muumba wa ulimwengu, kwa nini tunatafakari na kudadisi?**

**1. Kupenda kutambua na kuujua ulimwengu wa uwepo:**

Ndani ya kila mmoja wetu kunapatikana hali ya kupenda kuelewa na kujua ulimwengu wa uwepo. Kwa hakika sisi sote tunataka kujua: Je, hii mbingu iliyonyanyuka, kwa nyota zake na sayari zake nzuri, ardhi hii iliyopanuka kwa mandhari yake mazuri, na viumbe hivi mbalimbali, ndege wazuri, samaki wa aina mbalimbali, bahari, milima, miti na maua, na aina mbalimbali za miti iliyochanua na mengi mengineyo. Je, vyote hivi vimetokea vyenyewe au muonekano huu wa ajabu umetengenezwa na mtengenezaji mahiri na muweza?

Kwa kufumbia macho hayo, hakika swali la kwanza linalojitokeza katika akili zetu katika maisha ni: Tumetoka wapi? Tuko wapi na tunaelekea wapi? Tutakuwa na furaha kiasi gani kama tutajua majibu ya maswali haya matatu? Yaani kujua wapi yameanzia maisha yetu na wapi tunaelekea? Na nini wajibu wetu hivi sasa?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 3 1/13/2017 3:33:19 PM

Hakika roho zetu zenye uelewa zinatuambia: Ni wajibu msizembee katika kutafuta majibu ya maswali haya. Wakati mwingine inatokea mtu anajeruhiwa na anazimia katika ajali ya gari, na kwa ajili ya matibabu yake anapelekwa hospitalini. Na hali yake inapokuwa nzuri hakika swali la kwanza atakalouliza kwa watu waliopo pembezoni mwake ni: Ni sehemu gani hii? Kwa nini nimeletwa hapa? Na lini ataondoka hapo?

Hakika hili linaonyesha kwamba mwanadamu hawezi kuyanyamazia maswali mfano wa haya. Na hivyo hakika cha kwanza kinachotupelekea kutafiti kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumjua Muumba wa ulimwengu na uhai ni roho hiyo yenye kiu yenye kujitokeza kwetu.

## 2. Hisia za shukrani:

Fikirieni kwamba nyinyi mmealikwa katika ugeni mtukufu na kwamba mmeandaliwa kila kitu, lakini wewe humjui mwenyeji vizuri kwa sababu ulimsindikiza ndugu yako mkubwa aliyealikwa katika ugeni huu. Hapana shaka kwamba cha kwanza kitakachokujia akilini mwako wakati wa kuingia kwako katika ugeni huu ni kumjua mwenyeji na kumshukuru.

Na sisi vilevile tunapoangalia katika meza hii ya Mwenyezi Mungu na kuona aina mbalimbali za neema ambazo ametuneemesha, macho yenye kuona, masikio yenye kusikia, akili yenye uerevu wa kutosha, nguvu mbalimbli za kimwili na kinafsi, na aina mbali mbali za njia za maisha na vyakula, na tunaona katika meza hii aina mbalimbali za neema, tunapata wazo la kujua mtoaji wa neema zote hizi. Hata kama hahitajii shukrani zetu, ni wajibu tumshukuru, na hatajisikia vizuri kama hatutafanya hivyo. Na hii ni dalili nyingine inayotusukuma kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 4 1/13/2017 3:33:19 PM

### 3. Uhusiano wetu na faida na madhara ya mas'ala haya:

Fikiria kwamba wewe katika safari yako unafika njia panda unakuta kifusi, na wote wanakuambia usisimame hapa, na kila kundi linakutaka uende upande maalum, mmoja wao anasema ni bora uende Mashariki, na mwingine anasema njia ya Magharibi ndio yenye matumaini zaidi, watatu anakuita kwenye njia iliyopo baina ya njia hizi mbili na anasema: Hakika njia hii ndio njia pekee yenye kukuokoa na hatari na kukuwezesha kufika salama salimini kwenye lengo.

Je, katika kuacha njia tutaziacha nafsi zetu bila ya kutafiti?

Je, akili zetu zinakubali kusimama hapo na kutoacha njia?

Bila shaka jibu ni hapana.

Hakika akili zitatuambia ni wajibu tufanye haraka kutafiti na kuhakiki, na kumsikiliza kwa makini kila mmoja kati ya hao, na kukubali tutakayekuta kwake ukweli na hoja zenye kukinaisha, na tutachagua kwa matumaini njia ambayo ametuelekeza.

Na hali yetu katika maisha ya dunia ni vivyo hivyo, madhehebu na mirengo yote vinatuita kwenda upande wake, lakini kwa kuwa hatima yetu, mafanikio yetu, kufeli kwetu, maendeleo yetu na kutoendelea kwetu kunahitajia utafiti na kuchagua njia bora, hakika sisi tunalazimika kuchagua njia inayotupeleka kwenye maendeleo na ukamilifu, na kuwa mbali na maporomoko yanayotupeleka katika ufisadi na upotevu. Na hii ni hoja nyingine inayotulingania katika kuhakiki juu ya muumba wa ulimwengu. Qur'ani Tukufu inasema:

الَّذِينَ يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ ۚ

**"Wabashirie waja Wangu ambao wanasikiliza kauli na kufuata iliyo nzuri zaidi." (Suratu Zumar: 18)**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 5 1/13/2017 3:33:19 PM

# FIKIRI NA UJIBU:

1. Je, umefikiria juu ya kumjua Mwenyezi Mungu, zaidi na alivyokutajia mzazi wako juu ya maudhui haya?
2. Je, unaweza kutaja tofauti baina ya kutafiti juu ya Mwenyezi Mungu na kumjua Mwenyezi Mungu?
3. Je, wakati wa dua na kumuomba Mwenyezi Mungu umehisi utamu wa kiroho wa kina wa aina yoyote ile?

# SOMO LA PILI:

**Athari za kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu katika maisha yetu.**

**1. Kumjua Mwenyezi Mungu na Maendeleo ya Elimu:**

Tujaalie kwamba rafiki yako amekuja toka safarini na amekuletea zawadi ya kitabu na akakwambia hakika ni kitabu chenye faida sana, kwa sababu mtunzi wake ni mwanachuoni mashuhuri. Ana taarifa nyingi na yuko makini. Ni mahiri na mwerevu katika ubobezi wake na ni profesa. Kwa haya hakika wewe hutosoma kitabu hiki kijuu juu bali utadadisi katika kila sentensi na ibara, na ikitokea hujafahamu sentensi miongoni mwazo, basi pengeine utasoma mara nyingi na kwa saa nyingi, na pengine kwa siku nyingi. Na kila unapopata fursa unarejea kusoma ili upambanukiwe na usichokijua, kwa sababu mtunzi wa kitabu hiki sio mtu wa kawaida, bali ni mwanachuoni mkubwa, haandiki neno bila ya kulipigia mahesabu.

Na ikitokea kinyume chake na wakakuambia hakika kitabu hiki pamoja na mwonekano wake mzuri, ni cha mtunzi jahili asiye na elimu na wala haiwezekani kutegemea rai yake, hakika wewe



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 6 1/13/2017 3:33:19 PM

utaangalia kitabu kwa mtazamo mwepesi, na kila unapokuta ibara au sentensi usiyoijua, hakika wewe utasema hakika mtunzi hajui kitu katika anayoyazungumza, na ni upuuzi kupoteza mwanadamu wakati wake katika kusoma kitabu hiki.

Hakika ulimwengu wa uwepo unafanana na kitabu kikubwa, na kila kilichopo kinatengeneza neno au sentensi, na kwa mwanadamu muumini hakika chembe chembe zote za ulimwengu huu ni sehemu ya utafiti. Na mwanadamu katika mwanga wa ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu anakuwa na shauku maalum ya utafiti wa siri za kuumbwa. Na maudhui haya yanasaidia sana katika kuendelea elimu ya mwanadamu kama ambavyo anajua kwamba muumba wa kiumbe hiki ana elimu na uwezo usio na kikomo, na vitendo Vyake vyote ni kwa hekima na falsafa. Kwa ajili hii hakika mwanadamu anafanya utafiti makini na wa kina ili afahamu siri kwa namna bora zaidi.

Ama mwanadamu wa kimada hakika hamiliki msukumo ili afanye utafiti wa kina wa siri za kuumbwa, kwa sababu yeye anaitakidi kuwa muumba wake ni mazingira ambayo hayana hisia. Na ikiwa tunaona baadhi ya wavumbuzi wa kimada miongoni mwa wavumbuzi wa sayansi, ni kwa sababu wao aghlabu wanaitakidi uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini wao wanalipa nguvu na utukufu jina la mazingira, na kwa sababu wao wanaitakidi uwepo wa mpangilio na ratiba katika kazi ya mazingira.

Hitimisho ni kwamba ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni njia ya kufikia maendeleo ya kisayansi.

### 2. Ibada ya Mwenyezi Mungu, Juhudi na Matumaini:

Yanapotokea matukio magumu yenye kutatiza katika maisha ya mwanadamu, na milango ikafungwa mbele yake kila upande, na anahisi udhaifu mbele ya matatizo, hakika imani ya kumwamini Mwenyezi Mungu inakuja ili kumsaidia na kumpa nguvu humo.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 7 1/13/2017 3:33:19 PM

Hakika wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu hawakuti nafsi zao zikiwa pweke, wala dhaifu, hawahisi kukata tamaa, wala hawahisi unyonge na kushindwa, kwa sababu wanaamini uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu uko juu ya matatizo yote, na yaliyo mbele yake ni mepesi. Hawa wanasimama imara mbele ya matatizo kwa rehema ya Mwenyezi Mungu, ulinzi Wake na msaada Wake. Wanakusanya nguvu zao zote na wanakwenda mbio kwa raghaba na matumaini, na hivyo wanashinda dhidi ya matatizo.

Ndio, hakika kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu ni tegemeo kubwa kwa mwanadamu, na kumwamini Mwenyezi Mungu kunaleta azima na uimara. Na kumwamini Mwenyezi Mungu kunaleta matumaini daima katika nyoyo. Na kwa sababu hii hakika waumini hawajinyongi kamwe, kwa sababu kujinyonga sababu yake ni kukata tamaa na kuhisi kushindwa. Ama waumini hakika wao hawatokata tamaa wala hawatohisi kushindwa.

### 3. Ibada ya Mwenyezi Mungu na Kuhisi Majukumu:

Tunajua matabibu wanapoendewa na mgonjwa masikini, sio tu hawachukui haki ya juhudi zao za kujituma, bali pia wanawaondolea gharama za dawa. Na wanapohisi kwamba hali ya mgonjwa ipo hatarini, hakika wao wanakesha usiku pembezoni mwake katika nyumba yake duni. Hakika hawa matabibu ni watu wanaomwabudu Mwenyezi Mungu na ni waumini. Kama ambavyo tunajua pia kuna matabibu ambao hawanyanyui unyayo bila malipo, kwa sababu wao wanakosa nguvu ya imani. Na mwanadamu muumini katika tawi lolote liwalo, anahisi majukumu na anahisi wajibu, nalo ni jambo la kheri, na anabeba daima ndani mwake sura ya sharti la kimaanawi, inayofuatilia vitendo vyake vyote.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 8 1/13/2017 3:33:19 PM

Ama watu wasiokuwa waumini hakika wao wana ghururi. Ni hatari na hawakubali jukumu lolote, na dhulma na kukandamiza haki ya wengine ni jambo jepesi sana kwao, na ni nadra sana wao kufanya kitendo cha kheri. Maulamaa wa nafsi wanasema hakika maradhi ya nafsi katika zama zetu hizi za leo yameenea zaidi kuliko zama zilizopita, na pia wanasema, hakika moja ya sababu za maradhi haya ni kuhisi huzuni kutokana na matukio ya mustakabali, kutokana na mauti, vita, ufakiri, kufeli na kushindwa.

Na wanaongeza: Hakika baina ya vitu ambavyo vinaondoa huzuni katika nafsi ya mwanadamu ni kumwamini Mwenyezi Mungu Mtukfu, kwa sababu kila sababu za huzuni zinapotaka kupenya katika nafsi yake basi imani yake kwa Mwenyezi Mungu huziondosha kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole Mwenye huruma, Mwenye kuruzuku, ambaye anajua hali za waja Wake ambao daima wanamwelekea kwa maombi. Anawasaidia hawa waumini na anawaweka mbali na huzuni.

Na kwa sababu hii waumini wa kweli wanahisi utulivu na wala haipatikani huzuni katika nafsi zao. Na kwa kuwa amali zao ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hata kama wakipatwa na madhara, wao wanahisi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapa badala yake, bali tabasamu linakuwa katika midomo yao katika wakati wa vita.

Na Qur'ani Tukufu inasema:

الَّذِينَ آمَنُوا وَلَمْ يَلْبِسُوا إِيمَانَهُمْ بِظُلْمٍ أُولَٰئِكَ لَهُمُ الْأَمْنُ وَهُمْ مُهْتَدُونَ

**"Wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na upotevu, hao ndio watakaopata amani." (Sura al-An'am: 82).**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 9 1/13/2017 3:33:19 PM

# TAFAKARI:

**1.** Je, unakumbuka shakhisiya ya kihistoria inayoakisi mwonekano wa imani na athari zilizotajwa katika somo?

**2.** Je, unajua kwa nini baadhi ya watu ambao wanazungumzia juu ya imani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, bali wana tabia mbaya, wanakosa athari nne zilizotajwa katika somo?

# SOMO LA TATU:

**Kumjua Mwenyezi Mungu katika njia mbili zenye matumaini:**

Kuhusu kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu vimetungwa vitabu vingi tangu zamani hadi leo, na kulikuwa na utafiti mrefu baina ya maulamaa katika nyanja hii. Na kila kundi lilikuwa linachagua mbinu ya kufikia kwenye kiini cha uhalisia huu, na mbinu bora na njia ambazo zinaweza kutufikisha katika kumjua Muumba Mkubwa wa ulimwengu wa uwepo; ni njia mbili nazo ni:

**1.** Njia ya ndani (njia za karibu zaidi)

**2.** Njia ya nje (njia zilizo wazi zaidi).[1]

Katika njia ya kwanza tunaelekea katika undani wa uwepo wetu na tunasikia sauti ya tauhidi kutoka ndani mwetu. Na katika njia ya pili tunatembea katika ulimwengu mpana wa viumbe na tunashuhudia alama zinazoonyesha juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika viumbe vyote vilivyopo na katika kila chembe. Na kila moja ya njia hizi mbili kuna utafiti mrefu. Ama juhudi yetu, itakuwa ni muhtasari katika hadithi moja fupi, ambapo tutazungumzia njia mbili kwa sura ya jumla.

[1] Utakuja ufafanuzi wa njia ya pili (ya nje) katika somo la sita.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 10 1/13/2017 3:33:19 PM

**Njia ya ndani:** Tutafakari maudhui haya:

**1.** Maulamaa wanasema: Kila mwanadamu kutoka sehemu yoyote na tabaka lolote lile, akiachwa mwenyewe bila ya kupewa taarifa maalum, na akawa mbali na utafiti wa waumini na watu wa mada, hakika yeye mwenyewe ataelekea upande wa nguvu iliyokadiriwa inayopita nguvu zote za ulimwengu wa kimada na kuhukumu juu yake. Na atahisi katika kona za moyo wake na undani wa nafsi yake wito mwororo uliojaa upendo, lakini ulio wazi na wenye nguvu unaomwita kuelekea kwa Muumba Mtukufu wa elimu na uwezo, sisi tunamwita 'Mwenyezi Mungu' Mtukufu. Na wito huu ndio wito wa kimaumbile safi ambao hauchanganyiki na shaka yoyote.

**2.** Inawezekana fujo la ulimwengu na maisha ya kila siku na mapambo yake kumshughulisha mwanadamu, na kughafilika kwa muda na kutosikia wito huu, lakini anapokuta nafsi yake mbele ya matatizo na changamoto, na anaposhuhudia matukio ya kimazingira yenye kuangamiza kama vile matetemeko, vimbunga, mafuriko, nyakati zenye kutisha katika ndege inayokumbwa na anga lenye upepo na hatari, katika nyakati hizi ambazo anakosa njia yoyote ya kimada au kimbilio, hakika wito unakuwa na nguvu ndani mwake na anahisi kwamba nguvu inamwita kutoka ndani mwake, na nguvu hii ndio yenye nguvu zaidi kuliko nguvu zote. Nguvu iliyofichikana inarahisisha mbele yake matatizo yote na magumu yote.

Na ni nadra kukuta mtu asiyeelekea mwelekeo huu katika maisha mbele ya matukio magumu, wala hamtaji Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maudhui haya yanaonyesha juu ya upeo wa ukaribu wetu kwa (swt), ni kiasi gani yuko karibu nasi. Yeye ndio Mwenyezi Mungu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 11 1/13/2017 3:33:19 PM

Mtukufu katika roho zetu na nafsi zetu. Hakika wito wa maumbile upo ndani ya mwanadamu, lakini katika mfano wa nyakati hizi za matatizo unakuwa na nguvu zaidi.

**3.** Hakika historia inatuoyesha kwamba wengi kati ya wenye nguvu ambao walikuwa wanajizuia kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu katika wakati wa kawaida katika maisha yao, lakini wao katika wakati ambao humo wanaona kwamba nguzo za maisha yao zinaelekea kusambaratika, hakika wao wakati huo wanaelekea kwa Muumba Mtukufu, na wakati huo wanasikia sauti ya maumbile ambayo inadhihirika ndani mwao.

Historia inasema: Firaun alipoona nafsi yake iko baina ya mawimbi makubwa, maji haya ambayo ndio chanzo cha nguvu zake zote za kimada yamekuwa hivi sasa yanatekeleza hukumu ya mauti, akaona kwamba anashindwa mbele ya mawimbi haya, haikuwa kwake isipokuwa alipiga kelele: "Hivi sasa nimeamini kwamba hakuna Mungu isipokuwa Mola wa Musa." Hakika wito huu kwa hakika umetoka ndani mwake. Na sio Firaun peke yake bali ni watu wote ambao wanakuwa katika mfano wa nyakati zake wanasikia wito huu.

**4.** Hakika nyinyi mnapozirejea dhamira zenu mtakuta kwamba ndani kuna nuru inaangaza na inakulinganieni kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na pengine imewakabili katika maisha yenu mengi miongoni mwa matatizo na shida ngumu. Mnazikuta nafsi zenu zinashindwa mbele yake, na katika nyakati hizi kwa uhakika mlifikiria kuwa kuna nguvu kuu katika ulimwengu wa uwepo. Nguvu hii inaweza kutatua matatizo kwa wepesi na kwa raha. Na katika nyakati hizi yanaangaza matumaini yenye kuchanganyika na upendo wa huyo 'mwanzilishi' mtukufu, na matumaini haya yanajumuisha roho na nafsi na kusambarataisha mawingu ya kukata tamaa yenye kugubika katika nyoyo zenu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 12 1/13/2017 3:33:19 PM

**5.** Ndio, hakika hii ndio njia fupi ambayo inawezekana kwa kila mmoja kuikuta ndani mwake, na ambayo inamuongoza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba Mtukufu wa ulimwengu wa uwepo.

SWALI MOJA: Sisi Tunajua kwamba inawezekana mmoja wenu kujiuliza swali hili: Je, haiwezi kudhaniwa kwamba fikra hii imetujia kwa matokeo ya mafunzo ambayo tumeyapata katika jamii yetu na kutoka kwa wazazi wetu katika nyakati ngumu? Kisha tukanyoosha mkono wa dua kwa Mwenyezi Mungu? – Sisi tumelipa haki swali hili na tunalo jawabu linalokinaisha tutalitaja katika somo lijalo.

**Qur'ani Tukufu inasema:**

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ

**"Na wanapopanda katika jahazi, humwomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafia dini, lakini anapowaokoa wakafika nchi kavu mara wanamshirikisha." (Ankabut; 29: 65).**

**TAFAKARI:**

**1.** Jaribu kuhifadhi Aya iliyotajwa, Sura na maana yake neno kwa neno, na kuifahamu Qur'ani Tukufu kidogo kidogo.

**2.** Je, imetokea kwako kukabiliwa na tukio gumu na ukabakia mbele yake ni mwenye kushindwa, na tumaini lako pekee ni huruma na uangalizi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu? Fafanua hilo ndani ya makala au mawaidha machache.

**3.** Kwa nini tumeita njia hii kwamba ni njia fupi zaidi?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 13 1/13/2017 3:33:20 PM

# SOMO LA NNE:

**Jawabu la Swali Muhimu.**

Katika somo lililotangulia tumefikia kwamba sauti ya tauhidi na ibada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu tunaisikia ndani mwetu, husୁsan katika shida na matatizo, ambapo inapaa sauti hii na inakuwa na nguvu zaidi, na sisi bila ya matakwa tunamkumbuka Mwenyezi Mungu na tunaomba msaada kwenye nguvu Yake isiyo na kikomo na rehema Yake ambayo inakienea kila kitu.

Huenda hapa linajitokeza swali katika akili; Je, wito huu wa ndani, ambao tumeuita ‘wito au sauti ya maumbile’, inawezekana umezaliwa kutokana na mafunzo ambayo tumeyapata kutoka katika jamii na madrasa, au kutoka kwa wazazi na hayo yakawa ni mazoea yetu?

**Jawabu:**

Linafahamika vizuri swali hili kwa utangulizi mfupi.

Hakika mazoea na ada, ni vitendo na vitu vinavyobadilika, yaani sisi haiwezekani kukuta ada au mila imebakia katika hali yake muda wote wa historia ya mwanadamu kwa ummah na wananchi. Mas’ala ambayo leo yanakuwa ni ada au mila yenye kufuatwa na wananchi inaweza kubadilika, na inawezekana yasiwe ni yenye kufuatwa na wananchi wa nchi au eneo jingine.

Na hivyo tunaposhuhudia maudhui fulani katika watu na mataifa yote bila ya kubagua katika zama na nyakati, wakati huo ni wajibu tujue kwamba yana mizizi ya kimaumbile katika roho na nafsi ya mwanadamu. Mfano uhusiano wa mama na mtoto haiwezekani kuwa ni matokeo ya kujifunza au ada, kwa sababu haiwezekani sisi



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 14 1/13/2017 3:33:20 PM

kumkuta mama katika kaumu yoyote, au taifa lolote na katika zama au wakati wowote ambaye hampendi mwanawe.

Ndio, inawezekana mama kuuwa nafsi yake kwa matokeo ya msongo wa kinafsi, au baba katika zama za ujahilia kumzika binti yake kwa matokeo ya fikra na dhana ya kimakosa, lakini hali hizi ni nadra na chache, na zinatoweka haraka na badala yake kudhihiri hali ya kupenda watoto kwa sura iliyo wazi. Pamoja na kuuchukulia kwa mazingatio utangulizi huu, tutaangalia katika mas'ala ya ibada ya Mwenyezi Mungu kwa watu wakati uliopita na hivi sasa:

**Angalizo:** Somo hili ni gumu kiasi fulani hivyo inahitajia umakini.

**1.** Hakika kutokana na kauli za maulamaa wa elimu ya jamii na wanahistoria wakubwa, hatukuti zama au wakati hakupatikani humo madhehebu na dini kwa wanaadamu. Kulikuwa kunapatikana aina ya madhehebu katika kila zama na katika kila sehemu ya dunia. Na hii ni dalili ya wazi kwamba ibada ya Mwenyezi Mungu inatoka ndani ya roho na maumbile ya mwanadamu, na sio matokeo ya mafunzo, mazoea na mila, kwa sababu kama ingekuwa hivyo isingekuwa ni ya jumla na ni yenye kudumu kiasi hiki.

Na tunazo dalili zinazobainisha kwamba kulikuwa na watu walioishi kabla ya historia,[2] ambao walikuwa na aina fulani ya dini au madhehebu. Kwa kuzingatia kuwa Mwenyezi Mungu ni uwepo ulio nje ya mazingira, alikuwa anatafutwa kupitia kwa viumbe vilivyopo katika mazingira, hivyo mwanadamu akawa anatengeneza masanamu na mizimu. Lakini kwa msaada wa maendeleo ya kifikra, ameweza hatua kwa hatua kuipata haki, na kuacha mtazamo wa vitu

[2] Tunaposema – kabla ya historia – tunakusudia zama ambayo uandishi ulikuwa bado haujavumbuliwa ili kuacha athari yenye kuandikwa ya mwadamu wa zamani.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 15 1/13/2017 3:33:20 PM

vya kimada na kujua uwezo mkubwa wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kupitia ulimwengu wa kimada.

**2.** Baadhi ya maulama wa kubwa wa kinafsi wanasema wazi kwamba kuna pande nne au kuna hisia nne katika roho ya mwanadamu.

**a.** **Hisia ya maarifa:** Ambayo inamsukuma mwanadamu katika elimu na maarifa, na kumfanya kuwa na kiu ya elimu vyovyote itakavyokuwa, sawa iwe ni yenye manufaa kimada au laa.

**b.** **Hisia ya kheri:** Nayo ni chanzo cha mambo ya tabia ya mwanadamu katika ulimwengu wa kibinadamu.

**c.** **Hisia ya uzuri:** Nayo ni chimbuko la mashairi, fasihi na sanaa kwa maana yake halisi.

**d.** **Hisia ya dini:** Ambayo inamlingania mwanadamu katika kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu na kutekeleza amri zake. Na ndivyo tunavyoona kwamba hisia ya kidini ni moja ya hisia zenye mizizi katika roho ya mwanadamu, yaani haitengani naye na haitotengana naye daima.

**3.** Tutaona katika utafiti ujao vilevile kwamba watu wengi wa kimada na walahidi wanakubali kwa njia moja au nyingine, uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hata kama hawataji jina la Mwenyezi Mungu na wanampa jina la 'mazingira' au majina mengine, lakini sifa ambazo wanazisifia zinafanana na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mfano wanasema: Hakika mazingira yalipompa mwanadamu figo mbili ni kwa sababu yanajua kwamba akichomolewa figo moja, hakika mwanadamu anaweza kuishi kwa figo moja.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 16 1/13/2017 3:33:20 PM

Vivyo hivyo hakika wao wanatumia mfano wa maneno haya, lakini je maudhui haya yanaafikiana na mazingira ambayo hayahisi? Au ni ishara ya Mola ambaye elimu yake haina kikomo wala nguvu zake haziishi hata kama jina lake ni mazingira?

Hakika ambayo tunaweza kuyapata katika utafiti huu ni:

Hakika uhusiano wetu na mapenzi yetu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu vipo daima katika uwepo wetu na vitaendelea kuwepo.

Hakika kumwamini Mwenyezi Mungu kutabakia kuwa ni mshumaa wenye kudumu unaotoa vuguvugu katika nyoyo zetu na roho zetu.

Katika kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu hatulazimiki kukata masafa marefu, bali ni juu yetu kushuhudia kina cha uwepo wetu ambapo tutapata kumwamini Yeye, Qur'ani Tukufu inasema:

وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ

**"Sisi tuko karibu zaidi kuliko mshipa wa shingo." (Sura Qaf: 16).**

# TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Lete mifano ya ada na mifano ya maumbile.

**2.** Kwa nini watu majahili walikuwa wanaelemea katika ibada ya masanamu na mizimu?

**3.** Kwanini watu wa mada wanayapa mazingira jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 17 1/13/2017 3:33:20 PM

# SOMO LA TANO:

**Kisa cha kweli.**

Tulisema hakika watu ambao wanapinga uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ndimi zao, kunapatikana ndani mwa roho zao imani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hakuna shaka kwamba mafanikio maalum ya baadhi ya watu miongoni mwa wanyonge hutengeneza ghururi ambayo ndio chanzo cha usahaulifu, kwa kiasi kwamba mwanadamu anasahau hata maumbile yake. Lakini anapotikiswa na matukio na kutetereka maisha yake na kupatwa na matatizo toka kila upande, wakati huo linaondoka pazia la ghururi mbele ya macho yake na yanadhihirika maumbile ya tauhidi na kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Historia inatukumbusha mifano mingi miongoni mwa mifano ya watu hawa, na hapa nawaletea mmojawapo:

Kulikuwa na Waziri mwadilifu na mwenye nguvu sana, ambaye alikuwa anashikilia hatamu za mambo yote na hakuna yeyote aliyejaribu kumpinga. Siku moja aliingia katika kikao kilichohudhuriwa na maulamaa wote wa dini, akawaambia: "Hadi lini tutasema kuwa ulimwengu una Mola? Hakika mimi nina hoja elfu moja zinazopinga hilo."

Waziri alitamka maneno yake kwa kiburi, na maulamaa waliohudhuria walikuwa wanajua kuwa yeye sio mtu wa mantiki na hoja, bali nguvu yake imemfanya awe na ghururi kwa kiasi kwamba hajui tena neno la haki, na hivyo wao walinyamaza kimya chenye kumaanisha dharau.

Ukapita muda tangu tukio hilo kutokea. Baada ya muda serikali ikamtuhumu Waziri na ikamkamata na kumfunga jela. Akatafaka-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 18 1/13/2017 3:33:20 PM

ri mmoja wa maulamaa waliokuwepo katika kikao kile kwamba umeshawadia wakati wa kumfahamisha Waziri, kwani yuko katika hali inayovunja kiburi chake na kuondoa pazia katika macho yake, na kuamsha humo hisia za kuikubali haki. Kama atawasiliana naye na kumnasihi kutakuwa na matokeo yenye matunda. Mwanachuoni akaomba kukutana naye, kisha akaenda kumuona huko jela. Aliposogea alimuona Waziri anatembea hali ya kutafakari na anasoma beti za mashairi, akasikiliza. Akamsikia anasoma shairi hili mashuhuri:

> "Sisi sote ni simba (mashujaa),
> lakini ni simba (mashujaa) katika elimu,
> shambulio letu linatakiwa kuwa kama upepo (la kasi),
> liwe la dhahiri na la kificho, tuwe tayari kujitolea roho zetu
> kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."

Na hii inamaana kwamba sisi ni kama alama nyeusi katika bendera inayopepea kwa kupeperushwa na upepo, na kudhihiri weusi kana kwamba inashambulia, wakati ambapo uhalisia ni kwamba sio zaidi ya picha inayopeperushwa na upepo ambao unaipa uwezo huu, hivyo vyovyote sisi tutakavyokuwa na nguvu hakika sisi hatumiliki nguvu yoyote isipokuwa ni Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anayetupa nguvu hii, na Yeye anaweza kutupokonya wakati wowote anaotaka.

Na mwanachuoni alimuona Waziri si mlahidi tena, bali amekuwa ni muumini mwenye imani zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Akamuuliza kuhusu hali yake kisha akasema: "Je, unakumbuka siku ambayo ulisema una hoja elfu moja za kutokuwepo Mwenyezi Mungu Mmoja? Mimi nimekuja ili nikujibu hilo kwa dalili moja tu, hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliyekupokonya wewe kwa wepesi, ule uwezo na nguvu kubwa ambayo ulikuwa unaimiliki."



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 19 1/13/2017 3:33:20 PM

Waziri akainamisha kichwa kwa haya na hakujibu kwa sababu ameshajua kosa ambalo alikuwa nalo, na ameshaona nuru ambayo imeanza kuangaza ndani mwake. Qur'ani Tukufu inasema:

حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْغَرَقُ قَالَ آمَنْتُ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا الَّذِي آمَنَتْ بِهِ بَنُو إِسْرَائِيلَ

**"…..Mpaka kulipofikia kufa maji, akasema: Nimeamini kwamba hakuna Mola isipokuwa yule wanayemwamini Wana wa Israeli….." (Surat Yunus; 10:90).**

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Andika mistari michache kutokana na kisa hiki cha kweli.
2. Kwa nini wameitwa (Wana wa Israili) kwa jina hili?
3. Firaun alikuwa ni nani, alikuwa anaishi wapi, na alikuwa anadai nini?

## SOMO LA SITA:

**Nja ya pili ya kumjua Mwenyezi Mungu.**

**Njia ya nje:**

Kwa kutupia macho kwa haraka katika ulimwengu ambao tunaishi humo, hakika sisi tunafikia kwenye ukweli kwamba ulimwengu wa uwepo sio kitu chenye mkanganyiko bali kila kitu humo kinakwenda kulingana na mpangilio maalum, na kwamba vyombo vya ulimwengu vinafanana na mfumo uliopangiliwa uliogawika unakwenda kwa lengo maalum.

Nukta ifuatayo inaweza kuweka wazi kila kisichofahamika katika nyanja hiii:

1. Ili kubakia muonekano wowote katika kila kiumbe kilicho hai ni lazima kuwe na mnyororo wa kanuni na masharti maalum, kwa mfano kuota mti inalazimu kuwepo na ardhi, maji, hewa inayofaa na joto maalum ili tuweze kupanda mbengu, na hivyo kupata virutubisho na kupumua, kustawi na kukua, na utangulizi unahitajia akili, elimu na maarifa.
2. Hakika kila kiumbe kina athari yake maalum, mfano maji na moto kila kimoja kina athari yake makhususi ambayo haitengani nayo, na inabaki kuwa ni kanuni maalum.
3. Kuna ushirikiano baina ya viumbe hai vilivyopo, mfano mwili wa mwanadamu ambaye yeye binafsi ni ulimwengu, hakika viungo vyake vyote vinafanya kazi kwa kujiendesha vyenyewe (otomatiki) kwa uelewano na kwa namna maalum. Kama mwili utapatwa na hatari basi viungo vyote vitashirikiana katika kukabiliana na hatari hiyo na kuutetea mwili. Hivyo mafungamano haya na ushirikiano huu makini ni dalili nyingine juu ya kuwepo utaratibu katika ulimwengu wa uwepo.
4. Hakika kuutazama ulimwengu kunabainisha kwamba sio tu ni kiwiliwili hai kilichopo, bali viumbe vyote mbalimbali vilivyopo katika ulimwengu vilevile vina uhusiano maalum baina yake na vingine, mfano kwa kumea viumbe hai inalazimu kuwepo mwanga wa jua, anga linalonyesheleza mvua, upepo unaovuma, kuendeleza ardhi na zana za ardhi na vifaa vyake, yote hayo ni dalili juu ya kuwepo utaratibu maalum katika ulimwengu wa uwepo.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 21 1/13/2017 3:33:20 PM

**Mafungamano ya mpangilio na akili:**

Hakika ukweli huu unadhihiri mbele ya kila mwanadamu kwamba utaratibu katika kila kiumbe unaonyesha juu ya akili, fikra, mpangilio na lengo. Kwa sababu mwanadamu anapoona katika kila sehemu utaratibu, hesabu na kanuni madhubuti, anajua kwamba ni lazima kuwepo na chanzo cha elimu na uwezo. Na kujua hayo haihitajii kutoa hoja nyingi, kwani yeye anajua kwamba mtu mjinga na kipofu hawezi kuandika insha au makala ya kijamii ya ukosoaji katika mashine ya kuandikia. Vilevile mtoto wa umri wa miaka miwili hawezi kushika kalamu au penseli na kuchora kibao kizuri, bali hakika sisi tunapoona makala tutajua kwamba mtu mwenye uerevu mkubwa amechora, ama tunapoona kibao kizuri sana katika makumbusho hakika sisi hatutopata shaka kwamba ni mchoraji hodari amechora, hata kama hatukuwa tumeshamuona huyo mwandishi au mchoraji.

Hivyo katika sehemu yoyote panapokuwa na chombo humo kilichopangiliwa, hakika pembezoni mwake kutakuwa na akili, na kila chombo hicho kitakapokuwa kikubwa na makini hakika elimu na akili zitakuwa kubwa kwa kiwango hicho.

Na kwa kuthibitisha maudhui haya, kwamba kila chombo kilichopangiliwa kinahitajia akili na elimu, inafahamika kutokana na hesabu za makisio zilizopo katika elimu ya mahesabu ya kisasa, kuwa njia hii inawezekana kuthibitisha. Mfano, mtu mjinga akitaka kuandika makala, hakika atabonyeza herufi katika mashine ya kuandikia, na kuandika makala hayo kwa njia ya kubahatisha, na kulingana na hesabu za makisio, hakika dalili hii au uthibitisho huu hauwezi kuthibitisha hilo katika mabilioni ya miaka, au hata kwa kurefusha umri wa ardhi. Kwa ufafanuzi wa maudhui haya zaidi rejea kitabu Muumba wa Ulimwengu, au kitabu cha Utafiti kuhusu Mwenyezi Mungu. Qur'ani Tukufu inasema:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 22 1/13/2017 3:33:20 PM

سَنُرِيهِمْ آيَاتِنَا فِي الْآفَاقِ وَفِي أَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ الْحَقُّ ۗ أَوَلَمْ يَكْفِ
بِرَبِّكَ أَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

**"Tutawaonyesha ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao mpaka iwabanikie kwamba haya ni kweli, je haikutoshi Mola Wako kuwa yeye ni Shahidi wa kila kitu" (Sura Fuswilat; 41:53).**

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** 1. Lete mifano kadhaa (isiyotajwa katika somo) ya baadhi ya vyombo vilivyotengenezwa, ambavyo vinaonyesha kwamba mtengenezaji ana akili na uerevu.

**2.** 2. Nini tofauti baina ya (upeo) na (nafsi)? Taja mifano katika upeo na katika nafsi inayoonyesha katika uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## SOMO LA SABA:

### Mifano ya mpangilio (Uumbaji).

Katika sehemu zote za ulimwengu wa uwepo tunakuta utaratibu, lengo na mkakati kwa namna ya wazi, na sasa hivi tunasoma mifano katika hayo: Na sisi tumeshawachagulia mifano midogo na mikubwa.

Kwa bahati nzuri leo, pamoja na maendeleo ya elimu ya mazingira na kufichua siri na maajabu ya ulimwengu wa mazingira, na umakini wa umbo la mwanadamu, mnyama na mimea, na jengo la ajabu, chembechembe hai za mwili, na mpangailio wa ajabu wa sayari angani, hakika milango ya kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu imefunguka mbele yetu kiasi kwamba tunaweza kusema kwa ujasiri kwamba hakika vitabu vyote vya elimu ya mazingira hakika ni vi-

tabu vya tauhidi. Ni vitabu vinavyotufundisha utukufu wa Muumba (swt), kwa sababu vitabu hivi vimeondoa pazia katika mpangilio wa ajabu uliyopo katika ulimwengu huu, na vinaonyesha upeo wa elimu na uwezo wa Muumba wa ulimwengu huu.

**1. Kituo cha uongozi wa dola (mwili):**

Mada ya rangi ya kijivu inajaza fuvu la kichwa la kila mmoja wetu, ambayo tunaiita ubongo, na ubongo huu ndio muhimu zaidi na chombo makini zaidi katika miili yetu, kwa sababu kazi yake ni kuongoza viungo vyote na kuendesha mambo yote ya viungo vya mwili. Na kwa kujua umuhimu wa kituo hiki muhimu hakuna ubaya kunukuu kwenu habari hii kwanza:

Imekuja katika magazeti kwamba kijana wa Chuo Kikuu kutoka Shirazi alipata pigo katika ubongo wake katika ajali ya gari, lakini yeye katika dhahiri hakupatwa na ubaya wowote, kwani viungo vyake vyote vilikuwa salama. Lakini kwa mshangao, alisahau matukio yote katika maisha yake wakati ambapo akili ilikuwa inafanya kazi vizuri, na alikuwa anafahamu maudhui anayoyasoma, na anafanya kama mtu mwingine yeyote. Lakini walipokuwa wanamwambia kuwa huyu ndio mama yako, yeye alikuwa anashangaa ambapo hakuwa anawajua tena wazazi wake. Wakamchukua hadi kwenye nyumba yake huko Shirazi na wakamuonyesha kazi za mikono ambazo alizifanya yeye mwenyewe, na ambazo zimetundikwa ukutani. Akawa anaziangaalia kwa mshangao na anasema kwamba hakika hii ni mara ya kwanza kuona vitu hivi. Kisha ikabainika kwamba pigo ambalo lilipata sehemu ya chembe ambayo inaunganisha baina ya fikra na hazina inayohifadhi akili ndilo lililosababisha hali hiyo. Na hii inafanana na kukata mawasiliano ya umeme katika nyaya, na kwa hiyo sehemu ya kumbukumbu zake zilizopita zimezama katika giza la usahaulifu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 24 1/13/2017 3:33:20 PM

Na pengine sehemu ambayo imepatwa na uharibifu katika ubongo haizidi ukubwa wa ncha ya pini, lakini angalia wigo wa athari ambayo imeiacha katika maisha ya huyu mtu, na hapa inabainika ni unyeti ulioje wa kiungo hiki cha ubongo na upeo wa umuhimu wake.

Ubongo na mnyororo wa mishipa unaundwa na sehemu mbili muhimu:

1. Seheumu ya mishipa ya matakwa ambayo ni chimbuko la harakati zote za matakwa katika mwili, kwa mfano: kutembea, kuangalia, kuzungumza n.k.
2. Sehemu ya mishipa isiyokuwa ya matakwa, ambayo inaendesha harakati za moyo, utumbo na viungo mfano wa hivi, na kusimama sehemu hii ya ubongo kunatosha kusimamisha moyo au kiungo kingine chochote kufanya kazi.

Hakika kituo cha akili, matakwa, hisia na hifadhi ni sehemu nyeti sana katika ubongo, na yenye hisia za nafsi kama vile ghadhabu, hofu na mfano wa hayo yanayofungamana nayo. Na kama ikiondolewa sehemu hii ya ubongo kwa mnyama na mishipa yake ikawa ni salama basi atabaki hai, lakini atapoteza kabisa fahamu na hisia, kwani iliondolewa sehemu hii kwa ndege na akabakia hai kwa muda mrefu, lakini hakujua tena namna ya kula punje ambazo zilikuwa zinawekwa mbele yake pamoja na kwamba ana njaa, na wakimrusha ili aruke, basi alikuwa anagonga kila kilichopo mbele yake na kuanguka.[3]

---

[3] **Ubongo** ndio kiini cha mfumo wa neva katika wanyama wote wenye uti wa mgongo, na wengi wa wanyama wasio na uti. Baadhi ya wanyama wasiostawi kama vile konyeza na kiti cha pweza wana mfumo wa neva uliogatuliwa bila ubongo, huku tipwatipwa wa bahari wakiukosa mfumo wa neva kabisa. Katika wenye uti, ubongo uko katika kichwa ukilindwa kwa fuvu na ukiwa karibu na viungo vya hisia za msingi; yaani kuona, kusikia, usawa, ladha na harufu. Ubongo unaweza kuwa changamani sana.

Gamba la ubongo wa binadamu lina takribani niuroni bilioni 15-33, labda zaidi, kutegemeana na jinsia na umri, zilizounganishwa na takribani miunganiko ya sinepsi 10,000



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 25 1/13/2017 3:33:20 PM

**2. Sehemu nyingine ya ajabu katika ubongo ni kasha la kumbukumbu:**

Je, mmejaribu kufikiria hata siku moja kwamba ni ajabu ilioje ya nguvu ya kumbukumbu? Na kama tukikosa nguvu ya kumbukumbu kwa muda wa saa moja ni hali mbaya ilioje tutakuwa nayo?

Hakika kituo cha kumbukumbu ambacho kinachukua sehemu ndogo katika ubongo kinatuhifadhia kumbukumbu za umri wote, kwani kinatuhifadhia kila kinachofungamana na watu waliopo pembezoni mwetu kwa maumbo, rangi, tabia, hali za kinafsi na mengineyo yasiyokuwa hayo. Kwa hiyo kinatuhifadhia mafaili kamili na maalum ya kila mmoja, na kwa hiyo hakika sisi tunapokutana na mtu, ubongo unaanza kutoa faili la huyu mtu na kutupa taarifa haraka kuhusiana naye. Kisha unatuamuru kutoa jibu mwafaka, kama ni rafiki tunamheshimu na kama ni adui tunakabiliana naye kwa

---

kila mmoja. Kila milimita ya kizio cha ukubwa wa gamba la ubongo ina takribani sinepsi bilioni moja. Niuroni hizi huwasiliana na nyingine kwa njia ya fumwele ndefu za protoplazimu ziitwazo akzoni, ambazo hubeba mifuatano ya mipigo ya vichocheo viitwavyo matendo tarajiwa kuelekea sehemu mbali za ubongo au mwili na kulenga seli maalum zitakazovipokea. Ubongo hudhibiti mifumo mingine ya viungo vingine vya mwili, iwe kwa kusisimua misuli au kwa kusababisha kutolewa kwa kemikali kama vile homoni. Udhibiti huu kutoka mahali pamoja unaruhusu majibu ya haraka na yaliyoratibiwa kwa mabadiliko katika mazingira.

Baadhi ya mwitikio wa kimsingi inawezekana bila ubongo: hata viumbe walio na chembe moja wanaweza kufasiri yaliyo katika mazingira na kutenda kulingana na mabadiliko hayo. Tipwatipwa wa bahari, wasio na mfumo mkuu wa neva, wanaweza kujikunyata na hata kusonga kwa namna iliyotibiwa. Katika wenye uti, uti wa mgongo wenyewe una viungo vya neva vinavyoweza kuanzisha tendohiaria pamoja na kuelekeza mifumo rahisi ya kusonga kama vile kuogelea au kutembea. Hata hivyo, udhibiti changamani wa tabia kwa msingi ya mchango wa hisia tete unahitaji uwezo-unganishaji wa ubongo wa kati. Licha ya maendeleo ya kasi ya sayansi, mengi kuhusu jinsi ubongo unavyofanya kazi bado ni siri. Majukumu ya neva na sinepsi zikiwa pekee sasa inaeleweka kwa undani mkubwa, lakini jinsi yanavyoshirikiana katika majumuiya ya maelfu au mamilioni imekuwa vigumu sana kufumbua. Mbinu za uchunguzi kama vile unakili wa EEG na upigaji picha ubongo unaofanya kazi umetuambia kwamba utendaji wa ubongo unatendeka kwa utaratibu sana, huku kunakili kitengo kimoja kukiweza kufichua shughuli za neva moja, jinsi chembe moja inavyochangia michakato changamani haijulikani – **MHARIRI.**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 26 1/13/2017 3:33:20 PM

chuki, lakini vitendo vyote hivi vinatokea kwa haraka kiasi kwamba hatuhisi muda wake.

Hakika ajabu katika mas'ala haya inabainika kwetu tunapotaka kuandika kila kitu kilichopo katika akili zetu au kukifikiria, hakuna shaka kwamba hayo yanatutaka kutumia sehemu kubwa sana ya karatasi na kaseti zinazoweza kujaa hifadhi kubwa. Na ajabu zaidi kuliko hayo tunapotaka kutoa karatasi au kanda katika rundo hilo, hakika inahitajia kazi ya idadi kubwa ya watu kufanya kazi hii. Ama akili zetu – ambazo tumezipa istilahi ya kasha – zinafanya kazi hii kwa haraka na kwa wepesi.

Vipi mazingira ambayo hayana hisia yanaweza kuumba hisia?!!

Kuhusu maajabu ya ubongo wa binadamu vimetungwa vitabu vingi, sehemu miongoni mwayo yametajwa katika masomo ya sekondari na chuo kikuu. Lakini je, inawezekana kuamini kwamba chombo makini sana na kigumu sana na kisichofahamika kiwe kimetengenezwa na mazingira yasiyo na hisia? Na cha ajabu zaidi kuliko hayo ni kufikiria kwamba mazingira yasiyo na akili yanaweza kuumba akili!!

Qur'ani tukufu inasema:

وَفِي أَنْفُسِكُمْ ۚ أَفَلَا تُبْصِرُونَ

**"Na katika nafsi zenu je hamuoni." (Sura Dhariyati: 21).**

# TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Je unajua sehemu nyingine za ajabu kuliko ubongo wa mwanadamu?

**2.** Ni upi mpangilio aliouleta Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kuhifadhi ubongo wa mwanadamu mbele ya matukio mbalimbali?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 27 1/13/2017 3:33:20 PM

# SOMO LA NANE:

## Ulimwengu wa ajabu katika ndege mdogo

Na tutoke katika somo hili, katika nchi ya miili yetu mikubwa, pamoja na kwamba sisi bado tungali katika mwanzo wa viunga vya miji yake saba, kisha tupitie kwa haraka hapa na pale, na kuona mifano ya mpangilio wa viumbe vilivyopo:

Tunaangalia mbinguni usiku wa giza na kuona ndege wa ajabu na anaruka kwa ushujaa baina ya pazia la giza kama vile kivuli kisichoonekana nyuma ya giza lake. Hakika ndege huyu ni popo, ambaye kila kitu humo ni cha ajabu lakini kuruka kwake katika giza la usiku ni ajabu zaidi kuliko kila kitu. Anaruka kwa wepesi katika giza totoro bila ya kugongana na kizuizi chochote, na sisi kila tunaposoma hayo tunaangalia katika upande wa siri za ndege huyu. Yeye anaruka ndani ya giza la usiku kwa ushujaa na haraka kabisa kama ndege ambaye anaruka katika weupe wa mchana.

Yeye kama asingepewa zana inayomzuia kugongana na vizuizi, asingeweza kuruka. Na kama angeachwa katika handaki lililojaa moshi na lenye makorongo mengi, hakika atavuka makorongo haya kwa haraka na kwa wepesi bila ya kugonga kuta hata mara moja, na bila ya kuudhiwa na moshi. Hakika hali hii ya ajabu kwa popo ni kwa sababu maalum kwake inayofanana na rada.

Hapa ni wajibu kujua kidogo juu ya rada ili tufahamu rada iliyopo katika umbile la popo mdogo. Kuna utafiti katika fizikia kuhusu mawimbi ambayo yako juu ya sauti, nayo yana mawimbi ya masafa marefu kiasi kwamba masikio ya mwanadamu hayasikii, na kwa sababu hii yameitwa mawimbi yaliyo juu ya sauti. Na iwapo ikitokea mtumaji mwenye nguvu ametuma mawimbi kama haya, hakika mawimbi haya huenda mbele, na kama yatagongana na ki-

zuizi mfano wa ndege au ukuta au kizuizi kingine, huwa kama mpira unaotoa sauti pindi unapogongana na jabali au ukuta. Ni kama sauti tunayoitoa mbele ya jabali kubwa au ukuta, hivyo katika hali ya sauti kujirudiarudia tunasikia mwangwi na hapo tunaweza kujua masafa yaliyopo na hata uwepo wa jabali hilo au ukuta huo. Hilo ni kupitia sauti hiyo na kujirudia rudia kwake.

Hakika ndege wengi na meli zinaongozwa kwa njia ya chombo hiki, rada, ambapo wahusika wanaweza kwenda upande wowote wanaoutaka, au kugundua ndege na meli za maadui.

Maulamaa wanasema kwamba kuna chombo kidogo kinachofanana na rada katika ndege huyu, kwa dalili kwamba kama sisi tukimwachia ndege huyu katika chumba na tukaweka kipaza sauti kinachoweza kumfanya mtu asike mawimbi yaliyo juu ya sauti, hakika sisi tutasikia mtikisiko unagonga masikio ndani ya chumba, na tutasikia katika kila sekunde mara 30 - 60 mawimbi yaliyo juu ya sauti yanatoka kwa popo. Na hapa linajitokeza swali, kiungo kipi kwa popo kinatoa mawimbi haya, kiko wapi chombo cha kutuma mawasiliano, na ni chombo kipi cha kunasia mawimbi?

Maulamaa wanasema kwa kujibu swali hili, hakika mawimbi yanaletwa na vishipa vyenye nguvu katika shingo ya popo, na yanatoka kupitia kwenye pua yake hadi nje, na masikio yake makubwa yanafanya kazi ya kunasa mawimbi yanayopita. Na hivi ndivyo popo anavyotegemea masikio yake katika kuruka kwake usiku. Na mwanachuoni wa Kirusi jina lake ni Joreen, amethibitisha katika utafiti ambao aliufanya, kwamba kama yataondolewa masikio ya popo hakika hatoweza kuruka katika giza bila kugonga vizuizi. Lakini yakiondolewa macho yake hakika anaweza kuruka kwa umahiri, na hii inamaanisha kwamba popo anaona kwa masikio yake na sio kwa macho yake! Na hili ni jambo la ajabu!!



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 29 1/13/2017 3:33:20 PM

Na sasa hivi fikirieni na zingatieni, nani aliyeweka vyombo hivi viwili vyenye kushangaza katika mwili mdogo wa huyu ndege; na nani aliyemfundisha namna ya kunufaika navyo na namna gani ananusurika kupitia kwavyo kutokana na hatari nyingi ambazo zinamkabili wakati wa kuruka kwake usiku?

Je, mazingira ambayo hayana akili wala hayahisi yanaweza kufanya kazi hii? Na kufanya kazi ya kuweka vyombo hivi viwili ambavyo vinagharimu sana, ni vipi ili maulamaa wakubwa wavitengeneze katika mwili wa popo!!

Anasema Amirul-Muuminina Imamu Ali bin Abutalib عليه السلام katika *Nahjul-Balaghah* katika hotuba ndefu kuhusu popo: "Hakumzuii kuruka humo giza linapotanda, ametakasika Mwenyezi Mungu Muumba wa kila kitu pasipo na mfano." (Hotuba ya 155).

# TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Una taarifa gani nyingine kuhusu popo?

**2.** Je, unajua kuhusu mabawa ya popo, namna anavyozaa, hata namna ya kulala kwake, kunatofautiana na wanyama wengine? Na hii inamaanisha kwamba ni mnyama wa kipekee.

# SOMO LA TISA:

**Urafiki baina ya wadudu na maua**

Siku moja kati ya siku za vuli, wakati joto linaanza kuongezeka piteni katika mabustani na mashamba mazuri ya kijani, hakika mtaona makundi makubwa ya wadudu wadogo, nyuki, nzi na vipepeo wanaruka kwa utulivu na bila ya sauti. Yanaruka hapa na pale na



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 30 1/13/2017 3:33:20 PM

wadudu hao wanahama toka kwenye ua hadi jingine, na kutoka kwenye tawi moja hadi jingine. Wakiwa katika uchangamfu na harakati kana kwamba kuna kiongozi anawaamuru kuendelea na kazi kwa bidii. Wanaruka hapa na pale na mbawa zao na miguu yao imefunikwa kwa utovu wa njano kutoka kwenye maua ambayo wanatua juu yake, vivyo hivyo kana kwamba ni wafanyakazi wenye kushughulika kwa bidii katika kiwanda ambacho wanafanya kazi humo. Na hakika wana kazi muhimu, na kazi hii ni kubwa kiasi kwamba Profesa Leon Peter anasema: - “Ni watu wachache wanajua kwamba kama si wadudu basi meza zetu zingekosa matunda.”

Na sisi tunaongezea sentensi hii katika kauli yake: “Mashamba yetu na bustani zetu zingekosa kwa muda mrefu kijani hicho, hewa nzuri, ubaridi na uchangamfu,” na hivyo hakika wadudu katika uhalisia ndio ambao wanafanya kazi ya kulea matunda na kufikisha mbegu za uzalishaji kwenye maua.

Bila shaka mtauliza kwa nini? Kwa sababu kazi muhimu ya maisha ya maua ni kazi ya kupeleka mbegu za kiume na inatimia kwa njia hiyo. Na kwa hakika vile vile mmeshasikia kwamba maua na mimea ni kama wanyama wengine, yana viungo vya uzazi, vya kiume na vya kike, kama haijatimia kuingiliana baina yao hatutopata matunda na maua.

Lakini je, mmefikiria kwamba kuna aina mbalimbali hazitembei, hivyo ni namna gani hizi zinavutika kwa baadhi yake, na vipi kukutana baina ya utomvu wa kiume ambao unafanana na mbegu za kiume, na utomvu wa kike unaofanana na mbegu za kike, na kwa hili inakuwa utangulizi wa kuoana umeshatimia. Hakika kazi hii mara nyingi hufanywa na wadudu, na wakati mwingine ni upepo. Lakini jambo hili sio kwa wepesi huu ambao tunaufikiria, ndoa hii tukufu na iliyojaa kheri na baraka na ambayo inatimia kwa njia ya posa ya wadudu, ina historia na ufafanuzi mrefu na mzuri. Katika maelezo yafuatayo tutaeleza moja ya ufafanuzi huu:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 31 1/13/2017 3:33:20 PM

**Marafiki wawili vipenzi na wa zamani:**

Hakika maulamaa wa mazingira, baada ya utafiti wamefikia katika hitimisho kwamba mimea na maua yamedhihiri katika nusu ya pili ya jiolojia ya pili ya ardhi, na cha ajabu ni kwamba wadudu wamedhihiri katika ulimwengu katika zama hizo hizo, na walikuwa ni marafiki wakati huo hadi hivi sasa kupitia matukio ya kihistoria yenye msongamano katika kuumba viumbe, kiasi kwamba kila mmoja miongoni mwao amekuwa anamkamilisha mwingine. Maua ili yapate upendo kwa marafiki wa kudumu, hakika yanalimbikiza ndani mwake utomvu wenye ladha tamu, na yanautoa asubuhi kwa wadudu ambao wanafanya kazi ya kuhamisha mbegu za kiume ili mimba ipatikane, na sukari hii maalum ni tamu kiasi kwamba wanavutika kwayo wadudu bila ya hiyari yao.

Na baadhi ya maulamaa wa mimea wanaitakidi kwamba rangi nzuri na manukato mazuri ya maua yana nafasi muhimu katika kuwavutia wadudu kwenye maua. Na yamethibitisha majaribio mengi yaliyofanywa katika nyuki, kwamba nyuki anatofautisha baina ya rangi na anahisi manukato ya maua.

Na kwa hakika ni kwamba maua ndio ambayo yanafanya kazi ya kujipamba kwa ajili ya wadudu. Yananukia kiasi kwamba vipepeo na nyuki wanavutika kwayo, na wadudu hawa wanakaribisha wito huu, na kuitikia na kula utomvu. Na utomvu huu kwa hakika ni chakula muhimu kwa wadudu, na unapokusanywa hakika unatutengenezea asali, ambapo nyuki anakula sehemu ya utomvu na uliobaki inauleta na kuuhifadhi katika sega lake kwa ajili ya sherehe. Na vivyo hivyo hakika kipindi cha mapenzi na urafiki kinasimama juu ya msingi wa manufaa na maslahi yakubadilishana baina ya wadudu na maua.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 32 1/13/2017 3:33:20 PM

# SOMO LA TAUHIDI:

Mwanadamu anaposoma mambo haya ya ajabu katika maisha ya wadudu na maua, hakika anajiuliza bila ya kupenda: Nani aliyetengeneza upendo na urafiki baina ya maua na wadudu? Nani aliyeyapa maua utomvu huu maalum na mtamu? Nani aliyeyapa maua rangi hizi nzuri na manukato haya mazuri ili yawavutie wadudu? Nani aliyeipa miguu hii na mwili huu mwembamba wadudu, vipepeo na nyuki ili kuhamisha mbegu za kiume za maua? Na kwa nini nyuki anaelekea kwenye aina hii maalum ya maua. Na kwa nini yameanza maisha ya maua na wadudu pamoja katika ulimwengu katika historia? Je, kunapatikana yeyote vyovyote atakavyokuwa na kasumba kuamini kwamba matukio yote haya yametokea bila ya lengo kabla yake? Na kwamba kanuni zenye kudumaa ambazo hazihisi katika mazingira zimeumba mambo haya ya ajabu kwa kujiendesha zenyewe?

Hapana abadani. Qur'ani tukufu inasema:

وَأَوْحَىٰ رَبُّكَ إِلَى النَّحْلِ أَنِ اتَّخِذِي مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا وَمِنَ الشَّجَرِ وَمِمَّا يَعْرِشُونَ

ثُمَّ كُلِي مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ فَاسْلُكِي سُبُلَ رَبِّكِ ذُلُلًا ۚ يَخْرُجُ مِنْ بُطُونِهَا شَرَابٌ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ فِيهِ شِفَاءٌ لِلنَّاسِ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

**"Na Mola wako akampa wahyi nyuki kwamba, tengeneza nyumba katika milima na katika miti na katika wanayoyajenga. Kisha kula katika kila matunda na ufuate njia za Mola Wako zilizo dhalili. Na katika matumbo yao kinatoka kinywaji chenye rangi mbalimbali, ndani yake kina matibabu kwa watu. Hakika katika haya kuna ishara kwa watu wanaofikiri." (Sura Nahli: 68- 69).**

# TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Nini faida ya mada tamu ndani ya maua, na nini faida ya rangi yake?

**2.** Unajua nini katika maisha ya ajabu ya nyuki?

# SOMO LA KUMI:

**Katika ulimwengu usio na kikomo wa viumbe vidogo**

Hakika sisi tunaishi pamoja na maajabu katika ulimwengu wa viumbe, na tunaamiliana navyo na tunavizoea. Na kwa sababu hii hakika sisi tunaghafilika kuhusu umuhimu wa viumbe vya ajabu, mfano:

**1.** Wanaishi wanyama na wadudu wadogo sana pembezoni mwetu, na huenda umbo la baadhi yao halizidi milimita moja au milimita mbili. Pamoja na hayo hakika wao ni kama wanyama wakubwa, wana mikono miguu, masikio na macho na hata ubongo, akili na mnyororo wa mishipa na chombo cha kumeng'enya chakula.

Na kama tukiweka ubongo wa sisimizi chini ya darubini na tukachunguza umbo lake la ajabu, basi tungeshikwa na mshangao na kutahayari. Kila sehemu yake inawakilisha kituo cha uongozi wa kiungo katika mwili mdogo wa nyuki. Na viungo hivi vimeshikamana pamoja. Na kwa kutokea dosari ndogo katika hali zake kunapelekea sehemu ya mwili kupatwa na hali ya kupooza. Na cha ajabu ni kwamba ubongo huu mdogo ambao ukubwa wake hauzidi ncha ya pini ndogo, ndani yake kuna ulimwengu wa uerevu, ustaarabu, vionjo na fani, kiasi kwamba kundi la maulamaa wamepitisha miaka



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 34 1/13/2017 3:33:21 PM

mingi katika utafiti wa maisha ya huyu mdudu wakakusanya katika vitabu vyao taarifa za ajabu zenye kustaajabisha.

Je, ambaye amekusanya uerevu wote huu na akili kwa huyu kiumbe mdogo anaweza kuwa ni mazingira yasiyomiliki kiasi cha ncha ya pini katika uerevu na akili?

**2.** Katika ulimwengu wa Atomu[4] usiojulikana, na sisi tunajua kwamba kidogo zaidi kinachojulikana hadi sasa hivi ni Atomu na sehemu zake, nayo ni ndogo kiasi kwamba darubini yenye nguvu zaidi ambayo inadhihirisha punje ndogo mno kana kwamba ni jabali inashindwa kuiona. Ikiwa mnataka kujua Atomu ni ndogo kiasi gani, inatosha kujua kwamba katika tone la maji kuna idadi ya Atomu sawa na idadi ya binadamu waliopo katika ardhi hii. Na tukitaka kuhesabu protoni[5] ya sentimita moja ya waya mrefu na tu-

[4] **Atomu na Nyukliasi** ni chembe ndogondogo sana kabisa zinazotofautisha elementi mbalimbali. Kila maada imeundwa na chembechembe ndogo za aina moja zinazojulikana kama molekyuli. Hizi molekyuli huwa ni muungano wa elementi za aina moja au aina tofauti (kiingereza huitwa compounds). Chembe ndogo ya kila elementi huitwa atomu. Kila elementi ina atomu za aina yake kulingana na asili yake. Ndani ya kila atomu kuna chembechembe za aina tofauti mojawapo ikiwa ni nyukliasi yake.

Ugunduzi wa nadharia ya atomu na kuwa ndani yake kuna elektroni ulileta maswali mengi ambayo hayakupatiwa majibu. Atomu ilijulikana kiumeme kuwa haikuwa na chaji ya aina yeyote lakini chembe cha elektroni zilizo ndani ya atomu zilijulikana kuwa na chaji hasi za umeme. Hivyo lazima ndani ya atomu (ambayo haina chaji) kutakuwa na chaji aina nyingine (ambayo ni lazima iwe chaji chanya) ambayo inaleta uwiano sawa wa kuifanya atomu kutokuwa na chaji. Fumbo gumu zaidi lilikuwa ni kwa namna gani hizo aina mbili za chaji zinaweza kuwa zimejipanga ndani ya atomu – **MHARIRI.**

[5] Ilikuwa imejulikana kuwa chaji chanya zilizokuwa zinaifanya atomu kutokakuwa na chaji hata kama kuna chaji za elektoni, zilikuwa zinapatikana ndani ya nyukliasi. Hivyo hizi chaji ndani ya nyukliasi ziliaminika kutoka ndani ya chembechembe zilizokuja kufahamika kama protoni. Kwa kuwa atomu haina chaji, basi chaji ya protoni ni sawa kabisa na ile ya elektroni isipokuwa yenyewe ni chanya na ile ya elektroni ni hasi. Njia iliyotumika katika kuthibitisha uwepo wa protoni ilitumia sana kifaa kilichoitwa *mass spectrograph*. Muundaji wa kifaa hiki alikuwa F. W. Aston. Katika kifaa chake, atomu zilizochajiwa chanya zilipitishwa katika eneo la usumaku. Eneo hili liliundwa ili kuleta atomu zenye



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 35 1/13/2017 3:33:21 PM

kawa tumewaanda watu elfu moja kwa ajili ya kazi hiyo, na akaweza kila mmoja baada ya kila sekunde moja kutenganisha protoni moja, basi tutahitaji miaka 30 – 300 (kulingana na tofauti ya aina za Atomu) ili tuweze kumaliza kuhesabu protoni za waya wa sentimita moja, na hiyo ni pamoja na kufanya kazi hiyo usiku na mchana.

Sasa tumeshafahamu kwamba sentimeta moja ya waya mrefu ina idadi hii ya Atomu, fikiria mbingu, ardhi, maji, hewa na katika sayari mfumo wa jua (*solar system*), kuna kiasi gani humo cha idadi za Atomu? Je, akili ya binadamu haichoki kufikiria hayo, na kwamba hakuna katika kiumbe cha ulimwengu kinachojua hesabu yake?

**Atomu inatoa somo katika tauhidi:**

Hakika elimu ya Atomu ni katika elimu muhimu sana katika zama zetu na yenye shughuli nyingi zaidi. Atomu, kiumbe hiki kidogo kinatupa somo katika tauhidi. Katika elimu ya Atomu kuna sehemu nne zinazovutia:

1. **Mpangilio wa kipekee:** Umetimia hadi hivi sasa uvumbuzi wa zaidi ya sehemu mia moja, elektroni zake hizo zinato-

---

tungamo tofauti tofauti kwenye filamu. Wakati filamu ilipoboreshwa, mistari ingeweza kuonekana kulingana na ayoni zilivyoifikia. Kwa jinsi Aston alivyounda kifaa chake ilimaanisha mistari ingekuwa katika umbo la *parabola*. Suala la msingi kuhusu kifaa *mass spectrograph* ni kuwa njia inayopitiwa na ayoni inakuwa imepinda wakati ikisafiri katika eneo la usumaku. Kupinda huku kunategemea vitu wiwili: chaji ya ayoni, q, na tungamo lake, m. Ayoni iliyokuwa na uwiano sawa wa chaji kwa tungamo, q/m zitawasili katika sehemu kwenye filamu. Kwa kufanya jaribio hili kwa uangalifu na hisabati, Aston aliweza kupima uwiano wa chaji kwa tungamo wa idadi kubwa ya ayoni. Kutokana na matokeo aliunda "*kanuni ya namba ya jumla*." Kutokana na kanuni hii uwiano wa chaji na tungamo wa kila ayoni ulikuwa mara kadhaa ya ule wa ayoni za *Hydrogen*. Ilionyesha Haidrojeni kuwa ni ayoni iliyojenga ayoni (na atomu) zingine. Hivyo jina protoni, kutoka neno la Kigiriki '*protos*' ikimaanisha 'ya kwanza' ilipewa ayoni ya hydrogen – **MHARIRI**.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 36 1/13/2017 3:33:21 PM

kana na elektroni moja na zinamalizikia katika zaidi ya elektroni mia moja. Hakika mpangilio huu wa ajabu haiwezekani kamwe kuwa unatokana na vitu visivyokuwa na hisia.

2. **Uwiano:** Sisi tunajua kwamba katika umeme kuna nguvu mbili zinazotofautiana, kila moja inamvuta mwenzake kuelekea kwake. Hivyo elektroni hasi na chanya zinavutana. Na katika upande mwingine hakika sisi tunajua kwamba mzunguko wa elektroni katika kituo cha Atomu unatengeneza nguvu yenye kusukuma inayojaribu kuziweka mbali elektroni kutoka katika mzunguko wa Atomu, na inazigawa chembe za Atomu, na nguvu ya mvutano inakwenda mbio kuzivuta elektroni na kuteketeza chembe za Atomu.

Hapa ni wajibu kujua kwa hesabu makini kwamba nguvu ya mvutano na nguvu ya msukumo zimetengeneza utaratibu katika chembe ya Atomu ambapo elektroni haziwezi kuponyoka wala kuvutika, bali zinabakia katika hali ya uwiano na zinaendelea katika mzunguko wake. Je, inawezekana uwiano huu kuwa umeletwa na mazingira yasiyoona wala kusikia?

3. **Kila moja katika mapito yake:** Tumesema hakika baadhi ya chembe chembe za Atomu zina elektroni nyingi, mzunguko wake hauko katika mwelekeo mmoja, bali hakika zinazunguka katika mielekeo mbalimbali, na zinazunguka kwa haraka tangu mamilioni ya miaka katika utengano maalum na katika mpaka wake bila ya kutokea mgongano wowote. Je, hali ya kila elektroni kuwa katika mapito yake na mzunguko wake kwa mpangilio wa ajabu ni kazi nyepesi?

4. **Nguvu kubwa ya chembe za Atomu:** Ili tujue ukubwa wa nguvu ya Atomu inatosha kujua kwamba mwaka 1945 lilifanywa jaribio la mlipuko wa Atomu katika jangwa la



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 37 1/13/2017 3:33:21 PM

Mexico, lilirushwa bomu dogo la Atomiki katika jengo la chuma na baada ya mlipuko jengo la chuma liliyeyuka kisha likawa moshi na likapaa kwa wepesi na kwa sauti ya kutisha. Na maulamaa walipokuja ili kuangalia jengo hawakuona athari yoyote.

Na katika ulimwengu huo huo yalirushwa mabomu mawili madogo huko Japani, moja katika mji wa Nagasaki na jingine katika mji wa Heroshima. Katika mji wa kwanza waliangamizwa watu elfu 70 na idadi kama hiyo walijeruhiwa. Muhanga katika mji wa pili idadi yao ilifikia watu elfu 30 na idadi kama hiyo walijeruhiwa. Baada ya hapo Japani ililazimika kujisalimisha, bila ya kikwazo wala sharti kwa Marekani.

Je, haitoshi kutafiti siri za Atomu moja ili mwanadamu kumjua Muumba Mtukufu? Hivyo tunaweza kusema hakika idadi ya Atomu katika ulimwengu ni dalili tosha ya kuwepo Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Qur'ani Tukufu inasema:

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَامٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ أَبْحُرٍ مَا نَفِدَتْ كَلِمَاتُ اللَّهِ ۗ

**"Na lau miti yote iliyopo ardhini ikawa ni kalamu na bahari na ikaongezewa bahari nyingine saba (kuwa wino) maneno ya Mwenyezi Mungu yasinge malizika." (Sura Luquman: 27).**

# TAFAKARI NA UJIBU:

1. Je, unajua kitu kingine katika siri za maisha ya nyuki?
2. Je, unaweza kuchora ubaoni umbo la Atomu?

# UTAFITI WA UKAMILISHO WA SOMO LA KUMI: NI UTUKUFU ULIOJE WA SIFA ZA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU

**Sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

Ni wajibu tuzinduke kwamba kwa wepesi ule ule uliotuwezesha kuwa na yakini ya uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa njia ya kusoma siri za ulimwengu wa viumbe, hakika unatuwezesha kujua sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini inahitajia umakini na tahadhari kubwa.

Ni lazima nyinyi mjiulize kwa nini? Hakika dalili juu ya hilo iko wazi, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hafanani na chochote kilichoko kwetu au katika tunavyoviona na kuvisikia. Na kwa hivyo, hakika sharti la kwanza katika kujua sifa zake (swt) ni kukana sifa zote za viumbe katika dhati yake, yaani kutofanana na yeyote katika viumbe vyenye ukomo, na hapa jambo linakuwa makini, kwa sababu sisi tumekulia ndani ya mazingira haya na mawasiliano yetu yalikuwa ya daima pamoja nayo, tumeburudika kwayo na tumeyazoea, na kwa hiyo sisi tunaelemea katika kulinganisha kila kitu kwayo.

Kwa maneno mengine, hakika yote tuliyonayo yalikuwa ni kiwiliwili na yanayohusiana na kiwiliwili, yaani viumbe vyenye wakati na sehemu maalum, na vina maumbo na upeo maalum, na hivyo hakika ni vigumu kumfikiria Mola ambaye hana kiwiliwili wala wakati wala sehemu. Na wakati ule ule anakuwa ni Mwenye kujua nyakati na sehemu zote, na anakuwa hana kikomo katika pande zote. Hakika jambo hili linamaanisha kupiga hatua katika nyanja hii kwa umakini mkubwa na kwa tahadhari.

Lakini ni dharura kwamba tunakumbuka kuwa sisi hatuwezi kamwe kujua uhalisia wa dhati ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ni wajibu tusitarajie hilo, kwa sababu linafafana na jaribio letu la kuweka bahari kwenye kikombe! Au kitoto kilichopo tumboni mwa mama yake kujua yote yaliyopo ulimwenguni, je jambo hili linawezekana?

Na hasa ukizingatia kwamba upotuvu mdogo unaweza kumuweka mbali mwanadamu maili nyingi na njia sahihi ya kumjua Mwenyezi Mungu, na hatimaye akajikuta anazama katika ibada ya mizimu na watu, ambapo sio wajibu kulingana sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu na sifa za viumbe.

**Sifa za uzuri na utukufu:**

Kwa kawaida wanazigawa sifa za Mwenyezi Mungu sehemu mbili: Sifa za *Thubutiyyah*: Yaani sifa za Mwenyezi Mungu, na sifa za *Salbiyyah*: Yaani sifa alizotakasika nazo Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na sasa hivi linajitokeza swali hili: Sifa za dhati za Mwenyezi Mungu Mtukufu ni ngapi?

Hakika jawabu la swali hili ni: Hakika sifa za Mwenyezi Mungu hazina idadi na hazina mwisho katika upande wa mtazamo, na katika upande mwingine wa mtazamo hakika sifa zinakusanywa na sifa moja, kwa sababu sifa zote za *Thubitiyyah* za Mwenyezi Mungu zinakusanywa katika sentensi hii: Hakika dhati ya Mwenyezi Mungu haina kikomo katika pande zote na ina ukamilifu wote. Na mukabala wake sifa za *Salbiyyah* zinakusanywa na sentensi hii: Hakuna upungufu wowote katika dhati ya Mwenyezi Mungu.

Lakini katika upande mwingine wa mtazamo hakika ukamilifu na upungufu una madaraja, yaani inawezekana kufikiria ukamilifu usio na kikomo, na upungufu usio na kikomo, hivyo tunaweza



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 40 1/13/2017 3:33:21 PM

kusema: Hakika Mwenyezi Mungu ana sifa *Thubutiyyah* zisizo na kikomo, na sifa za *Salbiyyah* zisizo na kikomo. Kwa sababu Yeye anamiliki ukamilifu wowote ambao tunaweza kuufikiria, na kwamba (swt) ametakasika na upungufu wowote ambao tunaweza kuufikiria. Hivyo hakika sifa za *Thubutiyyah* na *Salbiyyah* za Mwenyezi Mungu Mtukufu hazina kikomo.

**Sifa za Mwenyezi Mungu zilizo mashuhuri:**

Sifa za *Thubutiyyah* za Mwenyezi Mungu zilizo mashuhuri ni zile ambazo zimekusanywa katika beti ya shairi lifutalo:

"Mjuzi, muweza hai, mwenye kutaka na Mwenye kudiriki, wa zamani, wa tangu, mzungumzaji na mkweli."

1. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mjuzi, hivyo anafahamu na anajua kila kitu.
2. Hakika Yeye ni Muweza, yaani ni muweza wa kila kitu.
3. Hakia Yeye ni Hai, yaani ni hai ambaye ana elimu na uwezo na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mjuzi na Muweza hivyo Yeye ni Hai,
4. Hakika ni Mwenye kutaka, yaani ni Mwenye matakwa na sio mwenye kulazimishwa katika vitendo Vyake, na anatekeleza kazi yoyote na ana lengo na hekima na hakipatikani chochote mbinguni wala ardhini bila ya falsafa na lengo.
5. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufahamu, anafahamu kila kitu anaona kila kitu na anasikia kila kitu, naye ni Mwenye kufahamu kila kitu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 41 1/13/2017 3:33:21 PM

**6.** Hakika Mweneyzi Mungu ni wa zamani na wa tangu, yaani Yeye alikuwepo daima na uwepo wake hauna mwanzo, kwa sababu uwepo wake upo katika dhati yake, Yeye ni Mtukufu ni wa kudumu na wa milele, kwa sababu ambaye uwepo wake upo katika dhati yake hakika kumalizika hakuna maana yoyote kwake.

**7.** Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mzungumzaji, yaani anaweza kutikisa mawimbi ya sauti hewani na kuzungumza na Mitume wake na Manabii wake عليهم السلام, na hii haimaanishi kwamba Mwenyezi Mungu ana ulimi, mdomo na shingo.

**8.** Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mkweli, na hii inamaanisha yote anayoyasema ni kweli, na kiini cha uhalisia, kwa sababu uongo ama unakuwa kwa sababu ya ujinga au kwa udhaifu na kushindwa, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Muweza haiwezekani kuwa ni muongo.

Hakika sifa za *Salbiyyah* zilizo mashuhuri zaidi ni zile ambazo zimekusanywa katika ubeti wa shairi hili:

"Si kiungo wala kiwiliwili, haonekani wala hana sehemu maalum, hana mshirka wala mwana, jua kwamba ni Mkwasi, Muumbaji."

**1.** Sio kiungo, yaani hana viungo vilivyoungwa kwa sababu katika hali hii atahitajia viungo vyake, wakati ambapo (swt) hahitajii kitu nchochote.

**2.** Hakika Mwenyezi Mungu sio kiwiliwili, kwa sababu kiwiliwili kina kikomo, na kinabadilika na kumalizika.

**3.** Haonekani, kwa maana ya kwamba Yeye haonekani, kwa sababu kama angeonekana angekuwa ni kiwiwili, chenye kikomo na chenye kumalizika.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 42 1/13/2017 3:33:21 PM

**4.** Hana mahali wala sehemu maalum, kwa sababu sio kiwiwili hadi ahitajie sehemu.

**5.** Hana mshirika, kama angekuwa na mshirika basi angekuwa ni mwenye mpaka, na ni muhali kuwepo vitu viwili visivyo na mipaka kwa sura yoyote kati ya sura. Kisha umoja wa kanuni katika ulimwengu huu unaonyesha juu ya upweke wake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

**6.** Mwenyezi Mungu hana maana, yaani hakika sifa zake ndio dhati yake.

**7.** Hakika Mwenyezi Mungu hahitaji, Yeye amejitosheleza, kwa sababu ni uwepo usio na kikomo katika elimu, uwezo na kila kitu, hahitajii kitu chochote.

Qur'ani Tukufu inasema:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ

**"Hafanani na kitu chochote." (Sura Shuraa: 11).**

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Je, una dalili nyingine juu ya upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ya kutokuwa na mshirka?

**2.** Je, umesikia kwamba baadhi ya dini zinaitakidi utatu wa Mwenyezi Mungu, au uwili? ni madhehebu gani hayo?

# 2

# MASOMO KUMI KATIKA UADILIFU WA MWENYEZI MUNGU

## SOMO LA KWANZA:

**Uadilifu ni nini?**

Kwa nini uadilifu umehesabiwa katika sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ni miongoni mwa misingi ya dini?

Nini tofauti kati ya uadilifu na usawa?

**Kwa nini umechaguliwa uadilifu katika sifa zote?**

Ni wajibu iwe wazi kabla ya kila kitu, katika utafiti huu, ni kwa nini Maulamaa wakubwa wameuzingatia uadilifu katika sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa ni moja ya misingi mitano ya dini? Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mjuzi, Muweza, Mwadilifu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa kurehemu, ni wa zamani, ni wa milele, Muumba, na ni Mwenye kuruzuku, kwa nini katika sifa zote umechaguliwa uadilifu na umekuwa moja ya misingi mitano ya dini?

Jawabu la swali hili muhimu ni wajibu kuangalia mambo kadhaa:

1. Hakika uadilifu una umuhimu mkubwa miongoni mwa sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, kiasi kwamba nyingi kati ya sifa nyingine zinarejea kwenye sifa hiyo, kwa sababu uadilifu kwa maana ya neno pana, ni kuweka kila kitu ma-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 44 1/13/2017 3:33:21 PM

hali pake ambapo kinastahiki. Vivyo hivyo hakika mwenye hekima na mwenye kuruzuku na Mwingi wa rehema na mwingi wa kurehemu na mfano wa sifa hizi zote zinaingia katika sifa hiyo.

**2.** Hakika kadhia ya miadi (marejeo) vilevile inategemea juu ya kadhia ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu. Pia ujumbe wa Manabii na jukumu la Maimamu Ma'asumina pia vinafungamana na mas'ala ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu.

**3.** Ilitokea ikhilafu kuhusu mas'ala ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu katika mwanzo wa Uislamu: Hakika kundi moja la Waislamu miongoni mwa Ahlus-suna, wale wanaoitwa Ashairah walikataa uadilifu kabisa, na wakasema: Hakika hakuna maana ya uadilifu na dhulma kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani ulimwengu wote ni miliki yake, na kila kitendo anachokifanya ndio kiini cha uadilifu. Ashairah hawaamini hata uzuri na ubaya wa kiakili, na walikuwa wanasema: Hakika sisi hatuwezi kwa akili zetu kufahamu uzuri na ubaya, hata uzuri wa kitendo cha kheri na ubaya wa dhulma, na walikuwa na rai nyingi za kimakosa.

Na kundi jingine katika Ahlus-Sunna miongoni mwa wanaoitwa Mu'tazilah kando na Shia, wanaitakidi msingi wa uadilifu katika mambo yanayohusu Muumba Mtukufu na wanasema: Hakika Yeye hatodhulumu abadani.

Na kwa kutenganisha baina ya makundi haya mawili, kundi la pili limeitwa *Adliyyah*, ambapo walikuwa wanazingatia kuwa uadilifu ni katika misingi ya dini, na kundi la kwanza likaitwa kwa jina la *Laa Adliyyah*. Na Shia walikuwa na bado wangali wako katika kundi la *Adliyyah*. Ili Shia kutofautisha Madhehebu yao na *Adliyyah* wengine, wamezingatia kwamba Uimamu ni sehemu ya misingi ya dini.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 45 1/13/2017 3:33:21 PM

Na hivyo kila yanapokuja mazungumzo kuhusu uadilifu na uimamu, hakika inaonyesha juu ya Shia Imamiyyah.

4. Na kwa kuwa matawi ya dini yanatokana na misingi ya dini, na uadilifu wa Mwenyezi Mungu katika jamii ya kibinadamu una mchango mkubwa sana, na kwamba nguzo muhimu za jamii ya kibinadamu ni uadilifu wa kijamii. Hakika kuchagua msingi wa uadilifu kama msingi kati ya misingi ya dini; ni alama ya kuhuisha uadlifu katika jamii za kibinadamu na kupiga vita kila aina miongoni mwa aina za dhulma na ukandamizaji.

Kama ambavyo kumpwekesha Mungu katika dhati na sifa, na katika ibada, ni nuru ya umoja na muungano wa jamii ya kibinadamu, kwani hakika kumpwekesha huko kunaunga mkono, kunatia nguvu na kuunganisha safu.

Na uongozi wa Manabii na Maimamu vilevile unaelezea mas'ala ya uongozi wa haki katika jamii za kibinadamu, na hivyo hakika msingi wa uadilifu wa Mwenyezi Mungu ambao unahukumu katika ulimwengu wote wa uwepo, ni alama na ishara ya ulazima wa kuwepo uadilifu katika jamii ya kibinadamu katika nyanja zote. Hakika ulimwengu mkubwa wa viumbe umesimama kwa uadilifu, na jamii ya kibinadamu haitobakia bila ya uadilifu.

## Uadilifu ni nini?

Hakika uadilifu una maana mbili zenye kutofautiana:

1. Hakika maana pana ya neno hili kama tulivyosema ni: Kuweka kila kitu mahala pake, au kwa maana nyingine ni uwiano na ulingano. Hakika maana hii ya uadilifu ndio inayotawala katika ulimwengu wote wa viumbe na mifumo.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 46 1/13/2017 3:33:21 PM

Na pia ndani ya chembe, na katika mwili wa mwanadamu, na mimea yote na vilivyo hai. Na haya ni ambayo yamepokewa katika hadithi tukufu kutoka kwa Nabii Mtukufu ﷺ: "Kwa uadilifu zimesimama mbingu na ardhi."

Kwa mfano kama nguvu za mvutano na zenye kusukuma zitakosa uwiano wake, na moja kushinda nyingine, basi ima ardhi itavutwa upande wa jua na kuungua na kumalizika, na ima dunia itatoka kutoka katika mhimili wake na kuelea katika anga pana lisilo na mwisho. Na haya ndio aliyoyasema mshairi ambapo amesema:

Uadilifu ni nini? Ni kuweka kitu katika mahala pake,
Na dhulma ni nini? Ni kuweka kitu mahala si pake,
Uadilifu ni nini? Nywesha mti maji,
Dhulma ni nini? Ni kunywesheleza miba maji.

Ni jambo la kawaida kama mti wa maua na mti wa matunda utamwagiliwa maji, hakika hilo ni wajibu na ndio kiini cha uadilifu. Na ikiwa maji yamemwagwa kwenye majani yenye kudhuru na miiba hakika ni kupoteza na hii ndio kiini cha dhulma.

**2.** Maana nyingine ya uadilifu ni kuchunga haki za wengine, na nukta ya mkabala wake ni dhulma, yaani kupokonya haki za wengine kwa ajili ya nafsi yake mtu au kuwapa wengine au kufarakisha. Yaani kutoa haki kwa baadhi na kuzuia kwa wengine. Na katika hili inabainika wazi kwamba maana ya pili ni maalum na maana ya kwanza ni ya jumla.

Na kitu kinachoonekana ni kwamba uadilifu kwa maana zake mbili ni ukweli kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ingawa maana ya pili ndio iliyokusudiwa katika utafiti huu.

Hakika maana ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu ni kutodharau haki ya mtu na wala kutotoa haki ya mtu kwa mwingine, wala kufa-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 47 1/13/2017 3:33:21 PM

rakisha baina ya watu na kumpendelea mtu dhidi ya mwingine, na hivyo ni Yeye mwadilifu kwa maana kamilifu. Na tutajua dalili za uadilifu wake katika utafiti ujao.

Dhulma haiafikiani na dhati safi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, vyovyote itakavyokuwa umbo lake, ikiwa itakuwa ni katika njia ya kupora haki ya mtu au kutoa haki ya mtu kwa mwingine au kupunja na kufarakisha. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu hawaadhibu watu wazuri wema wala hashajiishi waovu, na wala hamwadhibu mtu kwa dhambi ya mwingine, kama ambavyo hateketezi kibichi na kikavu kwa pamoja. Na hata kama kukiwepo na mwenye dhambi katika jamii, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hamhisabu kama asiyekuwa mwenye dhambi, na ikiwa katika jamii watu wote ni wenye madhambi isipokuwa mtu mmoja, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hamuweki mtu huyu katika kiwango cha wenye madhambi bali atamtenga nao.

Ama kauli ya Ashairah kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni kwamba kama angewapeleka Manabii wote Jahanam, na akawapeleka wenye madhambi na waovu peponi, basi kitendo hiki sio dhulma. Hakika kauli hii ni mbovu na mbaya, na sio sahihi kabisa. Na kama kungekuwa na akili isiyoingiliwa na ukhorafi na kasumba, basi ingejua ubovu wa kauli hii.

**Tofauti baina ya usawa na uadilifu:**

Nukta nyingine muhimu ambayo ni wajibu kuiashiria ni: Wakati mwingine kunachanganywa baina ya uadilifu na usawa, na kudhaniwa kwamba maana ya uadilifu ni kuchunga usawa, wakati ambapo sivyo hivyo. Katika uadilifu hauzingatiwi usawa kuwa ni sharti, bali ni wajibu kuchukua ustahiki na kipaumbele kwa kuangalia mazingatio. Mfano: Sio uadilifu kuwapa mwanafunzi wa darasa moja dara-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 48 1/13/2017 3:33:21 PM

ja zinazolingana, na sio uadilifu wafanyakazi wawili kupewa haki sawa, bali uadilifu ni kupewa kila mwanafunzi daraja kwa kiwango cha elimu yake na anayostahiki, na kupewa kila mfanyakazi kwa kiwango cha uwezo wake na elimu yake.

Na uadilifu una maana hii pana katika ulimwengu wa mazingira. Kama moyo wa nyangumi mwenye uzito wa tani nyingi unalingana na moyo wa ndege ambaye ana uzito wa gramu kadhaa, usingeweza kuitwa huo ni uadilifu, kama ambavyo sio katika uadilifu kuwa sawa baina ya mizizi ya mti mkubwa na mizizi ya jani dogo, bali hii ndio kiini cha dhulma. Hakika uadilifu ni kupata kila kiumbe kwa kiasi cha haki yake na uwezo wake na ambacho anakistahiki.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Kwa nini uadilifu umezingatiwa kuwa ni moja ya misingi ya dini katika sifa zote za Mwenyezi Mungu Mtukufu?
2. Ashairah ni nani? Na unajua nini katika itikadi yao?
3. Nini radiamali katika uadilifu wa Mwenyezi Mungu katika jamii ya Mwanadamu?
4. Ni zipi maana za uadilifu? Fafanua?
5. Je, uadilifu una maana ya usawa?

## SOMO LA PILI:

### Dalili za uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu

### 1. Uzuri na ubaya katika akili:

Kujua mas’ala haya ilikuwa ni dharura katika akili zetu kujua uzuri na ubaya wa vitu kiasi fulani, na haya ndio wanayoyaita Maulamaa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 49 1/13/2017 3:33:21 PM

'uzuri na ubaya katika akili.' Mfano, hakika sisi tunajua kwamba uadilifu na wema ni kitu kizuri, na dhulma na ubakhili ni kitu kibaya. Na hili liko wazi hata kabla ya dini na madhehebu kutueleza hayo, pamoja na kwamba kuna mambo mengine ambayo ufahamu wetu unashindwa kuyajua kwa namna ya kutosha, ambapo ni wajibu kunufaika kutokana na mafunzo ya uongozi wa wachamungu na Manabii.

Na hivyo kama kundi la Waislamu wanaoitwa Ashairah wanapinga uzuri na ubaya katika akili, na wanazingatia kujua uzuri na ubaya katika uadilifu na dhulma ndio sharia na madhehebu, hakika hili ni kosa kabisa. Na kama akili zetu zingeshindwa kufahamu uzuri na ubaya basi ni wapi sisi tungejua kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hampi muujiza mtu muongo? Lakini sisi tunasema kwamba uongo ni mbaya na wala haiwezekani abadani utoke kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hakika sisi tunajua kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ahadi ya haki, na maneno yake ni ya kweli, wala haielemei katika uongo abadani, na wala hampi muujiza muongo. Na hapa inawezekana kutegemea ambayo yamepokea katika sharia na madhehebu.

Na sasa hivi tunarejea kwenye dalili za uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na katika kufikia katika uhalisia huu ni wajibu kwanza kujua:

## 2. Ni nini chanzo cha dhulma?

Hakika chanzo cha dhulma ni moja ya mambo haya:

- **i. Ujinga:** Wakati mwingine hajui dhulma anayoifanya, hakika hajui kuwa ni kupunja haki ya mtu.
- **ii. Haja**: Wakati mwingine haja inamsukuma mtu kwenye kuchukua kilicho mikononi mwa watu wengine na kufanya ki-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 50 1/13/2017 3:33:21 PM

tendo hiki cha kishetani, wakati ambapo kama asingekuwa na haja kusingekuwa na sababu ya kudhulmu.

iii. **Kushindwa:** Wakati mwingine mwanadamu anaona kwamba hapendi kutotekeleza haki ya wengine, lakini yeye anashindwa kutenda haya, hivyo analazimika kufanya dhulma.

iv. **Ghururi, Chuki na kulipiza kisasi:** Wakati mwingine kunakuwa hakuna sababu za awali, lakini ghururi inamsukuma mwanadamu kufanya uadui katika haki za wengine. Au zinamsukuma hisia za kulipiza kisasi na husuda katika dhulma na ukandamizaji, na pengine zinamsukuma kwa msukumo wa kulimbikiza, kwenye uadui dhidi ya wengine na mfano wa hayo.

Lakini kwa kuwa yoyote kati ya sifa hizo mbaya na upungufu huu hazipatikani katika dhati tukufu ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni Mjuzi wa kila kitu na hamhitajii yeyote, na ni Muweza wa kila kitu na ni mwenye huruma kwa wote, hivyo hakuna sababu yoyote ya kufanya dhulma. Yeye yupo bila ya kikomo, hana mpaka, na hivyo haitoki kwake isipokuwa kheri, Uadilifu, upole na huruma. Ikiwa ataadhibu wenye dhambi basi kwa hakika ni matokeo ya vitendo vyao, sawa kabisa na kama vile mtu mwenye kudumu katika mihadarati au vileo anavyopatwa na aina mbalimbali za maradhi. Qur'ani Tukufu inasema:

هَلْ تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

**"Kwani mnalipwa isipokuwa yale mliyoyatenda?" (Sura Namli: 90).**

## 3. Qur'ani Tukufu na uadilifu wa Mwenyezi Mungu:

Kunapatikana katika Aya za Qur'ani zinazotia mkazo sana juu ya mas'ala haya, tunakuta katika mahala:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 51 1/13/2017 3:33:21 PM

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَٰكِنَّ النَّاسَ أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ

**"Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu chochote. Lakini watu wanajidhulumu wenyewe." (Sura Yunus: 44).**

Na katika sehemu nyingine tunakuta:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ

**"Hakika Mwenyezi Mungu hadhulumu (hata uzani) wa chembe." (Sura Nisaa: 40).**

Na kuhusu hisabu na adhabu katika Akhera anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۖ

**"Na tutaweka mizani ya uadilifu siku ya Kiyama. Basi nafsi yoyote haitodhulumiwa kitu." (Sura Anbiyai: 47).**

Ni wajibu kuangalia kwamba kipimo hapa ni kwa ajili ya kupima wema na ubaya, na sio kama vipimo vilivyopo katika ulimwengu huu.

## 4. Kulingania uadilifu:

Tumeshasema hakika sifa za mwanadamu ni wajibu ziwe zinaakisi sifa za Mwenyezi Mungu Mtukfu, ambazo zinaangaza katika jamii ya kibinadamu. Na kwa msingi huu Qur'ani Tukufu inatilia mkazo uadilifu wa Mwenyezi Mungu kwa kiasi ambacho inatia mkazo katika jamii ya kibinadamu, na kwa kila mmoja katika binadamu, Qur'ani Tukufu inaelezea dhulma kuwa ni sababu ya kupotea na kuanguka jamii na kwamba hatima ya madhalimu ni yenye machungu sana.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 52 1/13/2017 3:33:21 PM

Qur'ani Tukufu inataja uhalisia wa hatima ya watu wa zamani na inatutaka sisi tuone athari za dhulma na ufisadi namna gani iliwasababishia adhabu ya Mwenyezi Mungu na wakamalizika, na tuogope hatima yetu isije ikawa kwa matokeo ya dhulma kama hatima ya watu waliotangulia.

Na Qur'ani Tukufu inasema kama mwanzo wa msingi:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ ۚ

**"Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na ihisani na kuwapa jamaa na anakataza uchafu, uovu na ubaya." (Sura Nahli; 16:90).**

Na kitu ambacho inapasa kuzinduka ni kwamba, kama ambavyo dhulma ni kitendo kibaya, hakika kukubali dhulma na kuinyenyekea katika upande wa mtazamo wa Uislamu na Qur'ani Tukufu ni kosa. Imekuja katika Qur'ani Tukufu Aya ya 279 katika Sura al-Baqarah: "Msidhulumu wala msidhulumiwe.." Hakika kujisalimisha kwa madhalimu inapelekea kushajiisha dhulma, kuisambaza na kumsaidia dhalimu.

# TAFAKARI NA UJIBU:

1. Je akili zetu zinaweza kujua uzuri na ubaya kwa namna inayojitegemea mbali na maelekezo ya Sharia?
2. Dhulma inatokana na mambo gani? Na ni ipi dalili ya kiakili juu ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu?
3. Qur'ani Tukufu inasema nini kuhusu uadilifu wa Mwenyezi Mungu na kupinga dhulma Kwake (swt)?

**4.** Nini wajibu wa mwanadamu mkabala na dhulma?

**5.** Je, kujisalimisha katika dhulma na kuikubali ni kosa?

# SOMO LA TATU:

## Falsafa ya majaga na shari

Tangu zamani na hadi wakati wetu huu, baadhi ya wajinga wamekosoa uadilifu wa Mwenyezi Mungu na wakauliza baadhi ya mas'ala ambayo katika itikadi yao hayaendani na uadilifu wa Mwenyezi Mungu, bali kwa rai yao wakati mwingine yanaonyesha juu ya kupinga uadilifu wake, jambo ambalo linaonyesha moja ya kukanusha uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Miongoni mwa mas'ala haya ni matukio yenye kusikitisha kama vile vimbunga, matetemeko, na masaibu mengine. Vilevile ikhitilafu baina ya watu, shari na majanga ambayo yanaipata mimea na viumbe vingine na maradhi ambayo yanamsibu mwanadamu.

Hakika utafiti huu wakati mwingine hutolewa na baadhi ya watu wa mada ndani ya utafiti unaohusiana na kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na wakati mwingine ni katika utafiti unaohusu uadilifu wa Mwenyezi Mungu, na sisi tutalizungumzia jambo hili. Na ili tujue ni kwa wigo na kwa uchambuzi makini, kutosihi fikra hizo, ni wajibu tufanye utafiti wa ufafanuzi katika nyanja hii na tudurusu kwa makini mambo yafuatayo:

### 1. Hukumu ya uwiano na utambuzi finyu:

Hakika sisi mara nyingi katika kutoa kwetu hukumu na kubainisha uhalisia tunategemea mafungamano ya vitu hivyo. Na sisi, kwa mfano tunasema hakika kitu fulani kiko karibu au mbali na sisi, yaani kuhusiana na sisi. Au fulani ni mtu mwenye nguvu au dhaifu, hii kinaweze-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 54 1/13/2017 3:33:21 PM

kana ulinganisho na hali yetu ya kiroho au kimwili. Na vilevile hakika hukumu ya watu kuhusiana na kheri na shari, majanga na balaa, aghlabu inakuwa katika maana hii. Mfano inapoteremka mvua katika sehemu fulani, hakika sio muhimu kwetu kiwango cha athari yake na namna ya mvua hii, hakika sisi hatuangalii isipokuwa mazingira ya maisha yetu na mashamba yetu au kwa sura pana zaidi tunaangalia mji wetu, ikiwa mvua ni ya mafanikio tunasema ni neema ya Mwenyezi Mungu, Na ikiwa ina madhara sisi tunaizingatia kuwa ni balaa.

Wanapovunja nyumba ya zamani ili kujenga jengo jipya, na ikatokea tumepitia sehemu hiyo na likatupata vumbi na udongo, hakika tunasema: Ni tukio baya lilioje, pamoja na kwamba hospitali itakayojengwa hapo watafaidika nayo watu wengine.

Kwa hukumu ya haraka na ya kawaida tunazingatia kung'atwa na nyoka ni shari. Walighafilika kwamba kung'atwa na nyoka na sumu yake ni njia ya kujilinda ya mnyama huyu, kama ambavyo dawa zinazotengenezwa zenye kuponya kutokana na sumu hii zinaponya na kunusuru maisha ya maelfu ya watu.

Na hivyo tukitaka tusitumbukie katika kosa, ni wajibu wetu tuzinduke katika utambuzi wetu finyu na tusitegemee katika hukumu zetu katika mafungamano ya vitu na sisi, bali tuchukue sehemu zote kwa mtazamo na tutoe hukumu yetu baada ya hapo.

Uhalisia ni kwamba matukio ya kiulimwengu yanafanana na mnyororo, kila moja lina uhusiano na jingine: Kimbunga ambacho kinavuma leo katika mji wetu, na mvua ambayo inasababisha mafuriko ni sehemu ya mnyororo mrefu unaounganisha matukio na mengine yaliyotokea katika sehemu wakati uliopita, au ambayo yatatokea katika mustakabali. Na matokeo ni kwamba ni makosa kuweka kidole katika sehemu ndogo na kutoa hukumu juu yake, kwa sababu tu iko mbali na akili na mantiki.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 55 1/13/2017 3:33:22 PM

Hakika kitu ambacho kinawezekana kukikataa ni kukizingatia kiumbe kuwa ni kiovu kabisa, lakini ikiwa kitu kina sehemu ya shari na sehemu ya kheri, na sehemu ya kheri ni zaidi kuliko sehemu ya shari basi hakuna kizuizi. Hakika upasuaji wa jeraha ni mchungu kwa upande mmoja lakini pande zake zingine zina faida, hivyo hakika kheri ni kitu cha uwiano.

Na kwa ajili ya kufafanua zaidi tuchukue tetemeko. Ni kweli linasababisha uharibifu katika sehemu fulani, lakini mafungamano yake na mlolongo katika mas'ala mengine linatufanya tubadilishe rai zetu. Je, tetemeko ni matokeo ya joto na mvuke unaotoka chini ya ardhi, au ni matokeo ya nguvu ya mvutano wa mwezi na gamba la ardhi iliyoganda na hivyo huvunjika kutokana na nguvu hii ya mvutano, au ni kitendo cha hivi viwili? Maulamaa wana nadharia mbalimbali, lakini pamoja na hayo ni lazima kuwepo na athari itokanayo na sababu zote hizi mbili, yaani sisi ni wajibu tujue kwamba athari ya joto la ardhi katika kuleta vyanzo vya mafuta, nayo ni mada muhimu inayozalisha nishati katika zama zetu, na vilevile uzalishaji wa mkaa wa mawe na mfano wa hayo. Hivyo kheri ni kitu cha uwiano.

Na vilevile kujaa na kupwa inatokea kwa matokeo ya nguvu ya mvutano wa mwezi na bahari, na wigo wa athari ya hilo katika kubakisha maji ya bahari hai, na vilevile vinavyoishi humo, kwa kuongezea kunywesheleza ufukwe kame kiasi kwamba yanamiminwa maji matamu katika bahari. Na hili pia linaonyesha kwamba kheri ni jambo la uwiano.

Na kuanzia hapa tunafahamu kwamba hukumu zetu ni za uwiano, na utambuzi wetu finyu ndio unaotufanya tufikirie kwamba muonekano wa dunia ni kama nukta nyeusi, na sisi kila tunapofikiria mafungamano baina ya matukio na mwonekano tunaona umuhimu wa maudhui na tunayajua zaidi. Na Qur'ani Tukufu inasema: "Na



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 56 1/13/2017 3:33:22 PM

hamkupewa elimu isipokuwa kidogo tu" (Sura Israi: 85). Na hivyo hakika pamoja na elimu hii chache ni wajibu tusifanye haraka katika kutoa hukumu.

## 2. Majanga yanayosikitisha na tahadhari:

Sote tumeshaona kwamba baadhi ya watu zinapowakunjukia neema wanapatwa na ghururi na wanasahau. Katika hali hii, hughafilika na mas'ala mengi muhimu ya kibinadamu na ya wajibu ambayo yako juu yao. Kama ambavyo sisi tumeshaona maisha yanapokuwa katika hali ya utulivu na raha kikamilifu, hakika hali ya usingizi ghafla humpata mwanadamu, na kama itaendelea hali hii hakika itasababisha uovu wa kibinadamu.

Hapana shaka kwamba sehemu ya majanga yanayosikitisha katika maisha hakika inatokea kumaliza hali hiyo ya ghururi, kwa ajili ya kuondoa usingizi huo na kughafilika huko. Na kwa uhakika nyinyi mmewahi kusikia kwamba madereva wanalalamikia njia isiyokuwa na mabonde na miinuko, na wanaelezea njia hizi kwamba ni hatari, kwa sababu inawapelekea kwenye usingizi kwa ajili ya mafungamano yao, hapa ndio chimbuko la hatari. Na imeshaonekana katika baadhi ya nchi kwamba viongozi wanategemea kuleta mabonde na miinuko na miteremko kwa ajili ya kuondoa mfano wa hatari hiyo. Hakika hatima ya maisha ni sawa kabisa na mfano huo, kama maisha yangeepukana na mabonde hayo na mitikisiko na majanga yasiyotarajiwa, hakika kumsahau Mwenyezi Mungu na hatima kutamwenea mwanadamu na kumfanya aghafilike kuhusu wajibu wake aliopewa. Hakika sisi hatusemi ni juu ya mwanadamu atengeneze matatizo katika nafsi yake na majanga yenye kusikitisha, kwa sababu majanga haya yanatokea katika maisha ya mwanadamu, lakini sisi tunasema hakika falsafa ya baadhi ya majanga haya ni kusimama mbele ya ghururi na kughafilika, ambapo yote mawili ni katika maadui wa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 57 1/13/2017 3:33:22 PM

mafanikio ya mwanadamu. Tunakariri na tunasema hakika falsafa hii inaafikiana na baadhi ya majanga haya yenye kusikitisha na sio yote, kwa sababu kunapatikana falsafa nyingine ambayo tutaizungumzia kwa idhini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu baadaye.

Kinasema Kitabu chetu kitukufu cha mbinguni katika nyanja hii: "Basi tukawachukua kwa dhiki na neema huenda watanyenyekea." (Sura al-An'am: 42).

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Ni nani ambao wametoa mas'ala ya maafa na shari katika utafiti wa kiitikadi?

**2.** Toa baadhi ya mifano kuhusu maafa na shari, je, uliwahi kukabiliwa na baadhi yake katika maisha yako?

**3.** Nini makusudio ya hukumu ya uwiano na ya jumla, na shari ya jumla na kheri ya uwiano?

**4.** Je, vimbunga na matetemeko ni kweli yanadhuru?

**5.** Ni athari ipi ya kinafsi ni nzuri katika majanga yenye kusikitisha katika maisha ya mwanadamu?

## SOMO LA NNE:

### Falsafa ya majanga yenye kusikitisha katika maisha

Tumesema hakika kundi la wenye shaka wanatoa hoja katika mas'ala ya majanga yenye kusikitisha na maafa, matatizo na kufeli, ambayo yanasibu maisha ya mwanadamu, kwa kupinga kuwepo uadilifu wa Mwenyezi Mungu, wakati mwingine kupinga msingi wa kuwepo Mwenyezi Mungu Mtukufu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 58 1/13/2017 3:33:22 PM

Katika utafiti uliotangulia tumefanya uchambuzi na utafiti wa baadhi ya majanga haya na tukajua falsafa mbili miongoni mwayo, na hivi sasa tunaendelea na utafiti huu.

## 1. Mwanadamu analeleka katika hali ya kupambana na matatizo:

Tunakariri kwa mara nyingine kwamba sisi ni wajibu tusitengeneze matatizo katika nafsi zetu, lakini pamoja na hayo, mara nyingi inatokea kwamba matukio yenye kusikitisha na magumu ndio ambayo yanaimarisha matakwa yetu na uwezo wetu na kuwa kama chuma imara. Sisi tunakuwa imara kama chuma katika ugumu wa matatizo haya.

Hakika vita ni kitu kibaya, lakini wakati mwingine inatokea vita ngumu na ya muda mrefu inakuza vipaji vya wananchi, na kubadilisha mparaganyiko na kuwa ni umoja, na kutokuendelea kuwa uvumbuzi na maendeleo ya haraka. Hakika muamala wa watu wote na jamii haulingani mbele ya matatukio machungu katika maisha. Ama watu ambao wana mapambano hakika wao wanadhihirisha muamala wao mbele ya matukio na wanafanya harakati, kisha wanaanza kurekebisha nukta za udhaifu na kushindwa kwao. Lakini kwa kuangalia kuwa wengi miongoni mwa watu wanahukumu hukumu ya kijuu juu katika mfano wa nyakati hizi, hakika hawa hawaoni isipokuwa masaibu na machungu na wanaghafilika na matokeo mazuri yenye kujenga.

Hakika sisi hatudai kuwa matukio yote machungu katika maisha yana mfano wa athari hizi kwa mwanadamu, lakini kwa uchache sehemu miongoni mwayo ni hivyo. Hakika nyinyi mnaposoma sira ya waerevu wa ulimwengu, hakika mtaona kwamba wao takriban wamekulia katika ugumu wa matatizo na masaibu makubwa. Na ni nadra kukuta mtu mwenye mafanikio na mwerevu anafikia upevu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 59 1/13/2017 3:33:22 PM

wake katika daraja la juu. Viongozi wa kijeshi wakubwa ni wale ambao wamepigana vita vigumu na vya muda mrefu katika medani za mapigano. Akili kubwa za kiuchumi ni zile ambazo zimeishi katika matatizo ya kiuchumi katika masoko, na wanasiasa wenye nguvu na wakubwa ni wale ambao walikabiliana na matatizo magumu ya kisiasa.

Muhtasari: Hakika matatizo ndio ambayo yanamlea mwanadamu katika mikono yake. Tunasoma katika Qur'ani tukufu:

فَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا

**"Huenda mnaweza kuchukia kitu na Mwenyezi Mungu akajaalia humo kheri nyingi." (Sura Nisaa: 19).**

## 2. Matatizo yanasababisha kurejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Tumesoma katika utafiti uliopita kwamba kila sehemu katika uwepo wetu ina lengo. Jicho lina lengo, sikio lina lengo, na pia ubongo, moyo, mishipa, hata mistari katika vidole vyetu pia ina falsafa.

Hivyo, vipi inawezekana uwepo wetu usiwe na lengo na falsafa. Na vilevile tumesoma katika utafiti uliopita kwamba lengo hili halivuki kitu isipokuwa ni ukamilifu wa mwanadamu katika hali zote. Na katika ambayo hakuna shaka humo ni kwamba kufikia katika ukamilifu huu ni lazima kuwe na ratiba ya kielimu na kimalezi ya kina inayohusu uwepo wote wa mwanadamu, kwa ajili hii Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuongezea kwamba Yeye amempa mwanadamu maumbile ya tauhidi dhahiri, alituma Manabii watukufu na vitabu vya mbinguni ili wabebe katika mabega yao uongozi wa huyu mwanadamu katika njia hii. Kisha kukamilisha lengo hili ni lazima wakati mwingine kuweka na kufichua makosa yake na madhambi



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 60 1/13/2017 3:33:22 PM

yake mbele yake, na kukabiliana na machungu katika maisha kwa kukhalifu kwake utii na amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu, ili ajue hatima mbaya ya vitendo vyake na arejee kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hapa inakuwa sehemu ya balaa na matukio machungu katika uhalisia, ni rehema na neema ya Mwenyezi Mungu, imekuja katika Qur'ani Tukufu:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُمْ بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

**"Ufisadi umedhiri bara na baharini kwa sababu ya iliyoyafanya mikono ya watu, ili Mwenyezi Mungu awaonjeshe baadhi ya waliyoyatenda huenda wakarejea." (Sura Rum: 41).**

Kwa kujengea juu ya hayo tulioyataja, hakika ni mbali na mantiki na akili kuzingatia matukio machungu kuwa ni kielelezo cha shari, na kwamba ni balaa na ni kukhalifu uadilifu wa Mwenyezi Mungu, hakika kila tunapozama katika mas'ala haya hakika sisi tunafikia kwenye falsafa nyingi.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Nini lengo la kuumbwa kwetu? Na ni kwa njia gani tunaweza kufikia lengo hilo?
2. Namna gani mwanadamu anakuwa imara na mpambanaji kupitia njia ya matatizo?
3. Je, umeona au umesoma katika historia kwamba watu wamekulia katika matatizo magumu makubwa na wamefikia katika vituo muhimu? Fafanua sira ya watu hawa.
4. Qur'ani Tukufu inasemaje kuhusu muamala mkabala wa madhambi yetu?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 61 1/13/2017 3:33:22 PM

5. Ni aina gani ya watu wanapata matokeo mazuri kutokana na matukio machungu? Na aina gani wanapata matokeo mabaya?

# SOMO LA TANO:

**Falsafa ya maafa na shari kwa mara nyingine:**

Kwa kuwa mas'ala ya maafa, shari na majanga machungu na magumu kiasi fulani ni magumu kwa wasomaji wa utafiti wa kumjua Mwenyezi Mungu na tauhidi, hakika sisi tunalazimika kurudia utafiti na uchambuzi kuhusu mas'ala haya na falsafa ya shari na matatizo.

**1. Matatizo na majanga yanajenga ari katika maisha**

Huenda ni vigumu kwa baadhi kufahamu kwamba neema kama ikiendelea na maisha yakaendelea katika namna moja yatakosa thamani yake na umuhimu wake. Imethibiti leo kwamba kama mwili ungewekwa katikati ya chumba na ukamulikwa na mwanga wenye nguvu kila upande kwa namna yenye uwiano, na chumba kikawa ni duara kikamilifu, katika hali hii huwezi kuuona ule mwili, kwa sababu kivuli kinapoonekana pembezoni mwa mwanga hakika hudhihirisha sehemu za mwili kuziainisha, katika hali hii unaweza kuona mwili.

Na vivyo hivyo hakika huwezi kuhisi thamani ya neema bila ya hali mbalimbali za matatizo. Na kama kusingekuwa na maradhi ya muda mrefu hakika haiwezekani kuhisi thamani ya afya njema. Na baada ya mkesha wa usiku, maradhi na homa kali, na kisha kukatika kwa homa asubuhi, ndipo mwanadamu wakati huo anahisi utamu wa afya. Na kila anapokumbuka machungu ya usiku ule anajua wakati huo thamani ya afya ambayo ananeemeka nayo.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 62 1/13/2017 3:33:22 PM

Kwa hakika maisha ni mpangilio, hata kwa ambaye anaishi maisha ya utajiri, yenye kuchosha, kutaabisha na kufisha. Na mara nyingi inashuhudiwa watu wanaoishi maisha ya utajiri yenye kuepukana na kila aina za fujo au machungu, wanakuwa na mashaka ya maisha na hivyo hujinyonga.

Hakika nyinyi hamuwezi kupata fundi mahiri anayejenga kuta za ukumbi mkubwa mfano wa jela, akawa anajenga kwa namna ya ulingano bali atajenga baadhi ya kona na mteremko, au kwa maneno mazuri zaidi analeta baadhi ya mtindo.

Kwa nini mazingira katika ulimwengu ni mazuri kiasi hiki?

Kwa nini ni mazuri na ya kuvutia, mandhari ya pori katika vilele vya milima, na mandhari ya mito nayo inatiririka kwa namna ya mteremko baina ya miti midogo na mikubwa?

Hakika ni dalili wazi ya kutokuwa kwake kwa namna moja.

Hakika mpangilio wa nuru na giza na mfuatano wa usiku na mchana, na kuna Aya nyingi katika hayo ambazo ziko katika Qur'ani Tukufu, zina athari muhimu. Ni kumaliza uchovu katika maisha ya mwanadamu. Kama jua lingekuwa linaangaza kwa namna moja tu toka mbinguni kuelelea ardhini bila ya mabadilko yoyote na bila ya kuingia giza mahala pa mwanga wa dhahabu wa jua, tukiachilia mbali matatizo mengine, hakika mwanadamu ndani ya muda mfupi atasikia uchovu na kuchoka.

Na juu ya yote hayo ni wajibu tukubali kwamba sehemu ya matatizo na majanga machungu katika maisha ina falsafa, nayo ni kumpa mwanadamu maisha ya umri uliobakia na kuyafanya matamu tunayoweza kuyavumilia, kama ambavyo inabainisha thamani ya neema na kutoa fursa kwa mwanadamu ili anufaike na neema alizopewa katika upeo wa juu zaidi.

## 2. Matatizo tunayoyatenegeneza wenyewe:

Nukta nyingine ambayo inapasa tuashirie kwayo mwisho wa utafiti huu ni kwamba watu wengi mara nyingi wanakosea katika sababu na visababishi vya majanga yenye kusikitisha na masaibu, na wanaziweka dhulma ambazo zinafanywa na madhalimu katika jukumu la muumba mtukufu, kama ambavyo wanazingatia fujo ya vitendo vya mwanadamu kuwa ni katika kazi za utaratibu wa uumbaji. Kwa mfano wanaulizana: Kwa nini matetemeko yanasababisha hasara ndogo katika miji wakati hasara na muhanga inakuwa kubwa katika vijiji na sehemu za mashambani, ambako wanafukiwa chini ya tani za vifusi? Ni uadilifu gani huu? Ikiwa imepangwa kutokea balaa, kwa nini isigawanywe kwa namna ya usawa katika sehemu na watu, kwa nini wanapatwa wanyonge peke yao majanga machungu? Na kwa nini inaondoka idadi kubwa ya wanyonge wahanga wa maradhi ambayo yanawapata wote. Lakini halifungamani lolote kati ya maswali haya na uumbaji na uadilifu wa Mwenyezi Mungu, bali ni matokeo ya dhulma na kunyonyana kwa binadamu wao kwa wao.

Kama wanakijiji wasingepatwa na dhulma ya wakazi wa mijini na kuwa ni wenye kunyimwa, basi wasingekuwa mafakiri, na kama wao wangejenga nyumba imara mfano wa nyumba za mijini wasingetoa wahanga wengi. Lakini nyumba zao zinapokuwa zimejengwa kwa udongo na baadhi ya mawe na miti na mara nyingi zinakosa tofali na sementi, hivyo mtikisiko wa nguvu au mtikisiko mdogo wa ardhi unavunja kila kitu, na wala haiwezekani kutarajia kitu bora zaidi katika hayo. Ni uhusiano upi wa mas'ala haya na kazi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu?

Hakika sisi ni wajibu tusirudie kauli ya mshairi "Hakika umeshawapa baadhi yao neema elfu moja, wakati ambapo umewaweka wengine katika udhalili, umempa mmoja wao kasiri, na mwingine kibanda dhalili!"



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 64 1/13/2017 3:33:22 PM

Hakika ukosoaji ni wajibu tuuelekeze kwenye hali ya mkanganyiko na utaratibu wa kimakosa wa jamii yenyewe. Ni wajibu kusimama na kumaliza dhulma hii ya kijamii, na kupiga vita ukosefu na ufakiri, na kuwapa wanyonge haki zao ili kusijitokeze mfano wa muonekano huu. Kama tabaka zote zinapata chakula cha kutosha na uangalizi wa kiafya wangepata kinga mbele ya maradhi mengi.

Lakini tunashuhudia mandhari mengi yanaonyesha juu ya hali ya makosa katika utaratibu wa kijamii, ambapo tunakuta mtu ni tajiri sana kiasi kwamba mbwa wake na paka wake wana matabibu, na uangalizi wa kitabibu, na mtu mwingine hamiliki hata wasila mdogo wa kiafya kwa ajili ya malezi ya mtoto wake. Na sisi badala ya kujaalia mapungufu katika kitendo cha Mwenyezi Mungu, ni wajibu tuzihesabu nafsi zetu katika hilo. Ni wajibu tumwambie dhalimu, usidhulumu na tumwambie mwenye kudhulumiwa usikubali dhulma.

Na ni wajibu twende mbio ili watu wote waneemeke kwa uwiano katika huduma za afya na uangalizi wa kitabibu, chakula na makazi, utamaduni, malezi na mafunzo.

Hitimisho hakika sisi ni wajibu tusijalie makosa yetu juu ya majukumu ya utaratibu wa muumbaji. Yule anayesema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ametulazimisha maisha kama haya, ni lini Mungu aliusia utaratibu kama huu? Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuumba huru kwa sababu uhuru ni alama ya ukamilifu na utukufu, lakini sisi ndio ambao tunawadhulumu wengine kwa matokeo ya fujo hili la kijamii. Na kwa masikitiko, hakika wengi kati ya watu wametumbukia katika kosa hadi mifano ya hilo tunaikuta katika mashairi ya washairi. Imekuja katika Qur'ani Tukufu: "Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu chochote lakini wao wanajidhulumu wenyewe."



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 65 1/13/2017 3:33:22 PM

Na hivyo tunafika katika mwisho wa utafiti wa falsafa ya majanga na shari. Pamoja na kwamba mazungumzo ni marefu katika utafiti huu, lakini kwa maudhui haya mafupi na ya muhtasari yanatosha yale ambayo tumeyaleta katika mlango huu.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Kwa nini tumeendeleza utafiti wa falsafa ya majanga na shari katika masomo matatu?

**2.** Nini athari mbaya ya uchovu wa maisha katika muundo mmoja? Je, umemuona mtu anateseka katika maisha yake yenye raha?

**3.** Unajua nini katika falsafa ya utaratibu wa nuru na giza katika ulimwengu wa viumbe?

**4.** Je, masaibu yote ya jamii yanaletwa na utaratibu wa maumbile au sisi tuna mchango na fungu katika hayo?

**5.** Je, kuna njia ya kuondoa masaibu ya kijamii? Nini wajibu wetu mbele ya wanyonge?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 66 1/13/2017 3:33:22 PM

# SOMO LA SITA:

## Mas'ala ya jaala[6] na hiyari

Miongoni mwa mas'ala ambayo yako karibu na mas'ala ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu ni mas'ala ya jaala na hiyari. Watu wa jaala wanaamini kwamba mwanadamu hamiliki hiyari yoyote katika vitendo vyake, harakati zake na maneno yake na kwamba harakati za viungo vyake zinafanana na harakati za kulazimishwa za vifaa vya mashine.

Na swali hili linajitokeza lenyewe: Namna gani inawezekana kuafikiana itikadi hii na uadilifu wa Mwenyeezi Mungu? Huenda kwa sababu hii tunapata kwamaba Ashairah, nao ni wale ambao tumewataja mwanzo kwamba wanapinga uzuri na ubaya wa akili, wamekubali jaala na wamepinga uadilifu, kwa sababu kukubali jaala kutayafanya mas'ala ya uadilifu yasiwe na maana. Na kwa ajili ya ufafanuzi juu ya utafiti huu sisi tunalazimika kusoma maudhui mengi kwa umakini:

## 1. Chanzo cha itikadi ya jaala:

Kila mwanadamu anahisi ndani mwake kwamba yeye yuko huru katika yale anayoazimia, mfano mtu fulani anataka kumsaidia rafiki yake au laa. Au yeye ana kiu na mbele yake kuna maji, yuko huru kunywa au kutokunywa. Rafiki yake akifanya kitendo dhidi yake, yuko huru kumsamehe au kutomsamehe. Au kila mtu anaweza kutengeneza tofauti baina ya mkono unaotetemeka kutokana na uzee au ugonjwa, na baina ya mkono unaotikisika kwa matakwa ya mwenye mkono.

[6] Yaani mwanadamu hana hiyari na uamuzi wake mwenyewe katika kutenda au kutokutenda jambo. Kwa mfano mtu anaposimama na kuchukua silaha na kwenda kupora mali ya mtu, kwa mtazamo huu huwa si kwa uamzi wake na hiyari yake bali ni kwa shinikizo la moja kwa moja toka kwa Muumba asiloweza kuliepuka!!! - **MHARIRI**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 67 1/13/2017 3:33:22 PM

Pamoja na kwamba mas'ala ya uhuru ni matakwa ya hisia ya wanadamu wote, kwa nini basi baadhi ya watu wanaelekea kwenye jaala? Hakika kuna dalili nyingi mbalimbali, zilizo muhimu zaidi ni kwamba mwanadamu anaona mazingira yanaathiri watu, na malezi ni sababu nyingine, kama ambavyo kujifunza, propaganda, utamaduni wa kijamii vile vile bila ya shaka unaathiri katika fikra na roho ya mwanadamu. Na wakati mwingine inakuwa hali ya uchumi ni msukumo wa kujitokeza harakati kwa mwanadamu, kama ambavyo haiwezekani kupinga sababu ya kurithi katika nyanja hii.

Hakika mkusanyiko wa mambo haya yote yanamfanya mwanadamu aitakidi kwamba hamiliki matakwa katika nafsi yake, na kwamba sababu za ndani na za nje zenyewe ndio zinatusukuma kuchukua maamuzi na kama sio kuwepo sababu hizi huenda visingetokea kwetu vitendo hivi. Mambo haya tunaweza kuyaita na kuyaelezea kuwa ni jaala ya mazingira, na jaala ya mazingira ya kiuchumi, jaala ya nyakati na uchumi, jaala ya malezi na mafunzo na jaala ya kurithi, na hizi ni miongoni mwa sababu muhimu ambazo zimewafanya wanafalsafa kutilia maanani mas'ala ya jaala.

## 2. Nukta ya kimsingi katika kosa la watu wa jaala:

Ama watu wanaofikiri hayo hakika wao wanaghafilika juu ya nukta muhimu, nayo ni kwamba utafiti sio katika misukumo na sababu pungufu, bali utafiti unahusu sababu kamilifu. Au kwa maneno mengine, hapatikani mwanadamu anayeweza kukana mchango wa mazingira, utamaduni na sababu za kiuchumi katika fikra na vitendo vya mwanadamu. Hakika utafiti ni kwamba sisi pamoja na sababu zote hizi hakika maamuzi ya mwisho yako mikononi mwetu, kwa sababu tunahisi kwa uwazi kwamba katika utaratibu wa kimakosa na wa kitwaghuti kama vile utaratibu wa Shah, pamoja na uwepo wa nyanja nyingi za upotovu, hakika sisi hatukuwa ni wenye kulazimishwa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 68 1/13/2017 3:33:22 PM

katika upotovu, hakika sisi tulikuwa tunaweza katika utaratibu huo na utamaduni huo kutokubali rushwa, na tusiende kwenye kituo cha ufisadi na tusiwe kati ya wasiojali.[7]

Hivyo, ni wajibu kutenganisha sehemu na mchango, na sababu kamilifu. Na kwa hiyo kuna watu wengi ambao wamekulia katika familia tulivu au zenye utamaduni ulioporomoka, au katika familia zenye urithi usiofaa, lakini wao pamoja na yote hayo wamefuata njia nyingine, na wakati mwingine wamepinga hali hiyo au mazingira yale ambayo wamekulia humo. Kama mwanadamu angekuwa ni mtu wa mazingira yao na utamaduni wa zama zao, basi watu wasingefanya mapinduzi yoyote ya kimsingi katika ulimwengu, na wangeshikamana na mazingira yao, na asingesimama yeyote kujenga mazingira mapya na jamii mpya.

Mambo yote hayo yanaonyesha kwamba sababu zilizotajwa si kila kitu, bali zinaandaa mazingira tu, ama maamuzi ya kimsingi hakika mwanadamu anayatengeneza kwa matakwa yake na azima yake. Hii inafanana kabisa na sisi tunavyoamua katika siku ya kiangazi cha joto kali, kufunga kwa kuitikia amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hakika sisi tunatii pamoja na kwamba kila chembe katika maisha yetu inahitaji maji, lakini sisi tunafumbia macho juu ya hayo kwa kumtii Mwenyezi Mungu Mtukfu, wakati ambapo inawezekana kupatikana mtu mwingine anayesikiliza amri hizi lakini hafungi. Matokeo yake ni kwamba nyuma ya misukumo yote kunapatikana

[7] Kuna mifano mingi katika hilo, mara ngapi tunashuhudia wavulana wawili wa mzazi mmoja, wa familia moja na wa kaya moja wanaoshirikiana mazingira katika kila kitu, lakini mmoja hatimaye anakuwa jambazi mkubwa kwa kisingizio cha ufakiri na hali mbaya ya maisha mathalan. Lakini mwingine anabakia kuwa raia mwema, japo ni fakiri kama nduguye. Mara ngapi tumeshuhdia wasichana wawili wa mazingira sawa yanayofanana, mmoja anajiingiza katika ukahaba kwa kigezo cha hali ngumu ya maisha, wakati huo huo mwenzake anaendelea kuwa raia mwema licha ya hali yake ngumu ya maisha. Hii ni kwa sababu mazingira si kila kitu katika kuamua utendaji wa mtu, bali hiyari na maamuzi ya nini mtu atende ni ya kwake mwenyewe.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 69 1/13/2017 3:33:22 PM

sababu ya maamuzi, nayo ni matakwa na azima ya mwanadamu mwenyewe.

### 3. Sababu za kijamii na kisiasa katika nadharia ya jaala:

Hakika mas'ala ya jaala na hiyari yametumiwa vibaya ndani ya historia, kiasi kwamba mlolongo wa sababu za pembezoni zilikuwa ni zenye athari katika itikadi ya jaala na kupinga uhuru wa matakwa ya mwanadamu kwa sura ya daima, miongoni mwayo ni:

**Sababu za kisiasa:**

Wanasiasa wengi wenye kuamini jaala, ili kuendelea katika utawala wao wa kidikteta na kuzima mwenge wa mapinduzi kwa wanyonge, walikuwa wanaeneza fikra ya kwamba sisi hatuko huru na hatuna hiari katika vitendo vyetu, na kwamba kadari na jaala ya historia ndio ambayo inaamua hatima yetu. Ikiwa kuna kundi la watawala na kundi lingine la mateka hiyo ni kwa sababu ya hukumu ya majaaliwa, makadara na jaala ya kihistoria.

Na ni wazi ni kiasi gani fikra hii inaweza kuwapumbaza watu na kusaidia kuendeleza siasa za ukoloni, wakati ambapo katika akili na sharia tunakuta kwamba hatima yetu imetegemezwa kwetu, na kwamba majaaliwa na makadara kwa maana ya jaala hayapo. Majaaliwa na makadara ya Mwenyezi Mungu yanasaidia kulingana na harakati zetu na matakwa yetu na imani yetu na juhudi zetu.

**Sababu za kinafsi:**

Kuna watu wavivu na wanyonge mara nyingi wanafeli katika maisha na wala hawataki abadani kukubali kwamba uvivu wao na udhaifu wao ni sababu ya kufeli kwao, na kwa hiyo ili kuzinasua nafsi zao wanakimbilia kwenye jaala na wanaibebesha dhambi zao. Wa-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 70 1/13/2017 3:33:22 PM

nadai ni hatima ya kulazimishwa ili wapate nyuma ya hayo utulivu wa uongo, na wanasema: Tutafanya nini? Tulikuwa na bahati mbaya tangu siku ya kwanza, hakika sisi tunamiliki uwezo na utayari lakini kwa masikitiko bahati haituangukii.[8]

**Sababu za kijamii:**

Baadhi wanataka kuwa huru na kuzama katika matamanio yao na kufanya kosa lolote linaloafikiana na matamanio yao ya kinyama. Na wakati ule ule wanazikinaisha nafsi zao kwamba wao hawana dhambi na hivyo kuidanganya jamii yao. Na vivyo hivyo katika hali hii wanakimbilia kwenye itikadi ya jaala na kusingizia vitendo vyao kwamba wao wanalazimishwa na hawako huru. Lakini sisi tunajua kwamba madai yote ni ya uongo, na kwamba hawa watu wanajua vizuri udhaifu wa imani yao kwa wanayoyadai. Hakika ni manufaa yao na kukimbilia kwao nyuma ya utamu ambao unawazuia kusema ukweli. Na kwa hiyo ili kutwaharisha jamii ni wajibu kupiga vita fikra ya kulazimishwa ambayo ni njia na zana kati ya zana za ukoloni na ukandamizaji, na ni njia kwa ajili ya kisingizio cha uongo na kueneza dhambi katika jamii.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Nini tofauti kati ya jaala na hiyari?
2. Juu ya kitu gani watu wa jaala wanategemea katika hoja zao?

[8] Kila kitu Mungu hakutujaalia. Tuna bahati mbaya. Ni mipango ya Mungu. Kama tunavyoshuhudia uzembe mwingi unaofanywa na baadhi ya madereva barabarani na hatimaye kusababisha ajali vifo, au uzembe mwingine unaofanywa na baadhi ya watendaji wa umma ambao hulisababishia taifa hasara kubwa na kulirudisha nyuma kimaendelea, lakini mwisho wa siku mzigo huo anabebeshwa Mungu kwa kauli kama hizo za ni mipango ya Mungu. Mungu hakupenda. Tuna bahati mbaya – MHARIRI.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 71 1/13/2017 3:33:22 PM

3. Nini msimamo wako mbele ya athari za mazingira, jamii na kurithi?
4. Ni zipi sababu za kisiasa na kinafsi na kijamii ambazo zinasaidia katika kusambaza itikadi ya jaala?
5. Ni namna gani unapaswa kuwa msimamo wetu mbele ya sababu hizi?

## SOMO LA SABA:

**Hoja za wazi juu ya uhuru wa matakwa na hiyari:**

**1. Hakika maumbile ya wanadamu wote yanapinga kulazimishwa:**

Pamoja na kwamba wanafalsafa na maulamaa wa dini wana utafiti na dalili mbalimbali kuhusu mas'ala ya uhuru wa matakwa ya mwanadamu, lakini ili tufupishe njia tunaelekea kwenye hoja zilizo wazi zaidi za wafuasi wa uhuru na matakwa, nayo ni maumbile ya ulimwengu wa mwanadamu.

Kwa ufafanuzi tunasema: Hakika sisi kama tutapinga kila kitu lakini hatuwezi kupinga kwamba bila kujali tofauti zao, sawa awe ni yule anayeamini Mwenyezi Mungu, au anayeamini mada, wa Mashariki au wa Magharibi, wa zamani au wa sasa, tajiri au masikini, katika jamii zote za kibinadamu zenye kuendelea au zisizoendelea, kwa utamaduni wake mbalimbali na bila ya kutofautisha, wote wanaafikiana kwamba kanuni ni wajibu itawale katika jamii ya kibinadamu, na kwamba watu ni wenye kuwajibika mbele ya kanuni, na kwamba mwenye kukhalifu ni wajibu aadhibiwe.

Na hii inamaanisha kwamba kanuni na wajibu wa watu, mkabala wa kanuni, na kumwadhibu mwenye kukhalifu, ni katika mambo



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 72 1/13/2017 3:33:22 PM

ambayo yameafikiwa na jamii zote, wenye akili wote, na ulimwenguni kote, na hawakhalifu hilo isipokuwa wanyama wanaopinga mambo haya matatu. Hakika mas'ala ambayo tumeyaita kuwa ni maumbile ya binadamu ndio dalili iliyo wazi zaidi juu ya uhuru na matakwa ya binadamu, na kwamba ni mwenye hiyari. Hivyo vipi inawezekana kuamini kwamba mwanadamu anakuwa mwenye kutenzwa nguvu mbele ya kanuni? Na anapokhalifu tunampeleka mbele ya mahakama na anakuwa chini ya uchunguzi kisha tunamuuliza: Kwa nini umefanya hivyo? Na baada ya kutiwa hatiani tunampeleka jela au tunamhukumu kunyongwa.

Na hii inafanana kabisa na kuleta mawe ambayo yanaangukia barabarani kutoka mlimani, na tukio hilo linaweza kusababisha mauti kwa baadhi ya watu, tunayapeleka mawe haya mahakani. Ndio, ni sahihi kwamba kuna tofauti baina ya mwanadamu na mawe, lakini sisi tunapotaka kupinga uhuru wa matakwa ya mwanadamu hakika tofauti hii dhahiri haina athari yoyote, bali wote wawili watakuwa na kisingizio, nacho ni kulazimishwa. Mawe yanaanguka juu ya barabara kwa kitendo cha kanuni ya nguvu ya mvuatano, na mwanadamu mwenye kuuwa anafanya kitendo chake chini ya athari ya sababu ya jaala nyingine. Na kwa matokeo hakutakuwa na tofauti yoyote baina ya wawili hawa kulingana na itikadi ya watu wa jaala, ambapo kila mmoja miongoni mwao amefanya kitendo bila ya matakwa kutoka kwake, na hivyo kwa nini anahukumiwa mmoja wao na mwingine anaachwa na mambo yake?

Sisi hivi sasa tuko njia panda; ama tutie makosa dhamira na rai ya watu wote katika ulimwengu, na kuzingatia kanuni zote na mahakama kwamba ni upuuzi hakuna faida yoyote nyuma yake na ni dhuluma, au tupinge itikadi ya jaala na kutenzwa nguvu. Hakuna shaka kwamba chaguo la pili ndilo linalofaa zaidi.

Uzuri ni kwamba hata wale ambao wanaelemea kwenye jaala kifikra na kifalsafa na wanatoa ushahidi kutetea, wanapoingia katika ugomvi wa kimaisha wanakuwa ni katika wafuasi wa msingi wa uhuru wa matakwa. Kwa sababu anapofanya yeyote uadui katika haki zao, au akiwaudhi, wanamuona anastahili adhabu na wanamshitaki mahakamani. Na wanaweza kumpigia kelele mbele ya uso wake, wala hawatatulia kwa maamuzi hadi aadhibiwe!

Kwa vyovyote vile, hakika hii ni dalili hai katika dhamira ya wenye akili wote wa ulimwenguni, kuwa wanaafikiana katika undani wao katika uhuru wa matakwa, na kwamba wao wanaamini hayo na wala hawawezi kuishi hata siku moja bila ya itikadi hii, kama ambavyo hawawezi kutekeleza ratiba yao ya kijamii. Na alishasema mwanafalsafa mkubwa wa Kiislamu, Sheikh Nasir Din Tusi: "Dharura inahukumu katika kutegemeza vitendo vyetu kwetu."[9]

## 2. Mantiki ya jaala inapingana na mantiki ya dini:[10]

Hakika tuliyoyataja hapo nyuma yalikuwa ni kupingana kwa itikadi ya jaala na dhamira au akili. Kwa kufumbia macho wale ambao wanafuata madhehebu na dini au wale wanaopinga madhehebu na dini lakini katika fikra ya kidini kuna dalili nyingine isiyo na shaka juu ya ubatili wa itikadi ya jaala, kwa sababu haiwezekani kuafikiana itikadi ya kidini na itikadi ya jaala. Kama dini zingekubali fikra ya jaala hakika utaratibu wake wote ungetetereka na kuporomoka, ni namna gani tunaweza kutekeleza uadilifu wa Mwenyezi Mungu ambao tumeuelezea katika utafiti uliotangulia? Namna gani Mwenyezi Mungu anaweza kumlazimisha yeyote kufanya kosa? Kisha baada ya hapo amwadhibu? Hii sio mantiki kabisa! Katika upande mwingine hakika kukubali itikadi ya jaala itazifanya thawabu na ad-

[9] Kitabu cha *Tajribatu al-Aqaaid*

[10] (kupingana) ni neno ambalo analitegemea Sh. Naswir Diyn Tusiy, na Ibnu Siinaa - Rejea *Tanbihaati wal-Irshaad* cha Ibnu Siinaa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 74 1/13/2017 3:33:22 PM

habu, pepo na moto visiwe na maana. Kama ambavyo pia itaondoa maana ya uandishi wa amali, maswali, hisabu ya Mwenyezi Mungu, na lawama iliyopokewa katika Aya za Qur'ani kuhusiana wenye madhambi, na kuwasifia wema, hiyo ni kwa sababu inaafikiana na majaaliwa haya kwani mwenye madhambi na mwema hawakuwa na matakwa katika waliyoyafanya.

Kwa kuongezea katika hayo ni kwamba hakika cha kwanza kitakachotukabili katika dini ni: Mas'ala ya taklifu na wajibu, lakini mtu anapokuwa ameondolewa hiari je, kuna maana ya taklifu na majukumu kuhusiana naye?

Je, inawezekana kumwambia mtu ambaye mikono yake inatetemeka: Usifanye hivyo? Au kumtaka mtu anayeteremka katika mteremko mkali asimame ghafla?

Na kwa sababu hii anasema Amirul-Muuminina Ali bin Abutalib عليه السلام kuhusu itikadi ya jaala: "Hayo ni maneno ya ndugu waabudu mizimu na maadui wa Mwingi wa rehema na kundi la shetani."[11]

# TAFAKARI NA UJIBU:

1. Ni ipi dalili ya wazi juu ya ubatili wa itikadi ya jaala?
2. Fafanua rai ya jumla ya ulimwengu kuhusu msingi wa uhuru na hiyari
3. Je, wafuasi wa itikadi ya jaala ndio wenye kulazimishwa kivitendo vilevile?
4. Je, itikadi ya jaala inaafikiana na audilifu wa Mwenyezi Mungu? Na kama si hivyo ni kwa nini?
5. Namna gani uhuru na matakwa (hiari) yanatengeneza nguzo ya kukubali taklifu na wajibu?

---

[11] *Usulul-Kaafiy*, Juz. 1, uk. mlango wa al-Jabri wal-qadar.

# SOMO LA NANE:

**Nini maana ya jambo ni baina ya mambo mawili**

## 1. Kutelekezwa mbele ya jaala:

Hakika mbele ya itikadi ya jaala ambayo inakuwa katika kiwango cha kuchupa mkapa, kuna madhehebu mengine kwa jina la *Tafwidhi* (kutelekezwa), ambayo yanaafikiana na kuchupa mpaka. Hakika ambao wanaitakidi *Tafwidhi* wanaona kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuumba na ameumba kila kitu na ametegemeza kwetu kila kitu, na kwamba yeye hajui chochote kuhusu amali zetu na hivyo kila kinachoingia katika nyanja ya vitendo vyetu tuko huru navyo bila ya kuingiliwa na yeyote.

Hakuna shaka kwamba itikadi hii haiafikiani pamoja na msingi wa tauhidi, kwa sababu tauhidi imetufundisha kwamba ulimwengu wote ni wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, wala hakitoki kitu katika amali yake hata amali zetu, pamoja na kwamba vimeachwa katika hiyari yetu na uhuru wa matakwa yetu, haiwezekani kutoka katika elimu yake, vinginevyo hiyo ingekuwa ni shirki. Kwa maneno mengine hakika sisi haiwezekani kuamini kuwepo kwa waungu wawili, mmoja wao mkubwa ameumba ulimwengu na mwingine mdogo, yaani mwanadamu aliye huru katika amali zake ambazo hata Mwenyezi Mungu haingilii chochote (*audhubillahi*) katika mipaka ya vitendo vyake. Na hii ni shirki kwa sababu inaonyesha juu ya ibada za ushirikiano. Na cha muhimu sasa hivi ni kumzingatia mwanadamu huru na ni mwenye matakwa na hiyari, na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mtawala na mwenye kuchunga vitendo vyake.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 76 1/13/2017 3:33:22 PM

**2. Madhehebu ya kati:**

Hakika nukta makini hapa ni tusifikiri kwamba ni baina ya vyenye kupingana na kukinzana, na nukta hii ni kukubali uadilifu kamili wa Mwenyezi Mungu, na kumzingatia mwanadamu kuwa yu huru na ni mwenye kuulizwa, na kwamba tauhidi ndio yenye kufuatilia kila kitu katika maisha. Na jambo hili ndilo linaloitwa kuwa ni 'jambo baina ya mambo mawili', kwa maana kwamba ukweli upo baina ya itikadi mbili za kuchupa mpaka na kuzembea.

Kwa kuzingatia kwamba maudhui hii ni ngumu kiasi fulani, turuhusuni tulete mfano kwa ajili ya kuifafanua: Jaalieni kuwa nyinyi mnasafiri kwa treni ya umeme na dereva ni wewe, na kuna waya wa umeme wenye nguvu umetandazwa katika njia ya treni. Kipenyo maalum kimeunganishwa na waya na unapita juu yake, na kupitisha umeme hadi kwenye injini ya treni. Umeme ukikatika kwa sekunde hakika treni itasimama mahala pake na wala haitasogea. Hakuna shaka kwamba wewe uko huru kwenda sehemu nyingine yoyote unayotaka na kusimama njiani au kwenda kwa spidi unayotaka, lakini pamoja na uhuru wote huu hakika mtu ambaye anawasha umeme anaweza kukufanya usimame kutembea wakati wowote anaotaka, kwa sababu nguvu zote ambazo unazimiliki zinatoka katika waya. Na funguo zake ziko mkononi mwa yule mtu.

Tukichunguza kwa makini katika mfano huu tutaona kwamba huyu mtu pamoja na kumiliki kwake uhuru, hiyari na jukumu, lakini yuko chini ya nguvu nyingine, na hii haikinzani na nyingine.

Mfano mwingine:

Jaalieni kwamba mtu kutokana na maradhi au ajali, mishipa ya mikono imepooza, na akakosa nguvu ya kutembea, lakini sisi kama tutafunganisha mishipa hiyo kwa nguvu ya umeme wenye nguvu ndogo hakika joto litapenya kwenye mishipa na kuanza kufanya



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 77 1/13/2017 3:33:22 PM

kazi. Hakika mtu huyu akitekeleza kazi kwa mkono huo au akifanya kosa la kupiga mtu au kuchoma kifua cha mtu kwa kisu hakuna shaka kwamba yeye atakuwa na jukumu juu ya kitendo chake kwa sababu anamiliki uwezo na hiyari na ni mwenye kuulizwa juu ya vitendo vyake. Lakini pamoja na hayo hakika mtu anayeupa nguvu ya umeme mkono uliopooza ndio mtawala wa mtu aliyepooza, pamoja na kwamba anamiliki uhuru na hiyari.

Hakika Mwenyezi Mungu Mtukfu ametupa nguvu, uwezo, akili, busara, na uwezo huu unatujia kidogo kidogo, na unapokatika msaada wake na uangalizi wake kwetu punde moja tu, na ukakatika uhusiano wetu naye hakika sisi tutakufa, na sisi tunapoweza kutekeleza kitendo, hakika hiyo ni kwa nguvu ambayo tumepewa, yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaka tuwe huru, na tunufaike na kipawa hiki kikubwa cha Mwenyezi Mungu ili tufupishe njia ya kufikia ukamilifu.

Na hivyo hakika sisi tunamiliki uhuru isipokuwa sisi tuko chini ya mamlaka Yake yenye uwezo na chini ya rehema Yake na hatuwezi kutoka katika mamlaka Yake, na hii inamaanisha wakati huo huo kwamba sisi pamoja na uwezo wetu tunafungamana Naye (swt) na bila ya Yeye sisi si chochote, hii ndio maana ya ‘jambo ni baina ya mambo mawili’ kwa sababu sisi hatujui kiumbe kilicho katika kiwango cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, hadi idhihiri kwetu shirki, na wala waja sio wenye kulazimishwa katika vitendo vyao, hadi dhulma idhihiri kwa Mwenyezi Mungu, tafakari hilo.

Hakika somo hili tunajifunza kutoka katika madrasa ya Maimamu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام walipokuwa wanaulizwa: Je, inapatikana njia nyingine baina ya jaala na kutelekezwa? Wakajibu: Ndio, na ni pana kuliko masafa yaliopo baina ya ardhi na mbingu.[12]

[12] *Usul-Kafiy*, Juz. 1, uk. 121, Mlango wa al-Jabri wal-Qudra wal-amru bainal-amraini.

## 3. Qur'ani Tukufu na mas'ala ya jaala na hiyari:

Qur'ani Tukufu iko wazi katika maudhui haya, na inasisitiza kwa uwazi uhuru wa matakwa ya mwanadamu, na hilo limezungumziwa katika mamia ya Aya Tukufu.

a. Hakika Aya zote zilizoko kwenye kuamrisha na kukataza, taklifu na utaratibu, ni dalili juu ya hiyari na uhuru wa matakwa, kwa sababu mwanadamu kama angekuwa anatenzwa nguvu ingekuwa kuamrisha na kukataza ni jambo lisilo na maana.

b. Hakika aya zote ambazo zinazungumzia kulaumu wakosaji na kuwasifu wema ni dalili ya hiyari kwa sababu lawama na kusifu hazina maana katika kulazimisha.

c. Hakika Aya zote zinazohusiana na Siku ya Kiyama na hisabu katika siku hiyo, kisha malipo na adhabu, pepo na moto, ni dalili juu ya hiyari, kwa sababu hali ya kulazimisha haina maana katika dhana zote hizo, kuanzia kuhisabu na kuwaadhibu wenye madhambi, kwa sababu itakuwa ni dhulma halisi.

d. Hakika Aya zote zinazozungumzia kwamba mwanadamu ni rehani wa vitendo vyake, mfano: "Kila nafsi iko kwenye rehani kwa iliyoyachuma." Sura al-Mudathir: 38. Na "Kila mtu ni rehani wa aliyoyachuma" Sura Tuur: 21. Na mfano wa Aya hizi, zinaonyesha kwa uwazi kwamba mwanadamu anamiliki hiyari.

e. Hakika Aya mfano: "Hakika sisi tumemwongoza njia ama awe ni mwenye kushukuru, na ama awe ni mwenye kukufuru." Sura Dahari: 3. Vilevile ni dalili ya tuliyoyasema.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 79 1/13/2017 3:33:23 PM

**Hitmisho:** Hakika maelezo yaliyopokelewa katika Qur'ani Tukufu yanaonyesha juu ya mas'ala ya jambo ni baina ya mambo mawili, na wakati mwingine baadhi ya wenye kughafilika wanaitakidi kwamba hiyo inaonyesha juu ya kutenzwa nguvu. Mfano Aya hii: "Na wala hamtotaka hadi Mwenyezi Mungu atake." Sura Dahari: 30.

Ni wazi kwamba Aya hii na mfano wake hazitaki kupokonya hiyari ya mwanadamu, bali zinataka kuthibitisha ukweli huu, nao ni kwamba wewe pamoja na kumiliki hiyari ila hakika wewe uko chini ya amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na tumeshafafanua hayo katika masomo yaliyotangulia.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Nini makusudio ya *Taf'widh*? Na ni kasoro ipi iliyopo katika itikadi hiyo?
2. Fafanua kwa ibara iliyo wazi itikadi ya "jambo baina ya mambo mawili" ambayo tumejifunza kutoka kwa Maimamu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام na taja mifano juu ya hilo.
3. Aya za Qur'ani zinasemaje kuhusiana na jaala na hiyari?
4. Tukikubali itikadi ya hiyari vipi kuhusu ufufuo, pepo, moto na hisabu siku ya Kiyama?
5. Je, aya mfano wa "Wala hamtotaka hadi atake Mwenyezi Mungu" ni dalili juu ya jaala?

## SOMO LA TISA:

**Je, uongofu na upotovu uko chini**

**ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu!**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 80 1/13/2017 3:33:23 PM

## 1. Migawanyo ya uongofu na upotovu:

Anakuja kwako msafiri mbele yako, na mkononi mwake kuna anwani na anakuuliza, ili umuonyeshe anayoyataka. Bila shaka mbele yako kuna njia mbili: Kwanza ni kwenda pamoja naye na kufikia katika hatua ya ukamilifu katika amali ya kheri ambayo unaifanya, na msafiri anafikia lengo lake kisha unamuaga. Na mfano wa pili ni kumuonyesha kwa ishara mbalimbali kuhusu anayoyauliza. Kwa kila hali hakika wewe unamuongoza katika lengo lake, lakini kuna tofauti baina ya njia hizi mbili. Ya pili ni kumuonyesha njia wakati ambapo ya kwanza ni kumfikisha mahala husika. Na katika Qur'ani Tukufu na hadithi za Kiislamu hakika uongofu una maana mbili. Wakati mwingine hakika uongofu unabeba maana ya sharia, yaani ni kwamba unatimia kupitia kanuni na maamuzi. Na wakati mwingine unakuwa na maana ya kimaumbile, yaani kupitia vyombo vya uumbaji, kama vile tone la mbegu kuwa mwanadamu kamili, na maana zote hizi mbili zimekuja katika Qur'ani Tukufu na katika riwaya na habari za Maimamu عليهم السلام. Lakini pamoja na kufafanua vigawanyo vya uongofu bado hakika nukta ya mkabala wake ni upotovu. Hebu sasa turejee katika asili ya maudhui.

Tunasoma katika Aya nyingi kwamba uongofu na upotovu ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anaonyesha njia kwa sababu Yeye (swt) ametuma Manabii عليهم السلام na ameteremsha vitabu vya mbinguni ili kumuonyesha mwanadamu njia. Ama kufikia lengo kwa jaala na kutenzwa nguvu hakuafikiani kabisa na msingi wa uhuru wa matakwa ya hiyari, lakini kwa kuangalia kwamba sisi tunahitaji nguvu zote ili kufikia kwenye lengo hakika Mwenyezi Mungu anatutayarishia hayo na kutufanya tushinde yale ambayo tunakwenda mbio kwa ajili yake. Na aina hii ya uongofu ni kutoka upande wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hiyo ni kwa kupitia kuandaa sababu na utangulizi na kuuweka chini ya matumizi ya mwanadamu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 81 1/13/2017 3:33:23 PM

## 2. Swali muhimu:

Sasa swali linajitokeza lenyewe: Hakika Aya nyingi katika Qur'ani zinataja yaliyotajwa katika Aya hii:

فَيُضِلُّ اللَّهُ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**"…..Basi (Mwenyezi Mungu) humpoteza amtakaye na humuongoza amtakaye na Yeye ni Mwenye nguvu Mwenye hekima" (Surat Ibrahim; 14:4).**

Hivyo bila ya kuangalia Aya nyingine ambazo baadhi yake zinazifasiri nyingine, tunakuta baadhi ya watu wanapinga na kuhoji: Namna gani Mwenyezi Mungu anampoteza amtakaye na anamuongoza amtakaye? Kisha nini dhambi yetu katika nyanja hii?

Hakika nukta muhimu ni kwamba Aya za Qur'ani ni wajibu tuzichukue kwa mazingatio kwa msingi wa kwamba baadhi yake zina uhusiano na baadhi, ili tufike kwenye ufahamu halisi. Na sisi hapa tutaeleza Aya nyingine kuhusu uongofu na upotofu ili mziweke pembeni mwa hizo kisha mtafakari wenyewe.

وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ ۚ

**"…..Na Mwenyezi Mungu anawapoteza madhalimu….." (Surat Ibrahim; 14:27).**

كَذَٰلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ مُرْتَابٌ

**"…..Kama hivyo Mwenyezi Mungu humpoteza aliyepita kiasi mwenye shaka." (Sura al-Ghafir; 40:34).**

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا ۚ وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 82 1/13/2017 3:33:23 PM

**"Na wale wanaofanya juhudi kwa ajili yetu, hakika tutawaongoza kwenye njia Zetu….." (Surat al-Ankabut; 29:69).**

Kama ambavyo tunaona hakika maamuzi na matakwa ya Mwenyezi Mungu sio ya bahati mbaya na bila ya hisabu, Yeye (swt) hamuongozi yeyote bila ya hisabu, wala hapokonyi haki ya yeyote bila ya hisabu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameahidi kumuongoza mwenye kujitahidi kwenye njia Yake, na wenye kujitolea kutatua matatizo, na wenye kupiga vita matamanio ya nafsi na wanaopambana vikali na maadui, na kwa hiyo hakika hiki ni kiini cha uadilifu. Ama wale ambao wanaeneza dhulma na ukandamizaji, na wanasambaza wasiwasi katika nyoyo kwa njia ya israfu, shaka na kusitasita, hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapokonya taufiki ya uongofu na kutia dhulma katika nyoyo zao, na anawanyima kufikia kwenye wema. Na hii ndio maana ya 'Mwenyezi Mungu huwapoteza,' na ambayo si kingine isipokuwa ni matokeo ya vitendo vyetu ambavyo vimetegemezwa kwetu, na hiki ndio kiini cha uadilifu.

### 3. Kujua tangu mwanzo sababu ya uasi:

Maudhui ya mwisho katika kutafiti jaala (kulazimisha) na ambayo tunaona ni lazima kuyaeleza ni hoja ambayo wanashikamana nayo watu wa jaala katika elimu, nayo ni elimu ya zamani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, wao wanasema:

Je, Mwenyezi Mungu alikuwa anajua kwamba mtu fulani atafanya kosa la kuua saa fulani au atakunywa vinywaji vya kulevya? Kama utasema "hakuwa anajua" hakika utakuwa umepinga elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ukisema "alikuwa anajua" basi ilikuwa ni wajibu na lazima mtu afanye kitendo hicho, kwani kinyume chake hakika elimu ya Mwenyezi Mungu ingekuwa ni kinyume na ilivyo. Hivyo ili ibakie elimu ya Mwenyezi Mungu imehifadhiwa na



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 83 1/13/2017 3:33:23 PM

inafanya kazi ni lazima wakosaji wafanye makosa yao na waumini watiifu wafanye utiifu wao.

Ama wale ambao wamepanga hoja hizi ili kufunika makosa yao na dhambi zao, kwa hakika wameghafilika juu ya nukta muhimu. Hakika sisi tunasema: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa anajua tangu zamani kwamba sisi tunafanya kwa matakwa yetu na hiyari zetu katika hali ya kutii au ya kufanya dhambi. Na hii inamaanisha kwamba matakwa yetu na hiyari zetu zilikuwa katika elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ikiwa tumelazimishwa hakika elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu itakuwa ni ujahili (tafakari hilo).

Turuhusuni tufafanue maudhui haya kwa swali moja au mawili: Jaalieni kuwa ustadhi au mwalimu anajua kwamba mwanafunzi fulani ni mzembe na atafeli katika mtihani wa mwisho. Hakika elimu hii ya ustadhi ni ya uhakika na ni kwa asilimia mia moja na imejengwa katika msingi wa uzoefu wa miaka mingi. Je, inawezekana mwanafunzi huyu aliyefeli kumshika mwalimu na kumwambia hakika kujua kwako ndio ambako kumenifanya nifeli katika mtihani?

Twende mbali zaidi; hakika chombo kipya kimevumbuliwa kinaweza kutangaza kuhusu matukio ambayo yatatokea baada ya saa kadhaa kwa umakini, na kusema kwamba mtu fulani atafanya kwa matakwa yake katika saa fulani kitendo fulani. Je, maudhui haya yatafanya kitendo hicho ni kumlazimisha mtu mtendaji?

**Hitimisho:** Hakika elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu haimfanyi mtu yeyote kuwa ni mwenye kulazimishwa katika kitendo chochote.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1. Ni zipi aina za uongofu? Fafanua hilo?**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 84 1/13/2017 3:33:23 PM

1. Taja mifano ya Aya za Qur'ani ambazo zinanasibisha uongofu na upotofu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
2. Nini tafsiri ya uongofu na upotofu wa Mwenyezi Mungu?
3. Nini makusudio ya elimu ya zamani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu?
4. Je, elimu ya zamani inapokonya hiyari na jukumu letu? Taja mfano.

# SOMO LA KUMI:

**Uadilifu wa Mwenyezi Mungu na mas'ala ya kukaa milele.**

Sisi tunajua kwamba Qur'ani Tukufu inazungumzia juu ya adhabu ya baadhi ya makafiri na wenye madhambi, na kwamba malipo yao ni adhabu ya milele, imekuja katika Sura Tauba: 68:

وَعَدَ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ هِيَ حَسْبُهُمْ ۚ وَلَعَنَهُمُ اللَّهُ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُقِيمٌ

**"Mwenyezi Mungu amewaahidi wanafiki wa kiume na wanafiki wa kike na makafiri kwamba watakaa katika moto wa Jahanam milele."**

Na imekuja katika Aya ya 72:

وَعَدَ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

**"Na Mwenyezi Mungu amewaahidi waumini wanaume na waumni wanawake pepo inayotiririrka chini yake mito humo watakaa milele."**

Na hapa linakuja akilini swali lifuatalo: Namna gani inawezekana kukubali kwamba mwanadamu umri wake wote ambao hauvuki



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 85 1/13/2017 3:33:23 PM

miaka 80 au miaka 100, na amefanya dhambi katika kipindi hicho tu anabakia mamilioni ya miaka akionja adhambu!?

Hakika maudhui haya kulingana na thawabu sio muhimu, kwa sababu rehema ya Mwenyezi Mungu ni pana sana na kila thawabu zinapozidi rehema ya Mwenyezi Mungu inakuwa ni bora zaidi na pana zaidi. Ama kuhusiana na vitendo viovu namna gani inawezekana kuwa ni adhabu yenye kudumu mbele ya makosa machache? Na namna gani inawezekana kufasiri hayo pamoja na msingi wa uadilifu wa Mwenyezi Mungu? Je, haipaswi kuwa na uwiano baina ya kosa na adhabu?

**Jawabu:**

Ili kufikia kwenye utatuzi wa mwisho katika utafiti huu ni wajibu kuangalia baadhi ya nukta kwa umakini:

**a.** Hakika adhabu na thawabu siku ya Kiyama hazifanani na adhabu na thawabu katika dunia hii. Kwa mfano, hakika mtu anayefanya uadui na wizi atatupwa jela, wakati ambapo adhabu siku ya Kiyama aghlabu itakuwa kwa namna ya athari za vitendo, na umahususi wa vitendo vya mwanadamu mwenyewe. Na kwa maneno yaliyo wazi zaidi, hakika machungu na adhabu ambazo atapata mwandamu katika ulimwengu wa Akhera hizo ni athari na matokeo ya kitendo chake, Qur'ani Tukufu inasema:

فَالْيَوْمَ لَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَلَا تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

**"Leo nafsi haitodhulumiwa chochote wala hamtalipwa isipokuwa mliyokuwa mnayafanya."** [13]

[13] Suratu Yaasin; 36:54



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 86 1/13/2017 3:33:23 PM

Na tunaweza kufahamu kwa mfano mmoja ukweli huu:

Mtu anaelekea kwenye madawa ya kulevya na vinywaji vyenye kulevya, na vyovyote anavyoambiwa kwamba madawa haya ni sumu yanaharibu tumbo lako na moyo wako, na yanaharibu mishipa yako, hakika hasikii, na anazama kwa wiki kadhaa na miezi katika utamu wa ndoto ya madawa haya yenye kuangamiza, na pole pole anapatwa na vidonda kwenye tumbo, na mapigo ya moyo wake yanakwenda mbio na mishipa inaharibika, na vivyo hivyo anabakia ni mgonjwa katika umri wake uliobakia. Na anateseka kwa maumivu ya ugonjwa usiku na mchana. Hapa je, inawezekana kusemwa juu ya mtu huyu: Kwa nini anateseka katika umri uliobakia, kwa sababu ya wiki chache au miezi kadhaa aliyofanya makosa?

Itasemwa haraka kujibu hilo; Hakika ni matokeo ya vitendo vyake? Hakika hata kama angeishi umri mrefu kama Nabii Nuhu عليه السلام na kuishi maelfu ya miaka hakika sisi tungemuona angali akiteseka kwa maradhi. Na tungesema: Hali aliyonayo hakika amejisababishia yeye mwenyewe katika nafsi yake. Adhabu Siku ya Kiyama aghlabu itakuwa katika aina hii, na hivyo haibakii lawama yoyote katika mas'ala ya uadilifu.

**b.** Hakika ni makosa sana kwa baadhi ya watu kudhani kwamba muda wa adhabu ni wajibu uwe kulingana na kiwango cha muda wa kosa, kwa sabau uhusiano baina ya kosa na adhabu sio uhusiano wa muda bali unafungamana na matokeo na namna ya kosa. Kwa mfano mtu anafanya kosa la kuuwa mtu kwa sekunde, na kulingana na kanuni za ulimwengu wa leo, muuwaji anahukumiwa kufungwa jela maisha. Katika hali hii tunaona kwamba muda wa kuuwa hauzidi sekunde, wakati ambapo adhabu inaendelea makumi ya miaka, na mtu hawezi akadhani kwamba hukumu ni ngumu, kwa sababu katika maudhui haya, dakika au saa

au mwezi au mwaka sio muhimu bali ni matokeo na aina ya kosa.

**c.** Hakika kukaa milele katika Jahanam na malipo ya milele na ya kudumu, ni katika aina ya wale ambao wamefunga milango yote ya kufaulu katika nafsi zao, na wakazama katika ufisadi na upotevu kwa kujua na kwa makusudi. Hakika giza limezunguka uwepo wote wa hawa hadi wamekuwa na rangi ya kosa lenyewe na ukafiri wenyewe. Na Qur'ani Tukufu ina msemo mzuri katika nyanja hii:

بَلَىٰ مَنْ كَسَبَ سَيِّئَةً وَأَحَاطَتْ بِهِ خَطِيئَتُهُ فَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

**"Ndio! Wanaochuma ubaya na makosa yao yakawazunguka, hao ndio watu wa motoni, humo watadumu."[14]**

Hakika mfano wa watu hawa wamekata mafungamano na Mwenyezi Mungu Mtukufu kabisa, na wamefunga njia zote za kufaulu na mafanikio katika nafsi zao. Hakika watu hawa wanafanana na ndege aliyevunja bawa lake na akalichoma, na kwa hiyo analazimika kubakia daima chini ya ardhi na ananyimwa kuruka angani.

Angalizo katika nukta tatu zilizotajwa hapo juu linaweka wazi uhalisia huu, nao ni kwamba mas'ala ya adhabu ya milele ambayo inawapata kundi la wanafiki na makafiri, haitoki kabisa katika duara la msingi wa uadilifu, bali hakika ni matokeo ya vitendo vya hao, na kabla ya hapo walifikishiwa matokeo kwa njia ya Manabii na Mitume عليهم السلام, na kwamba itakuwa ni chungu na yenye kuumiza. Na hakuna shaka kama hawa wangekuwa ni watu wajinga, na haikuwafikia daawa ya Manabii na wakafanya vitendo vyao kwa kutokujua, hakika mfano wa adhabu hii kali haitowajumuisha.

[14] Suratul- Baqara; 2:81



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 88 1/13/2017 3:33:23 PM

Na ni lazima tukumbuke kwamba Aya za Qur'ani na hadithi za Kiislamu zinataja kwamba rehema ya Mwenyezi Mungu ni pana kiasi kwamba inawaenea kundi kubwa miongoni mwa wakosaji. Kundi kwa njia ya vitendo vya kheri na kundi kwa njia ya msamaha, na kundi kwa njia ya vitendo vya kheri ndogo. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa utukufu Wake anatoa malipo makubwa kwa vitendo hivi vidogo. Na kundi lingine baada ya kuadhibiwa kwa muda katika Jahanamu na kumaliza hisabu yao katika mtihani wa Mwenyezi Mungu, wanarejea katika rehema ya Mwenyezi Mungu na huruma Yake.

Na linabaki kundi, na kwa matokeo ya uasi wake na uadui wake dhidi ya haki, na kuzama kwake katika dhulma na ufisadi na unafiki zaidi na zaidi, linazungukwa na giza la ukafiri na kutokuwa na imani, hawa wana malipo ya adhabu ya milele.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Namna gani baadhi ya watu wanafikiri uwepo wa kutoafikiana baina ya adhabu ya milele na uadilifu wa Mwenyezi Mungu?
2. Je, adhabu na thawabu katika ulimwengu wa akhera inafanana na adhabu na thawabu katika ulimwengu huu? Ikiwa sio hivyo, ni vipi?
3. Je, uadilifu unapelekea kulingana baina ya muda wa kosa na muda wa malipo?
4. Malipo ya adhabu ya milele ni kwa ajili ya fungu gani la aina ipi ya watu?
5. Ni aina ipi ya watu watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 89 1/13/2017 3:33:23 PM

# 3

# MASOMO KUMI KATIKA UNABII

## SOMO LA KWANZA:

**Haja yetu kwa viongozi wa kiungu:**

**Ufinyu wa elimu yetu:**

Inawezekana baadhi ya watu wakafikiria; Je, ni lazima kutuma na kuleta Manabii kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kuwaongoza watu? Je, haitoshi akili zetu kujua ukweli? Je, elimu iliyovumbuliwa haimsaidii mwanadamu kuvumbua siri na kuweka wazi ukweli? Kisha hakika wanayoweza kuyaleta Manabii kwetu hayatoki nje ya hali mbili; Ama akili zetu zinayajua hayo, au haziyafahamu.

Katika hali ya kwanza, hakika sisi hatuhitaji kuwepo kwa Manabii, na katika hali ya pili hakika sisi hatuwezi kukubali yanayokhalifu akili zetu!! Kwa upande mwingine, je ni sahihi mwanadamu kuweka nafsi yake chini ya usimamizi wa mtu mwingine na kukubali maneno yake bila ya kuuliza na kujibiwa? Je, Nabii si mtu binadamu kama sisi? Hivyo namna gani tunaweka nafsi zetu chini ya usimamizi na uangalizi wa watu kama sisi?

**Majibu:**

Kwa kuangalia nukta kadhaa yanabainika majibu ya maswali yote haya, na inabainika nafasi ya Manabii عليهم السلام katika mpangilio wa maisha ya mwanadamu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 90 1/13/2017 3:33:23 PM

Sisi ni wajibu tujue kwamba elimu yetu ni finyu, pamoja na maendeleo ambayo ameyapata mwanadamu; hakika tunayoyajua hayazidi tone katika bahari ya elimu na gamba mbele ya jabali, au kama walivyosema baadhi ya maulamaa wakubwa: Hakika elimu yote ambayo tunaimiliki leo haizidi herufi ya alifu katika kitabu cha ulimwengu mkubwa wa uwepo. Na kwa maneno mengine hakika upeo wa uelewa wetu wa kiakili ni sehemu ndogo iliyoangaziwa na mionzi ya elimu na sisi kwa hakika hatujui yaliyo nje ya sehemu hii.

Na Manabii عليهم السلام wanakuja na kuangazia sehemu hii kwa upana ambao tunauhitajia. Na kwa hakika akili zetu zinafanana kabisa na taa kubwa yenye nguvu, lakini Manabii na wahyi wa mbinguni ni jua lenye kuangaza. Je, mmoja wetu anaweza kusema nini haja ya kuwa na jua, na mimi ninamiliki taa yenye nguvu?

Na pia kwa maneno yaliyo wazi zaidi, tunaweza kugawa mambo ya kimaisha sehemu tatu: Yanayoingia akilini, yasiyoingia akilini, na yasiyojulikana. Manabii abadani hawatamki yanayopinga akili, yaani maneno yasiyoingia akilini, na wakiyasema hayo basi wao sio Manabii. Lakini wao wanatusaidia sana sisi katika kufahamu na kutambua yasiyofahamika, na hii ni muhimu sana kwetu, na hivyo hakika watu ambao walikuwa wanasema hakuna haja ya kuwa na Manabii maadamu akili ya mwanadamu ipo, kwa mfano Barahimiya ambao wanaishi India na baadhi ya sehemu nyingine, na wale ambao wanasema leo, kwamba hakika pamoja na uvumbuzi na ugunduzi wote huu hakuna haja ya Manabii na mafunzo yao, wote hawa hawajajua mipaka ya elimu ya binadamu wala ujumbe wa Manabii.

Na hii inafanana kabisa na yule mtoto ambaye amejifunza ABCD katika darasa la kwanza na kusema hakika mimi nimejifunza kila kitu na wala sihitaji mwalimu na ustadhi.. Je, huoni kwamba maneno haya hayana maana kabisa? Kisha hakika Manabii عليهم السلام sio waalimu tu, hakika uongozi wao ni kadhia ambayo tutaifafanua baadaye.

Pili, hakuna yeyote anayesema kwamba mwanadamu ni wajibu aweke nafsi yake moja kwa moja chini ya usimamizi wa mtu mwingine. Hakika Manabii عليهم السلام - kama tutakavyothibitisha baadae – wana mafungamano na elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isiyo na kikomo kwa njia ya wahyi. Na sisi ni wajibu tujue kwa njia ya hoja thabiti mafungamano yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa sababu kwa njia hii tunaweza kukubali maneno ya hawa viongozi wa mbinguni na mafunzo yao ya kimantiki kwa moyo mkunjufu. Hivi kama tukitenda kulingana na mafunzo ya tabibu mahiri tutakuwa tumeshafanya kitendo kibaya? Hakika Manabii عليهم السلام ni matabibu mahiri na wachamungu wakubwa. Je kiakili na kifikira nitakuwa nimetenda jambo baya kama nitakubali somo la mwalimu na ustadhi? Hakika Manabii ni waalimu wakubwa wa binadamu.

Ni lazima tusome kwa makini dalili za kutumwa Manabii kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hakika sisi kwa dalili tatu tunahitaji mafunzo ya Manabii عليهم السلام.

**1. Haja ya mafunzo:**

Hakika sisi kama tukipanda safina iliyotengenezwa kwa mionzi ya nuru inayotupeleka kwa kasi ya kilometa 300 kwa sekunde, hakuna shaka hakika sisi tunahitaji maelfu kwa kiasi cha umri wa Nuhu عليه السلام, ili tuweze kuona kona ya ulimwengu mkubwa na mpana. Na hakuna shaka kwamba ulimwengu huu, kwa upana huu wa ajabu haukuumbwa bure, kama tulivyojifunza katika sehemu ya kwanza katika kitabu hiki. Hakika kuumbwa ulimwengu huu si kwa manufaa na faida ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa sababu ni uwepo uliokamilika kwa pande zote, hana haja ya kitu, ni Mkamilifu hana upungufu hadi ahitajie kuumba ulimwengu na binadamu ili kuondoa upungufu.

Na kwa sababu hii tunafahamu kwamba lengo lake ni kufanya ukarimu kwa viumbe vingine kwa kukamilishana, kama vile jua am-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 92 1/13/2017 3:33:23 PM

balo linatuangazia kwa nuru bila ya kuwa na haja na sisi, vinginevyo sisi tunaweza kulinufaisha nini jua?

Na kwa upande mwingine, je maarifa yetu peke yake yanatosha katika kuandaa njia ya ukamilifu ili kufikia kwenye hatua ya mwanadamu mkamilifu? Ni kiasi gani sisi tunajua siri za ulimwengu.. ni upi uhalisia wa uhai? Lini umeumbwa au lini umepatikana ulimwengu huu? Hakuna yeyote anayejua kwa umakini jawabu la mas'ala haya. Hadi lini utabakia ulimwengu huu? Hawezi yeyote kujibu hilo vilevile?

Hakika kila mtaalamu kati ya wataalamu ana nadharia ya maisha ya kijamii na kiuchumi. Mfano kundi moja linalingania ubepari, na kundi lingine linalingania ujamaa na ushoshalisti, na kundi la tatu linapinga ulingano wa yote hayo mawili na unayazingatia kuwa ni yenye madhara. Vilevile katika mas'ala mengine ya maisha, hakika ikhitilafu ya rai za wataalamu ni nyingi. Na mwanadamu anabaki huru kuchagua, nani kati ya hawa anamkubali!

Hapa ni wajibu kukubali kwamba kufikia kwenye lengo la msingi la kuumba inamaanisha kukua na kukamilika kwa mwanadamu katika nyanja zote. Na inahitaji mlolongo wa mafunzo sahihi yaliyoepukana na makosa, na yanayotegemea uhalisia wa maisha. Na kuna mafunzo yanamsaidia mwanadamu katika kufikia kwenye lengo kupitia njia hii ndefu. Na yanapatikana hayo kwa njia ya elimu ya Mwenyezi Mungu, yaani wahyi ambao unashuka kwa Manabii, na kwa sababu hiyo hakika Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba ili tupite katika njia hii ni lazima atupe mfano wa elimu hii.

## 2. Haja ya kiongozi katika nyanja za kijamii na kitabia:

Na hakuna shaka kwamba sisi kama hatukuweza kuzima uasi wa matamanio yetu, hakika yatafunga akili zetu, na mwanadamu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 93 1/13/2017 3:33:23 PM

kubadilika na kuwa mwenye kiburi na mkandamizaji, na anakuwa ni hatari kuliko mbwa mwitu wakali.

Hakika sisi ili tuleleke katika malezi ya tabia tunahitaji mwalimu. Tunahitaji mfano na kigezo ili tujifunze kulingana na msingi unaoelezwa kwa maneno na utendaji wa kigezo. Na katika maisha haya yenye mawimbi sisi tunahitajia mwanadamu mkamilifu mwenye malezi kamilifu ili atauongoze na kuzuia uasi wa matamanio yetu, na kuzatiti kwetu tabia njema kwa vitendo vyake na maneno yake na kukuza kwetu ushujaa na utukufu, upendo wa mwanadamu, utu na kupendelea kheri kwa wengine, utekelezaji, ukweli, uaminifu na usafi.

Ni nani wasiokuwa Manabii Maasumina ambao wanaweza kuchaguliwa kama walezi na walimu? Na kwa sababu hii haiwezekani Mwenyezi Mungu Muweza na mwenye huruma, kuweza kutunyima uwepo wa mfano wa hawa viongozi walezi. - **(Utafiti uliobakia utakuja katika somo lijalo)**

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Inapozidi elimu yenu je mnahisi kwamba yasiyofahamika ni mengi kuliko maarifa yenu? Lete mfano.
2. Je, unaweza kuelezea tofauti baina ya ufuataji wa upofu na kufuata Manabii ?
3. Kama sisi tunapita katika njia isiyofahamika bila ya kiongozi, ni hatari zipi ambazo zinaweza kutupata?
4. Fafanua wigo wa haja yetu katika uongozi wa Manabii.
5. Je, inawezekana kufikiria utafiti mwingine ambao umebakia katika somo lifuatalo ambalo bado hatujalitaja?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 94 1/13/2017 3:33:23 PM

# SOMO LA PILI:

**Kuweka kanuni na haja ya kuwepo Manabii:**

Tumekwishajua katika somo lililotangulia haja ya kuwepo Manabii, katika nyanja mbili, mafunzo na malezi, na sasa hivi umewadia wakati wa kuzungumzia kuhusu kanuni za kijamii na jukumu muhimu ambalo wanalibeba Manabii عليهم السلام katika nyanja hii.

Sisi tunajua kwamba jambo la muhimu ambalo linatofautisha maisha ya mwanadamu – na ubora huu wakati huo huo ni msingi wa maendeleo yote katika nyanja zote za maisha – ni maisha ya kijamii yenye kusonga mbele.

Ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba kama wanadamu wangeishi kwa kuwa kila mmoja mbali na mwingine, wote katika upande wa fikra na maendeleo wangekuwa wanaishi kama mwanadamu wa zama za mawe! Ndio, hakika juhudi za pamoja ambazo zinawakilisha taa ya utamaduni na maendeleo ndio msingi wa uvumbuzi wote huu na ugunduzi wa kielimu. Mfano kama tukichukua kwa mazingatio kadhia ya safari ya kwenda mwezini, tunaona kwamba kazi hii sio matokeo ya juhudi za mtaalamu au wataalamu wakubwa kadhaa, bali ni juhudi za mamilioni ya wataalamu na wajuzi za maelefu ya miaka kupitia utafiti na uvumbuzi na uzoefu ambao ulipatikana katika mazingira ya maisha ya kijamii hadi imefikia katika ukubwa huu.

Na ikitokea kwamba tabibu mahiri sana amepata moyo mzima, katika kifua cha mtu mwingine, akafaulu katika kupanda moyo huo kwa anayekabiliwa na umauti, na kumuokoa na mauti yasiyo na shaka, hakika hayo ni matokeo ya uzoefu wa maelfu ya matabibu na wapasuaji katika historia, umenukuliwa kutoka kwa maprofesa kwenda kwa wanafunzi.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 95 1/13/2017 3:33:23 PM

Na katika yasiyo na shaka ndani yake ni kwamba maisha haya ya kijamii pamoja na baraka zote hizo yana matatizo vilevile, yanaonekana katika mwingiliano na mgongano wa haki na maslahi ya binadamu, baadhi yao wao kwa wao, wakati mwingine yanafikia kwenye uadui na hata vita. Hapa inabainika dharura ya haja ya kuwepo kanuni, mipango na maamuzi. Na kanuni zinaweza kututatulia matatizo matatu makubwa:

**1.** Kanuni ya kuweka mpaka wa wajibu wa kila mtu mbele ya jamii na wajibu wa jamii mbele ya kila mtu, jambo ambalo linafanya vipaji kuongezeka na juhudi kushindana.

**2.** Kanuni inaandaa mazingira na kuweka usimamizi katika kazi za watu

**3.** Kanuni zinazuia watu kupora haki za wengine, na zinazuia kutokea mkanganyiko, fujo, ugomvi wa watu na makundi, na wakati wa dharura zinaainisha adhabu inayofaa kwa wakosaji.

**Ni nani mbora wa kuweka kanuni?**

Na sasa hivi tuone nani ambaye anaweka kanuni, ili kutatua haja za mwanadamu, ambaye ni mbora zaidi kuliko wengine, kiasi kwamba anachunga katika hayo misingi mitatu iliyotajwa hapo juu, na kubainika mipaka, wajibu na haki za mtu binafsi na jamii, sambamba na kuwepo usimamizi sahihi na unaofaa katika kazi na kuzuia uadui.

Turuhusuni sasa tulete mfano mwepesi:

Inawezekana kufananisha jamii ya binadamu na treni kubwa, na mamlaka yanayoongoza injini ya treni kubwa. Na kanuni ni sawa na njia ya reli ambayo inaainisha njia ya mapito ya treni hii kufikia lengo, kwa yaliyomo humo miongoni mwa mabonde, miinuko, mi-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 96 1/13/2017 3:33:23 PM

teremko na milima. Na kwa kawaida reli ya chuma ni wajibu iwe na sifa zifuatazo: Ardhi ni wajibu iwe ni ngumu ili kuhimili mbinyo na uzito uliopo. Kama ambavyo ni wajibu utenganisho umbali uwe na uwiano makini baina ya matairi. Na vilevile kuta za madaraja na mwinuko wake ni wajibu uwe unawiana na kiwango cha juu cha urefu wa treni. Na katika upande mwingine ni wajibu mataruma yawe katika hali nzuri. Na mteremko na mwinuko usije kwa haraka, kwani la sivyo itakuwa vigumu kudhibiti breki za treni. Na ni wajibu iangaliwe kwa mazingatio na kwa umakini uwezekano wa kudondoka mawe ya milima juu ya pande mbili, na kuporomoka kuta za bonde ambalo treni inapita katika sehemu zake, kwa kuongezea uwezekano wa mafuriko na kuanguka barafu kutoka kwenye miinuko ili treni iweze kufikia lengo, pamoja na mazingira yote hayo.

Pamoja na kuchukua mazingatio yanayofaa, ambayo tumeyataja, tunarejea kwenye jamii ya kibinadamu:- Hakika anayeweka kanuni bora kwa mwanadamu ni wajibu asifike kwa sifa zifuatazo:

1. Ajue aina ya mwanadamu kwa ukamilifu, katika utashi, matamanio, mahitaji na matatizo.
2. Aangalie kwa mazingatio vipaji vyote alivyonavyo, na afaidike na kanuni za ustawi wa vipaji hivi.
3. Apigie mahesabu ya matukio ambayo yanaweza kujitokeza kwa jamii, vyovyote itakavyokuwa aina yake. Na vilevile changamoto katika nyanja hii.
4. Asiwe na maslahi yoyote binafsi katika jamii, ili asifikirie katika maslahi binafsi au yenye kufungamana naye katika jamii, wakati wa kuweka kanuni.
5. Awe anajua aina zote za maendeleo ambazo inawezekana kuzipata mwanadamu na vile vile kutokuendelea kwake, katika nyanja hii.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 97 1/13/2017 3:33:23 PM

6. Ni wajibu muweka kanuni awe amehifadhiwa (maasumu) katika upeo wa juu kutokana na makosa na usahaulifu.

7. Na ni wajibu awe anaweza kumuogopesha mtu yeyote vyovyote atakavyokuwa katika jamii, na wakati ule ule awe ni mpole.

**Ni kwa mtu gani yanapatikana masharti haya?**

Je, mwanadamu anaweza kuwa ni muwekaji bora wa kanuni?

Je, kuna yeyote anayemjua mwanadamu kama huyo kwa sura kamilifu hadi sasa?

Wakati ambapo mmoja wa maulamaa wakubwa katika zama zetu za sasa ameandika kitabu kwa anwani: Mwanadamu ni yule asiyejulikana. Je, imetimia kujua utashi, matamanio na hisia za mwanadamu kwa namna nzuri?

Je, haja za mwanadamu za kimwili na za kiroho zinafahamika kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu?

Je, unaweza kupata mwanadamu wa kawaida katika jamii, mwenye maslahi binafsi maalum?

Je, mwanadamu amehifadhiwa kutokana na makosa, na ana elimu ya masaibu yote yanayotokea kwa watu na jamii?

Hivyo haiwezikani akawepo aliye bora kuliko Mwenyezi Mungu Mtukufu na wale wanaopokea wahyi wa Mwenyezi Mungu, Mwenye kuweka kanuni yenye kutosheleza na bora zaidi.

Hivi ndivyo tunafikia kwenye natija; Kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye amemuumba mwanadamu ili afupishe njia ya ukamilifu, ni wajibu awakalifishe watu kwa ajili ya kumuongoza mwanadamu, wanaoweza kuweka kanuni za mbinguni za kiungu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 98 1/13/2017 3:33:23 PM

kamilifu chini ya uangalizi wa mwanadamu mwenyewe. Na hakuna shaka humo kwamba watu wanapojua kwamba kanuni hizi ni kanuni za Mwenyezi Mungu, wanatekekeleza kwa matumaini na kama wanavyosema, hakika maarifa haya ni dhamana ya utekelezaji wa kanuni hizi kwa ukamilifu.

**Mafungamano ya Tawhidi na Utume:**

Hapa ni lazima vilevile tuzingatie nukta hii nayo ni kwamba mfumo wa kuumba wenyewe ni dalili hai juu ya kuwepo Manabii na ujumbe wao. Kwa ufafanuzi tunasema: Hakika utafiti mfupi katika mfumo huu wa ajabu wa ulimwengu unatuonyesha kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hakusahau haja yoyote kati ya mahitaji yaliyopo. Mfano hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ametupa macho ili tuone na tuangalie na amelizungushia jicho kope na nyusi ili kulihifadhi. Na ameumba (swt) tezi zenye maji maji nayo ni machozi katika kona ya jicho kwa ajili ya kulipa unyevunyevu, bila ya jicho kukauka na kuharibika. Kama ambavyo (swt) ameumba tundu katika kona ya jicho vilevile linaungana na njia ya kupeleka maji ya ziada kwenye pua na kama isingekuwepo njia hii machozi yote yangetiririka katika mashavu yetu. Kisha (swt) amejaalia weusi katika jicho na hususan mboni. Ni nyeti kiasi kwamba inatanuka na kusinyaa kulinga na ukali wa mwanga ili kuzuia jicho lisipatwe na adha. Na kunapatikana pembezoni mwa mboni ya jicho mishipa mbalimbali kwa ajili ya harakati za jicho katika pande zote bila ya kuhitajia kugeuza shingo, kichwa na mwili.

Hivyo je, Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye amemneemesha mwanadamu kwa mahitaji yote haya inawezekana kumnyima dalili na kiongozi mwenye kutumainiwa. Ma’asumu na mwenye kuungwa mkono na wahyi wa Mwenyezi Mungu?

Mwanafalsafa maarufu Abu Ali bin Sina anasema katika kitabu chake mashuhuri (*al-Shifau*): "Hakika haja ya mwanadamu ya kutumiwa Manabii ni kwa ajili ya kubakia kwake na kupata ukamilifu, ni dharura zaidi kuliko uwepo wa nyusi za jicho na kope, na kujipinda sehemu ya chini ya unyayo na mfano wa hayo, na kwa hiyo haiwezekani kuenea uangalizi wa Mwenyezi Mungu wa milele upande huu na kuacha upande mwingine.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Ni mafanikio yapi makubwa zaidi katika maisha ya mwanandamu?
2. Kwa nini mwanadamu hawezi kuishi bila ya kanuni?
3. Lete mifano hai ili kufafanua nafasi ya kanuni katika maisha ya mwanadamu?
4. Ni sifa zipi bora zaidi kwa mwenye kuweka kanuni?
5. Kwa nini ni wajibu Manabii wawe ni katika binadamu?

## SOMO LA TATU:

### Kwa nini Manabii ni Maasumu?

### Kuhifadhiwa kutokana na kosa na kukosea:

Hakuna shaka kwamba ni lazima kwa kila Nabii awe tegemeo la watu na tumaini lao kwa kiasi kwamba wao hawatashuku katika maneno yake wala hawatotarajia humo kosa na ikhitilafu, vinginevyo hakika nafasi ya uongozi wake italegalega. Na kama Manabii hawatakuwa maasumu hakika wenye kusitasita kwa hoja kwamba Manabii wanakosea, na wale watafuta ukweli wa itikadi yao, kwa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 100 1/13/2017 3:33:23 PM

hoja ya kutetereka malengo ya daawa yao, wote wataacha kukubali daawa, au kwa uchache hawatoitikia daawa kwa hamasa. Na Kwa hiyo “dalili ya kutegemewa” ndio dalili muhimu sana ya umaasumu wa Manabii.

Kwa maneno mengine, namna gani inawezekana Mwenyezi Mungu Mtukufu kutoa jambo kumpa mwanadamu bila ya kikwazo wala sharti, wakati ambapo inawezekana mwanadamu huyu kukosea au kufanya kosa, katika hali hii je, inawezekana watu kumtii mwanadamu huyu? Hakika kama watafanya hivyo basi ni kufuata kosa na kukosea, na kama hawatofanya hakika nafasi ya uongozi italegalega na kuporomoka, hususan ukizingatia kwamba hakika nafasi ya uongozi wa Manabii inatofautiana kabisa na yaliyopo kwa watu, kwa sababu watu wanachukua imani yao na ratiba yao kutoka kwao.

Na kwa sababu hii tunaona wafasiri wakubwa wanapofika katika aya ya 59 ya Sura Nisaa: “Mtiini Mwenyezi Mungu, Mtume wake na wenye mamalaka miongoni mwenu” hakika wao wanasema: Hakika jambo la kutii kwa jumla ni dalili juu ya kwamba Nabii ﷺ ni maasumu, na vilevile wenye mamlaka, na makusudio ya wenye mamlaka ni Maimamu Maasumina, ni Maasumu kama Nabii ﷺ, vinginevyo Mwenyezi Mungu Mtukufu asingetoa amri ya kutii, ya jumla bila ya kikwazo wala sharti.

Na njia nyingine ambayo inawezekana kwa njia yake kuthibitisha umaasumu wa Manabii dhidi ya kila kosa ni kwamba sababu za kosa zimehukumiwa kushindwa katika uwepo wa Manabii. Na kwa ufafanuzi tunasema: Hakika sisi tunaporejea nafsi zetu tutaona hakika sisi ni Maasumu katika baadhi ya makosa na vitendo vibaya na visivyokubalika, angalieni mifano ifuatayo:

Je, mnapata mtu mwenye akili anafikiria kula moto? Au kumeza uchafu? Je, inawezekana kumpata mtu anayemiliki hisia na dhamira



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 101 1/13/2017 3:33:24 PM

anatembea barabarani uchi? Ni jambo la kawaida kwamba hamtopata!

Na tukimuona yeyote anafanya vitendo hivyo hakika sisi bila shaka tunapata tumaini kwamba mtu huyo hayuko katika hali ya kawaida, au ya sawa sawa na kwamba ameathirika kinafsi, au ana kichaa, vinginevyo haiwezekani mtu mwenye akili kufanya vitendo hivyo. Hivyo tukichambua mfano wa hali hizi tutaona kwamba ni vitendo vibaya na ni wazi kwamba mwanadamu mwenye akili havisogelei. Na hapa tunaweza kuthibitisha ukweli huu kwa sentensi ndogo na kusema; Hakika kila mtu mwenye akili na mzima anamiliki kinga mbele ya mlolongo wa vitendo hivi au kwa maneno mengine anamiliki umaasumu.

Tunakwenda mbali zaidi ya hatua hii, tunaona baadhi ya watu wanamiliki kinga mbele ya vitendo vibaya na viovu, wakati ambapo baadhi ya watu wa kawaida wengine hawamiliki hayo. Mfano hakika tabibu mahiri ambaye anajua vizuri aina za vijidudu vya magonjwa hawezi kamwe kunywa maji yaliyooshewa humo nguo za mgonjwa aliyepatwa na maradhi hatari, wakati ambapo mtu jahili hajali kufanya hivyo. Na kwa uchambuzi mwepesi tunapata natija kwamba kila kinapozidi kiwango cha uelewa wa mwanadamu ndivyo inavyozidi kinga yake mbele ya vitendo vibaya.

Na hivyo hakika kila kinapozidi kiwango cha imani na uelewa wa mwanadamu na itikadi yake kwa Mwenyezi Mungu na uadilifu wake, kana kwamba yeye anaona yote hayo mbele ya macho yake, inazidi kinga yake mbele ya aina zote za makosa, na kila kosa kwake linakuwa ni sawa na kuwa uchi kama alivyozaliwa na mama yake na kwenda barabarani katika hali hii. Na mali ya haramu kwake ni sawa na moto wenye kuwaka ambao hatuwezi kuusogeza katika vinywa vyetu, hivyo hasogezi mali ya haramu mdomoni mwake.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 102 1/13/2017 3:33:24 PM

Tunapata natija kupitia mkusanyiko wa mazungumzo haya kwamba Manabii wanachukia kufanya maasi kwa kuwa na elimu na uelewa na imani madhubuti, na kwa hiyo sababu za kufanya makosa hazi-wezi kutawala imani yao na akili zao, na kwa sababu hii tunasema: Hakika Manabii ni maasumu na wameepushwa na makosa.

**Fahari ya Nafsi ya Umaasumu:**

Hakika baadhi ya watu ambao hawana elimu juu ya dhana ya umaasumu na sababu za kinga hiyo, wanasema Mwenyezi Mungu anapomuweka mbali mtu na makosa na akahukumu juu ya visababi-shi vya makosa hakika hii sio fahari kwake!

Hakika hii ni kinga ya kulazimisha na wala haihesabiwi kuwa ni fadhila. Lakini kwa ufafanuzi ambao tumeutanguliza katika yaliyo-tangulia hakika jawabu litakuwa linajulikana kabisa:

Hakika umaasumu wa Manabii sio wa kulazimisha abadani, bali ni zao la imani yenye nguvu na yakini kamilifu, uelewa na elimu ya kipekee kwao, na hii ndio fahari kubwa. Na kama tabibu mahiri anakuwa mbali na sababu za maradhi je, kitendo hiki kitakuwa cha kulazimisha? Je, mfano wa mtu huyu kama ataamua kwa uangalifu wa kiafya je hii haihesabiwi kwake kuwa ni fadhila?

Na kama mtu wa haki anajua matokeo mabaya ya kosa kubwa, na akajizuia kulifanya je, mtu huyu atakuwa ni mwenye kukosa fa-dhila? Vivyo hivyo tunafikia kwenye natija kwamba umaasumu wa Manabii una upande wa hiyari na pia una fahari kubwa.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Ni yapi matawi ya umaasumu?
2. Nini kingetokea kama Manabii wasingekuwa maasumu?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 103 1/13/2017 3:33:24 PM

3. Ni upi uhalisia wa nafasi ya umaasumu?
4. Je, unaweza kutaja mifano isiyokuwa ile iliyotajwa katika somo, ambamo watu au kundi miongoni mwao wanakuwa ni maasumu humo?
5. Je, umaasumu wa Manabii ni wa kulazimisha au ni wa hiyari? Ni ipi dalili yako?

## SOMO LA NNE:

**Njia bora katika kumjua Nabii:**

Hakuna shaka kwamba kukubali madai yoyote ya mwenye kudai ni kinyume cha akili na mantiki. Hakika kudai unabii na ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu inawezekana kuwa ni sahihi, lakini kuna uwezekano wa dhana hii pia, nayo ni mtu kutumia fursa kudai unabii. Na kwa sababu hii ni wajibu tuwe na kipimo cha kupima daawa ya Manabii na mafungamano yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na ili kufikia lengo hili kuna njia mbalimbali, zilizo muhimu zaidi ni njia mbili:

1. Kutafiti madhumuni ya daawa ya Nabii na kukusanya alama zote na viambatanisho.
2. Muujiza, na vitendo ambavyo haiwezekani kutokea kwa mwanadamu.

Kuna kundi la watu linashangaa neno muujiza, au hakika wao wanaitakidi kwamba miujiza ni sawa na uongo na ukhorafi. Lakini tukidadisi katika maana ya kina na ya kielimu ya muujiza, tutakuta kwamba hayo mawazo ni kosa kabisa. Hakika muujiza sio kitendo kisichowezekana, na sababu isiyokuwa na sababu, bali kwa uchambuzi mwepesi ni kitendo kinachokiuka mazoea. Kinatoka nje ya



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 104 1/13/2017 3:33:24 PM

wigo wa yale ambayo wanayafanya watu wa kawaida, bali unatokea kwa nguvu iliyo juu ya nguvu ya mazingira ya kawaida.

Na vivyo hivyo hakika muujiza una masharti, nayo ni:

1. Hakika ni kitendo kinachowezekana na inawezekana kukikubali.
2. Mwanadamu wa kawaida hawezi kukifanya, bali hata werevu hawawezi kwa uwezo wao wa kibinadamu.
3. Hakika mwenye muujiza ni wajibu awe na matumaini sana na kazi yake kwa kiasi kwamba anatoa changamoto kwa wengine.
4. Hawezi yeyote kuleta mfano wake, na kama inavyojulikana katika jina lake wanabakia wengine ni wenye kushindwa juu yake.
5. Muujiza ni wajibu uwe unaafikiana na daawa ya Nabii au Imamu, na ikiwa kuna vitendo visivyokuwa vya kawaida vinatokea kwa asiyekuwa nabii na Maimamu hakika hivyo vinaitwa karama na sio muujiza.

**Mifano iliyo wazi:**

Tumeshasikia sote kwamba moja ya miujiza ya Masihi عليه السلام ni kuhuisha wafu, na kutibu wagonjwa ambao haitarajiwi kupona kwao. Je, tunayo dalili ya kielimu na kiakili inayotuthibitishia kwamba baada ya kusimama viungo vya mwanadamu, vinaanza kazi tena na kurejea katika uhai? Je, tunayo dalili ya kielimu na kiakili inayotuthibitishia kwamba maradhi ya kansa ambayo tunashindwa kuyatibu yatakuwa ni maradhi yasiyo na tiba milele?

Hakuna shaka kwamba mwanadamu kwa uwezo ambao anaumiliki na katika mazingira ya hivi sasa hawezi kuhuisha wafu, au kutibu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 105 1/13/2017 3:33:24 PM

baadhi ya maradhi, hata kama wakikusanyika matabibu katika ulimwengu wote na wakakusanya waliyonayo miongoni mwa uzoefu na maarifa. Lakini kuna kizuizi gani mwanadamu kwa nguvu ya Mwenyezi Mungu na elimu kati ya elimu pana ya Mwenyezi Mungu, na kwa ishara kurejesha roho kwenye mwili uliokufa na kutibu maradhi yasiyopona? Hakika elimu inasema sijui na sina uwezo juu ya hilo, lakini haisemi kuwa haiwezekani na haingii akilini.

Mfano mwingine: Hakika safari ya kwenda mwezini bila ya kutumia roketi za angani na vyombo vingine haiwezekani, lakini wakati ule ule hakuna kizuizi kwamba nguvu yenye nguvu zaidi kuliko nguvu zetu, na roketi isiyojulikana, ya kisasa zaidi kuliko ile roketi aliyoivumbua mwanadamu, inakuwa chini ya usimamizi wa mtu anayeweza kusafiri kwa njia yake kwenda kwenye mwezi au kwenye sayari nyingine. Na kama mtu akiweza kufanya mambo hayo yenye kukiuka ada au mfano wake na kuambatanisha hayo na daawa ya unabii, na kutoa changamoto kwa watu katika mambo haya, na watu kubaki ni wenye kushindwa mbele yake, hakika yakini itapatikana kwetu kwamba ametumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu hawezi kabisa Mwenyezi Mungu kumpa nguvu ya mfano huu mwanadamu muongo apoteze watu kwayo. (Tafakari hilo kwa makini).

**Haipasi kuchanganya miujiza na ukhorafi:**

Ilikuwa ufurutu na kuzembea daima ni chanzo cha ufisadi, kupotea na kupotosha haki. Na jambo hili linajitokeza pia juu ya muujiza. Wakati ambapo wanaojifanya wasomi wanapinga kwa uwazi au kwa kificho aina yoyote ya muujiza, wengine wanachanganya miujiza na habari dhaifu na uongo, na kwa hiyo wanakuwa ni msaada kwa adui asiyejulikana ambaye anakwenda mbio kuchafua miujiza, na kufunika upande halisi wa elimu ya miujiza ya Manabii kwa uongo wa kuzua na dhana ambazo hazina msingi. Na muujiza haudhihiri



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 106 1/13/2017 3:33:24 PM

katika uhalisia wake kama haijatimia kuondoa uongo huo wa kuzua ambao unakwenda mbio kuchafua mtazamo halisi wa miujiza. Na kwa sababu hii maulamaa wetu wakubwa daima walikuwa wanadadisi na wanaangalia hadithi za Kiislamu katika nyanja za miujiza ili kuzipembua kutokana na uongo na uzushi. Na kwa sababu hii imedhihiri Elimu ya Wapokezi wa Hadithi, ili kujua wapokezi wa hadithi kwa sura kamilifu, na kuzichambua hadithi sahihi na dhaifu, na ili kusichanganywe maudhui ya uongo ambayo hayana msingi wowote wa ukweli.

Hakika siasa ya ukoloni na ulahidi leo inakwenda mbio vilevile katika kuchanganya fikra za uongo na itikadi safi za kidini, ambazo wanazielezea kuwa sio za kielimu. Na sisi ni juu yetu kuangalia njama hizi haribifu za adui kwa umakini.

**Tofauti baina ya miujiza na vitendo vya kikhorafi:**

Tumekwishasikia mara nyingi kwamba wenye kuridhiwa wanafanya vitendo vyenye kukiuka ada, na sio wachache wale ambao wameona vitendo hivi vya ajabu na vya kushangaza. Hapa linajitokeza swali hili lenyewe; Nini tofauti baina ya vitendo vyenye kukiuka ada na miujiza ya Manabii? Na sisi kwa vipimo gani tunaweza kupambanua baina yao?

Swali hili lina majibu mengi na yaliyo wazi zaidi ni mambo mawili:

**1.** Wenye kuridhiwa daima wanafanya vitendo finyu, na kwa maneno mengine hakika wao hawako tayari kufanya vitendo ambavyo wanavipendekeza watu wengine, bali hakika wao wanafanya vitendo vyenye kukiuka ada ambavyo wanavitaka wao, yaani vile vitendo ambavyo wamevifanyia mazoezi na wamevisoma vizuri, na dalili ya hilo iko wazi,



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 107 1/13/2017 3:33:24 PM

kwa sababu uwezo wa kila mwanadamu ni mfinyu na inawezekana akawa mahiri katika kitendo au vitendo viwili. Ama vitendo vinavyokiuka ada vya Manabii havijulikani mpaka wake na havina kikwazo wala sharti. Wao wanaweza wakati wa dharura, kufanya muujiza wowote unaotakiwa kwao, kwa sababu wao wanategemea nguvu isiyo na kikomo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na sisi tunajua kwamba hakuna mpaka wala kikomo cha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, wakati ambapo uwezo wa mwanadamu una kikomo.

**2.** Hakika kitendo anachokifanya mwenye kuridhiwa anaweza kukifanya mwingine mwenye kuridhiwa, na hii inamaanisha kwamba hatoki katika uwezo wa mwanadamu. Na kwa sababu hii hakika mwenye kuridhiwa ambaye anafanya kitendo chenye kukiuka ada hatoi changamoto kwa watu wala hataki kwao malipo, kwa sababu anajua kwamba wanapatikana katika mji ule ule au katika miji mingine watu wengine mfano wake. Ama Manabii hakika wao wanatoa changamoto kwa tumaini na wanasema kama wanadamu wangekusanyika ili kuleta mfano wake wasingeweza. Na ikhitilafu hii inasadikisha vilevile katika yanayoambatana na uchawi. Hizi ni tofauti mbili ambazo tumezitaja zinapambanua baina ya mipaka ya uchawi na muujiza kabisa.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Kwa nini wanakiita kitendo kinachokiuka ada kuwa ni muujiza?

**2.** Je, Muujiza ni wa kipekee katika kanuni ya sababu?

**3.** Ni zipi njia za kujua muujiza kwa kutofautisha na vitendo

vya wenye kuridhiwa, na wachawi?

**4.** Nini masharti ya msingi katika Muujiza?

**5.** Je, umeona katika umri wako kitu kinachofanana na muujiza?

# SOMO LA TANO:

**Muujiza mkuu wa Nabii wa Uislamu ﷺ:**

**Muujiza wenye kudumu:**

Maulamaa wote wa Kiislamu wanaitakidi kwamba Qur'ani Tukufu ndio muujiza mkuu wa Nabii wa Uislamu ﷺ na hiyo ni kwa:

**Kwanza:** Qur'ani ni muujiza wa kiakili. Unafungamana na roho na fikra ya watu.

**Pili:** Kwa sababu ni muujiza wa milele na wa daima.

**Tatu:** Kwa sababu ni muujiza, tangu karne zilizopita 14 unapiga kelele: "Kama nyinyi mnasema kwamba sio kitabu cha mbinguni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu basi leteni mfano wake." Hakika wito huu wa changamoto umekuja katika sehemu nyingi katika Qur'ani Tukufu miongoni mwazo ni:

قُلْ لَئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَٰذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا

**"Sema hata kama watakusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani hawataleta hata kama baadhi yao watasaidiana na baadhi." (Sura al- Israi; 17:88).**

Na katika sehemu nyingine changamoto inatoa sharti jepesi:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 109 1/13/2017 3:33:24 PM

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۖ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوَرٍ مِثْلِهِ مُفْتَرَيَاتٍ وَادْعُوا مَنِ اسْتَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

**"Au mnasema ameizua sema, basi leteni sura kumi mfano wake zilizozuliwa na waiteni mnaoweza, asiyekuwa Mwenyzi Mungu kama nyinyi ni wa kweli." (Sura Hudi; 11:13).**

Na baada ya hayo inaongeza katika Aya ifuatayo: "Kama hawatowaitikieni, basi jueni kwamba hakika imeteremshwa kwa elimu ya Mwenyezi Mungu."

Na baada ya hapo inarahisisha masharti ya changamoto kwa kiasi cha chini kabisa inasema:

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِنْ مِثْلِهِ وَادْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

**"Na ikiwa mna shaka kwa (hayo) tuliyomteremshia mja Wetu basi leteni sura moja iliyo mfano wake na waiteni mashahidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu ikiwa mnasema kweli." (Sura al- Baqarah; 2:23).**

Na katika Aya ifuatayo inasema wazi: "Na msipofanya, na hamtofanya, basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe uliowekewa makafiri." (Sura al- Baqarah: 23).

Hakika wito huu wenye kufululiza kwa kutoa changamoto kwa wapinzani unaonyesha kwamba Nabii mtukufu ﷺ tegemeo lake katika mas'ala ya muujiza lilikuwa katika Qur'ani tukufu pamoja na kwamba imenukuliwa kutoka kwake miujiza mingi katika vitabu vya historia. Na kwa kuwa Qur'ani ni muujiza hai uliopo katika jamii hakika sisi tutaitegemea katika utafiti huu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 110 1/13/2017 3:33:24 PM

**Namna gani wamebaki ni wenye kushindwa mbele ya changamoto hii?**

Uzuri ni kwamaba Qur'ani Tukufu inaita wapinzani kwa ujasiri kwenye medani ya changamoto na inawatikisa kwa meneno yenye hamasa katika uwanja wa kujitokeza ili kuondoa udhuru kwa kila mtu. Na maneno yafuatayo ni ukweli wa hayo: "Ikiwa ni wa kweli", "Hamtofanya", "waiteni mnaoweza" na "Leteni sura moja iliyo mfano wake" na mfano wa hayo.

Hii ni katika upande mmoja, na katika upande mwingine hakika mapambano ya Nabii Mtukufu ﷺ dhidi ya wapinzani hayakuwa ni mapambano mepesi. Kwa sababu Uislamu sio tu ulikuwa unatishia hatma ya dini yao ambayo walikuwa wameshikamana nayo, bali hata maslahi yao ya kiuchumi na kisiasa. Na uwepo wao ulikuwa katika hatari ya kutoweka. Na kwa maneno mengine ni kwamba nguvu ya Uislamu ilikuwa inasambaratisha maisha yao kabisa, na kwa hiyo hakika wao walikuwa wanalazimika kuteremka kwenye medani kwa kila wanachomiliki katika nguvu. Na wao ili waondoe silaha kwa Nabii wa Uislamu ﷺ ilikuwa ni lazima walete Aya mfano wa Qur'ani ili asitoe changamoto baada ya hapo na kuwazingatia kuwa ni wenye kushindwa na kubainika ukweli wake. Na kwa sababu hii inawaambia: Ombeni kwa mafasihi wote wa kiarabu wawasaidieni katika jambo hili, lakini wao kila mara walikuwa wanashindwa na wanarejea nyuma kwa haraka, na umepokelewa ufafanuzi wa matukio haya katika vitabu vya historia.

**Kisa cha Walid bin Mughirah:**

Na miongoni mwa watu ambao waliitwa katika changamoto ni Walid bin Mughirah, naye ni katika Bani Makhuzum, na alikuwa ni mashuhuri miongoni mwa Waarabu katika zama zake kwamba yeye ni mwerevu sana na mwenye fikra ya sawa.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 111 1/13/2017 3:33:24 PM

Walimuomba awaletee fikra ili kukabiliana na Qur'ani Tukufu ya ajabu na nguvu yake yenye kuathiri. Walid akamtaka Nabii wa Uislamu ﷺ amsomee Aya za Qur'ani. Mtume ﷺ akamsomea Aya katika Sura Sajdah. Na Aya hizi zilisababisha hali iliyomfanya aamke na kuelekea katika kikao kilichokuwa kinafanyika kwa Bani Makhuzum, na akasema: "Wallahi nimesikia maneno kutoka kwa Muhammad hayafanani na maneno ya watu wala malaika." Kisha akaongeza: "Na hakika yana utamu na yana mvuto na hakika kilele chake kina matunda na shina lake ni imara, na hakika yako juu na hakuna kitu kitakuwa juu yake."

Na maneno haya yaliwafanya Makuraishi wanong'onezane na kusema: "Walidi amelogwa na Muhammad." Abu Jahali akamjia akiwa na hofu na amechanganyikiwa, na akanukuu kwake wanayoyasema Makuraishi, akawaendea katika majilisi yao na akawaambia:

"Hakika nyinyi mnadai kwamba Muhammad ni kichaa, je, mmekwishaona kwake kichaa?"

Wakasema: Hapana.

Akawaambia: "Mnadai kuwa ni muongo, je mmekwishaona chochote katika uongo? Je, hakuwa maarufu kati yenu kwa ukweli na uaminifu hadi mkamwita Mkweli, Mwaminifu?"

Baadhi ya viongozi wa kikuraishi wakasema: Hivyo, ni kitu gani?

Walid akatafakari kidogo kisha akasema: "Hakika yeye ni mchawi."

Pamoja na kwamba wao walikuwa wanataka kwa maneno haya kuwaweka mbali watu ambao wamevutiwa na Qur'ani ila dalili hai juu ya mvuto wenye nguvu iliyonao Qur'ani Tukufu iliwafanya



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 112 1/13/2017 3:33:24 PM

wapinzani wakauita mvuto huu kwamba ni uchawi, wakati ambapo hakuna uhusiano wowote na uchawi.

Vivyo hivyo Makuraishi walisambaza uvumi huu mpya kila sehemu kwamba Muhammad ﷺ ni mchawi hodari, na kwamba Aya ndio uchawi wake. Hivyo kuweni mbali naye, na jaribuni kutosikia maneno yake. Lakini pamoja na hayo yote hakika mbinu yao hii haikuzaa matunda, bali waliokuwa na kiu ya ukweli, wengi walikuwa wanamiliki nyoyo safi na hivyo walikwenda makundi kwa makundi kwenye Qur'ani Tukufu ili wakate kiu kutokana na maji yake matamu ya ujumbe wa mbinguni, na kuwalaumu maadui na kuwalazimisha kurejea nyuma.

Na leo hii Qur'ani Tukufu inatoa changamoto kwa watu wote, na inatangaza kwa sauti yake ya juu: "Na ikiwa mna shaka kwa tuliyomteremshia mja wetu basi leteni sura moja tu mfano wake." Enyi maulamaa, wanafalsafa, wanafasihi na waandishi kutoka katika kaumu yoyote mliyopo.

Na sisi tunajua vilevile hakika maadui wa Uislamu na hususani watawala wa kinaswara ambao waliona Uislamu ni dini ya mapinduzi na yenye ushindani hatari kwao, hakika wao wanatoa mamilioni ya dola kila mwaka ya kufanya mahubiri dhidi ya Uislamu kwa njia mbalimbali, kiutamaduni, kielimu na kiafya. Na wanaharakati katika nchi mbalimbali za Kiislamu, ili wafupishe njia walitaka katika kundi la Waarabu wakristo na wataalamu wa mashairi na waandishi na wanafalsafa waandike sura mfano wa sura ya Qur'ani tukufu na waisambaze miongoni mwa Waislamu ili wawanyamazishe. Na hakuna shaka kwamba kama jambo hili lingekuwa linawezekana basi wangelifanya kwa gharama yoyote. Lakini ilishinda dalili yenye nguvu dhidi ya wapinzani wa muujiza wa Qur'ani Tukufu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 113 1/13/2017 3:33:24 PM

# TAFAKARI NA UJIBU:

1. Kwa nini Qur'ani Tukufu inazingatiwa kuwa ni muujiza mkubwa wa Nabii Mtukufu ﷺ?
2. Namna gani Qur'ani Tukufu inatoa changamoto?
3. Kwa nini maadui waliiita Qur'ani Tukufu kuwa ni uchawi?
4. Kwa nini Uislamu unazingatiwa kuwa ni mshindani mwenye nguvu kwa unaswara leo?
5. Ni kipi kisa cha Walid bin Mughirah al-Makhuzumiy?

# SOMO LA SITA:

### Upenyaji katika muujiza wa Qur'ani

### Herufi za mkato ni za nini?

Tunajua kwamba kunapatikana katika mwanzo wa Sura nyingi za Qur'ani herufi za mkato mfano: *Alif Lamu Mim*, *Alif Lam Raa*, *Yaasin*, na nyinginezo. Moja ya siri na falasafa ya hizi herufi, kulingana na baadhi ya riwaya za Kiislamu ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka kubainisha kwamba mfano wa muujiza mkubwa na wa milele, yaani Qur'ani tukufu, unatokana na mjengo huu mwepesi wa herufi, na namna gani mfano wa maneno haya matukufu, yanatokana na herufi na matamko anayoweza kila mtoto kuyatamka, na kwamba utengenezaji wa jambo hili muhimu ni katika mfano wa maneno haya mepesi, nayo ndio muujiza mkubwa.

Na sasa hivi linajitokeza swali hili lenyewe:

Kwa nini Qura'ni inazingatiwa kuwa ni muujiza? ni kwa ufasaha wake au ni kwa balagha yake? Yaani utamu wa ibara zake na uwazi



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 114 1/13/2017 3:33:24 PM

wa maneno yake au ni nguvu ya kupenya kwake au ni kwa pande zingine?

Hakika sisi kila tunapoangalia katika Qur'ani Tukufu katika pande zake mbalimbali unadhihirika muujiza katika kila upande humo, miongoni mwao kwa mfano:

1. Fasaha, balagha, utamu, mvuto mkubwa na wa ajabu katika matamko na maana.
2. Maana kubwa katika kila nyanja, itikadi isiyo na ukhorafi wowote.
3. Miujiza ya kielimu, yaani kuweka wazi kadhia nyingi ambazo mwanadamu hakuzijua katika zama hiyo.
4. Utabiri wa wazi na makini juu ya matukio ya mustakabali, Qur'ani kutoa habari za ghaibu.
5. Kutokuwepo mgongano, kupingana na mparaganyiko humo.

Hakika utafiti katika mas'ala haya matano ni mpana sana, lakini sisi kupitia masomo machache tutazungumzia pande muhimu, miongoni mwazo ni:

## 1. Fasaha na balagha:

Sisi tunajua kwamba kila neno lina pande mbili: matamko na maana. Kila matamko na maneno yanapokuwa mazuri yenye mshikamano na mafungamano imara na yameepukana na ugumu wowote, na sentensi ikawa ni yenye maana yenye kuvutia kwa sura ya ukamilifu, maneno hayo yanaitwa ni fasaha na balagha. Na Qur'ani Tukufu hakika inazo pande hizi mbili kwa daraja zake za juu kiasi kwamba hakuweza yeyote hadi hivi sasa kuleta Aya na Sura zenye kuvutia na zenye utamu na sauti yenye mizani kama iliyopo katika Qur'ani Tukufu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 115 1/13/2017 3:33:24 PM

Na tumekwishasoma katika masomo yaliyotangulia kwamba Walid bin Mughirah aliyeteuliwa na Waarabu alishikwa na tahayari wakati aliposikia Aya za Qur'ani Tukufu na akazama katika kutafakari. Na baada ya muda katika kutafakari katika kuleta njia ya kutoa changamoto kwa Qur'ani akasema kwa wakuu wa kikuraishi kuwa waseme kwamba Qur'ani ni uchawi na kwamba Muhammad ni mchawi!!

Walinasibisha kwa Nabii Mtukufu sifa hii mara nyingi, na pamoja na kwamba wao walikuwa wanataka nyuma ya hayo kumlaumu ila hakika wao kwa uhakika walimsifu bila ya kujua. Kwa sababu wao kwa sifa hii walikiri kwa kiasi fulani muujiza wa Qur'ani Tukufu, kiasi kwamba haiwezekani kufasiri hayo kwa njia ya kawaida, bali ni wajibu tukiri kwamba yana mvuto usiofahamika na usiojulikana. Lakini wao badala ya kuunyenyekea ukweli huu na kuuzingatia kuwa ni muujiza na waamini, wakaizingatia Qur'ani kuwa ni uongo. Wakaghafilika na wakasema hakika ni uchawi.

Imeonekana mara nyingi katika historia ya Kiislamu kwamba watu wagumu walikuwa hawaendi mbele ya Mtume ﷺ na kusikiliza Aya za Qur'ani Tukufu isipokuwa hubadilika mwendo wao na kuangaziwa nyoyo zao na nuru ya Uislamu, na hii inaonyesha kwa uwazi juu ya mvuto wa Qur'ani Tukufu na ufasaha wake, balagha yake na muujiza wake.

Kwa nini tunakwenda mbali! Hakika wote wenye kufahamu fasihi ya kiarabu, kila wanaposoma Qur'ani Tukufu na wakarudia kusoma inazidi shauku yao na utamu wao katika kusoma na wala hawapatwi na uvivu kwa kusoma zaidi. Hakika maneno ya Qur'ani Tukufu ni makini na yana mtiririko kwa namna nzuri, ukiongezea kwenye utukufu, usafi na ubainifu imara, na wakati ule ule iko wazi kwa ukamilifu, na wakati wa dharura ni madhubuti na imara.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 116 1/13/2017 3:33:24 PM

Na kinachofaa kukumbukwa ni kwamba Waarabu katika zama hizo walikuwa wanamiliki lugha yenye kuendelea wakati huo, na mifano ya mashairi na kaswida za zama za ujahiliya hivi sasa zinazingatiwa ni kati ya mashairi bora zaidi ya Waarabu. Na ni maarufu kwamba washairi wakubwa na wanafasihi wa Hijazi walikuwa wanakusanyika kila mwaka ili kutoa kaswida bora zaidi za ushairi katika soko la Akaadhi. Na soko hili lilikuwa ni kituo cha biashara, na kaswida zilikuwa zinapembuliwa ili kuchagua iliyo bora zaidi na kuizingatia kuwa ni kaswida ya mwaka. Hivyo walikuwa wanaibandika katika Kaaba, na mwanzoni mwa Unabii wa Nabii wa Uislamu ﷺ kulikuwa na kaswida saba zinazoitwa *al-Mualaqati Saba'ah*.

Lakini baada ya kushuka Qur'ani Tukufu, hizo zikawa ni duni mbele ya fasaha na balagha ya Qur'ani, wakaziondoa moja baada ya nyingine na kuziweka katika kapu la kusahaulika.

Wafasiri wameashiria kadiri ya uwezo wao katika maana makini na ya ajabu ya Aya, na nyinyi mnaweza kurejea tafsiri hizo ili mfahamu ukweli huu.

Hakika kutambua na kuifahamu Qur'ani Tukufu kunaonyesha kutokuzama katika maneno ya Nabii mtukufu ﷺ aliposema: "Dhahiri yake ni nzuri, ndani mwake kuna kina, hayahesabiki maajabu yake na wala hayamaliziki maajabu yake." Na anasema Amirul-Muuminina Imamu Ali عليه السلام, naye ni mwanafunzi katika madrasa ya Qur'ani katika nyanja hii: "Humo kuna utulivu wa nyoyo, chemchem za elimu, na moyo hauna mwangaza usiokuwa huo."

## TAKARI NA UJIBU:

1. Nini falsafa ya herufi za mkato?
2. Je, Qur'ani Tukufu ni muujiza katika upande mmoja? Au ni katika pande mbalimbali?

3. Kwa nini wapinzani wa Nabii ﷺ wanamwelezea kuwa ni mchawi?

4. Nini tofauti kati ya fasaha na balagha?

5. *al- Mualaqati Saba'ah* zinahusiana na zama ipi katika historia, na nini maana yake?

# SOMO LA SABA:

**Mtazamo wa ulimwengu katika Qur'ani Tukufu:**

Kabla ya kila kitu ni wajibu kuangalia mazingira ambayo humo imedhihiri Qur'ani Tukufu, katika upande wa kifikra na kiutamaduni. Wanahistoria wanakubali kwamba ardhi ya Hijazi wakati huo ilikuwa ni sehemu isiyo na maendeleo kabisa, hadi wao walikuwa wanawazingatia wakazi wake katika zama za ujahiliya kuwa ni kati ya wanyama au wenye unyama. Walikuwa katika upande wa ibada wanapenda masanamu ambayo yalikuwa yametapakaa na kutumika sehemu zote za utamaduni wao, na kulikuwa na masanamu ya aina mbalimbali ya mawe na miti, hata inasemekana kwamba baadhi yake yalikuwa yanatengenezwa na tende. Wanasujudu mbele yake na wanapopatwa na njaa wanayala!!

Pamoja na kwamba walikuwa wanachukia watoto wa kike kiasi kwamba wao walikuwa wanawazika wakiwa hai, ila wao walikuwa wanazingatia malaika ni miongoni mwa wasichana, na wakapunguza hadhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hadi wao walimfikisha katika daraja la mwanadamu. Na walikuwa wanashangaa ibada ya kumpwekesha, na alipowalingania Nabii wa Uislamu ﷺ katika tauhidi wakashangaa: "Je, amewafanya waungu kuwa Mungu mmoja? Hakika hili ni jambo la ajabu." (Sura Swadi: 5).

Na walikuwa wanamzingatia anayepuuza ngano (uongo), ukhorafi na fikra ambazo walikuwa wanaziamini kuwa ni kichaa. Na



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 118 1/13/2017 3:33:24 PM

walikuwa wanatawaliwa na mfumo wa makabila, na kulikuwa na ikhitilafu mbaya sana na nyingi baina ya makabila, kiasi kwamba moto wa vita ulikuwa hauzimiki baina yao. Na mara nyingi ardhi ilikuwa inatapakaa damu zao zilizomwagwa, na walikuwa wanazingatia uporaji kuwa ni fahari na ni kitendo cha kawaida baina yao.

Ama waliokuwa wanajua kusoma na kuandika katika mji mtukufu wa Makkah ambacho kilikuwa ni kituo muhimu, hawakuwa wanazidi idadi ya vidole vya mkono. Ndio, katika mfano wa mazingira hayo, alitokea mtu asiyejua kusoma wala kuandika na wala hakusoma kwa mwalimu, na akaja na Kitabu kitukufu na maulamaa baada ya zaidi ya karne kumi na nne bado wangali wanahangaika nacho, na bado wangali wanatoa uhakika.

Hakika Sura ambayo Qur'ani Tukufu inaitoa katika ulimwengu wa uwepo na mfumo wake ni sura makini, yenye kupigiwa mahesabu nyanja zake, na inawasilisha tauhidi kwa sura kamilifu zaidi. Na siri za kuumbwa ardhi, mbingu, usiku, mchana, jua, mwezi, mimea, nyasi na uwepo wa mwanadamu inazingatiwa kuwa ni alama na dalili zinaonyesha juu ya Mwenyezi Mungu mpweke Mwenye kutegemewa. Hayo yamekuja kwa wingi katika Qur'ani na kwa ubainifu kamili na wa aina mbalimbali.

Mara nyingine inapenya ndani ya mwanadamu na kuzungumzia juu ya tauhidi ya maumbile:

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ

**"Wanapopanda katika safina wanamuomba Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini, anapowaokoa nchi kavu basi wao wanamshirikisha." (Sura al- Ankabuti; 29:65).**

Na wakati mwingine kwa njia ya akili na fikra, inazungumzia juu ya tauhidi kwa kutoa dalili, na kutembea katika anga, na katika nafsi, na siri za kuumbwa ardhi na mbingu, wanayama, milima na bahari, kuteremka mvua na kuvuma upepo na umakini wa mshipa katika mwili na roho ya mwanadamu. Na wakati wa kubainisha sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu anachagua njia za kina zaidi anasema katika sehemu moja:

"Hafanani na kitu chochote." (Sura Shuraa: 11). Na katika sehemu nyingine anasema:

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۖ هُوَ الرَّحْمَٰنُ الرَّحِيمُ

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۚ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ

هُوَ اللَّهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ ۖ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۚ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**"Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipokuwa Yeye tu, Mwenye kuyajua yaliyofichikana na yanayoonekana. Yeye Ndiye Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana Mungu isipokuwa Yeye tu. Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Muangaliaji, Mwenye nguvu, Jabari, Mkubwa. Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomshirikisha nayo. Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mtia sura, Mwenye Majina mazuri kabisa kinamsabihi kilicho katika mbingu na ardhi. Naye ni Mwenye nguvu Mwenye hikma."**
**(Sura al- Hashir; 59:22- 24).**

Na inatumia ibara nzuri ili kubainisha na kusifu elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isiyo na kikomo:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 120 1/13/2017 3:33:24 PM

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَامٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ أَبْحُرٍ مَا نَفِدَتْ كَلِمَاتُ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

**"Na lau miti yote iliyomo ardhini ikawa ni kalamu na bahari (kuwa wino wa kuandikia) na ikaongezewa bahari saba, maneno ya Mwenyezi Mungu yasingemalizika. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo, Mwenye hekima." (Sura Luquman: 27).**

Na Qur'ani ina maneno matukufu kuhusu Mwenyezi Mungu kukizunguka kila kitu na uwepo wake kila sehemu inayohusika nayo: "Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu popote mtakapoelekea basi mtaje Mwenyezi Mungu." (Sura al- Baqarah: 115). "Naye yuko pamoja nanyi popote mlipo na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mnayoyafanya." (Sura al- Hadid: 4).

Na yanapokuja mazungumzo katika miadi na Siku ya Kiyama, Qur'ani tukufu inasema mbele ya mshangao wa washirikina na ukanushaji wao:

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۖ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيمٌ

قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ

الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ مِنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنْتُمْ مِنْهُ تُوقِدُونَ

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَادِرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۚ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ

**"Na ametupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atayeihuisha mifupa nayo imemung'unyuka. Sema:**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 121 1/13/2017 3:33:24 PM

**Ataihuisha aliyeiumba mara ya kwanza. Na Yeye ni Mjuzi wa kila uumbaji. Yeye ambaye aliwajaalia moto kutokana na mti wa kijani nanyi mkawa mnauwasha. Kwani aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwa nini? Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kinakuwa." (Sura Yasin; 36:78 -82).**

Na katika siku hizo ambazo sanaa ya uchoraji na kunasa sauti haikuwepo, hakika Qur'ani Tukufu imesema kuhusu kazi za mwanadamu: "Siku hiyo itahadithia habari zake. Kwa sababu Mola wako ameipa wahyi." (Sura Zilzalah; 99:4-5).

Na wakati mwingine yanakuja mazungumzo kuhusu ushahidi wa mikono na miguu: "Leo tunaviziba vinywa vyao, na iseme Nasi mikono yao, na itoe ushahidi miguu yao." (Sura Yasin; 36:65). "Na wataziambia ngozi zao: Kwa nini mmeshuhudilia? Zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu ambaye ametamkisha kila kitu." (Sura Fuswilati; 41:21).

Hakika thamani ya maarifa na utukufu wa madhumuni yake, na vile utwahara na usafi wa maarifa haya kutokana na ukhorafi inabainika wakati tunapolinganisha baina yake na baina ya Taurati na Injili zilizopotoshwa. Mfano tunaona inayoyasema Taurati na Injili kuhusu kuumbwa Adamu, na inayoyasema Qur'ani katika hilo. Inayoyasema Taurati juu ya visa vya Manabii na inayoyasema Qur'ani Tukufu, na namna gani Taurati na Injili inamwelezea Mwenyezi Mungu, na namna gani Qur'ani inavyomwelezea? Hapo inadhihirika kabisa sura ya utofauti.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Ni zipi sifa mahususi za mazingira ambayo Qur'ani Tukufu imedhihiri humo?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 122 1/13/2017 3:33:24 PM

2. Nini athari ambayo wameiacha waabudu masanamu katika fikra za watu katika zama hizo?
3. Nini tofauti baina ya tauhidi ya kimaumbile na tauhidi ya kutoa ushahidi?
4. Nini mantiki ya Qur'ani katika kumweleza Mwenyezi Mungu Mtukufu na kubainisha sifa Zake?
5. Namna gani inawezekana kufahamu kwa sura bora zaidi kwa mustawa wa Qur'ani Tukufu?

# SOMO LA NANE:

**Qur'ani Tukufu na uvumbuzi wa kielimu leo:**

Katika ambayo hakuna shaka humo ni kwamba Qur'ani Tukufu sio kitabu cha elimu ya mazingira au tiba au elimu ya nafsi au elimu ya hesabu. Qur'ani ni Kitabu cha kuongoza na kumjenga mwanadamu, na wala haukosekani wasila katika njia hiyo. Sisi ni wajibu tusitegemee Qur'ani Tukufu kuwa ni duara la maarifa la elimu mbalimbali, bali ni wajibu kutaka kutoka katika Qur'ani nuru na imani, uongofu, uchamungu, ubinadamu, tabia njema, nidhamu na kanuni nayo inakusanya yote hayo.

Lakini Qur'ani Tukufu na kwa kufikia lengo hili, inaashiria kwenye baadhi ya mas'ala katika elimu ya mazingira na siri za kuumba na maajabu ya ulimwengu wa uwepo, hususani utafiti wa tauhidi kwa namna itakayoafikiana pamoja na hoja za utaratibu, kiasi kwamba inaondoa pazia kuhusu siri za ulimwengu wa kuumba, na kubainisha mas'ala na kadhia ambazo hazikuwa zinafahamika hata kwa wataalamu wa zama hizo. Na tafsiri hii na ubainifu wa Qur'ani inatengeneza kundi ambalo sisi tunaliita miujiza ya Qur'ani ya kielimu. - Na hapa tunaashiria kwenye baadhi ya miujiza ya kielimu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 123 1/13/2017 3:33:24 PM

**Qur'ani na kanuni ya nguvu ya mvutano:**

Kabla ya Neuton hapakuwa na yeyote aliyevumbua kanuni ya nguvu ya mvutano ya jumla kwa sura kamilifu. Na ni maarufu kwamba Neuton alikuwa amekaa chini ya mti wa mtufaha, tufaha likaanguka kutoka mtini, juu ya ardhi, na tukio hili dogo na jepesi lilishughulisha fikra yake kwa muda mrefu: Ni nguvu gani imevuta tufaha kuja chini? Kwa nini tufaha halikwenda juu angani?

Na baada ya miaka ikagunduliwa kanuni ya nguvu ya mvutano.

Na katika mwanga wa uvumbuzi wa kanuni hii umethibiti mpangilio wa mfumo wa jua. Kwa nini dunia hii kubwa inazunguka jua katika mzunguko wake? Na kwa nini haikimbii na kuwa mbali, na kila moja kwenda upande kati ya pande zilizopo? Na kwa nini haiwi moja baada ya nyingine katika mstari mmoja? Ni nguvu gani hii ambayo inazifanya ziogelee katika mhimili wake makini na mahususi bila kutoka hata kidogo?

Ndio, hakika Neuton amevumbua kwamba harakati ya mwili inapelekea kukimbia na kuwa mbali, na kanuni ya mvutano inapelekea kuvuta mwili kwenye kipenyo. Wakati nguvu hizi mbili zinapokuwa katika hali ya mvutano zinazalisha kwa haraka harakati ya mzunguko, nguvu ya mvutano na kusukuma kutoka katika kipenyo cha nguvu ya mvutano, hakika uwiano huu unaopatikana unaruhusu mwili kuzunguka katika mhimili wake maalum.

Lakini Qur'ani Tukufu kabla ya Neuton kwa miaka elfu moja ilieleza hilo katika Aya ya pili katika Surat ar-Ra'ad ambapo inasema:

اللَّهُ الَّذِي رَفَعَ السَّمَاوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۖ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۖ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۖ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُسَمَّى ۚ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ

**"Mwenyezi Mungu ndiye aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona; kisha akatawala kwenye Arshi na amelitiisha Jua na Mwezi, kila kimoja kinaendelea mpaka muda uliotajwa. Anayapanga mambo anapambanua ishara, ili mpate kuwa na yakini….." (ar-Ra'd; 13:2).**

Na imepokewa katika hadithi ya Imamu Ali bin Musa Ridhaa عليه السلام mwisho wa Aya hii: "Je, Mwenyezi Mungu si anasema 'bila ya nguzo mnazoziona?' Nikasema ndio, akasema (a.s.): Ametaja nguzo lakini hamzioni!!" Je, kuna maneno yaliyo wazi na mepesi katika fasihi ya kiarabu, ya kubainisha nguvu ya mvutano baina ya watu kuliko ibara ya 'nguzo msizoziona?'

Imekuja katika hadithi ya Amirul-Muuminina Imamu Ali عليه السلام: "Hizi nyota ambazo zipo katika mbingu ni miji kama miji iliyopo ardhini, kila mji umefungwa katika nguzo ya nuru."

Wataalamu wa leo wanakiri kuwepo mamilioni ya nyota miongoni mwa nyota za mbinguni ambamo humo kuna viumbe hai na vyenye akili, pamoja na kwamba ufafanuzi bado haujavumbuliwa.

## Kuvumbuliwa kwa harakati ya ardhi kuzunguka yenyewe na kulizunguka jua:

Ni maarufu kwamba mtu wa kwanza kuvumbua harakati ya ardhi ya kujizungusha yenyewe ni Galileo Galilei Mtaliani, kabla ya karne nne, na kabla yake wataalamu katika ulimwengu walikuwa ni watiifu kwa nadharia ya Ptolemy mtaalamu wa zamani ambaye alikuwa anasema: Hakika ardhi ndio kipenyo cha ulimwengu na kwamba sayari zingine zote zinalizunguka.

Hakika kukanusha Galileo Galilei kwa uvumbuzi wake wa kielimu, na alinusurika na mauti alipotangaza toba yake na kujuta kwake kwa uvumbuzi wake, lakini pamoja na hayo hakika wataalamu wengine walifuatilia nadharia zake. Na leo mas'ala haya yamekuwa ni



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 125 1/13/2017 3:33:25 PM

maudhui ya kawaida ya kielimu, na hata kwa majaribio ya kihisia vile vile inawezekana kuthibitisha hayo kwamba ardhi inazunguka katika mhimili wake, na baada ya safari za angani imewezekana kuthibitisha mas'ala katika uhalisia.

**Muhtasari:** Ilikataliwa kuwa ardhi ni kipenyo. Inajulikana kwamba ni kosa la kihisia kutoka kwetu, ambapo tunachanganya kati ya harakati ya ardhi pamoja na harakati za kundi la sayari, nyota na sayari zingine, ambapo sisi katika harakati tunajaalia kwamba zinaizunguka ardhi.

Kwa vyovyote iwavyo, nadharia ya Ptolemy imeangazia kwa mwanga wake katika fikra za wataalamu kwa muda wa miaka elfu moja na mia tano, na kabla ya kudhihiri Qur'ani hapakuwa na yeyote aliyejasiri kukhalifu nadharia hiyo.

Na tunaporejea aya za Qur'ani tunaona Aya ya 88 katika Sura Namli inasema:

وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسَبُهَا جَامِدَةً وَهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ ۚ صُنْعَ اللَّهِ الَّذِي أَتْقَنَ كُلَّ شَيْءٍ ۚ إِنَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَفْعَلُونَ

**"Na unaiona milima unadhania imetulia nayo inakwenda mwendo wa mawingu. Ni sanaa ya Mwenyezi Mungu aliyekitengeneza vizuri kila kitu. Hakika Yeye ana habari za mnayoyatenda."**

Aya hii inazungumzia Aya za Qur'ani kuhusu mwendo wa milima wakati ambapo tunaitakidi sote kwamba imetulia. Na kufananisha mwendo wake na mwendo wa mawingu hakika ni dalili ya juu ya mbio na utulivu bila ya kelele. Na kama tunaangalia badala ya mwendo wa ardhi msemo wa mwendo wa milima hakika ni kudhihirisha utukufu wa maudhui, kwa sababu ni jambo la kawaida kwamba milima haitembei bila ya ardhi ambayo ipo pembezoni mwake. Mwendo wake ndio kiini cha mwendo wa ardhi yenyewe,



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 126 1/13/2017 3:33:25 PM

mzunguko katika mhimili wake na kulizunguka jua au yote mawili kwa pamoja.

Na sasa hivi fikiria kwamba sehemu zote za kielimu katika zama ambayo walikuwa wanaitakidi humo kwamba ardhi imetulia, na kwamba mwendo wa jua na sayari zote hakika zinaizunguka, je, haitoshi mazungumzo juu ya mwendo wa ardhi kwa uwazi huu kwamba ni muujiza wa kielimu? Haya, tunapojua kwamba hayo yamekuja kutoka kwa mtu ambaye hajasoma na amedhihiri katika mazingira ambayo hapakuwepo humo madarasa na vipindi vya kusoma na inazingatiwa kuwa ni katika jamii zisizoendelea, kielimu na kiutamaduni, je waraka huu si uthibitisho wa Kitabu hiki cha mbinguni?

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Nini makusudio ya miujiza ya kielimu katika Qur'ani Tukufu?

**2.** Ni nani mtu wa kwanza ambaye amevumbua kanuni ya nguvu ya mvutano, na alikuwa anaishi katika zama gani?

**3.** Katika Aya gani na kwa maneno gani Qur'ani Tukufu imezungumzia juu ya nguvu ya mvutano?

**4.** Nadharia ya kutulia ardhi ni ya nani, na kwa muda gani imebakiwa ikitawala miongoni mwa watu? Na nani amevumbua kuzunguka kwa ardhi?

**5.** Ni katika Aya gani Qur'ani Tukufu imezungumza kuhusu kuzunguka kwa ardhi na kwa maneno gani?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 127 1/13/2017 3:33:25 PM

# SOMO LA TISA:

**Waraka mwingine juu ya haki ya Nabii wa Uislamu ﷺ:**

Hakika sisi ili tuwe na uhakika katika madai ya mtu kudai unabii, au uongo wake, tuna njia nyingine isiyokuwa ya kumtaka alete muujiza, nayo ni dalili hai ya kufikia kwenye lengo, nayo ni kusoma vielelezo vifuatavyo:

1. Sifa za kitabia na historia yake kijamii.
2. Mazingira ya nyakati.
3. Malengo ya wito wake.
4. Ratiba ya utekelezaji na njia za kufikia kwenye lengo.
5. Upeo wa kuathiri katika mazingira.
6. Upeo wa imani na kujitolea kwa mwenye daawa katika njia ya lengo.
7. Kutokuwa na suluhu mbele ya wanaofanya uovu.
8. Uharaka wa kuathiri katika rai kuu.
9. Kusoma imani ya watu walimwamini, na wao ni wako katika tabaka lipi?

Hakika sisi kama tukisoma mas'ala haya kumi kwa makini kwa mwenye kudai unabii, hakika sisi tunaweza wakati huo, kwa uhakika kugundua ukweli na uongo wa yule mtu. Kwa kuangalia yaliyotangulia hakika sisi tutafanya utafiti mfupi kuhusu mas'ala yaliyotajwa kuhusiana na shakhisiya ya Nabii wa Uislamu ﷺ, pamoja na kwamba kusherehesha hayo inahitajia mijaladi mingi:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 128 1/13/2017 3:33:25 PM

**1.** Hakika ni kitu cha kawaida kwetu katika sifa za maadili ya Nabii wa Uislamu ﷺ kupitia shughuli zake za kijamii, kama ilivyopokewa katika vitabu vya historia vilivyoandikwa na marafiki na maadui, kwamba ﷺ ni mkweli na mwaminifu kiasi kwamba alipewa lakabu katika zama ya ujahiliya kwa jina la mkweli, mwaminifu, historia inatuambia: Hakika yeye ﷺ alipotaka kuhama kwenda Madina alimwamuru Ali عليه السلام arejeshe amana zilizowekwa kwake kwa wenyewe. Kama ambavyo inawezekana kuangalia ushujaa wake na msimamo wake na tabia yake njema na usamehevu wake, utu wake, kujitolea kwake kupitia vita vya Kiislamu, hususan alipoamuru msamaha wa jumla kwa watu wakati wa ufunguzi wa Makka na maadui kujisalimisha katika Uislamu, na huu ni uthibitisho hai katika sifa hizi.

**2.** Sote tunajua kwamba watu wa kawaida, hata werevu miongoni mwao wanachukua tabia ya jamii yao, bila shaka hayo yanaendana na jinsi walivyoathirika na jamii hiyo. Na sasa hivi tufikirie mtu ameishi miaka arobaini katika jamii inayosifika kwa ujahili na ibada ya masanamu. Na utamaduni wake umejengeka katika shiriki na ukhorafi. Namna gani inawezekana mfano wa mtu huyu kuzungumza kuhusu tauhidi halisi, na kusimama mbele ya muonekano wote wa shiriki? Na vipi inawezekana kudhihirisha uwazi wa kielimu katika mazingira yote ya ujahili? Je, inawezekana kukubali muonekano kati ya muonekano wa ajabu bila ya kuungwa mkono na Mwenyezi Mungu nyuma ya mazingira?

**3.** Kwanza ni wajibu kuangalia katika zama aliyodhihiri huyu Nabii! Katika zama ambayo ulimwengu ulikuwa uko katika zama za kati, zama za ukandamizaji, mfarakano, ubaguzi wa dhulma na tabaka la ubaguzi, ni bora kusikia hayo



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 129 1/13/2017 3:33:25 PM

kutoka katika ulimi wa Amirul-Muuminina Imamu Ali عليه السلام ambaye ameshuhudia hatua za Uislamu na kabla yake. Na sasa hivi fikiria dini nembo yake ni usawa baina ya binadamu, na kuondoa mfarakano, ubaguzi na tabaka "Hakika waumini ni ndugu," inanasibiana vipi pamoja na mazingira ya zama hiyo?

**4.** Na madhumuni ya daawa yake صلى الله عليه وآله وسلم ni tauhidi katika nyanja zote na kuondoa upendeleo wa kidhalimu, wa kiubaguzi na kuunganisha ulimwengu wa kibinadamu, na kupiga vita dhulma na ukandamizaji na kutangaza serikali ya kiulimwengu na kutetea wanyonge na kukubali uchamungu na utwahara, amana kama sifa ya maadili ya ubinadamu na binadamu.

**5.** Na katika nyanja ya vipindi vya utekelezaji, haijaruhusu kabisa kusingizia wasila kwa ajili ya lengo, bali alikuwa anafuata njia zilizoendelea ili kufikia lengo tukufu, na anasema kwa uwazi "Wala usiwazuie uovu wa watu kufanya uadilifu" (Sura al- Maidah: 8). Na dalili juu ya jambo hili ni kwamba alikuwa analingania kuchunga misingi ya tabia njema kupitia katika vita na kutowagusa wasiokuwa wapiganaji kutokata kuchoma au kuharibu mitende na miti, kutochafua maji na kudhihirisha upendo kwa mateka wa kivita na makumi miongoni mwa hayo.

**6.** Hakika kuathiri daawa ilikuwa ni kwa kiasi kwamba maadui walikuwa wanaogopa kuwasogelea watu kwa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم kwa sababu athari na nguvu yake kwa wengine ilikuwa ni kubwa sana. Na walipokuwa wanaanzisha zogo na fujo ili watu wasisikilize maneno yake mazuri na yenye kuathiri, ambapo alikuwa anazikonga nyoyo zenye kiu, ili kufunika nguvu yake ya kimuujiza, basi walimwita mchawi na



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 130 1/13/2017 3:33:25 PM

kwamba maneno yake ni uchafu. Na haya kwa dhati yake ni kukiri kwa kimadhumuni athari ya ajabu ambayo daawa yake ilikuwa inaiacha.

**7.** Hakika kujitolea kwake katika njia ya daawa inaonyesha juu ya kwamba alikuwa anaamini zaidi katika daawa hii kuliko kila kitu. Katika baadhi ya nyanja za mapigano, Waislamu walipokimbia alibakia ﷺ yuko imara, na maadui walikuwa wanaamiliana naye kwa njia mbalimbali kwa njia ya kumpa tamaa na kumtisha. Lakini yeye hakujali mas'ala yote hayo bali alibakia imara katika msimamo wake na hakudhoofika wala kusitasita.

**8.** Walifanya juhudi mara nyingi kuzungumza naye au kumpotosha, lakini yeye hakujisalimisha abadani na alikuwa anasema: "Kama wataliweka jua kuliani kwangu na mwezi kushotoni kwangu ili niache jambo hili sitoliacha kamwe."

**9.** Sio tu kuathiri kwa daawa yake ilikuwa ni kukubwa baina ya safu za watu, na kwamba ilisambaa kwa haraka miongoni mwao, watu ambao walisoma vitabu vya *mustashiriqina* katika nyanja za Kiislamu waliona mshangao wa hawa *mustashiriqina* katika kudhihiri na uharaka wa kuenea Uislamu. Kwa mfano watatu kati ya wataalamu wa kimagharibi ambao wameandika *Tarikhul-Hadhwarati al-Arabiyati fil-Shariq* walitangaza wazi ukweli huu: "Hakika yeye pamoja na juhudi ambayo ameitoa ili kujua uharaka wa kuenea Uislamu katika Ulimwengu, na kwamba aliweza katika muda mchache chini ya karne moja kufunika sehemu kubwa katika ulimwengu wenye ustaarabu na wenye maendeleo katika zama hiyo, na mas'ala haya yamebakia hayafahamiki kwa *mustashiriqina*."



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 131 1/13/2017 3:33:25 PM

Ndio, ni kweli haifahamiki, namna gani Uislamu uliweza kwa wasila wa zama hiyo kuenea kwa haraka hiyo, na kujizatiti katika nyoyo za mamilioni na kushinda ustaarabu uliyokuwepo na kuleta ustaarabu mpya!

**10.** Na mwisho tunafikia kwamba hakika maadui walikuwa ni kundi la viongozi makafiri na shari na wenye kiburi, madhalimu na matajiri, wakati ambapo waumini aghlabu walikuwa ni katika vijana wenye nia njema. Na sehemu kubwa miongoni mwao walikuwa ni katika mafakiri wasiokuwa na kitu, bali na hata miongoni mwa watumwa, ambao hawamiliki isipokuwa nyoyo safi na wenye kiu ya haki.

Katika mkusanyiko wa masomo haya ambayo kwa hakika ni marefu na mapana, tunaweza kutoka na natija kwamba ilikuwa ni daawa ya Mwenyezi Mungu inatoka nyuma ya mazingira kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ili kumuokoa binadamu na ufisadi, kupotea, ujahili, shiriki na dhulma.

# TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Je, tunayo njia nyingine ya kuthibitisha haki ya Nabii ﷺ isipokuwa muujiza? Njia hiyo ni ipi?

**2.** Nini makusudio ya kukusanya viambatanisho? Na kabla ya kila kitu ni wajibu kutafakari katika jambo lolote?

**3.** Je, inawezekana kutoa natija ya kitu katika kulinganisha baina ya hali ya Waarabu kabla na baada ya Uislamu?

**4.** Fafanua unayoyajua kwa Waarabu na ulimwengu kwa ujumla katika zama za ujahili.

**5.** Kwa nini maadui wametuhumu Uislamu na Nabii wa Uislamu ﷺ kwa uchawi?

# SOMO LA KUMI:

**Nabii wa Mwisho**

**Dhana sahihi ya Nabii wa mwisho:**

Nabii wa Uislamu ﷺ ndio mwisho wa Manabii na Mitume, na vivyo hivyo mlolongo wa unabii unahitimishwa kwake. Na hii ni katika dharura ya dini ya Uislamu. Maana ya 'dharura' ni kwamba kila atakayeingia katika safu za Waislamu atafahamu kwa haraka kwamba Waislamu wote wanaamini hivyo na kwamba ni wazi na ni kawaida kwao. Yaani kila anayeungana na Waislamu anajua kwamba wao kidini wanatia mkazo juu ya msingi wa tauhidi na wanajua kwamba Waislamu wanaafikiana katika yanayohusu kuhitimishwa unabii kwa Nabii Mtukufu ﷺ, na kwa hiyo hapatikani Mwislamu yeyote anayesubiria kuja kwa Nabii mpya.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 133 1/13/2017 3:33:25 PM

Kwa hakika msafara wa binadamu umekata masafa makubwa moja baada ya mengine katika mwendo wake wa ukamilifu, na umefikia katika hatua ya kustawi na kukamilika kiasi kwamba unaweza kujitegemea wenyewe. Yaani hakika unaweza kunufaika na mafunzo makuu ya Kiislamu katika kutatua matatizo. Na kwa maneno mengine: Hakika Uislamu ni kanuni ya mwisho na yenye kukusanya hatua ya kupevuka kwa mwanadamu, nao katika itikadi unakusanya malengo kamilifu ya kidini, na katika matendo wao wamejipanga kiasi kwamba unaafikiana na mahitaji ya mwanadamu katika kila zama na sehemu.

**Dalili juu ya mwisho wa unabii wa Nabii Mtukufu ﷺ:**

Katika kuthibitisha hayo tunazo dalili nyingi, muhimu zaidi na zilizo wazi zaidi ni tatu:

1. Ulazima wa mas'ala haya: Tumesema hakika kila mwenye mawasiliano na Waislamu katika sehemu yoyote kati ya sehemu za ulimwengu, anajua kwamba wao wanaitakidi kuhitimishwa unabii kwa Nabii wa Uislamu ﷺ na hivyo mtu akikubali Uislamu kwa njia ya dalili na mantiki inayotosheleza, hakika hatamiliki isipokuwa msingi wa hitimisho hili. Na kwa kuwa sisi tumethibitisha katika masomo yaliyopita haki ya dini hii kwa dalili ya kutosheleza, hakika ni wajibu juu yetu kukubali msingi wa hitimisho pia, kwa sababu ni katika dharura ya dini hii.
2. Aya za Qur'ani Tukufu vile vile ni dalili ya wazi juu ya mwisho wa unabii wa nabii wa Uislamu ﷺ, miongoni mwazo ni:

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَٰكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 134 1/13/2017 3:33:25 PM

**"Muhammad hakuwa ni baba wa mmoja kati ya wanaume wenu lakini ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Manabii." (Sura al- Ahzab: 40).**

Maneno haya yameenea katika wakati ambao ilitolewa kadhia ya kujengea baina ya Waarabu, ambapo walikuwa wanamjengea mtu kutoka kwa wazazi wengine na wanamfanya kuwa ni mtoto wao, na anaingia katika familia kama mmoja wao, na anakuwa ni mahramu na anarithi. Lakini Uislamu umekuja kufuta mila hii ya kijahiliya na ukasema: Hakika wenye kujengewa hawapati haki ya kisharia ya mtoto halisi wa kisharia na miongoni mwa hawa ni Zayd ambaye Mtume wa Uislamu ﷺ alimjengea, hivyo hazingatiwi kuwa ni mtoto wa Mtume Mtukufu ﷺ. Na kwa hili Aya inaashiria kwamba badala ya kumwita Mtume, baba wa mtu yeyote basi mwiteni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Manabii. Hakika maneno haya yanaonyesha juu ya umwisho wa unabii wa Nabii Mtukufu ﷺ kama ambavyo ujumbe wake uko wazi na ni thabiti kwa wote.

Swali pekee ambalo linabakia hapa ni: Nini maana halisi ya mwisho?

Neno *Khaatami* linatokana na neno *khatam* yaani mwisho, ambalo linahitimisha na kumaliza kazi, mfano kuweka muhuri katika mwisho wa barua. Na ikiwa ni pete ambayo inavaliwa mkononi na kuwekwa kwenye kidole huitwa *Khaatam* ni kwa sababu ilikuwa inatumika kugongea muhuri katika barua ambapo ilikuwa inabeba jina la mwenye pete.

Tunasoma katika riwaya za Kiislamu: Hakika Mtukufu Mtume ﷺ alipokuwa anataka kutuma barua kwa mmoja wa Wafalme au watawala katika zama hizo na kumlingania katika Uislamu, aliambiwa ﷺ hakika watawala wasiokuwa Waarabu hawakubali barua isiyopigwa muhuri. Na Mtume ﷺ alikuwa anatuma barua bila ya kui-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 135 1/13/2017 3:33:25 PM

piga muhuri. Akaamuru wamtengenezee muhuri wenye maandishi haya '*Laa ilaaha illa llahu, Muhammad Rasulullahi'*, kisha akaamuru barua zake zigongwe muhuri huo. Na hivyo maana ni kwamba yeye ndio hitimisho la mlolongo wa Manabii.

Imekuja katika hadithi aliyoipokea Jabir bin Abdillahi al-Answariy kutoka kwa Nabii ﷺ amesema: "Hakika mfano wangu katika Manabii ni mfano wa mtu aliyejenga nyumba akaikamilisha, na akaitengeneza vizuri isipokuwa sehemu ya tofali moja, na anayeingia anaangalia humo anasema: Ni nzuri ilioje isipokuwa nafasi ya tofali hili." Akasema ﷺ: "Mimi ndio sehemu ya tofali, Manabii wamehitimishwa kwangu." Ameipokea Bukhari na Muslimu katika *Sahihi* zao. Imenukuliwa kutoka kwenye *al-Mizan* ya Twabatwabai, Juzuu 16, uk. 327, Chapa ya Ismailiyaan.

Na amesema Imamu as-Sadiq عليه السلام: "Halali ya Muhammad ni halali hadi Siku ya Kiyama na haramu yake ni haramu hadi Siku ya Kiyama."

Na kuna hadithi maarufu kwa Shia na Sunni ambayo imenukuliwa kutoka kwa Nabii Mtukufu ﷺ kwamba alimwambia Imamu Ali عليه السلام: "Wewe kwangu una daraja ya Haruna kwa Musa isipokuwa hakuna nabii baada yangu." Kuna maswali kuhusu kuhitimisha unabii kwa Nabii Mtukufu ﷺ ambayo ni lazima tuyazingatie:

**1.** Baadhi wanasema: Ikiwa kuletwa Manabii ni rehema kubwa ya Mwenyezi Mungu, hivyo kwa nini mwanadamu wa zama zetu ananyimwa rehema hii kubwa? Na kwa nini haji Nabii ili kuwaongoa na kumwongoza mwanadamu wa zama hii? Hakika ambao wanaulizana maswali haya wanasahau uhakika kuhusu nukta, nayo ni kunyimwa zama zetu si kwa sababu wao, yaani watu, hawastahiki hayo, bali ni kwa sababu msafara wa binadamu umeshafikia hatua katika



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 136 1/13/2017 3:33:25 PM

mwendo wake wa kifikra na uelewa wake kiasi kwamba unaweza kwenda kwa uliyonayo miongoni mwa mafunzo ya Nabii Mtukufu ﷺ.

Hakuna ubaya kuleta mfano hapa:

Hakika manabii Ulul-Azmi yaani ambao wana dini mpya na kitabu cha mbinguni ni watano: Nuhu, Ibrahim, Musa, Isa na Nabii wa Uislamu Muhammad ﷺ. Kila mmoja miongoni mwao ametekeleza wajibu wake maalum wa kihistoria kwa kuongoza watu, na amejitahidi katika ukamilifu wao, na alikuwa kila mmoja miongoni mwao anatumia kiasi fulani cha wakati ili kuacha hatua inayofuata kwa Nabii mwingine miongoni mwa Ulul-Azmi, hadi msafara huu ukafikia hatua ya mwisho, kama vile mwanafunzi ambaye anasoma hatua za masomo hadi anafikia hatua ya mwisho na kuhitimu, pamoja na kuchukua mazingatio kwamba mas'ala ya kusoma hayamaliziki abadani, ambapo kuna hatua ya msingi, ya kati, sekondari, chuo kikuu kisha hatua ya udaktari. Ikiwa anayepata daraja ya udaktari haendi chuo kikuu, hii haimaanishi kwamba hastahiki hayo, bali ni kwa sababu anayo maarifa ambayo anaweza kupitia kwayo kutatua matatizo yake ya kielimu, na aendelee kuyasoma.

**2.** Pamoja na kwamba jamii ya kibinadamu iko katika hatua ya mabadiliko yenye kuendelea, namna gani inawezekana kanuni za Kiislamu thabiti kutimiza mahitaji ya mwanadamu wa kileo? Jawabu tunasema: Hakika Uislamu una aina mbili za kanuni zenye mlolongo, baadhi yake ni kama vile sifa za mwanadamu. Ni thabiti kama vile ulazima wa kuamini tauhidi, kutekeleza misingi ya uadilifu na kupiga vita aina yoyote ya dhulma, tabia mbaya na uadui. Ama sehemu nyingine ni mlolongo wa misingi ya jumla jumuishi. Inachukua sura na muundo mpya pamoja na mabadiliko yanayojitokeza katika maudhui, na inatimiza mahitaji mbal-

imbali ya kila zama. Kwa mfano tunayo kanuni 'Ni wajibu kutekeleza makubaliano', katika yasiyo na shaka ndani yake ni kwamba kadiri muda unavyokwenda zinadhihirika aina mpya za mikataba na makubaliano yenye manufaa kijamii, makubaliano ya kijamii, kibiashara na kisiasa, hivyo mwanadamu anaweza kushikamana na msingi huu uliotajwa kutimiza mahitaji yake katika nyanja hii.

Na kuna misingi mingine chini ya anwani 'Kanuni ya Kutokukubali Madhara' ambapo kufuatana na kanuni hiyo ni kupinga kila hukumu na kanuni inayosababisha madhara ya mtu au jamii. Mtaona namna gani kanuni hizi za Kiislamu za jumla zinavyotatua matatizo! Kanuni hizi tunazo nyingi katika Uislamu, na kwa kunufaika tunaweza kutatua matatizo magumu baada ya kushinda Mapinduzi ya Kiislamu.

**3.** Hakuna shaka kwamba sisi tunahitaji kiongozi katika mas'ala yetu ya Kiislamu. Pamoja na kutokuwepo Nabii na kughibu kwa khalifa wake, hakika mas'ala ya uongozi yanasimama. Pamoja na hitimisho la unabii na kutotarajia kudhihiri nabii mwingine, je, hiyo si hasara katika jamii ya Kiislamu?

Jawabu tunasema: Katika hatua hii vile vile mas'ala yanachukuliwa kwa mazingatio, ambapo imeshatimia kutatua mas'ala kwa njia ya Wilayatul- Faqihi, ambapo uongozi uko kwa Faqihi mwenye kutimiza masharti na mwenye elimu na fat'wa na rai ya kisiasa katika kiwango cha juu. Na njia ya kumjua mfano wa kiongozi huyu imetajwa kwa uwazi katika kanuni za Kiislamu, ambapo hakuna hofu katika mas'ala haya. Na hivyo hakika Wilayatul-Faqihi ndio mwendelezo wa njia ya Manabii na Mawasii. Hakika uongozi wa Faqihi mwenye kutimiza masharti ni dalili juu ya kwamba jamii za Kiislamu hazikuachwa bila ya kiongozi.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 138 1/13/2017 3:33:25 PM

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Nini maana ya *khatam* kwa sura makinifu?

**2.** Namna gani inawezekana kujua *khatamu* katika Aya za Qur'ani?

**3.** Kwa nini wamenyimwa watu wa zama zetu Manabii wa Mweneyzi Mungu?

**4.** Ni idadi gani ya aina za kanuni za Kiislamu, na namna gani zinatimiza mahitaji ya zama?

**5.** Je, inawezekana jamii ya Kiislamu kuwa bila ya kiongozi? Namna gani yanatatuliwa mas'ala ya uongozi katika zama zetu?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 139 1/13/2017 3:33:25 PM

# 4

# MASOMO KUMI KATIKA UIMAMU

## SOMO LA KWANZA:

**Utafiti wa Uimamu umeanzia wapi?**

Sisi tunajua kwamba Waislamu wamegawanyika baada ya Nabii wa Uislamu ﷺ katika makundi mawili: Kundi moja lilikuwa linaitakidi kwamba Nabii ﷺ hakuteua khalifa baada yake, bali aliacha hilo kwa ummah wake, kukusanyika na kumchagua kiongozi wao, na hawa ni Ahlus Sunna. Kundi lingine lilikuwa linaitakidi kwamba khalifa wa Nabii ﷺ ni wajibu awe maasumu kutokana na makosa na kukosea kama Nabii ﷺ, na awe anayo elimu kubwa ili aweze kusimamia uongozi wa kimaanawi na wa kimada kwa watu, na kuhifadhi Uislamu na kuendelea kwake. Kama ambavyo walikuwa wanaitakidi kwamba kumteua mfano wa mtu huyu haiwezekani isipokuwa kwa njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa njia ya Nabii ﷺ. Kundi hili linaitwa Imamiya au Shia Ithnaasharia.

Hakika lengo letu katika utafiti huu mfupi ni kusoma mas'ala haya kufuatana na dalili za kiakili na kihistoria, na Aya za Qur'ani na Sunnah za Nabii ﷺ. Lakini kabla ya kuingia katika utafiti huu ni wajibu tuashirie kwenye baadhi ya nukta:

**1. Je, utafiti huu unapelekea kuhitalifiana?**

Baadhi wanaopinga wanaposikia mazungumzo juu ya mas'ala ya Uimamu wanashangaa na wanasema: Sasa hivi sio wakati wa ma-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 140 1/13/2017 3:33:25 PM

zungumzo haya! Sasa hivi ni wakati wa Umoja wa Waislamu na kuzungumzia juu ya khalifa wa Nabii ﷺ inapelekea mfarakano na mgawanyiko! Leo tuna adui wa pamoja, ni wajibu tumwangalie; Uzayuni na Ukoloni wa Kimagharibi na Mashariki, na hivyo ni wajibu tuache mas'ala haya ambayo yanapelekea kwenye mfarakano.

**Hakika njia hii ya kufikiria ni ya makosa bila ya shaka:**

**Kwanza:** Hakika utafiti ambao unapelekea kwenye mfarakano na mgawanyiko ndio ule utafiti ambao unategemea kasumba na kutokuwa na mantiki, na kuwa na chuki. Lakini utafiti wa mantiki wenye dalili, ulio mbali na kasumba ya upofu, na ulio katika mazingira yenye kutawaliwa na urafiki wa upendo, sio tu haupelekei kwenye mfarakano bali hakika unapunguza utengano na kutia nguvu nukta za ushirikiano.

Hakika mimi nimefanya ziara sana huko Hijazi kwa kutembelea Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu, na nilikuwa na utafiti mwingi pamoja na maulamaa wa Ahlus Sunnah na nilihisi kama walivyohisi wao, sio tu utafiti huu na mijadala hii haikuwa na athari mbaya juu ya uhusiano wetu, bali umepelekea kufahamiana na kushirikiana zaidi. Kwamba umeondoa utengano baina yetu, kama ambavyo umeondoa hisia zenye shaka, ambazo zinaweza kuwepo. Muhimu ni kwamba utafiti huu unapelekea kuweka wazi, kwamba baina yetu kuna nukta za ushirikiano nyingi tunazoweza kuzitegemea mbele ya adui yetu wa pamoja.

Hakika Ahlus Sunnah wao wenyewe wanagawanyika makundi manne: Hanafi, Maliki, Shafi na Hanbali. Hakika uwepo wa makundi haya haujapelekea mfarakano baina ya Ahlus sunna, na kama hawa wakikubali kwa uchache fikihi ya Shia kwa anwani ya madhehebu ya tano ya fikihi, hakika matatizo mengi na utengano utaondoka.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 141 1/13/2017 3:33:25 PM

Kama ilivyotokea mwishoni, kwamba Mufti Mkuu wa Ahlus Sunna na Mkuu wa chuo kikuu cha Azhar huko Misri, Sheikh Shaltuti alipiga hatua yenye kuathiri na kutangaza rasmi kutambua fikihi ya Shia miongoni mwa Ahlus sunna, na vivyo hivyo aliwasaidia wengi katika kuleta uelewano baina ya Waislamu na kukawa na mafungamano baina yake na Marja mkubwa Ayatollahi Burjurdiy na uhusiano wa urafiki.

**Pili:** Hakika sisi tunaitakidi kwamba Uislamu unafahamika na kuwa wazi katika madhehebu ya Kishia zaidi kuliko madhehebu mengine, pamoja na kwamba tunaheshimu madhehebu yote, isipokuwa ni kwamba madhehebu ya Kishia yanaweza kueleza Uislamu halisi katika nyanja zote kwa sura bora zaidi na kutatua mas'ala yanayoambatana na Serikali ya Kiislamu, kwa nini hatufundishi watoto wetu kwa dalili na mantiki ya madhehebu hii? Hakika sisi kama hatutafanya hivyo, kwa hakika sisi tutakuwa tunawafanyia hiyana!

Hakika sisi tunaitakidi kwamba Nabii ﷺ alikwishamteua khalifa wake, na kuna madhara gani kama sisi tumejadili maudhui haya kwa njia ya mantiki na hoja? Lakini ni wajibu katika utafiti huu tuwe katika tahadhari ya kujeruhi hisia za wengine.

**Tatu:** Hakika maadui wa Uislamu kwa lengo la kuteteresha Umoja wa Waislamu wamewazulia uongo Shia kwa Ahlus sunna. Wamesema uongo na wamewatuhumu Ahlus Sunna kwa Shia hadi kwamba wao wameweza katika baadhi ya nchi kumuweka mbali mmoja wao na mwingine.

Hakika sisi wakati tunaeleza mas'ala ya uimamu kwa njia ambayo tumeitaja, na tunapofafanua nukta ambazo wanazisisitiza Shia kwa hoja ya Kitabu na Sunnah, hapo inafahamika kwamba hayo madai si kingine isipokuwa ni uongo, na kwamba adui yetu wa pamoja amesambaza sumu miongoni mwetu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 142 1/13/2017 3:33:25 PM

Na kama mfano, hakika mimi sisahau katika ziara ya Hijazi ambapo nilikutana na mtu kati ya watu wa dini wenye kujulikana sana Saudia, na tulijadiliana, aliniambia: "Hakika Shia wana Qur'ani isiyokuwa Qur'ani iliyopo kwao." Nikashangaa na kumwambia: Hakika ukweli katika mas'ala haya ni mwepesi sana, na hakika mimi nakualika wewe mwenyewe au mwakilishi kutoka kwenu ili usafiri pamoja nasi baada ya kutekeleza ibada ya Umra hadi Iran, na bila ya kuwepo na maandalizi, na inapatikana katika mitaa na vichochoro misikiti mingi, na kunapatikana nakala katika kila nyumba za Waislamu. Na tutakwenda katika msikiti wowote au nyumba yoyote unayotaka na kuwaomba watupe nakala ya Qur'ani Tukufu, na itabainika kwako kwamba hakika sisi hatutofautiani katika neno na hata katika nukta moja. Na hakika nyingi katika nakala za Qur'ani ambazo tunazitumia ni kutoka Hijazi na Misri na dola zilizobakia za Kiislamu.

Hapana shaka kwamba mjadala huu na mazungumzo ya urafiki na yenye kuonyesha dalili yameosha sumu ya ajabu ambayo ilikuwa katika akili ya mmoja ya maulamaa wa dini wenye kujulikana. Makusudio ni kwamba hakika tafiti hizi zinazoambatana na uimamu kwa njia ambayo tumeitaja, zinatia nguvu Umoja wa Jamii ya Kiislamu, na kugundua ukweli na kusaidia katika kupunguza utengano baina ya Waislamu.

## 2. Uimamu ni nini?

Imamu, kama ilivyo maalum katika jina ni kwa maana ya Mkuu na Kiongozi wa Waislamu, na katika itikadi ya Shia hakika jina la Imamu Maasumu anaitwa mtu ambaye anakuwa Khalifa wa Nabii ﷺ katika kila kitu, pamoja na tofauti kwamba Nabii ﷺ ndio mwasisi wa dini, na Imamu ni mtunzaji, na mwaminifu wa dini. Wahyi unateremshwa kwa Nabii ﷺ, na wala hauteremshwi kwa Imamu, bali anachukua mafunzo yake kutoka kwa Nabii ﷺ na anayo elimu ya kipekee.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 143 1/13/2017 3:33:25 PM

Katika mtazamo wa Shia hakika Imamu Maasumu sio kwa maana ya kiongozi wa Serikali ya Kiislamu bali ni kiongozi wa kimaanawi na kimaada, nje na ndani, bali ni kiongozi katika kila kitu katika jamii ya Kiislamu, na mtunzaji wa itikadi na hukumu za Kiislamu bila ya kosa lolote au upotovu wowote na kwamba yeye ni mja mwema aliyechaguliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Lakini Ahlus Sunna hawafasiri uimamu kwa tafsiri hii, bali wanazingatia Imamu ni Rais wa Serikali ya jamii ya Kiislamu. Kwa uzuri zaidi hakika wao wanawazingatia watawala katika zama na sehemu ni Makhalifa wa Nabii ﷺ na ni Maimamu wa Waislamu.

Hakika sisi tutathibitisha katika utafiti ujao kwamba ni wajibu kuwepo katika ardhi na katika kila zama na sehemu, mwakilishi wa Mwenyezi Mungu, Nabii au Imamu Maasumu, ili kuhifadhi dini ya haki na kuongoza waumini. Na ikitokea kwa sababu maalum akatoweka katika macho ya watu hakika wawakilishi kutoka kwake wanakuwa ni manaibu katika kufikisha hukumu na kuunda serikali.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Nini mantiki ya wale ambao wanasema: Leo sio wakati wa utafiti wa uimamu?

**2.** Mbele ya mantiki hii kuna majibu mangapi yapo kwetu katika utafiti huu?

**3.** Namna gani wamesambaza maadui wa Uislamu mfarakano miongoni mwa Waislamu na ni ipi njia ya kutatua hayo?

**4.** Je, unakumbuka mifano ya njia za mfarakano ambazo walizifanya maadui?

**5.** Nini tofauti kati ya maana ya Imamu kwa Shia na kwa Sunni, na kuna tofauti gini baina yao?

# SOMO LA PILI:

## Falsafa ya uwepo wa Imamu:

Hakika kutokana na tafiti ambazo tumezifanya kuhusu dharura ya kutuma Manabii, tumejua kwa kiasi kikubwa juu ya dharura ya uwepo wa Imamu baada ya Nabii ﷺ kwa sababu wao wanashirikiana katika mambo mengi, lakini ni wajibu hapa kuelezea utafiti mwingine.

### 1. Ukamilifu wa kimaanawi sanjari na uwepo wa viongozi wa Mwenyezi Mungu:

Kabla ya kila kitu tunaelekea katika lengo la kuumbwa mwanadamu, nalo ndio lengo la kuumbwa ulimwengu. Nalo linafupisha njia ndefu katika mapito (mawimbi) mengi kuelekea kwa Mwenyezi Mungu. Kuelekea kwenye ukamilifu wa jumla, na kuelekea ukamilifu wa kimaanawi, katika nyanja zote. Na hakuna shaka kwamba haiwezekani kukata njia (masafa) hii bila ya mkuu na kiongozi maasumu na mwalimu wa kimbinguni, kwa sababu kuna giza, na naogopa hatari ya kupotea.

Ni sahihi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amemwandaa mwanadamu kwa nguvu ya akili na werevu, na amempa dhamira na utambuzi wenye nguvu, na ametuma kwake vitabu vya mbinguni. Lakini pamoja na nyenzo zote hizo za kimaumbile na kisharia, anaweza kukosea katika kuainisha njia yake na kutumbukia katika kosa. Na kwa msisitizo, hakika uwepo wa Imamu Maasumu kunapunguza hatari ya kupotoka na kupotea kwa kiasi kikubwa, na vivyo hivyo inakuwa "kuwepo Imamu ni ukamilisho wa lengo la kuumbwa mwanadamu."

Na jambo hili ndilo linaloitwa katika madrasa ya itikadi kwa jina la 'Kanuni ya Huruma', na kusudio lake ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweka chini ya tasarafu ya mwanadamu uweze-



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 145 1/13/2017 3:33:25 PM

kano wote ili afike kwenye lengo, na miongoni mwayo ni kutuma Manabii, na kuwepo Imamu, vinginevyo ingetokea kutengua lengo, tazama hilo vizuri.

**2. Kuhifadhi sharia za mbinguni:**

Sisi tunajua kwamba kuteremka dini za mbinguni katika nyoyo za Manabii kunafanana na kuteremka kwa matone ya maji safi na chemchem ambazo zinahuisha nyoyo. Lakini wakati yanapoteremka katika mazingira machafu na kwenye akili zenye kushindwa na zisizo twahara, hakika matone hayo huanza kuchafuka kidogo kidogo na kuingiliwa na ukhorafi na upotovu, hadi yanapoteza ule uzuri baada ya kupita siku nyingi, na katika hali hii yanakosa ule mvuto wake na athari yake ya kimalezi, na hivyo hayakati kiu ya wenye kiu na wala hayanywesheleza maua mazuri.

Hapa inajitokeza dharura ya kuwepo Imamu Maasumu kama mlinzi wa asili ya dini ili kuhifadhi utaratibu halisi wa kidini, ili kuzuia baina yake na baina ya upotovu na fikra za kuokota na rai zisizo sahihi, dhana na ukhorafi. Na kama dini ikibakia bila ya mfano wa kiongozi huyu hakika katika muda mfupi inakosa asili yake na usafi wake. Na kwa sababu hii anasema Imamu Ali عليه السلام katika moja ya maneno yake katika *Nahjul-Balaghah:*

"Ewe Mwenyezi Mungu, ndio, ardhi haiwi bila ya msimamizi wa Mwenyezi Mungu mwenye kusimamisha hoja, ima awe dhahiri anaonekana au mwenye hofu amefichikana, ili zisibatilike hoja za Mwenyezi Mungu na ubainifu wake."

Kwa hakika moyo wa Imamu عليه السلام unafanana na sanduku madhubuti ambalo linakusanya nyaraka muhimu na kuhifadhiwa kutokana na wezi, na ili libaki limehifadhiwa kutokana na majanga, na hii ni moja ya sababu za dharura ya uwepo wa Imamu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 146 1/13/2017 3:33:25 PM

**3. Uongozi wa kisiasa na kijamii katika ummah:**

Hakuna shaka kwamba kwa jamii yoyote isiyo na utaratibu wa kijamii wala kiongozi, haiwezi kuendelea katika maisha, na kwa sababu hiyo zimeshachagua jamii zote na wananchi kiongozi wake tangu zama za mwanzo. Mara nyingi walikuwa ni wema, na mara nyingine sio wema. Na mara nyingi imetokea kwa sababu ya haja ya ummah kuwa na kiongozi, watawala wamelazimisha nafsi zao kwa nguvu katika ummah na kushika hatamu za mambo. Hii ni kwa upande mmoja, na katika upande mwingine kwa kuwa mwanadamu ili aweze kufikia kwenye lengo la ukamilifu wa kimaanawi ni lazima kukata masafa ya njia hii, ni juu yake akate masafa haya pamoja na kundi na jamii, kwa sababu uwezo wa mtu peke yake ni dhaifu kifikira, kimwili, kimaada na kimaanawi, wakati ambapo uwezo wa kundi ni mkubwa sana.

Lakini ni wajibu kuwepo na utaratibu sahihi katika jamii, ili usaidie katika kukuza vipaji vya mwanadamu, na kupiga vita upotovu, na kuhifadhi haki za watu binafsi na, awe na mkakati wa kufikia kwenye malengo makubwa ya uongozi, kisha kwa kushirikiana kwa juhudi zote katika mazingira huru ya jamii.

Na kwa kuwa mwanadamu mwenye kukosea hamiliki uwezo wa kubeba ujumbe huu mkubwa kama ambavyo sisi tumeshaona kwa macho yetu daima, kupotoka wa watawala wa kisiasa katika ulimwengu kwenye njia ya sawa, hivyo ni lazima kuwepo Imamu maasumu aliyetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ili kuongoza jambo hili, na kuzuia baina ya ummah na upotovu kwa kutegemea nguvu ya ummah na fikra za maulama wema.

Na hii ni sababu nyingine ya dharura ya kuwepo imamu na ni moja ya matawi ya "kanuni ya huruma." Na tunakariri mara nyingine, hakika taklifu ya watu katika zama za kipekee za ghaiba ya

Imamu maasumu ni wazi, na inshaallah tutazungumzia kwa ufafanuzi juu ya hilo kupitia utafiti wa Serikali ya Kiislamu.

### 4. Ulazima wa kutimia hoja:

Hakika nyoyo ni wajibu ziwe zimeandaliwa katika kivuli cha uwepo wa Imamu, na kuendelea katika kukata masafa ya ukamilifu wa jumla, ili kutimia hoja juu ya wale ambao wanakwenda kwa makusudi katika njia ya kimakosa, ili isiwe tahadhari kwao bila ya dalili na bila ya adhabu, ili asitoe hoja yeyote kwa kusema kwamba kama kungekuwepo na kiongozi wa Mwenyezi Mungu wa mbinguni angetuongoza na tusingepotea.

Mwisho hakika njia ya udhuru imefungwa, Na dalili za haki ziko wazi vya kutosha kwa ajili ya kutangaza na kuwaelimisha wajinga na kwa kutia nguvu akili ya wenye uelewa na kuwapa matumaini.

### 5. Imamu ni wasita mkubwa wa rehema ya Mwenyezi Mungu:

Wengi kati ya maulamaa wanafananisha, kulingana na hadithi za Kiislamu, kuwepo Nabii na Imamu katika jamii ya kibinadamu au katika ulimwengu wa uwepo, na uwepo wa moyo katika mwili wa mwanadamu. Na sisi tunajua moyo unapopumua hakika unapeleka damu katika mishipa yote ili kufika kwenye chembe chembe zote na mishipa ili kuilisha.

Na kwa kuwa Imamu maasumu ni mwandamu kamilifu, anaongoza msafara wa mwanadamu, na ni sababu ya kuteremka rehema ya Mwenyezi Mungu, hakika kila mtu anapata kwa kadiri ya mafungamano yake na Nabii au Imamu katika rehema hii, hivyo ni lazima tuseme: Kwa kuwa moyo ni dharura kwa mwanadamu, hivyo hakika kuwepo wasila wa rehema ya Mwenyezi Mungu ni dharura katika mwili wa ulimwengu wa mwanadamu vilevile.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 148 1/13/2017 3:33:26 PM

Pamoja na kujua kwamba Nabii na Imamu hawamiliki wao wenyewe kitu ili kuwapa wengine, kila kilichopo hakika ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini kama ambavyo moyo ni wasila wa rehema ya Mwenyezi Mungu katika mwili, hakika Nabii na Imamu wao ni wasila wa rehema ya Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu vyovyote itakavyokuwa na katika tabaka lolote na kiwango chochote

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Nini nafasi ya Imamu عليه السلام katika ukamilifu wa kimaanawi kwa mwanadamu?
2. Kwa njia gani Imamu anakuwa ni mwenye kuhifadhi sharia?
3. Nini nafasi ya Imamu katika mas'ala ya uongozi wa serikali na utaratibu wa kijamii?
4. Nini maana ya kutimiza hoja? Na nini nafasi ya Imamu katika nyanja hii?
5. Nini wasila wa rehema? Na ni upi mfano bora zaidi kwa Nabii na Imamu katika nyanja hii?

## SOMO LA TATU:

### Masharti na mazingira maalum ya Imamu:

Kabla ya kila kitu inadhihiri hapa nukta ambayo ni wajibu kuizingatia, nayo ni: Hakika tunafahamu kutoka katika Qur'ani Tukufu kwa sura nzuri kwamba cheo cha Imamu ni cheo kikubwa anachoweza kukifikia mwanadamu, ni kikubwa kuliko cheo cha unabii na utume,



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 149 1/13/2017 3:33:26 PM

kwa sababu sisi tunasoma yafuatayo katika kisa cha Ibrahimu Khalili mvunja masanamu ﷷ:

وَإِذِ ابْتَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ رَبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۖ قَالَ إِنِّي جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۖ قَالَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِي ۖ قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِي الظَّالِمِينَ

**"Na Mola Wake alipomjaribu Ibrahim kwa matamko, naye akayatimiza. Alimwambia: Hakika mimi nimekufanya Imamu wa watu. Akasema: Na katika kizazi changu (pia)? Akasema: Ahadi yangu haiwafikii madhalimu." (Sura al-Baqarah; 2:124).**

Na vivyo hivyo Ibrahim ﷷ anakuwa baada ya kukata masafa ya unabii na utume na kunusurika katika hatua ya mitihani mbalimbali ya Mwenyezi Mungu, anafikia kwenye cheo kikubwa, cheo cha Uimamu wa dhahiri na siri, kimada na kimaanawi.

Na Nabii wa Uislamu ﷺ vilevile alikuwa nacho, ukiongezea na cheo cha unabii na utume alikuwa na cheo cha uimamu na uongozi kwa watu, na vilevile cheo hiki walikuwa nacho baadhi ya Manabii pia. Hii ni katika upande mmoja, na katika upande mwingine sisi tunajua mazingira na masharti na sifa za lazima ili kufikia katika cheo kinachonasibiana na wajibu wa majukumu ambayo anayabeba huyu mtu. Inamaanisha kwamba kila kinapopanda cheo basi majukumu yanakuwa ni makubwa zaidi.

Mfano, katika Uislamu, hakika kila mtu anayepata cheo cha ukadhi au kutoa ushahidi, Uimamu wa jamaa, ni lazima awe mwadilifu. Hakika uadilifu ni dharura kwa mwenye kutoa ushahidi au anasyeoma Sura Alhamdu na Ikhilasi katika Swala ya jamaa. Ni wazi masharti ambayo ni wajibu kutimia kwa mtu ili kupata cheo cha Uimamu ni muhimu sana. Kwa kila hali, hakika masharti ya lazima ambayo ni wajibu yatimie kwa Imamu ni:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 150 1/13/2017 3:33:26 PM

**1. Umaasumu kutokana na kosa na kukosea:**

Imamu ni kama Nabii, ni wajibu awe ni maasumu, yaani kahifadhiwa kutokana na makosa na kukosea, vinginevyo asingeweza kuwa ni kigezo, mfano na kiongozi kwa watu na mahala pa tegemeo la jamii. Imamu ni wajibu atawale nyoyo na roho za watu, na amri zake ziwe ni zenye kupita bila ya kusitasita. Na mwenye kuchafuka kwa makosa hawezi kuwa ni mahala pa kukubalika, tegemeo na tumaini la watu. Hakika mwenye kufanya kosa na kukosea wakati wa maisha yake ya kila siku namna gani inawezekana kumtegemea katika kazi za jamii na kuchukuliwa rai zake?

Hapana shaka kwamba Nabii ni wajibu awe maasumu, na sharti hili kwa dalili ambayo tumeitaja ni wajibu lipatikane kwa Imamu. Na inawezekana kuthibitisha hayo kwa njia nyingine, hakika 'Kanuni ya Huruma' ambayo ndio msingi wa kuwepo Nabii na Imamu hakika inawajibisha sifa hii vilevile. Kwa sababu malengo ya kuwepo Nabii na Imamu hayawezi kutimia bila ya cheo cha umaasumu, kama ambavyo sababu ambazo tumezitaja katika masomo yaliyotangulia zitabakia kuwa ni pungufu.

**2. Elimu nyingi:**

Imamu ni kama Nabii, yeye ni kimbilio la watu la kielimu, hivyo ni wajibu awe anajua misingi yote na matawi ya dini, dhahiri na siri ya Qur'ani Tukufu, na Sunnah ya Nabii, na yote yanayoambatana na Uislamu kwa sura kamilifu, kwa sababu ni mhifadhi, mlinzi wa sharia, kiongozi na mwalimu wa watu. Na kwamba watu ambao wanashindwa mbele ya mas'ala magumu na wanataka msaada wa wengine, na elimu yao inashindwa kutimiza haja za jamii ya Kiislamu, hawawezi kamwe kuchukua cheo cha Uimamu na uongozi wa watu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 151 1/13/2017 3:33:26 PM

Muhtasari ni kwamba Imamu ni wajibu awe ni mtu mjuzi zaidi wa dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kujaza pengo ambalo limepatikana kwa haraka kwa kufariki Nabii ﷺ, na kuendelea kueneza Uislamu sahihi ulioepukana na upotovu wowote ule.

**3. Ushujaa:**

Imamu ni wajibu awe ni shujaa na awe ni mtu shujaa zaidi katika jamii ya Kiislamu, kwa sababu haiwezekani kutenganisha ushujaa na uongozi, ili aweze kusimama mbele ya madikteta na madhalimu na maadui wa dola ya Kiislamu ndani na nje.

**4. Kujinyima Dunia na kujipa uhuru:**

Sisi tunajua kwamba mwenye kuwa mateka wa mapambo ya maisha anahadaika haraka. Uwezekano wa kupotoka kwake mbali na njia ya haki na uadilifu mara nyingi unaongezeka kwa njia ya tamaa au kwa njia ya vitisho, na kuangukia kuwa mateka wa dunia, na hatimaye anapotoka katika njia ya sawa. Na Imamu ni wajibu awe ni kiongozi na sio mateka kwa aliyonayo katika uwezo na vipaji, katika dunia hii. Hakika ni wajibu awe huru kutokana na kila kikwazo cha ulimwengu wa kimaada. Awe huru kutokana na matamanio ya nafsi. Awe huru kutokana na pingu za cheo, mali na utajiri, ili asidanganywe wala asiathiriwe ili asijisalimishe.

**5. Mvuto wa tabia njema:**

Qur'ani Tukufu inasema kuhusiana na Nabii ﷺ: "Kwa rehema itokayo kwa Mola Wako umekuwa mpole kwao. Ungekuwa mgumu wa moyo wangeondoka kwako." (Sura Imran: 159).

Sio Nabii ﷺ tu, bali na Imamu, na kila kiongozi wa kijamii anahitaji tabia njema yenye mvuto ili awavutie watu kwake kama sumaku. Na hakuna shaka kwamba aina yoyote ya ugumu na tabia



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 152 1/13/2017 3:33:26 PM

mbaya ni sababu ya kusambaratika watu na kuwaweka mbali. Na hii inazingatiwa kuwa ni aibu kubwa kwa Nabii yoyote na Imamu, wakati ambapo Manabii na Maimamu wametakaswa kutokana na aibu hii, vinginevyo uwepo wao usingekuwa na faida.

Haya ndio masharti muhimu ambayo wameyataja maulamaa wakubwa, ndio kuna sifa zisizokuwa katika hizi sifa tano zilizotajwa ambazo ni wajibu kupatikana kwa Imamu, lakini tuliyoyataja ndio muhimu zaidi.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Kwa dalili gani cheo cha Imamu kinazingatiwa kuwa ni cheo kikubwa zaidi kwa mwanadamu?
2. Je, Nabii Mtukufu ﷺ na Manabii wengine wana cheo cha uimamu?
3. Imamu asipokuwa Maasumu ni matatizo gani yatajitokeza?
4. Kwa nini ni wajibu Imamu awe ni shujaa zaidi na mwenye kujinyima zaidi na awe ni mtu huru sana, na awe ni mwenye mvuto wa tabia njema kwa watu?

## SOMO LA NNE:

### Ni nani anayemteua Imamu?

Kundi katika Ahlus Sunnah wanaitakidi kwamba Nabii ﷺ ameondoka katika dunia hii bila ya kuteua khalifa wa baada yake, na kwamba ameacha wajibu huu kwa Waislamu ili wachague kwa ajili ya nafsi zao Imamu na kiongozi, na hiyo itimie kwa njia ya kongamano la Waislamu, nayo ni moja ya dalili za kisharia kwao. Na wanaongeza



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 153 1/13/2017 3:33:26 PM

kwamba wajibu huu umetimia utekelezaji wake na khalifa wa kwanza amechaguliwa na kongamano la ummah, na yeye binafsi amemteua khalifa wa pili na khalifa wa pili ameteua baraza la mashauri la watu sita kwa ajili ya kuchagua khalifa wake. Na baraza hili lilikuwa linaundwa na: Ali bin Abutalib عليه السلام, Uthman bin Affan, Abdurahman bin Auf, Twalha, Zuberi na Saadi bin Abi Waqaasi. Na baraza hili lilimchagua Uthman kwa kura tatu yaani Sad bin Abi Waqaasi, Abdurahman bin Auf na Twalha, na khalifa wa pili alikwisha kueleza kwamba kama watu watatu watampigia kura mtu na ikawa miongoni mwao yupo Abdurahman bin Auf (mkwe wa Uthman) basi huyo ndiye atakayefaa.

Na watu walifanya mapinduzi kwa hoja mbalimbali katika mwisho wa utawala wa Uthman, na akauliwa bila ya kuweza kumchagua mtu mwingine. Na wakati huo Waislamu wakaelekea kwa Imamu Ali عليه السلام na wakampa kiapo cha utii kuwa khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu صلى الله عليه وآله وسلم, isipokuwa Muawiya ambaye alikuwa Gavana wa Sham kwa sababu alikuwa ana matumaini kuwa Ali عليه السلام hatombakisha katika cheo chake, akatangaza uasi na hilo likapelekea kutokea matukio yaliyofishwa na mabaya katika historia ya Kiislamu. Humo zilimwagwa damu nyingi za Waislamu wasio na hatia. Na kwa kufafanua baadhi ya maudhui ya kielimu na kihistoria tunalo rundo la maswali lakini tutaeleza yaliyo muhimu zaidi katika nyanja hii:

### 1. Je, ummah unaweza kumchagua Khalifa wa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم?

Hakika jawabu la swali hili sio gumu. Ikiwa makusudio ya Imamu ni uongozi wa dhahiri wa jamii ya Waislamu, hakika kumchagua kwake kwa njia ya kupiga kura ni jambo ambalo limeenea. Lakini ikiwa uimamu ni kwa maana ambayo tumeielezea kwa kutegemea maandiko ya Qur'ani Tukufu, haiwezekani kutimia hilo isipokuwa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 154 1/13/2017 3:33:26 PM

kwa njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Nabii ﷺ kwa sababu sharti la uimamu kulingana na tafsiri hii linahitajia elimu nyingi katika misingi na matawi ya dini, na elimu hii inategemeza rejea yake kutoka mbinguni na inategemea juu ya elimu ya Nabii ﷺ ili aweze kuhifadhi sharia ya Uislamu.

Na sharti lingine ni Imamu kuwa maasumu, yaani ameepushwa na kila kosa na kukosea na amehifadhiwa na kinga ya Mwenyezi Mungu, ili abebe jukumu la cheo cha uimamu na uongozi wa kimaanawi na kimada, dhahiri na siri, na vilevile ni wajibu ajipambe kwa kujinyima dunia, uchamungu na utukufu unaohitajika katika cheo hiki. Hakika kuainisha masharti haya, hakuna shaka haitimii isipokuwa kwa njia ya Mwenyezi Mungu Mtukfu na Nabii ﷺ, kwani ndio anayejua ni kwa nani aweke roho ya umaasumu. Naye ndiye anayejua kiwango cha elimu inayohitajika ili kupata cheo cha Uimamu, sambamba na kujinyima dunia, uhuru, ushujaa na utukufu.

Hakika wale ambao wameacha jukumu la kumsimika imamu na khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ mikononi mwa watu, hakika wao wamebadilisha dhana ya Qur'ani ya Uimamu na wamezingatia kuwa uimamu unahusiana na serikali ya kawaida na kuendesha mambo ya watu ya kidunia, vinginevyo hakika masharti ya uimamu kwa maana ya jumla na kamili unaainishwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kama ambavyo Nabii hachaguliwi kwa njia ya rai ya watu, bali huteuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na humtambulisha kwa njia ya miujiza, kwa sababu sifa za Nabii haziainishwi isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## 2. Je, Nabii ﷺ hakuteua khalifa wake?

Hakuna shaka kwamba dini ya Uislamu ni dini ya ulimwengu na ya milele. Na kulingana na maelezo ya Aya za Qur'ani Tukufu haihusiani na zama wala sehemu maalum.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 155 1/13/2017 3:33:26 PM

Na hakuna shaka kwamba Uislamu haukutoka nje ya Bara Arabu hadi alipofariki Nabii ﷺ. Na katika upande mwingine Nabii ﷺ alipitisha miaka 13 Makkah akipiga vita shirki na ibada ya masanamu, na miaka kumi tangu ahamie Madina wakati ambao ni zama za ustawi wa Uislamu, wakati mwingi aliutumia katika vita na mapigano yaliyolazimishwa na maadui.

Pamoja na kwamba Nabii ﷺ alikuwa anaendeleza usiku na mchana mafunzo ya mas'ala na mambo ya Uislamu, na kutambulisha Uislamu mpya katika nyanja zote, isipokuwa ilikuwa inahitaji muda mrefu ili kuchambua mas'ala mengi ya Uislamu, na ilikuwa ni lazima kuwepo na mtu atakayebeba jukumu la wajibu huu mzito kama vilevile Nabii ﷺ baada yake. Kwa kuongezea katika hayo yote hakika kufahamu mazingira ya mustakabali na kuandaa utangulizi wa kuendelea dini kunazingatiwa kuwa ni katika mambo muhimu ambayo anatafakari humo kiongozi na wala haruhusu katika nafsi yake kuacha mas'ala haya muhimu kufunikwa na usahaulifu.

Kisha hakika Nabii wa Uislamu ﷺ alikuwa anatoa amri katika mas'ala madogo, namna gani asiainishe ratiba katika mas'ala ya ukhalifa na uongozi na uimamu, jambo ambalo ni muhimu kwa Waislamu? Hakika mkusanyiko wa mambo haya matatu ni dalili ya wazi kwamba Nabii Mtukufu ﷺ alifanya kazi ya kuainisha khalifa baada yake, na sisi inshaallah tutaleta rundo la riwaya za Kiislamu katika nyanja hii inayofafanua hali hii ya kimantiki, ambayo inatia mkazo kwamba Nabii ﷺ hakughafilika katika muda wa maisha yake juu ya mas'ala haya muhimu, pamoja na mirengo ya kisiasa maalum ambayo ilipatikana baada ya kuondoka Nabii ﷺ na wakafanya juhudi baada yake kutia katika akili za watu kwamba Nabii ﷺ hakuteua khalifa baada yake.

Je, inaningia akilini kwamba Nabii ﷺ ambaye alikuwa anatoka kwenda vitani, kwa mfano vita vya Tabuki, hakuwa anaacha mji wa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 156 1/13/2017 3:33:26 PM

Madina, bali alikuwa anateua mtu ili kuuendesha, hivyo namna gani asifanye hivyo katika nyanja hii katika hatua ambayo ni baada ya kufariki kwake ﷺ na kuuacha ummah katika ugomvi na ikhitilafu na upotevu bila ya kudhamini uendelevu wa Uislamu kwa njia ya muongozo wake katika mustakabali?

Hapana shaka hakika kutoteua khalifa kulikuwa na hatari kubwa juu ya Uislamu mpya, na akili na mantiki vinahukumu kwamba haiwezekani Nabii ﷺ afanye hivyo. Hakika wao wanasema hakika Nabii ﷺ ameacha jambo hili kwa ummah, wakati ambapo hatupati waraka wowote unaoonyesha hivyo.

### 3. Kongamano la Shura:

Tujaalie kwamba Nabii Mtukufu ﷺ aliacha jambo muhimu la maisha, na Waislamu wao ndio wamekalifishwa kuchagua, lakini sisi tunajua kwamba kongamano linamaanisha kuafikiana Waislamu wote. Lakini haijatokea abadani maafikiano na kongamano kuhusiana na ukhalifa wa khalifa wa kwanza, bali lilikuwa ni kundi la Masahaba ambalo liliazimia katika hilo. Na hakushiriki yeyote kati ya Waislamu kutoka katika nchi za Kiislamu katika uchaguzi huu. Na katika mji wa Madina vilevile, Ali عليه السلام hakushiriki, na kundi kubwa katika Bani Hashimu katika uchaguzi, na hivyo hakika mfano wa kongamano hili haukubaliwi. Kisha kama njia hii ni sahihi kwa nini khalifa wa kwanza hakutumia njia hii kwa khalifa wake? Na kwa nini alimchagua yeye mwenyewe? Kama uteuzi wa mtu unatosha basi Nabii ndio anafaa zaidi kufanya hivyo. Na kama kiapo cha utii kinachofuata kinatatua tatizo hakika Nabii ﷺ alikuwa ni bora zaidi kutatua hilo.

Kwa kuongezea katika hayo hakika tatizo la tatu limekuja pamoja na khalifa watatu. Ni kwa nini khalifa wa pili aliacha njia ya khalifa wa kwanza katika uteuzi wake, na akafuata ile sunna ambayo

yeye alikuja kwa msaada wake? Na kwa nini alikwenda katika njia ya kongamano kwa njia ya Shura na hakumchagua yeyote? Kisha kama Shura ni sahihi, kwa nini alichagua watu katika sunna yake. Hivi rai tatu zinatosha kumchagua mtu? Maswali haya yanamkabili mhakiki yeyote katika historia ya Kiislamu, na kutoyajibu inaonyesha kwamba njia ya kumteua Imamu sio kwa njia hizo.

### 4. Imamu Ali ndiye aliyekuwa na haki zaidi kuliko wote:

Tujaalie kwamba Nabii ﷺ hakuteua yeyote baada yake. Kisha tujaalie vilevile kwamba yeye aliacha jambo hili kwa ummah, lakini je inawezekana kumwacha mtu katika uchaguzi, anayesifika kwa elimu na uchamungu na sifa zingine kuliko wengine, na kwenda kwa anayemfuata katika daraja katika hatua?

Kundi kubwa la maulamaa wa Waislamu hata katika Ahlus Sunna, kwa uwazi kabisa wanathibitisha kwamba hakika Imamu Ali عليه السلام alikuwa ni mjuzi zaidi kwa mas'ala ya Kiislamu na mbora zaidi kuliko Waislamu wote. Na athari na riwaya zilizonukuliwa juu yake عليه السلام zinashuhudia hivyo. Na historia ya Kiislamu inasema juu yake kwamba yeye ndio kimbilio la ummah katika matatizo yote ya kielimu. Na hata kama waliwaendea makhalifa na mas'ala yao magumu, makhalifa walikuwa wanayatuma kwa Imamu Ali عليه السلام.

Ama kuhusu sifa zake zingine kama vile ushujaa, utukufu, zuhudi, uchamungu na nyinginezo, zilikuwa wazi na ni bora kuliko wote. Na hivyo hakika wao kama wangetaka kumchagua yeyote kwa cheo hiki hakika Imamu Ali عليه السلام alikuwa anafaa zaidi na anastahiki zaidi kuliko wote. Hakika utafiti huu una nyaraka nyingi, hakuna nafasi hapa ya kurefusha.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 158 1/13/2017 3:33:26 PM

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Kwa nini watu hawawezi kumchagua Imamu na Khalifa wa Nabii ﷺ?
2. Je, akili na mantiki vinahukumu kwamba Nabii ﷺ hakuteua Khalifa wake?
3. Njia za kuwachagua makhalifa watatu wa mwanzo zilikuwaje?
4. Je, njia za kuwachagua zilikuwa zinaafikiana na vipimo vya kielimu vya Kiislamu?
5. Kwa dalili gani Imamu Ali عليه السلام alikuwa anafaa zaidi na anastahiki zaidi kuliko wote?

## SOMO LA TANO:

**Qur'ani na uimamu:**

Hakika Qur'ani Tukufu, Kitabu chetu cha mbinguni ni bora zaidi na kinafaa zaidi kututatulia mas'ala na hususan mas'ala ya uimamu, na hiyo ni kwa nyanja mbalimbali:

**1. Qur'ani Tukufu inazingatia uimamu kwamba ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

Na kama tulivyosoma katika utafiti uliotangulia kisa cha Ibrahim aliyevunja masanamu عليه السلام, Qur'ani inazingatia kwamba Uimamu wa Ibrahim umekuja baada ya kupata cheo cha unabii na utume, na akatekeleza mitihani migumu na mikubwa, Aya ya 124 katika Sura al-Baqarah inasema: "Na Mola Wako alipomjaribu Ibrahimu kwa tamko akatekeleza akasema: Hakika Mimi nimekufanya kuwa Imamu wa watu."



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 159 1/13/2017 3:33:26 PM

Hakika vielelezo mbalimbali vya Qur'ani na vya kihistoria vinaonyesha kwamba cheo hiki amekipata Ibrahim kipenzi cha Mwenyezi Mungu عليه السلام baada ya jihadi yake pamoja dhidi ya wapagani kwa upande mmoja, na kwa kuhamia kwake Sham, na kujenga Kaaba na kumchukua mtoto wake kwenda kumchinja. Ikiwa unabii na utume unateuliwa na Mwenyezi Mungu, hakika cheo cha uimamu na uongozi mkuu kwa viumbe, ambao unazingatiwa kuwa ni kiini cha ukamilifu wa uongozi, kinafaa zaidi kuteuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mas'ala haya sio mepesi hadi itimie kuteuliwa na watu.

Kisha hakika Qur'ani yenyewe inaeleza juu ya hilo katika sehemu hiyo hiyo inasema:

"Hakika Mimi nimekufanya kuwa imamu wa watu." Na kama anavyosema katika Sura al-Anbiyai aya ya 73 kuhusu kundi la Manabii nao ni Ibrahim, Lut, Is'haq, na Yaaqub: "Na tumewafanya ni maimamu wanaoongoza kwa amri yetu."

Mfano wa maneno haya utayaona katika Aya nyingine na inaonyesha kwamba cheo hiki cha Mwenyezi Mungu kinaainishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na tunapofuatilia Aya iliyotangulia inayohusiana na uimamu wa Ibrahim عليه السلام tunaiona anaomba عليه السلام cheo hiki kwa ajili ya watoto wake na wajukuu wake katika mustakabali ila jawabu ambalo analisikia ni kwamba "Hatopata ahadi yangu dhalimu." Ni ishara ya kwamba ombi lako limeshakubaliwa, lakini ambao wanafanya udhalimu katika watoto wako hawatofikia cheo hiki abadani.

Na pamoja na kwamba neno dhalimu kilugha lina maana nyingi na pana, hakika linajumuisha makosa yote ya dhahiri na ya siri na dhulma yoyote katika nafsi au kwa wengine, pamoja na kwamba elimu ya hayo kwa ukamilifu ni ya Mwenyezi Mungu peke Yake, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye ambaye anajua yanayofichikana



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 160 1/13/2017 3:33:26 PM

kwa watu na wanayoyadhamiria, na kwa haya inabainika kwamba uteuzi wa cheo hiki hautimii ila kwa njia ya Mwenyezi Mungu peke Yake (swt).

**2. Aya ya Tablighi:**

Inasema Aya ya 67 katika Sura al-Maidah:

يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۖ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ۚ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ

**"Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola Wako; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe Wake; na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu, hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri."**

Sauti ya Aya hii inaonyesha juu ya jukumu zito lililowekwa juu ya bega la Nabii ﷺ, linazungukwa na mkanganyiko kila pande, ujumbe unaweza kukabili upinzani wa watu, na hivyo hakika Aya inamwamuru Nabii ﷺ kuufikisha kwake, na unampa matumaini na hatari yoyote inayotarajiwa kuweza kumpata.

Hakika haya hayahusiani na tauhidi au shiriki au mapambano ya maadui miongoni mwa Mayahudi na wanafiki na wengeneo, kwa sababu mas'ala hayo yalikuwa yameshatatuliwa kabla ya kuteremka Sura al- Maidah.

Kama ambavyo kufikisha hukumu za Kiislamu, zile nyepesi, hakukuwa na mfano wa hofu hii na umuhimu huo, kwa sababu kulingana na dhahiri ya Aya iliyotajwa hakika ilikuwa ni jukumu kwa kiasi na kiwango cha ujumbe wenyewe. Je, haya sio mas'ala ya ukhalifa? Hususan na kwamba Aya hii imeshuka katika mwisho wa maisha ya Nabii ﷺ na inanasibiana na mas'ala ya ukhalifa, nao ni mwendelezo wa unabii na ujumbe wa Nabii ﷺ.

Kwa kuongezea katika riwaya nyingine nyingi zimenukuliwa kutoka kwa Masahaba wa Nabii Mtukufu ﷺ kama vile Zayd bin Arqam, Abu Said al-Khudiriy, Ibn Abbasi, Jabir bin Abdillah, Abu Huraira, Hudhaifa na Ibn Mas'ud, kiasi kwamba baadhi ya riwaya hizi zimefikia njia kumi, na wamezinukuu kundi kubwa kati ya maulamaa wa Ahlus Sunna miongoni mwa wafasiri, wanahadithi na wanahistoria. Wote wametaja kwamba Aya iliyotajwa imeshuka kwa Ali عليه السلام na vilevile kisa cha siku ya Ghadir Khum.[15]

Inshaallah tutataja mas'ala ya Ghadir katika utafiti wa riwaya na Sunnah, lakini inatosha kutaja kwamba mas'ala haya ni dalili ya wazi kwamba Nabii Mtukufu ﷺ alikalifishwa baada ya Hija ya mwisho, mwisho wa umri wake mtukufu, kumtangaza Imamu Ali عليه السلام kuwa khalifa wake na amtambulishe kwa Waislamu wote.

### 3. Aya ya kuwatii wenye mamlaka:

Inasema Aya ya 59 katika Sura Nisaa:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ ۖ

**"Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka katika ninyi….."**

Hapa tunapata kuwatii wenye mamlaka bila ya sharti wala kikwazo sambamba na kumtii Mwenyezi Mungu na Nabii ﷺ.

Je, makusudio ya wenye mamlaka ni watawala wa kila zama na kila sehemu? Na je, Waislamu katika kila nchi na kila zama, mfano zama zetu za sasa wanalazimishwa kuwatii bila ya sharti wala kikwazo watawala wao? Kama linavyosema kundi la wafasiri kutoka miongoni mwa Ahlus Sunna?

Hakika maneno haya hayaafikiani pamoja na mantiki yoyote,

[15] Rejea *Ihiaqaaqil- haqi, al- Ghadir, Muraajaati* na *Dalail swidiq*.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 162 1/13/2017 3:33:26 PM

kwa sababu watawala wengi katika zama mbalimbali walikuwa wamepotoka, madhalimu, na ni wenye kufuata. Je, makusudio katika hayo ni kwamba watawala ni wajibu hukumu yao isiwe ni yenye kukhalifu hukumu za Kiislamu? Na hii vilevile haiafikiani pamoja na mantiki ya Aya.

Je, makusudio yake ni Masahaba wa Nabii ﷺ? Na dhana hii haiafikiani pamoja na ujumla wa Aya katika kila sehemu na kila zama. Na hivyo hakika sisi tunafahamu kwa uwazi kwamba makusudio ni yule Imamu maasumu aliyepo katika kila sehemu na kila zama ndiye aliye wajibu kutiiwa bila ya kikwazo wala sharti, na amri yake ni wajibu kutekelezwa kama amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Nabii Mtukufu ﷺ.

Kuna hadithi nyingi zilizopo katika rejea za Kiislamu katika nyanja hii, ambazo zinaonyesha kwamba 'wenye mamlaka' inaafikiana na Imamu Ali عليه السلام na Maimamu Maasumina عليهم السلام.

**4. Aya ya Uwalii (uongozi):**

Inasema Aya ya 55 katika Sura al-Maidah:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ

**"Hakika walii wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukuu."**

Hakika Qur'ani Tukufu na kwa kuangalia neno *innamaa* ambalo lina maana ya kuzingira linaona kiongozi wa Waislamu katika watu watatu: Mwenyezi Mungu, Mtume Wake na ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukuu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 163 1/13/2017 3:33:26 PM

Hakuna shaka kwamba makusudio ya Uwalii hapa sio urafiki wa Waislamu baina yao, kwa sababu urafiki wa jamaa hauhitaji sharti na kikwazo kwa sababu waumini ni ndugu hata kama hawatoi Zaka na hata wakiwa hawarukuu, na hivyo hakika Uwalii hapa unamaanisha ukuu na uongozi wa kimada na kimaanawi, hususan unapoambatana na Uwalii wa Mwenyezi Mungu na Uwalii wa Nabii ﷺ.

Ni wazi kwamba Aya iliyotajwa kwa wasifu uliopo humo inaashiria kwa mtu maalum anayetoa Zaka naye akiwa amerukuu, vinginevyo sio dharura mtu kutoa Zaka wakati akiwa katika rukuu ya Swala, na ukweli huu ni alama na sio sifa.

Hakika mkusanyiko wa vielelezo hivi unaonyesha kwamba Aya iliyotajwa inaashiria kwenye kisa maarufu cha Imamu Ali عليه السلام ambapo alikuwa katika hali ya kurukuu, akaja muombaji msikitini na hakuna yeyote aliyempa. Muombaji akanyanyua mikono yake juu mbinguni na akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu, shuhudia hakika mimi nimeomba katika msikiti wa Nabii wa Mwenyezi Mungu na hakunipa kitu yeyote." Na Ali عليه السلام alikuwa amerukuu akamuashiria kwa kidole chake cha mkono wa kulia na alikuwa amevaa pete. Muombaji akaja hadi akachukua pete katika kidole chake, na hiyo ni mbele ya Nabii ﷺ. Alipomaliza Swala yake akanyanyua kichwa chake mbinguni na akasema ﷺ:

"Ewe Mwenyezi Mungu, Musa alikuomba na akasema: Mola nikunjulie kifua changu na ni sahalishie jambo langu na ondoa mfundo katika ulimi wangu ili ifahamike kauli yangu na nipatie msaidizi kutoka kwa ahali yangu Haruna ndugu yangu, na nipe nguvu kwake na mshirikishe katika jambo langu. Ikateremshwa kwake aya yenye kusema: Tutakupa nguvu kwa ndugu yako na tutawapa mamlaka na hivyo hawatofika kwenu kwa Aya zetu. Ewe Mwenyezi Mungu na mimi Muhammad Nabii Wako na mteule Wako, Ewe Mwenyezi Mungu nikunjulie kifua changu na nisahalishie jambo langu na nipe



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 164 1/13/2017 3:33:26 PM

msaidizi kutoka kwa Ahali yangu Ali, upe nguvu mgongo wangu kupitia yeye."

Kabla Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ hajakamilisha dua yake akateremka Jibril kutoka kwa Mwenyezi Mungu akasema: Ewe Muhammad soma: Akasema: Nisome nini? Akasema: Soma: "Hakika kiongozi wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukuu."[16]

Cha kuangalia ni kwamba aghlabu ya wafasiri wakubwa kati ya Ahlus Sunna na wanahistoria na muhaditihina wamenukuu kushuka Aya hii katika haki ya Ali عليه السلام, kama ambavyo kundi la Masahaba wa Nabii wanaozidi kumi katika idadi yao wao wenyewe wamenukuu hadithi hii kutoka kwa Mtukufu Nabii ﷺ.

Aya za Qur'ani ziko nyingi kuhusu Uwalii, lakini sisi tunatosheka na Aya nne ambazo tumezinukuu.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Kwa mujibu wa Qur'ani ni mamlaka ya nani kuteua na kumchagua Imam?
2. Nini madhumuni ya Aya ya Tablighi na katika mazingira yapi imeteremka?
3. Kwa nani umesadiki utii bila sharti wala kikwazo?
4. Kwa dalili gani inaashiria Aya "*Innamaa waliyukum llahu..*" uongozi na uimamu?
5. Katika mkusanyiko wa Aya za Qur'ani katika nyanja ya uongozi, ni mas'ala yapi inawezekana kufaidika nazo?

---

[16] *Tafsirul-Mizani*, Sura al-Maidah, Juzuu 6.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 165 1/13/2017 3:33:26 PM

# SOMO LA SITA:

## Uimamu katika Sunnah ya Nabii ﷺ:

Tunaposoma vitabu vya Hadithi hususan rejea za Ahlus Sunna, hakika mwanadamu anakutana na rundo kubwa la hadithi za Mtukufu Nabii ﷺ zinazothibitisha kwa uwazi nafasi ya uimamu na ukhalifa wa Imamu Ali عليه السلام. Hakika mwanadamu anapata mshangao kwamba pamoja na hadithi zote hizi ambazo haibakii nafasi ya shaka na kusitasita katika mas'ala haya, ni namna gani kundi linaweza kuchagua njia isiyokuwa ya Ahlul-Bayt عليهم السلام?

Hakika baadhi ya hadithi hizi zina mamia ya sanadi kama vile hadithi ya Ghadir, na baadhi ya nyingine zina makumi ya sanadi na zimenukuliwa katika makumi ya vitabu vya Kiislamu vinavyojulikana, nazo ziko wazi kiasi kwamba sisi kama tutaghafilika na hadithi zote hizi na tukaacha kuiga pembeni, hakika mas'ala haya yatabaki yako wazi kiasi kwamba hayahitajii dalili. Na kwa mfano hapa tutataja baadhi ya hadithi zilizo maarufu kati ya hadithi hizo, na mwenye kutaka ziada katika nyanja hii tutataja baadhi ya rejea kwa ajili ya kurejea huko.[17]

### 1. Hadithi ya Ghadir:

Wanahistoria wengi wanataja kwamba baada ya Mtukufu Nabii ﷺ kutekeleza Hija yake ya mwisho katika mwaka wa mwisho katika umri wake mtukufu alifuatana na idadi kubwa miongoni mwa Masahaba wake wa zamani na wapya, na waumini ambao walikusanyika kwa ajili ya kutekeleza ibada hiyo, hadi wakafika Juhufah katika njia ya kurejea kwao, ni baina ya Makka na Madina, kisha wakafika katika jangwa kavu na kame la Ghadir Khum, na sehemu hii kwa uhakika si kingine isipokuwa ni njia panda.

[17] Mfano: *Murajaati, al- Ghadir* na vinginevyo



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 166 1/13/2017 3:33:26 PM

Na kabla ya mahujaji kutawanyika kwenda sehemu mablimbali za Hijaz Mtume ﷺ aliamuru kusimama kisha wakaitwa wale waliokuwa wametangulia katika msafara ili warejee kama ambavyo waliokuwa nyuma pia waliwasili. Hali ya hewa ilikuwa ni ya joto sana na hapakuwa na kivuli katika jangwa, na Waislamu waliswali Swala ya Adhuhuri kwa kuongozwa na Nabii ﷺ. Na walipoazimia kurejea kwenye mahema yao Nabii ﷺ akawapa habari wakusanyike ili wasikilize ujumbe muhimu wa Mwenyezi Mungu ndani ya khutuba ndefu, kisha Nabii ﷺ akapanda juu ya matandiko ya ngamia akamshukuru Mwenyezi Mungu na akamsifu na akasema:

"Enyi watu hakika mimi ni binadamu kama nyinyi inahofiwa kunijia mjumbe wa Mola Wangu na kumwitikia, na mimi ni mwenye kuulizwa na hakika nyinyi mtaulizwa, sasa mtasemaje?

Wakasema: Tunashuhudia hakika wewe umeshafikisha, umepigana jihadi na umetoa nasaha, Mwenyezi Mungu akulipe kheri.

Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema: Je, simnashuhudia kwamba hakuna mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja Wake na mjumbe Wake, na kwamba pepo Yake ni ya haki na moto Wake ni wa haki na kwamba mauti ni ya haki, na kufufuliwa baada ya kufa ni haki, na Kiyama kitakuja na hakuna shaka humo, na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua waliopo makaburini?

Wakasema: Ndio, tunashuhudia juu ya hayo. Akasema ﷺ: Ewe Mwenyezi Mungu shuhudia. Kisha akasema ﷺ: Enyi watu, je mnasikia sauti yangu? Wakasema: Ndio. Akasema: "Hakika mimi ni mwenye kuacha kwenu vizito viwili; Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Ahlul-Bayt wangu, hakika viwili hivyo havitotengana hadi vitakaponijia kwenye hodhi (birika). Mkishikamana navyo hamtapotea.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 167 1/13/2017 3:33:26 PM

Kisha Nabii ﷺ akawa anaangalia pembezoni mwake kana kwamba anatafuta mtu, kisha akamuona Ali ؑ, akainama na akashika mkono wake na akaunyanyua hadi ukaoneka weupe wa kwapa zao na hapa ikapaa sauti ya Nabii ﷺ kwa kusema:

Enyi watu, ni nani mbora wa watu kwa waumini kuliko nafsi zao?

Wakasema: Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanajua zaidi.

Akasema ﷺ: Je, mimi sio bora kwenu kuliko nafsi zenu?

Alisema hivyo mara tatu na wakamjibu kwa: ndio.

Akasema ﷺ: Ambaye mimi nilikuwa ni kiongozi wake basi Ali ni kiongozi wake, Eee Mwenyezi Mungu mpende mwenye kumtawalisha na mfanye ni adui mwenye kumfanyia uadui, mpende mwenye kumpenda na mchukie mwemye kumchukia, mnusuru mwenye kumnusuru na msaidie mwenye kumsaidia na mfedheheshe mwenye kumfedhehesha na izungushe haki pamoja naye popote atakapozunguka.

Kisha akasema: Aliyepo ampe habari asiyekuwepo.

Na watu hawakutawanyika hadi akateremka Jibril ؑ mwaminifu wa wahyi na akasoma Aya hii:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا ۚ

**"Leo nimewakamilishia dini yenu na kuwatimizia neema yangu na nimewapendelea Uislamu kuwa dini." (al-Maida; 5:3)**

Kisha Mtukufu Nabii ﷺ akasema: "Allahu Akbar, Allahu Akbar 'Mwenyezi Mungu ni mkuu' kwa kukamilika dini na kutimizwa neema na ridhaa ya Mola Wangu kwa ujumbe wangu na kwa uongozi wa Ali baada yangu."

Yakatokea makelele katika mkusanyiko, na wakampongeza

Ali kwa cheo hiki, na miongoni mwao ni Abu Bakri na Umar na wakasema: "Hongera, hongera kwako ewe mtoto wa Abutalib, umekuwa ni kiongozi wangu na kiongozi wa kila muumini mwanaume na muumini mwanamke."

Hadithi ya hapo juu imetajwa na wengi kati ya maulamaa wa Kiislamu katika vitabu vyao kwa ibara tofauti tofauti. Wakati mwingine ni kwa muhtasari na wakati mwingine kwa kirefu. Na hadithi hii ni kati ya hadithi mutawatir hashuku yeyote kutokea kwake kwa Mtukufu Nabii ﷺ kiasi kwamba mwandishi na mhakiki Allammah Amini ametaja hadithi hii katika rejea yake maarufu *al- Ghadir*. Ametaja hadithi hii kutoka kwa mia na ishirini kati ya Masahaba wa Nabii ﷺ, na mia tatu na sitini miongoni mwa maulamaa na waandishi maarufu wa Kiislamu, kama ambavyo imepokewa katika vitabu vingi vya tafsiri, historia na hadithi vya ndugu zetu Sunni hadi maulamaa wakubwa wa Kiislamu wameandika vitabu mahususi kwa ajili ya hadithi hii, kati yao ni marehumu Allammah Amini katika kitabu chake cha pekee na cha aina yake ambacho hakuna mfano wake. Ametaja katika kitabu chake majina ishirini na sita kati ya maulamaa wa Kiislamu walioandika vitabu maalum juu ya hadithi hii.

Kundi kati ya wale ambao hawakuweza kupinga sanadi ya hadithi wamekimbilia katika hoja ya hadithi wakafasiri neno *Mawla* kwa maana ya rafiki, wakati ambapo uhalisia wa hadithi na mazingira, wakati, sehemu na viambatanisho vingine vinatia mkazo kwa uwazi kwamba lengo halitoki nje ya mas'ala ya uimamu na uongozi, kwa maana ya uongozi wa jumla:

**a.** Hakika Aya ya tablighi ambayo tumeitaja katika utafiti uliotangulia, na ambayo imeshuka kabla ya tukio hili kwa lugha yake isiyo na shaka, na viambatanisho ambavyo vipo humo, inaonyesha kwa uwazi kwamba mazungumzo hayakuwa

juu ya urafiki wa kawaida, kwa sababu sio muhimu wala hauhitaji umuhimu na mkazo wote huu, kama ambavyo Aya ya kukamilishwa dini ambayo iliteremka baada yake inaonyesha kwamba mas'ala ni muhimu sana nayo ni mas'ala ya uongozi na ukhalifa wa Nabii ﷺ unaoelezwa sasa hivi.

**b.** Dalili nyingine katika kauli yetu ni muundo wa mazungumzo pamoja na utangulizi huo wa ufafanuzi katika jangwa lenye joto, khutuba nzito, na kuchukua kukiri kwa watu katika mazingira hayo muhimu katika wakati na sehemu.

**c.** Maneno ya kupongeza ambayo aliambiwa Ali عليه السلام kutoka kwa makundi na watu mbalimbali, na yale mashairi ambayo yalitungwa katika siku hiyo, na baada ya siku hiyo, yote yanaonyesha juu ya ukweli huu, nayo ni kwamba mazungumzo yalikuwa ni kumuainisha Imamu Ali عليه السلام katika nafasi ya Uimamu na Uongozi wa juu na si kitu kingine.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Fafanua kisa cha Ghadir.

**2.** Hadithi ya Ghadir imepokewa kwa sanadi ngapi kutoka kwa Nabii ﷺ, na ni vitabu vingapi vimeinukuu?

**3.** Kwa nini neno *Mawla* katika hadithi linaonyesha juu ya uongozi na uimamu na sio urafiki?

**4.** Ni dua gani aliomba Nabii ﷺ katika haki ya Ali عليه السلام baada ya tukio la Ghadir?

**5.** Ghadir na Juhufah ni maeneo yaliyoko wapi?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 170 1/13/2017 3:33:27 PM

# SOMO LA SABA:

## Hadithi ya cheo na hadithi ya

## Siku ya Karamu ya Watu wa karibu:

Wamenukuu wengi miongoni mwa wafasiri wakubwa katika Shia na Ahlus Sunna hadithi ya cheo mwishoni mwa Aya ya 142 katika Sura al-A'araf ambayo inazungumzia juu ya Musa kwenda katika makutano yake na Mwenyezi Mungu Mtukufu, ya muda wa siku arobaini na Haruna kuwa khalifa wake kwa kaumu yake.

Na Hadithi ni: Nabii ﷺ alielekea Tabuk, nayo iko Kaskazini mwa Bara Arabu, ambapo kulikuwa na utawala wa Roma ya Mashariki, ambao uliandaa jeshi kubwa kushambulia Hijazi, Makka na Madina kabla ya Mapinduzi ya Kiislamu hayajatoa ratiba yake ya ubinadamu maalum na yenye ukombozi kwenda kwenye sehemu zao na kuumaliza.

Nabii ﷺ aliazimia kuelekea Tabuk pamoja na jeshi kubwa, na akamwacha Ali katika nafasi yake Madina. Ali عليه السلام akasema: "Je, unaniacha pamoja na watoto na wanawake? Na huniruhusu kwenda pamoja na wewe katika medani ya jihadi, na humo kuna ufahari mkubwa?"

Nabii ﷺ akasema: "Je, huridhii kuwa nafasi yako kwangu ni kama nafasi ya Haruna kwa Musa, isipokuwa hakuna Nabii baada yangu?"

Maneno haya yamo katika vitabu mashuhuri vya hadithi kwa Ahlus Sunna, yaani *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslimu*, pamoja na kuwepo tofauti, lakini imepokewa kiukamilifu katika *Sahihi Bukhari*. Na katika Sahihi Muslimu, imepokewa mara moja kiukamilifu na katika mara nyingine imepokewa kwa ibara hii: "Wewe kwangu una cheo cha Haruna kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu." kama maneno ya kawaida tu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 171 1/13/2017 3:33:27 PM

Na Abu Bakar al-Baghidadiy ananukuu katika *Tarikhul-Baghidadiy*, Juz. 7, uk. 452, akinukuu kutoka kwa Umar bin Khatwab kwamba yeye alimuona mtu anamkosea Ali عليه السلام adabu kwa maneno, Umar akamwambia: "Hakika mimi naitakidi kwamba wewe ni katika wanafiki kwa sababu mimi nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema: Hakika cheo cha Ali kwangu ni kama cheo cha Haruna kwa Musa isipokuwa hakuna Nabii baada yangu."

Na tunafahamu kutoka katika rejea za hadithi kwamba Nabii ﷺ hakusema maneno hayo katika kisa cha vita ya Tabuk tu, bali ameyataja katika sehemu saba, jambo ambalo linaonyesha ujumla wa maana ya ibara.

Katika siku ya kutengeneza udugu wa kwanza Makka, yaani siku ambayo alitengeneza udugu baina ya Masahaba wake hapo Makka na yeye akamchagua Ali عليه السلام kuwa ndugu yake, aliisema ibara hiyo ﷺ. Na katika siku ya udugu wa pili, alipofanya udugu baina ya Answari na Muhajirina, Nabii ﷺ alikariri hadithi ya cheo mara nyingine. Na katika siku hiyo Mtume ﷺ aliamuru kufungwa milango ambayo inafungukia kwenye msikiti mkubwa wa Mtume ﷺ na kubakia mlango wa nyumba ya Ali عليه السلام tu ndio uwe wazi, na akakariri ibara hiyo.

Na vile vile katika siku ya vita ya Tabuk na katika sehemu zingine tatu, nazo zimetajwa kwa sanadi katika vitabu vya Ahlus Sunna kiasi kwamba haibakii nafasi ya shaka au kusitasita katika ujumla wa maana ya hadithi ya cheo.

**Madhumuni ya hadithi ya cheo:**

Tukitazama hadithi bila upinzani wowote, na bila hukumu zilizotangulia, hakika sisi tutakuta kwamba vyeo vyote ambavyo alikuwa navyo Haruna katika nafasi ya Musa katika kaumu yake Bani Is-

rail isipokuwa unabii, pia alikuwanavyo Imamu Ali ﷷ kwa sababu hatupati kikwazo wala sharti katika hadithi hii.

**Na kwa haya tunapata natija ifuatayo:**

1. Hakika Imamu Ali ﷷ alikuwa mbora wa ummah baada ya Nabii ﷺ kwa sababu Haruna alikuwa na cheo hiki.
2. Ali ﷷ alikuwa ni masaidizi wa Nabii ﷺ na msaidizi wake maalum na mshirika wa ratiba yake katika uongozi, kwa sababu Qur'ani Tukufu imethibitisha vyeo hivi kwa Haruna. (Sura Twaha aya ya 29 na 32).
3. Ali ﷷ alikuwa Khalifa wa Nabii ﷺ, na anapokuwepo yeye mtu mwingine hana sifa ya kuchukua nafasi hii, kama ambavyo vyeo hivi alikuwa navyo Haruna kwa Musa ﷷ.

**Hadithi Karamu ya watu wa karibu:**

Kwa kujengea kwa yaliyokuja katika historia ya Kiislamu, Nabii ﷺ aliamriwa katika mwaka wa tatu tangu kupewa utume kutangaza daawa ambayo hadi wakati huo ilikuwa ni ya siri, kama ilivyokuja katika Aya ya 214 katika Sura Shuaraa: "Na waonye jamaa zako wa karibu." Nabii ﷺ aliwaita jamaa zake wa karibu katika nyumba ya ami yake Abutalib na baada ya kula chakula aliwaambia: "Enyi wana wa Abdul-Mutwalib, hakika mimi naapa kwa Mwenyezi Mungu, simjui kijana katika Waarabu aliyewajia watu wake na yaliyo bora kama niliyokuleteeni mimi. Nimewajia na kheri ya dunia na akhera, na ameshaniamuru Mwenyezi Mungu Mtukufu niwalinganie kwake. Ni nani kati yenu atanisaidia katika jambo hili ili awe ni ndugu yangu, Wasii wangu na Khalifa wangu kwenu?"

Wote wakanyamza kimya, Ali akasimama na akasema: "Mimi ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu nitakuwa msaidizi wako katika hilo." Mtume ﷺ akasema: "Hakika huyu ni ndugu yangu, Wasii wangu na Khalifa wangu kwenu, basi msikilizeni na mtiini."[18] Lakini kundi potovu halikuridhika kwa aliyoyasema Mtume ﷺ bali walimcheza shere.

Hakika hadithi hii maarufu kwa jina la *Hadithi Daar,* iko wazi vya kutosha na yaliyomo humo. Ama kuhusu nguvu ya sanadi, hakika wengi kati ya maulamaa wa Waislamu miongoni mwa Ahluls Sunna wameinukuu, mfano: Ibnu Abi al-Jarir, Ibnu Abi Hatimu, Ibnu Maruduwaihi, Abu Nuaim, al-Baihaqiy, Thaalabiy, Tabariy Ibnu al-Athir, Abu al-Fidaai na wengineo.

Na sisi tunapoangalia katika hadithi iliyotajwa bila upinzani, tunakuta hakika mas'ala ya uongozi na ukhalifa wa Imamu Ali عليه السلام yanabainika kwetu zaidi na zaidi, kwa sababu mas'ala ya uongozi na ukhalifa yametajwa humo kwa uwazi.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Ni ipi hadithi ya cheo? na imekuja katika rejea ngapi?
2. Ni cheo kipi hadithi inakithibitisha kwa Imamu Ali عليه السلام?
3. Ni kipi cheo cha Haruna kwa Musa kulingana na nususi za Qur'ani?
4. Ni maulamaa wapi ambao wamenukuu hadithi ya cheo?
5. Fafanua Hadithi ya Karamu ya watu wa karibu madhumuni yake na sanadi yake na natija yake.

[18] *Al-Kaamil* cha Ibnu al-Athiri, Jz. 2 uk: 63



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 174 1/13/2017 3:33:27 PM

# SOMO LA NANE:

## Hadithi ya Vizito Viwili na Safina ya Nuhu (a.s):

## Sanadi ya hadithi ya Vizito Viwili:

Hakika moja ya hadithi maarufu na mashuhuri miongoni mwa maulamaa wa Sunni na Shia ni hadithi ya Vizito Viwili. Limenukuu Hadithi hii kundi kubwa kati ya Masahaba bila ya wasita kutoka kwa Nabii (s.a.w.w), na baadhi ya maulamaa wakubwa wanawahesabu wapokezi wa hadithi kwamba ni zaidi ya Masahaba thelathini. Kama ambavyo wameitaja hadithi hii idadi kubwa sana katika wafasiri na muhadithina na wanahistoria katika vitabu vyao, na hivyo haiwezekani kusitasita yeyote au kushuku katika tawaturi ya hadithi hii.

Na amenukuu mwanachuoni mkubwa Sayid Hashim al-Baharaniy hadithi hii katika kitabu chake *Ghaayatul-Maraam* kutoka katika sanad 39 kutoka kwa maulamaa wa Ahlus Sunna na sanadi 80 kutoka katika Maulamaa wa Shia.

Na mwanachuoni mhakiki, Mir Hamid Husein al-Hindiy amefuatilia zaidi katika nyanja hii akanukuu hadithi kutoka kwa maulamaa mia mbili takriban kutoka kwa maulamaa wa Ahlus Sunna, na uhakiki wake katika nyanja hii una mijaladi sita mikubwa.

Na katika jumla ya watu mashuhuri ambao wamenukuu hadithi ni: Abu Saidi al- Khuduriy, Abu Dhari al-Ghafariy, Zayd bin Arqam, Zayd bin Thabiti, Abu Rafii Jubair bin al-Muadham, Hudhaifah, Dhamrah al-Aslamiy, Jabir bin Abdillahi al-Answariy na Ummu Salama. Asili ya hadithi kama alivyosema Abu Dhari al-Ghafariy: Ni pale alipokuwa ameshikamana na mlango wa Kaaba akawageukia watu na akamsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anasema: "Hakika mimi ni mwenye kuwaachieni vizito viwili: Kitabu cha

Mwenyezi Mungu na kizazi changu. Hakika hivyo viwili havitotengana hadi vitakaponifikia katika hodhi (birika)."[19]

Riwaya hii ipo katika vitabu muhimu sana vya Ahlus Sunna vyenye kuzingatiwa; Mfano *Sahihi Tirmidhiy*, *Anasaaiy, Musnad Ahmad, Kanzul- Ummal* na *Mustadrak Sahihayn.* Na imepokewa katika baadhi ya riwaya neno *Khalifataini, yaani* makhalifa wawili, badala ya neno *Thaqalain*, na katika maana hakuna tofauti kubwa. Na vizuri zaidi ni kwamba inafahamika katika hadithi za Kiislamu mbalimbali kwamba hadithi imepokewa kutoka kwa Nabii ﷺ katika sehemu mbalimbali.

Mfano: Katika hadithi ya Jabir bin Abdillahi al-Answariy kwamba Mtume ﷺ alisema katika ibada ya Hija siku ya Arafa. Wakati ambapo Abdillahi bin Hantwab anataja kwamba imepokewa Juhfah baina ya Makkah na Madina. Na Ummu Salama anasema Mtume ﷺ aliyasema katika siku za mwisho katika umri wake mtukufu akiwa mgonjwa kitandani. Na anasema mwenye kitabu *Murajaati* kwamba Mtume ﷺ alisema akiwa juu ya mimbari huko Madina. Na anasema mwenye *Swawaiqul-Muhriqah* – Ibnu Hajar: "Hakika Nabii ﷺ baada ya kusema hadithi hiyo alinyanyua mkono wa Imamu Ali na akasema: Huyu ni Ali yuko pamoja na Qur'ani na Qur'ani ipo pamoja na Ali عليه السلام na wala hawatotengana hadi wanifikie katika hodhi (birika)."

Vivyo hivyo inabainika kwamba Nabii ﷺ amekwishatia mkazo mara nyingi msingi huu muhimu, na hiyo ni katika minasaba mbalimbali ili kubainisha ukweli huu, na ili watu wasilisahau hilo.

**Madhumuni ya hadithi ya Vizito Viwili:**

Hapa kuna nukta nyingi inafaa kuziangalia:

---

[19] Asili iliyotajwa katika kitabu ni (kizazi changu) tu wakati ambapo mashuhuri ni (kizazi changu Ahlul-bait wangu)



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 176 1/13/2017 3:33:27 PM

1. Taarifa ya Qur'ani na Itrah kwa kuvizingatia hivyo kuwa ni makhalifa wawili au vitu viwili ni dalili wazi juu ya kwamba Waislamu ni wajibu washikamane navyo, hususan pamoja na sharti hili ambalo limepokewa katika riwaya nyingi: "Kama mtashikamana navyo hamtapotea baada yangu," jambo ambalo linaipa sura yenye msisitizo zaidi.

2. Uwiano wa Qur'ani na Itrah, na Itrah na Qur'ani, ni dalili juu ya kwamba maadamu Qur'ani haitopotoka na kwamba imehifadhiwa kutokana na kila kosa, vile vile Itrah, Ahlul-Bayt wa Nabii ﷺ wamehifadhiwa kutokana na makosa.

3. Imepokewa kwa uwazi katika baadhi ya riwaya kwamba Nabii ﷺ kwamba watu watahisabiwa siku ya Kiyama juu ya misimamo yao katika vizito viwili.

4. Hakuna shaka kwamba sisi vyovyote tutakavyotaka kufasiri Itrah na Ahlul-Bayt, hakika Imamu Ali عليه السلام anakuwa ni kielelezo wazi kwavyo. Na kulingana na riwaya mbalimbali hakika Imamu Ali عليه السلام hakutengana na Qur'ani au hakufarakana na Qur'ani abadani, na Qur'ani haikutengana naye.

5. Na kwa kuongezea katika hayo tunasoma katika riwaya mbalimbali kwamba wakati wa kuteremka Aya ya Mubahala, Mtukufu Nabii ﷺ alimwita Ali, Fatma, Hasan na Husein عليهم السلام na akasema: "Hawa ni Ahlul-Bayt wangu."[20]

6. Pamoja na kwamba mas'ala yanayoambatana na Siku ya Kiyama kuhusiana na sisi tuliozingirwa katika uzio wa ulimwengu huu sio wazi kabisa, isipokuwa inakuwa wazi kwetu kutokana na riwaya kwamba makusudio ya (hodhi) birika ni mto maalum peponi ambao una sifa nyingi nao ni

[20] *Mashuwatul- Maswaabihi* uk: 567 chapa ya Delhiy.

mahususi kwa waumini wema, Nabii ﷺ, Ahlul-Bayt wake عليهم السلام na wafuasi wa Uislamu.

Katika mkusanyiko tulioutaja inabainika kwetu kwamba marjaa wa ummah na kiongozi wa Waislamu baada ya Mtukufu Nabii ﷺ ni Imamu Ali na baada yake ni Maimamu wa Ahlul-Bayt عليهم السلام.

**Hadithi ya safina ya Nuhu:**

Miongoni mwa ibara zinazovutia zilizonukuliwa kutoka kwa Mtukufu Nabii 4 katika vitabu vya Ahlus Sunna na Shia ni Hadithi maarufu kwa jina la Safina ya Nuhu. Abu Dhari al-Ghafariy anasema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu 4: "Ee, hakika mfano wa Ahlul-Bayt wangu kwenu ni mfano wa safina ya Nuhu, aliyeipanda aliokoka na aliyeacha kupanda alizama."

Hadithi hii ni kati ya hadithi mashuhuri na inatia mkazo kwa Waislamu kumfuata Imamu Ali عليه السلام na Ahlul-Bayt wa Nabii ﷺ baada ya kufariki kwake. Pamoja na angalizo, hakika safina ya Nuhu ilikuwa ni kimbilio pekee na wasila pekee wa kuokoka wakati ilipokuja tufani kubwa ambayo ilienea ulimwenguni. Inabainika kwetu ukweli kwamba ummah wa Kiislamu na baada ya kufariki Mtukufu Nabii ﷺ na wakati wa kuvuma upepo na tufani, ni juu ya Waislamu kushikama na uongozi wa Ahlul-Bayt wa Nabii ﷺ.

# TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Nini madhumuni ya hadithi ya vizito viwili? Na inaeleza ubora gani wa Ahlul-Bayt عليهم السلام?

**2.** Nani amenukuu hadithi ya vizito viwili?

**3.** Nini maana ya vizito viwili, na je yamepokewa maneno mengine badala yake katika hadithi?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 178 1/13/2017 3:33:27 PM

4. Katika maeneo yapi Mtukufu Mtume ﷺ ametaja hadithi ya vizito viwili?

5. Fafanua hadithi ya safina ya Nuhu katika madhumuni na sanadi.

# SOMO LA TISA:

**Maimamu kumi na wawili:**

**Riwaya za Maimamu kumi na wawili عليهم السلام:**

Baada ya kuthibitisha Uimamu na Ukhalifa wa Imamu Ali عليه السلام, kwa hakika yanakuja mazungumzo juu ya Maimamu waliobakia. Kwa muhtasari tunasema:

**Kwanza:** Kunapatikana miongoni mwetu leo riwaya nyingi katika vitabu vya Ahluls Sunna na Shia zinazozungumzia kwa ujumla juu ya ukhalifa wa Makhalifa kumi na mbili baada ya Nabii ﷺ. Na hadithi hizi zimekuja katika rejea nyingi maarufu za Ahlus Sunna mfano *Sahihi Bukhari, Sahihi Tirmidhi, Sahihi Muslim, Sahihi Abi Daud, Musnad Ahmad* na mfano wa vitabu hivi. Na imekuja katika kitabu *Muntakhabul-Athar* hadithi mia mbili na sabini katika nyanja hii, nyingi kati yake ni kutoka katika vitabu vya Ahlus Sunna na zilizobakia ni kutoka katika rejea za Kishia. Na kwa mfano tunasoma katika *Sahih Bukhari*, nacho ni kitabu muhimu sana cha Ahlus Sunna katika hadithi. "Jabiri bin Samaratu amesema: "Nilimsikia Nabii ﷺ anasema: 'Kutakuwa na viongozi kumi na mbili', akasema neno sikulisikia, baba yangu akasema amesema kwamba: 'wote wanatokana na Makuraishi.'"[21]

Na hadithi hii imekuja katika *Sahihi Muslim* hivi: Jabir anasema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema: 'Uislamu hau-

[21] *Sahihul-Bukhariy,* Juz. 9 uk: 100



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 179 1/13/2017 3:33:27 PM

taacha kuwa na nguvu hadi wapatikane Makhalifa kumi na mbili', kisha akasema neno sikulisikia, nikamwambia baba yangu amesemaje? Akasema: 'Wote wanatokana na makuraishi.'"[22]

Na imekuja katika kitabu *Musnad Ahmad* kwa nukuu kutoka kwa Abdillah bin Mas'ud, Sahaba maarufu, hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliulizwa kuhusu makhalifa wake akasema: "Ni makhalifa kumi na mbili kama viongozi wa Bani Israil."[23]

**Madhumuni ya hadithi hii:**

Hadithi hizi, baadhi yake zimefungamanisha nguvu ya Kiislamu kwa hawa makhalifa kumi na mbili, na nyingine zimefungamanisha kwao uhai wa dini, na kwamba hakika wao wote wanatokana na makuraishi. Na katika baadhi ya hadithi hizi hakika wao ni kutoka katika Bani Hashim. Na jambo hili haliafikiani na madhehebu yoyote kati ya madhehebu isipokuwa madhehebu ya Shia, kwa sababu madhumuni yake yanaafikiana kabisa na itikadi ya Kishia, wakati ambapo Maulamaa wa Ahlus Sunna wamekuwa katika njiapanda walipotaka kufasiri hayo. Je, makusudio ya makhalifa waongofu, ni makhalifa wa Bani Ummayah na Bani Abbasi?

Wakati ambapo sisi tunajua kwamba makhalifa wa mwanzo idadi yao haikuwa kumi na mbili, Bani Ummaya hawakuwa kumi na mbili wala Bani Abbasi hawakuwa kumi na mbili, na idadi kumi na mbili haiafikiani pamoja na yeyote kati ya hawa.

Kisha hakika kunapatikana baina ya makhalifa wa Bani Ummayah watu mfano wa Yazid, na katika Bani Abbasi watu mfano wa Mansuru al-Dawaaniqiy na Haruna Rashid, watu ambao hashuku yeyote katika dhulma na udikteta wao, na wala haiwezekani wakawa

[22] *Sahihu Muslim,* Kitabul-Imaarati
[23] *Musnad Ahmad*, Juz. 1, uk: 398



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 180 1/13/2017 3:33:27 PM

ni makhalifa wa Nabii ﷺ na fahari ya Uislamu, wala haiwezekani kuwalinganisha na kipimo chochote.

Kisha hakika sisi hatupati idadi 12 katika jambo lolote isipokuwa Maimamu kumi na mbili wa Shia. Na sasa hivi tuache maudhui kwa mmoja wa Maulamaa wa Ahlus Sunna maarufu, naye ni Suleiman bin Ibrahim al-Qanduziy mwenye kitabu *Yanaabi'ul-Mawadah* ambapo anasema: "Amesema: Baadhi ya wahakiki wamesema: Hakika Hadithi ambazo zinaonyesha kwamba makhalifa baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kumi na mbili ni mashuhuri, na imenukuliwa kwa njia mbalimbali, na jambo ambalo inawezekana kuling'amua licha ya kupita muda ni kwamba hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anakusudia katika hadithi yake kizazi chake, kumi na mbili katika Ahlul-Bayt wake, kwa sababu haiwezekani kupatikana idadi ya kumi na mbili kwa makhalifa wa mwanzo, kwa sababu wao hawazidi wanne, wala kwa Bani Ummayah kwa sababu wao ni zaidi ya kumi na mbili, na wote ni madhalimu isipokuwa Umar bin Abdil-Aziz, kama ambavyo hawakuwa katika Bani Abbasi, na Nabii ﷺ amesema wote ni katika Bani Hashim, kama alivyonukuu Abdul-Maliki bin Umar kutoka kwa Jabir bin Samrati.

Na dalili juu ya hilo ni aliyoyasema Nabii ﷺ kwa sauti ndogo alipoulizwa wao ni kutoka katika kundi gani, kwa sababu watu wote hawakuwa na nia njema katika ukhalifa wa Bani Hashim. Kisha hadithi haiafikiani na makhalifa wa Bani Abbasi kwa sababu idadi yao inazidi kumi na mbili, na katika upande mwingine hakika wao hawafanyii kazi Aya ya Mawada: 'Sema siwaombeni malipo yoyote kwayo isipokuwa kuwapenda jamaa zangu.' (Sura Shuraa: 23).

"Kama ambavyo wao walipuuza hadithi ya Kisaa! Na hivyo hadithi inaafikiana tu na Maimamu kumi na mbili wa Ahlul-Bayt عليهم السلام, kizazi cha Nabii ﷺ, kwa sababu wao katika upande wa elimu na maarifa ni wajuzi zaidi kuliko wote, na katika upande wa zuhudi



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 181 1/13/2017 3:33:27 PM

wana zuhudi zaidi kuliko wote, na katika upande wa hadhi na nasaba wako juu kuliko wote. Wao wamerithi elimu kutoka kwa babu yao Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Na jambo ambalo linaunga mkono hayo ni hadithi ya vizito viwili na hadithi nyingi nyinginezo zilizonukuliwa kutoka kwa Nabii ﷺ."[24]

Na uzuri zaidi ni kwamba kupitia ziara yangu huko Makkah Tukufu nilikutana na baadhi ya Maulamaa wa Hijazi na nilisikia tafsiri ya hadithi hii, jambo ambalo linaonyesha kwamba wao walifikia kwenye njiapanda, wao wanasema: "Huenda makusudio ya makhalifa kumi na mbili ni makhalifa wanne wa mwanzo wa Uislamu na wengine watakuja katika mustakabali na hawajadhihiri hadi sasa!!" Vivyo hivyo hakika hawa wamesahau utaratibu wa mafungamano yenye kuungana ya makhalifa hawa katika hadithi ya Nabii ﷺ iliyo wazi.

Lakini sisi tunasema, ni kwa nini tunaacha tafsiri iliyo wazi ambayo inaafikiana pamoja na Maimamu kumi na mbili ya Mashia, na tunazitumbukiza nafsi zetu katika madimbwi na njia zilizofungwa?

**Uteuzi wa Maimamu kwa majina:**

Jambo ambalo linapasa kuangaliwa ni kwamba zimepokewa riwaya kwa njia za Ahlus Sunna kutoka kwa Nabii ﷺ zikiwa na majina ya Maimamu kumi na mbili kwa uwazi na shakhisiya zao. Ananukuu Sheikh Suleiman al-Qanduziy mwanachuoni wa Ahlus Sunna maarufu katika kitabu cha *Yanaabiul- Mawada*:

"Mwanaume wa kiyahudi anayeitwa Na'athal alihudhuria kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na katika maswali yake aliuliza kuhusu mawasii wa Nabii ﷺ na makhalifa wake. Mtume ﷺ akawatambulisha kama ifuatavyo: Hakika wasii wangu ni Ali bin

---

[24] *Yanabiul- Mawadah* uk: 446



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 182 1/13/2017 3:33:27 PM

Abutalib na baada yake ni wajukuu zangu wawili Hasan na Husein, watafuatiwa na Maimamu tisa kutoka katika kizazi cha Husein.

Akasema: Ewe Muhammad nitajie:

Akasema ﷺ: Akiondoka Husein ni mtoto wake Ali, akiondoka Ali ni mtoto wake Muhammad, akiondoka Muhammad ni mtoto wake Ja'far, akiondoka Ja'fari ni mtoto wake Musa, akiondoka Musa ni mtoto wake Ali, akiondoka Ali ni mtoto wake Muhammad, akiondoka Muhammad ni mtoto wake Ali, akiondoka Ali ni mtoto wake Hasan, akiondoka Hasan ni mtoto wake Hujah Muhammad Mahdi عليه السلام, hawa ni kumi na mbili."[25]

Na katika kitabu hicho hicho kwa kunukuu kutoka katika kitabu *al-Manaaqib* kuna hadithi nyingine kuhusu maimamu kumi na mbili, kwa jina la lakabu, na kuhusu Imamu Mahdi, na kuna ishara ya ghaiba yake kisha kudhihiri kwake na kuijaza ardhi usawa na uadilifu kama ilivyojazwa dhulma na ujeuri.[26] Hakika hadithi katika nyanja hii ni nyingi na hususani kwa Mashia ambapo zinazidi kiwango cha tawatur.

**Mwenye kufa na hakumjua Imamu wa zama zake:**

Imekuja katika moja ya vitabu vya Ahlus Sunna kutoka kwa Nabii ﷺ:

"Mwenye kufa na hakumjua Imamu wa zama zake anakufa kifo cha kijahiliya."[27] Hadithi hii imepokewa katika rejea za Kishia kwa sura hii: "Mwenye kufa na hakumjua Imamu wake anakufa kifo cha kijahiliya."[28] Hadithi hii inaonyesha wazi juu ya kuwepo Imamu

[25] *Yanaabiul-Mawada*, uk: 441
[26] *Yanaabiul-Mawada*, uk: 442
[27] *Al-Muujamul-Faharisi Lialfaadh al-Ahadithi nabawaiyat,* Juz. 6 uk: 302
[28] *Biharul-Anuwar*, Juz. 6 (chapa ya zamani) uk: 16



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 183 1/13/2017 3:33:27 PM

maasumu katika kila zama na kila sehemu ambaye ni wajibu kumfahamu, na kutomjua kunamdhuru mwanadamu kiasi kwamba kunamrejesha katika zama ya ukafiri na ujahiliya. Je, makusudio ya Imamu katika hadithi hii ni wale ambao wanaongoza serikali mfano wa Jenkizi na Haruna na watawala katika wafuasi wao? Hapana shaka kwamba jawabu ni la kukanusha, kwa sababu watawala mara nyingi ni kati ya madhalimu wakandamizaji wenye kufungamana na Magharibi na Mashariki na ni vibaraka wa siasa za kigeni. Na hakuna shaka kwamba kuwatambua hawa na kukubali uongozi wao kunamfikisha mwanadamu kwenye makazi mabaya ya Jahanam. Hivyo inabainika kwamba kila zama na wakati ina Imamu maasumu ambaye ni lazima tumpate na kukubali uongozi wake. Ndio hakika unapatikana uimamu wa Maimamu kwa kuongezea katika njia iliyotangulia kwa njia ya nususi na riwaya zilizopokewa kutoka kwa Imamu aliyetangulia akimwainisha Imamu anayekuja na kwa njia ya muujiza wao.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Riwaya za maimamu kumi na mbili zimekuja katika vitabu gani?

**2.** Nini madhumuni ya hadithi hizi?

**3.** Nini tafsiri zisizonasibiana na hadithi hizi?

**4.** Je, yamepokewa majina ya maimamu kumi na mbili katika vitabu vya Ahlus Sunna?

**5.** Ni zipi njia nyingine za kuthibitisha Uimamu wa maimamu kumi na mbili?

# SOMO LA KUMI:

## Mahdi Imamu wa kumi na mbili

## na mrekebishaji mkuu wa ulimwengu:

### Mwisho wa usiku wa giza:

Tukitupia macho juu ya hali ya ulimwengu leo na tukaona kuongezeka kwa makosa, mauaji, vita, umwagaji damu, mapigano na ikhitilafu ya dola na kuenea kwa kasi ufisadi wa maadili, tunauliza nafsi zetu: Je, hali itaendelea hivi? Na je, makosa na ufisadi utaenea hadi jamii ya kibinadamu ikabiliwe na aina za vita vya daima na kumalizika? Na je, utaenea upotovu wa kiitikadi na ufisadi wa kimaadili kama vile madimbwi ya uharibifu katika jamii na kuimeza? Au kuna matumaini katika kuokoka na kurekebisha?

### Kuna majibu mawili katika swali hili muhimu:

**Jawabu la kwanza:** Inaelezwa kutoka kwa wasiotarajia kheri na watu wa mada kwamba mustakabali wa ulimwengu ni giza na kila zama kunatarajiwa uwezekano wa kutokea hatari. Ama wale ambao wanaitakidi misingi ya dini za mbinguni, hususan Waislamu na hususan Shia miongoni mwao, wanatoa jawabu lingine na wanasema: Hakika usiku huu wa giza kuna mapambazuko ya matumaini yanayoufuatia na yataondoka haya mawingu ya giza na tufani hii yenye kufisha, na kimbuga hiki chenye kuangamiza, na mbingu itakuwa ni yenye kuangaza na jua kung'ara angani na utulivu kukienea kila kitu, na hakutakuwa na mambo yenye kufichikana mbele ya madimbwi haya, na kutanda angani karibuni, na haitakuwa mbali mistari ya ufukwe wa kufaulu. Hakika ulimwengu unamsubiria mrekebishaji mkubwa, ambaye atabadilisha ulimwengu kwa mapinduzi ya siku moja kwa maslahi ya haki na uadilifu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 185 1/13/2017 3:33:27 PM

Hakika wafuasi wa kila dini wanamwita mrekebishaji huyu mkubwa kwa jina, lakini mshairi wa kiarabu anasema: Maneno yetu ni mengi na wema wako ni mmoja na yote katika hayo yanaashiria kwenye uzuri.

**Maumbile na kudhihiri mrekebishaji mkubwa:**

Hakika ilihamu ya ndani ambayo mawimbi yake wakati mwingine yana nguvu zaidi kuliko mtazamo wa kifikira, sio tu katika mas'ala ya kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu, bali katika itikadi zote za kidini, kwetu yanaweza kuwa sawa na dalili, nayo katika mas'ala haya ni vivyo hivyo, na dalili katika hayo ni:

**1.** Mapenzi ya jumla ya uadilifu wa kiulimwengu, kwa sababu watu wote katika ulimwengu pamoja na yote waliyonayo miongoni mwa ikhitilafu bila ya upendeleo, wanapenda amani na uadilifu. Na sisi tunapiga kelele na tunakwenda mbio, na tunataka amani ya ulimwengu kwa uwepo wetu wote. Na hakuna dalili bora zaidi ya maumbile ya kudhihiri mrekebisha huyu mkubwa zaidi ya hii, kwa sababu kongamano la rai ni dalili juu ya maumbile hayo (fikirieni vizuri katika hayo).

Na kila upendo wa asili wa maumbile ni dalili ya uwepo wa mwenye kupendwa nje. Namna gani inawezekana Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ameumba upendo huu katika roho ya mwanadamu auache bila ya kushibisha kiu hii?

Na kwa sababu hii tunasema hakika maumbile ya uadilifu kwa mwanadamu yananadi kwa uwazi kwamba hakika amani na uadilifu utaenea ulimwengu mwishoni, na itaondoka dhulma na udikteta ili wanadamu waishi kama dola moja na chini ya bendera moja kwa uelewano na usafi.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 186 1/13/2017 3:33:27 PM

**2.** Dini zote na madhehebu zote zinasubiria kudhihiri kwa mrekebishaji mkubwa wa kiulimwengu, na katika dini zote kuna faslu muhimu yenye kuzungumzia upande huu. Na hakuna mas'ala ya imani ya kudhihiri mrekebishaji mkubwa kwa ajili ya kurekebisha mambo ya mwanadamu mongoni mwa Waislamu tu, bali kuna nyaraka zinaonyesha kwamba hilo lilikuwepo tangu zamani kama itikadi ya jumla miongoni mwa watu wote na wananchi wote pamoja na madhehebu zao, Magharibi na Mashariki. Na kwa kuwa Uislamu unazingatiwa kuwa ni dini kamilifu zaidi, hivyo unatia mkazo zaidi mas'ala haya.

Imekuja katika kitabu *Zandi*, nacho ni moja ya vitabu maarufu vya Zoroasta, baada ya mzozo wa muda mrefu baina ya Alaalatu na mashetani: "Na mwisho ushindi unakuwa wa Alaalatu na kumalizika mashetani, na ulimwengu kupata furaha ya kimsingi, na mwanadamu atakaa katika kiti cha enzi cha mafanikio."

Na katika kitabu *Jamaasibu name* cha Zoroasta yananukuliwa yafuatayo:

"Na atatoka mtu katika nchi ya kiarabu, mtu mwenye kichwa kikubwa, na mwili mkubwa na miundi mikubwa. Na kwa kupitia dini ya babu yake na kwa jeshi kubwa, atajaza ardhi uadilifu."

Na imekuja katika kitabu cha *Washin Jauku* katika vitabu vya Uhindu:

"Na hatimaye dunia itarudi kwa mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na miongoni mwa waja Wake maalum."

Na tunasoma katika kitabu *Basiki* kati ya vitabu vya Uhindu:

"Wakati wa kumalizika dunia atakuja mfalme mwadilifu katika zama za mwisho, na atakuwa Imamu wa malaika, majini na wanadamu.

Na haki itakuwa pamoja naye, na atapata kila kilichofichikana baharini, ardhini na milimani. Na atatoa habari ya yaliyopo ardhini na mbinguni, na hatokuwepo mkubwa zaidi kuliko yeye katika uso wa ardhi."

Tunasoma katika kitabu *Zaburi* cha Nabii Daudi عليه السلام, nacho ni kati ya vitabu vya agano la kale: "Na waovu watamalizika na watairithi ardhi wenye kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Na imekuja katika kitabu hicho hicho na katika fasili hiyo hiyo:

"Na watarithi wakweli ardhi na wataishi humo milele."

Na mfano wa maneo haya yamepokewa katika kitabu cha Isaya ndani ya vitabu vya Taurati, na katika Injili ya Mathayo tunasoma katika fasili ya 24: "Kwa sababu ujio wa binadamu unakuwa mfano wa radi inayomulika Mashariki na kuangazia Magharibi."[29] Na tunasoma katika fasili ya kumi na mbili katika Injili ya Luka: "Kuweni na utayari katikati yenu imefungwa na taa zenu zimewaka, kama wanaume wanaosubiria kurejea kwa bwana wao kutoka harusini hadi atakapokuja na akagonga mlango wanamfungulia haraka."[30]

Na imekuja katika kitabu *Alaaimu dhuhuri*:

"Inawezekana kupata itikadi ya kuja na kudhihiri mrekebishaji wa ulimwengu katika vitabu vya China vya zamani, katika itikadi za kihindi, na baina ya wakazi wa Skandanavia na hata baina ya Wamisiri wa zamani na wakazi wa asili wa Mexico."

**Dalili za kiakili:**

**a.** Mpangilio wa uumbaji unatoa kwetu somo hili, nalo ni kwamba, hakika ulimwengu wa kibinadamu ni lazima mwis-

[29] Injili ya Mathayo fasili ya 23 aya ya 28- kitabu kitakatifu. Agano jipya chapa ya Itihaadi jamaiyaati al- kitabi al-Muqadasi 1978.

[30] Injili ya Luka fasili ya 12 aya ya 35, 36 rejea iliyotangulia.

honi ujisalimishe katika kanuni adilifu na mrekebishaji wa kudumu. Ufafanuzi wa hilo: Hakika ulimwengu wa uwepo kama tunavyojua unaundwa na kundi la mifumo na uwepo wa kanuni zilizopangwa katika kila uwepo huu. Ni dalili ya umoja wa mafungamano ya utaratibu huu. Na mas'ala ya mfumo, kanuni na ratiba makini ni miongoni mwa mas'ala muhimu sana ya ulimwengu, mfumo mkubwa hadi kwenye (dhari) chembe ndogo kabisa ambazo kama zikikusanywa chembe milioni zingekaa katika ncha ya sindano, zote zikiwa zinanyenyekea chini ya mfumo makini.

Viungo mbalimbali katika miili yetu katika kiwango cha chembe ndogo za ajabu, na hata kazi ya ubongo na mlolongo wa mishipa ya moyo na mapafu mawili, yote yana mfumo kama walivyosema baadhi ya wataalamu kwamba kila moja kati ya vyombo hivi na viungo vinafanya kazi kwa makini kama vile saa, katika miili yetu na umakini wa mfumo wa kompyuta unashindwa juu yake.

Katika mfano wa ulimwengu huu, inawezekana kuwa mwanadamu ambaye ndiye sehemu ya hiki kizima, ni kitu kilicho nje na kisichopangiliwa, na kinaishi katika vita, umwagaji damu na dhulma?

Je, inawezekana dhulma, ukandamizaji na ufisadi wa kitabia na kijamii, na yote ni aina miongoni mwa aina zisizokuwa na utaratibu, kutulia na kudhibiti daima jamii ya kibinadamu?

**Natija:** Hakika mtazamo wa dhulma unatuonyesha juu ya ukweli huu kwamba jamii ya kibinadamu hatimaye itanyenyekea katika mfumo wa uadilifu na kurejea kwa mara nyingine mwendo wake wa msingi katika maumbile.

**b.** Mwenendo wa ukamilifu wa jamii, ni dalili nyingine juu ya mustakabali mzuri wa ulimwengu wa kibinadamu, kwa sababu sisi hatuwezi kupinga ukweli kwamba jamii ya ki-

binadamu, tangu umefahamika, haijasimama katika hatua yoyote, bali daima ulikuwa katika hali ya kuendelea.

Na katika upande wa kimada na katika makazi, mavazi, aina ya chakula, vyombo vya usafiri na vyombo vya uzalishaji, mwanadamu siku moja alikuwa anaishi katika hatua za mwanzo za nyakati za maisha, na leo amefika kwenye hatua inayofanya akili kuwa katika tahayari na macho kushangaa na hakuna shaka kwamba maendeleo haya yanaendelea. Na katika elimu na utamaduni pia, maendeleo yalikuwa yanaendelea, na mwanadamu kila siku alikuwa anapata uvumbuzi mpya na mafanikio mapya na maudhui mapya.

Na kanuni hii ya ukamilishaji inaenea pande zote za kimaanawi, kimaadili na kijamii pia, na kumsukuma mwanadamu na uanadamu kuelekea katika kanuni adilifu, amani na uadilifu wa daima, fadhila za tabia njema na maanawiya. Na ikiwa tunaona ufisadi wa kitabia unazidi kuongezeka, hakika vilevile inaandaa mazingira ya mapinduzi ya ukamilishaji hatua kwa hatua. Hakika sisi hatushajiishi ufisadi, lakini sisi tunasema ufisadi unapovuka mipaka, hakika kisasi chake kinakuwa ni mapinduzi ya kitabia. Na mwanadamu anapofikia kwenye njia finyu na hatima mbaya kutokana na makosa yake na kupatwa na kukata tamaa, hakika kwa uchache atakuwa tayari kukubali misingi ambayo anakuja nayo kiongozi wa kiungu.

**Qur'ani na kudhihiri kwa Mahdi:**

Kuna Aya nyingi katika Qur'ani Tukufu zinabashiria kudhihiri huyu mwanadamu mtukufu, na sisi tunatosheka na Aya moja tu miongoni mwa Aya hizo: Tunasoma katika Sura Nuur - aya ya 55:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 190 1/13/2017 3:33:27 PM

**"Mwenyezi Mungu amewaahidi ambao wameamini miongoni mwenu na wakatenda mema atawatawalisha katika ardhi kama alivyowatawalisha waliokuwa kabla yenu….." (an-Nuur; 24:55)**

Hakika aya hii inaonyesha kwa uwazi kwamba utawala mwishoni utatoka katika mikono ya watawala wakandamizaji ili watawale baada ya hapo waumini wema katika uso wa ardhi.

Kwa mwendelezo wa ahadi iliyotajwa, kuna ahadi nyingine tatu; Kuiwezesha dini, na kutia nguvu ya kimaanawi ya utawala wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika nyoyo "Na kwa yakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea," pili ni kuwatunuku amani "Atawabadilishia baada ya hofu yao awape amani." Na tatu ni kung'oa mizizi ya shiriki juu ya ardhi "Waniabudu Mimi na wasinishirikishe na chochote."

Na amesema Imamu Ali bin Husein عليه السلام katika tafsiri ya Aya hiyo: "Wao Wallahi ni wafuasi wetu, Mwenyezi Mungu atafanya hivyo kwao katika mkono wa mtu miongoni mwetu naye ni Mahdi wa Ummah huu."

## Mahdi katika rejea za Hadithi:

Nyingi ni hadithi zilizopokewa kuhusu kusimamisha serikali ya ulimwengu katika amani na uadilifu, kutoka kwa mwanaume kutoka kwa Ahlul-Bayt wa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم. Mwanaume huyo jina lake ni Mahdi, na hiyo ni katika rejea za hadithi za Shia na Sunni, kiasi kwamba zinavuka kiasi cha tawatur. Kama ambavyo kuna tawatur katika yanayohusiana naye, kwamba yeye ni Imamu wa kumi na mbili na Khalifa wa Nabii صلى الله عليه وآله وسلم, na mtoto wa tisa wa Imamu Husein عليه السلام na mtoto halisi wa Imamu Hasan al-Askariy عليه السلام.

Katika sehemu ya kwanza: Yaani tawatur ya hadithi juu ya kudhihiri Mahdi عليه السلام katika rejea za kisunni, inatosha kujua kwamba



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 191 1/13/2017 3:33:27 PM

Maulamaa wa Sunni wanataja hayo katika vitabu vyao hadi sisi tunasoma katika risala iliyotolewa kutoka *Rabitatul-Alamil-Islami*, nayo ni kituo kikubwa cha kidini cha watu wa Hijazi: "Yeye ni Khalifa wa mwisho katika makhalifa kumi na mbili waongofu ambao ametoa habari juu yao Mtukufu Nabii ﷺ katika hadithi sahihi, na hadithi kuhusu Mahdi عليه السلام zimenukuliwa kwa wingi kutoka kwa Masahaba kutoka kwa Nabii ﷺ."

Na baada ya risala kutaja majina ya Masahaba ishirini ambao wamenukuu hadithi ya Mahdi عليه السلام kutoka kwa Nabii ﷺ inasema: "Na wasiokuwa hawa kuna wengi kati ya walionukuu hadithi hizi, na baadhi ya maulamaa wa Ahlus Sunna wameandika vitabu katika habari za Mahdi عليه السلام miongoni mwao ni Abu Nuaim Isfahaaniy, Ibnu Hajar al-Haithamiy, Shaukaniy, Idrisi al-Magharibiy na Abu Abbas bin Abdil-Muumini."

Risala inaendelea kusema: "Baadhi ya maulamaa wakubwa wa Ahlus Sunna wameeleza zamani na sasa kwa tawatur habari za Mahdi عليه السلام." Na baada ya risala kutaja baadhi ya majina yao inahitimisha kauli yake: "Wamekwishasema baadhi ya mahufadhi na muhadithina wazi kwamba Hadithi za Mahdi ni miongoni mwa Hadithi sahihi na hasan, nazo ni mutawatir kwa namna madhubuti na kwamba kuamini kudhihiri kwa Mahdi ni wajibu, nayo ni katika itikadi ya Ahlus Sunna na wala hapingi hayo ila jahili na mzushi."

**Ama kuhusu hadithi za Shia:**

Inatosha kujua kwamba yamenukuliwa mamia ya hadithi katika nyanja hii kutoka kwa wapokezi mbalimbali kutoka kwa Mtukufu Nabii ﷺ na kutoka kwa Maimamu waongofu عليهم السلام, kiasi kwamba zinavuka kiwango cha tawatur. Na imekuwa kwa Shia ni katika dharura za kidini, ambapo haiwezekani kwa mmoja wao asiamini kudhihri



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 192 1/13/2017 3:33:27 PM

kwa Mahdi ﵇ na nyingi kati ya sifa zake na alama za kudhihiri kwake na serikali yake.

Na wameandika maulamaa wakubwa wa Kishia tangu karne ya kwanza ya Uislamu hadi leo, utunzi mwingi katika nyanja hii, humo wamekusanya hadithi, na sisi kama mfano tunaleta baadhi ya hadithi hapa, na kumuelekeza anayetaka ziada katika nyanja hii kusoma vitabu *al-Mahdiy Thauratul-Kubra*, *Bisharatul-Amni Wal-Amaan*, na kitabu *al-Mahdiy* utunzi wa mwanachuoni mkubwa Sayid Swadir Diyn Swadir.

Amesema Mtukufu Nabii ﷺ: "Hata kama haikubakia katika umri wa dunia isipokuwa siku moja tu, basi Mwenyezi Mungu angeirefusha siku hiyo hadi atume mtu kutoka katika Ahlul-Bayt wangu aijaze usawa na uadilifu kama ilivyojazwa dhulma na ujeuri."

Na imekuja katika hadithi ya Imamu as-Sadiq ﵇: "Atakaposimama al-Qaim atahukumu kwa uadilifu na utaondoka ujeuri katika utawala wake. Njia zitakuwa salama, ardhi itatoa baraka zake na atarejesha kila haki kwa mwenyewe, na atahukumu baina ya watu kwa hukumu ya Daudi na hukumu ya Muhammad ﷺ. Na wakati huo ardhi itadhihirisha hazina yake na kutoa baraka zake. Na mtu wakati huo hatapata nafasi ya sadaka yake na wema wake kwa kuenea utajiri kwa waumini wote."[31]

Sisi tunajua kwamba wakati wa zama za ghaiba, ghaiba ya Imamu Mahdi roho zetu ziwe fidia kwake, inaendelea njia ya uimamu kwa wasita wa manaibu wa Imamu ﵇ yaani Maulamaa na mafakihi.

[31] *Biharul-Anuwar*, Juz. 13



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 193 1/13/2017 3:33:28 PM

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Kuna tofauti gani katika pande za mitazamo ya waumini na watu wa mada kuhusu mustakabali wa ulimwengu?

**2.** Je, inawezekana kunufaika na kudhihiri kwa Mahdi عليه السلام kwa njia ya kimaumbile?

**3.** Je, tunayo dalili ya kiakili katika kudhihiri kwake? Dalili hiyo ni ipi?

**4.** Qur'ani Tukufu inasemaje kuhusu kudhihiri kwa Mahdi عليه السلام?

**5.** Nini mtazamo wa Sunni katika nyanja hii?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 194 1/13/2017 3:33:28 PM

# 5

# MASOMO KUMI KATIKA MIADI (MAREJEO)

**Somo la Kwanza:**

**Swali muhimu: Je, mauti ni mwanzo au ni mwisho?**

Watu wengi wanaoogopa mauti kwa nini?

Mauti daima yalikuwa yanaonekana kama mnyama mkali anayetisha mbele ya macho ya mwanadamu. Anashughulisha akili yake na anauguza hisia zake. Na sio tu kwamba mwanadamu anaogopa jina la mauti kwa kuogopa kwake kaburi, bali anapamba makaburi ili asahau uhalisia wake.

Na athari za hofu hii zinadhihirika katika fasihi mbalimbali katika ulimwengu, ambapo inaashiriwa katika mauti kwa misemo mbalimbali mfano 'Nyakuo la mauti' na nyinginezo. Na mwanadamu anapotaka kuashiria mtu aliyekufa, hakika anatumia ibara nyingi ili kuweka mbali hofu kwa anayemweleza. Lakini ni wajibu kufasiri na kuchambua kwa nini mwanadamu anaogopa mauti? Na kwa nini kunapatikana baadhi ya watu kinyume na hivyo, ambao hawaogopi mauti, bali hakika wao wanayapokea mauti kwa tabasamu na ufahari?

Tunasoma katika historia, wakati ambapo baadhi wanakimbilia maisha marefu, hakika baadhi ya wengine wanayapokea mauti kwa kifua kipana katika medani za jihadi na katika vinywa vyao,



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 195 1/13/2017 3:33:28 PM

hadi wao wakati mwingine wanashuku juu ya umri na wanatamani kufa kukutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama anavyokutana kipenzi na kipenzi chake. Na leo pia tunaona jambo hili wazi, jeshi la haki dhidi ya batili, na namna gani wao wanazibeba roho zao katika viganja vya mikono yao.

**Dalili ya msingi wa hofu:**

Kwa utafiti wa kina tunafikia kwenye sababu ya hofu, nayo haiepukani na mambo mawili:

**1. Kutafsiri mauti kwa maana ya kumalizika:**

Mwanadamu daima anakimbia kumalizika na anakimbia maradhi kwa sababu inamaanisha kutokuwa na amani, anaogopa giza kwa sababu linamaanisha kutokuwepo nuru. Na anaogopa ufakiri kwa sababu unamaanisha kutokuwepo na utajiri.

Na wakati mwingine anaogopa nyumba isiyo na mtu, na hofu inamtawala katika jangwa tupu kwa kutokuwepo yeyote huko. Na cha ajabu ni kwamba anaogopa maiti. Kwa mfano hakika hayuko tayari kubakia katika chumba pamoja na mwili wa marehemu, wakati ambapo tunamkuta alikuwa anakaa naye huyu alipokuwa yu hai!

Na tuangalie kwa nini mwanadamu anaogopa kufa. Dalili iko wazi, uwepo una uhusiano pamoja na ulimwengu na maarifa, na haiwezekani uwepo kuafikiana na kutokuwepo, hivyo sisi ni wageni wa hali ya kutowepo, na hili ni jambo la kawaida.

Na kama tukijua kwamba mauti humaanisha kumalizika kila kitu, na itikadi yetu ikawa kwamba kwa mauti kinamalizika kila kitu, hakika ukweli utakuwa pamoja nasi tunapoogopa, na tunapoogopa hata jina lake, kwa sababu mauti yanatupokonya kila kitu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 196 1/13/2017 3:33:28 PM

Lakini kama tutazingatia mauti ni mwanzo wa maisha mapya yenye kudumu yanayochungulia kwenye ulimwengu mkubwa, hakika itakuwa ni kawaida kutoyaogopa, bali tutawaombea baraka wale ambao wanayaelekea mauti hali wamenyanyua vichwa kuelekea kwenye mauti hayo.

## 2. Rundo jeusi:

Tunajua baadhi ya watu hawazingatii mauti kuwa ni kumalizika, wala hawakanushi maisha baada ya kufa, lakini wao pamoja na hayo wanaogopa mauti, kwa sababu kurasa za amali zao ni nyeusi. Na ni nyeusi kiasi kwamba wanaogopa kutokana na adhabu baada ya kufa. Na hawa wana haki ya kuogopa, wao wanafanana na waovu hatari wanaogopa kutoka jela, kwa sababu wao wanajua wakitolewa watakwenda kunyongwa.

Ama wale ambao hawaoni mauti kuwa ni kumalizika na hawana rundo jeusi kwa nini wanaogopa mauti? Hakuna shaka hakika wao wanataka maisha kwa kila uwepo wao vilevile, lakini ili wazidishe amali njema kwa kujiandalia maisha yao mapya baada ya mauti, na wao wanapokea mauti katika njia ya lengo, fahari na ridhaa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

## Mitazamo miwili yenye kutofautiana:

Tumekwishasema kwamba hakika watu wako makundi mawili. Walio wengi ni kundi ambalo linaogopa mauti, na wachache ni kundi ambalo linakaribisha mauti katika njia ya lengo kubwa, kama vile kufa shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, au kwa uchache wanapohisi kwamba maisha yao ya kawaida yanahofiwa kumalizika, hakika wao hawahisi huzuni juu ya hilo.

Dalili ni kwamba makundi haya mawili yana mitazamo miwili tofauti:

**Kundi la kwanza:** Ima haliamini ulimwengu wa baada ya mauti, na kama lina imani, hakika ni imani yenye kulegalega isiyo imara, na hivyo hakika linazingatia wakati wa mauti, ni muda wa kuagana na kila kitu. Ndio, jambo hili linaogopesha, na kwamba linaumiza, kutoka kwenye nuru kwenda kwenye giza kaburi la jumla, sawa kabisa na muovu ambaye wanampeleka mahakamani na kosa lake liko wazi, na hivyo hakika hofu inatawala kwake.

**Kundi la pili:** Linaona mauti ni uzao mpya, kutoka katika mazingira finyu ya giza la dunia kwenda kwenye ulimwengu mpana na mkubwa zaidi na wenye kuangaza. Kuwa huru mbali na tundu dogo na finyu, na kupaa katika mbingu pana. Na kutoka katika mazingira ambayo ni kituo cha mizozo na ugomvi, dhulma, chuki na vita na kuingia katika mazingira yaliyoepukana na sifa zote hizo. Na kwa hiyo ni kawaida hawa kutoogopa mfano wa mauti haya na wanasema kama alivyosema Imamu Ali عليه السلام: “Mtoto wa Abutalib anaburudika na mauti kuliko mtoto anavyoburudika na ziwa la mama yake.”

Na hivyo sio katika mlango wa bahati mbaya kukutana na historia ya Kiislamu na watu kama Imamu Husein عليه السلام na wafuasi wake wenye ikhilasi, ambao kila inapokaribia saa ya kufa kwao kishahidi nyuso zao zinang’ara kwa shauku kwa kuona na kukutana na kipenzi. Na kwa sababu hii vilevile tunasoma katika historia ya Imamu Ali عليه السلام iliyojaa ufahari na utukufu kwamba lilipoteremka pigo la upanga la huyu muovu juu ya kichwa chake alipaza sauti: “Naapa kwa Mola wa Kaaba hakika nimefaulu.”

Ni jambo la kawaida kwamba maana ya maneno haya sio mwanadamu kuitupia nafsi yake kwenye maangamizi na kuyaacha maisha bila ya kunufaika nayo katika njia ya malengo makubwa. Hakika makusudio ni kunufaika na maisha kwa njia sahihi, bila ya kuogopa mwisho wake, hususan ikiwa mwisho ni katika lengo tukufu.

# TAFAKARI NA UJIBU:

1. Kwa nini watu wanaogopa mauti? Na nini dalili juu ya hilo?
2. Kwa nini baadhi ya watu wanatabasamu kwa ajili ya mauti na wana shauku na shahada katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu?
3. Kwa kitu gani tunaweza kufafananisha wakati wa kufa? Nini anahisi kila muumini na kafiri katika wakati huo?
4. Je, mmeona katika maisha yenu watu wasiogopa mauti? Nini kumbukumbu yenu juu ya hao?
5. Nini mantiki ya Imamu Ali عليه السلام juu ya mauti?

**Somo la Pili:**

**Marejeo yanayapa maisha maana:**

Kama tukiangalia maisha katika dunia hii bila ya mazingatio yoyote ya maisha mengine, hakika yatakuwa bila ya maana. Hii inafanana kabisa na hatua ya maisha ya mimba isiyojua maisha ya dunia hii. Mimba inabakia miezi kadhaa katika giza ndani ya tumbo la mama, na kama akifikiria, yaani, mwanadamu kuhusu hatua ya mimba katika maisha yake hakika atastaajabu.

Kwa nini mimi ni mfungwa katika jela yenye giza?

Kwa nini ni wajibu niogelee kwenye maji na damu?

Na nini matokeo ya umri wangu?

Nimetoka wapi, na nini sababu ya kuja kwangu?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 199 1/13/2017 3:33:28 PM

Ama kama angejulishwa kwamba hatua hiyo ni utangulizi, ambapo viungo vyako vinajiunda na kuwa na nguvu, kwa ajili ya maandalizi ya harakati katika ulimwengu mpana. Na baada ya kupita miezi tisa, utatoka kwenye jela hii, na kwenda kutembea katika ulimwengu ambao humo kuna jua lenye kuangaza, mwezi wenye kutoa nuru, na miti ya kijani, mito yenye kutiririka na vitu vingine. Na wakati huo atapumua kwa furaha na kusema: Sasa nimeshafahamu falsafa ya uwepo wangu hapa. Hatua hii ni utangulizi, ni kanuni ya kuanzia, shule ya maandalizi ya kufikia chuo kikuu.

Ama ikiwa uhusiano wa maisha utakatika katika dunia hii, hakika kila kitu kitakuwa giza na bila ya kuwa na maana. Na maudhui ni yale yale kuhusiana na maisha katika dunia hii na ulimwengu wa baada ya mauti. Nini dharura ya kuishi takriban miaka sabini katika dunia hii baina ya matatizo? Sehemu ya muda wa umri wetu unakuwa bila ya uzoefu, na tunapopata uzoefu umri wetu unakuwa umeshamalizika! Na muda wa umri wetu ni wajibu tuutumie katika kusoma na kupata elimu. Na wakati tunapopata hayo mvi zinakuwa zimekwisha shambulia vichwa vyetu!

Kisha kwa nini tunaishi, kwa ajili ya kula, kuvaa na kulala? Na kuendelea katika maisha haya ya mazoea makumi ya miaka? Je, ni haki mbingu hii pana, na ardhi hii yenye kutandaa, na utangulizi wote huu wa kupata elimu na kuchuma uzoefu, walimu wote na walezi wote, je yote hayo ni kwa ajili ya kula na kuvaa, ni kwa ajili ya maisha haya yenye kuporomoka?

Ni kwa sababu hii unapatikana upotevu katika maisha kwa wale ambao hawakubali marejeo kuwa ndio msingi, kwa sababu wao hawawezi kuzingatia haya mambo madogo kuwa ni lengo katika maisha, na wala hawaamini ulimwengu wa baada ya mauti. Na mara nyingi inaonekana idadi ya hawa wanajinyonga ili kujinasua na mfano wa maisha haya ya kipuuzi ambayo hayana maana. Lakini



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 200 1/13/2017 3:33:28 PM

tukiamini kwamba dunia hii ni shamba la Akhera, hivyo ni lazima tupande mbegu na tuvune matunda katika maisha yetu ya kudumu na ya milele.

Dunia ni Chuo Kikuu, ni wajibu tupate kwacho elimu na tujiandae kwa ajili ya maisha katika ulimwengu wa kudumu, dunia ni daraja, ni wajibu tupitie juu yake. Katika hali hii maisha hayatakuwa katika dunia hii ni upotevu na bila ya maana, bali ni utangulizi wa maisha yenye kudumu milele, na vyovyote tutakavyojitahidi katika njia yake basi itakuwa ni kidogo.

**Kuamini marejeo ni sababu muhimu sana katika malezi:**

Kwa kuongezea katika hayo hakika kuamini uwepo wa mahakama kubwa katika Akhera ni dharura sana katika maisha ya sasa. Jaalieni kwamba itangazwe katika nchi fulani, kwamba ndani ya siku fulani mtu hatowajibishwa kwa kosa lolote litakalotokea, na kosa lake halitojumuishwa katika rundo la makosa aliyonayo, na watu wako huru bila kuwajibishwa na adhabu yoyote wakati watakapofanya wayatakayo, na kwamba polisi na jeshi hawatafanya kazi siku hiyo, na mahakama hazitafanya kazi pia. Fikiria hali ya jamii katika siku hiyo!

Hakika kuamini kufufuliwa katika Siku ya Kiyama, ni imani ya kuwepo mahakama kubwa ambayo haiwezekani kulinganishwa na mahakama hizi za kiulimwengu. Sifa za mahakama hii ni kama zifuatazo:

1. Ni mahakama isiyoathirika na ushauri, wala mafungamano na mahusiano, wala hazibadiliki rai za hakimu kwa nyaraka za uongo na za kuzua.
2. Ni mahakama isiyohitaji urasimu na utangulizi ambao mahakama za ulimwengu huu zinahitajia, na kwa hiyo hakika



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 201 1/13/2017 3:33:28 PM

haitorefusha, inatumia kusoma nyaraka kwa haraka na kwa umakini na kutoa hukumu.

**3.** Ni mahakama ambayo nyaraka za kutuhumiwa watu ni zilezile amali zao, yaani hakika amali zao zitahudhuria mahakamani na kujulikana mafungamano yao na mtendaji, kiasi kwamba hakutabakia nafasi ya kukanusha.

**4.** Mashahidi wa mahakama, ni mikono, miguu, masikio, macho, ulimi na ngozi ya mwili wa mwanadamu, hata ardhi na kuta za nyumba ambazo limefanyika kosa humo. Hawa ndio mashahidi ambao haiwezekani kuwakataa, nayo ni athari za kawaida za amali za mwanadamu ambazo hazikanushwi.

**5.** Katika mahakama hii, hakimu humo ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu ambaye anajua kila kitu, na wala hahitajii kitu au yeyote na ni mwadilifu kuliko wote.

**6.** Kisha adhabu katika mahakama hii sio kulingana na maamuzi na kanuni, bali ni amali zetu ambazo zitaunda na kuanza kutuadhibu au kwa kumiminiwa rehema juu yetu.

Hakika kuamini mfano wa mahakama hii inatufikisha kwenye nafasi ya kwenda katika hatua ya Imamu Ali عليه السلام aliposema:

"Wallahi kulala juu ya miba na kukesha au kukokotwa katika minyororo nikiwa nimefungwa, inapendeza zaidi kwangu kuliko kukutana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Siku ya Kiyama ilihali mimi ni mwenye kudhulumu baadhi ya waja Wake na mwenye kupora kitu katika mali."[32]

Hakika kuamini mahakama hii kunamsukuma mwanadamu kuweka mkono wa ndugu yake juu ya chuma cha moto, kwa saba-

[32] *Nahjul-Balaghah*, khutuba ya 224.

bu ametofautisha kati yake na wengineo katika kugawa Hazina ya Waislamu. Kelele yake inapopaa anamnasihi na kumwambia:

"Ewe Aqil unalia kwa chuma alichokipasha moto mwanadamu kwa mchezo wake, na unanikokota kwenda kwenye moto aliouwasha Muumba Wake kwa ghadhabu Yake?!!"

Je, inawezekana kumdanganya mtu anayemiliki imani hii? Je, unaweza kununua dhamira yake? Je, inawezekana kumuondoa katika mwendo wake wa haki na kumpa tamaa? Na Qur'ani Tukufu inasema: Wenye madhambi watakapoona daftari la amali zao watapiga kelele: "Eee ole wangu kina nini kitabu hiki, hakiachi dogo wala kubwa isipokuwa kimelihesabu."

Vivyo hivyo yanapanda mawimbi ya nguvu za hisia na kuhisi majukumu mbele ya kila amali katika undani wa roho ya mwanadamu. Inazuia uasi wa mwanadamu mbele ya upotovu na kupotea, dhuluma na uadui.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Ikiwa hakuna ulimwengu mwingine baada ya maisha finyu katika dunia, nini kitatokea?
2. Kwa nini watu wanaopinga msingi na marejeo wanajinyonga?
3. Nini tofauti baina ya mahakama ya Akhera na mahakama za dunia hii?
4. Amirul-Muuminina Imamu Ali عليه السلام amesemaje kwa ndugu yake Aqili? Alitaka nini, na Imamu Ali alimjibu nini?

**Somo la Tatu:**

**Mfano wa mahakama ya Akhera ndani ya nafsi zetu:**



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 203 1/13/2017 3:33:28 PM

Pamoja na kwamba mas'ala ya maisha baada ya mauti ni maudhui mpya, na mahakama kubwa siku ya Kiyama kwa mwanadamu aliyefungwa katika mipaka ya dunia hii, isipokuwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameshatujaalia mfano mdogo wa mahakama hiyo katika dunia hii. Jina lake ni mahakama ya dhamira, lakini ni wajibu tusisahau kwamba sisi tumekwishasema ni mfano mdogo. Acha tufafanue maudhui haya: Hakika mwanadamu anahukumiwa mbele ya mahakama nyingi juu ya amali ambazo anazifanya.

**Mahakama ya kwanza:** Ni ile mahakama ya kawaida ya mwanadamu. Pamoja na kwamba uwepo wa mfano wa mahakama hizi una athari kubwa katika kupunguza makosa, lakini mahakama hizi kwa muundo wake ulivyo hatuwezi kutarajia kutoka katika mahakama hizo utekelezaji wa uadilifu kwa sura ya ukamilifu. Kwa sababu kama wataingilia au kupenya katika mahakama hizo watawala wasio wema na kanuni zisizokuwa sahihi, hakika hali yake itakuwa inajulikana. Ni rushwa, kujuana, maslahi na uhusiano maalum, na mchezo wa siasa, na mas'ala mengine elfu, yote yanaathiri kwa namna fulani ukosefu wa uadilifu katika maamuzi, ni kama ilivyosemwa: Kutokuwepo kwake ni bora zaidi, kwa sababu kuwepo kwake kunakuwa ni kitendea kazi cha utekelezaji wa malengo ya ufisadi!

Na ikiwa kanuni zake ni adilifu, makadhi wake wamejipamba kwa uchamungu, basi hakika vilevile itatokea kwamba wengi miongoni mwa waovu watatekeleza kazi zao ovu kwa uhodari kiasi kwamba hawataacha njia juu yao. Au hakika wao watafanya vitendo vyao vya udanganyifu na vya uzushi kiasi kwamba watadhoofisha mkono wa makadhi na kuzifanya kanuni zisiwe na athari.

**Mahakama ya pili:** Ambayo ina hesabu kali zaidi na makini zaidi ni mahakama ya adhabu ya matendo. Hakika matendo yetu yana athari zitakazotufuata sasa hivi au baadaye. Ikiwa hukumu hii



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 204 1/13/2017 3:33:28 PM

si ya jumla basi kwa uchache hakika inasadiki kwa walio wengi.

Tumekwishaona serikali iliyoenea ujeuri na dhulma na ukandamizaji, na kufanya itakavyo, lakini ilitumbukia katika kisima ilichokichimba na ikafuatwa na vitendo vyake, na ikaanguka kiasi kwamba haikubakiwa isipokuwa na laana juu yake.

Na kwa kuwa adhabu ya matendo ni uhusiano wa sababu na kisababishi, na uhusiano wa kiini cha nje, hivyo ni nadra kuweza yeyote kukimbia kutoshikwa. Na kasoro pekee inayokubalika katika mahakama hii ni kwamba sio ya jumla kwa wote. Na kwa sababu hii hakika haiwezekani kutufanya tuwe mbali na kuihitajia mahakama kubwa Siku ya Kiyama.

**Makahama ya tatu:** Ni ile ambayo ina hisabu makini zaidi, nayo ni mahakama ya dhamira. Kwa hakika kama ambavyo mfumo wa jua kwa mpangilio wake wa ajabu umekusanywa katika umbo dogo ndani ya chembe, hivyo inawezekana kusema kwamba mahakama ya Akhera ipo kwa sura ndogo ndani mwetu kwa sababu inapatikana nguvu isiyojulikana ndani ya mwanadamu ambayo wanafalsafa wanaiita kwa jina la akili ya utendaji, na Qur'ani Tukufu inaiita (Nafsi yenye kujilaumu), na leo hii inaitwa kwa jina la dhamira. Mwanadamu hafanyi kitendo kibaya au kizuri ila haraka inajiunda mahakama hii bila ya fujo na kwa kila juhudi na kuanza kuhukumu, na matokeo ya hukumu yanakuwa kwa namna ya adhabu au kushajiisha nafsi.

Na wakati mwingine mahakama hii inafanya kazi ya kuwachapa waovu na kuwaadabisha kiasi kwamba wao wanatamani mauti kwa moyo mkunjufu, na wanapendelea mauti badala ya uhai, na wanaandika katika wasia wao kuwa hakika sisi tumejinyonga ili tuondokane na adhabu ya dhamira. Na wakati mwingine inamshajiisha mwanadamu katika kazi yake nzuri kiasi kwamba inamletea furaha,



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 205 1/13/2017 3:33:28 PM

sururi, utulivu wa kina ambao hauelezwi wala haujulikani mpaka wake kwa utamu wake wa ndani.

Hakika mahakama hii ya ajabu ina sifa kadhaa:

**1.** Kadhi, shahidi, mtekeleza hukumu na wanaoangalia katika mahakama hii ni mmoja tu, nayo ni dhamira ambayo inatoa ushahidi na kutoa hukumu na inafanya juhudi kwa nguvu zake ili kutekeleza hukumu.

**2.** Kinyume na mahakama zilizojaa fujo ya kawaida, ambapo inawezekana kurefuka muda wa hukumu, hakika mahakama ya dhamira ni ya haraka sana, ambapo haihitaji wakati na muda. Ndio, mara nyingi, na kuthibitisha tuhuma na kuondoa pazia la kughafilika ambalo linawezekana kutokea na kuwa ni haja katika wakati wa dharura, lakini baada ya kufichua nyaraka hakika kutoa hukumu inakuwa ni haraka na kwa uhakika.

**3.** Hukumu ya Mahakama hii isiyo na shaka haina kukata rufaa na kupitia upya, wala hukumu yake haitumwi mahakama ya juu ya rufaa.

**4.** Mahakama hii haiadhibu tu, bali inatoa zawadi kwa mwenye kustahiki hayo, na hivyo ni mahakama ambayo humo anahukumiwa mwenye dhambi na mwenye wema. Muovu anaadhibiwa na mwema analipwa thawabu kulingana na amali zake.

**5.** Adhabu ya mahakama hii haifanani abadani na adhabu ya kawaida, ambapo katika dhahiri hakuna jela wala fimbo wala ubao wa kunyongea, lakini mara nyingi inaunguza na kufunga kwa namna ambayo dunia inakuwa finyu kwa mwanadamu licha ya upana wake, na inabana na kuwa ndogo hadi inakuwa mfano wa jela binafsi ya kificho.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 206 1/13/2017 3:33:28 PM

**Hitimisho:** Hakika mahakama hii sio katika aina za mahakama hizi za duniani, bali ni katika mahakama za Siku ya Kiyama. Na mahakama hii ni tukufu kiasi kwamba Qur'ani Tukufu inaapa kwayo na kuisifia kwa kiwango cha mahakama ya Kiyama na kusema:

"Naapa kwa Siku ya Kiyama. Na naapa kwa nafsi yenye kujilaumu. Je, mwanadamu anadhani hatutokusanya mifupa yake. Ndio. Bali tunaweza kusawazisha vidole vyake." Pamoja na yote hayo hakika mahakama hizi, humo kuna baadhi ya kasoro za udunia wake, hivyo haitufanyi tusihitajie mahakama ya Siku ya Kiyama kwa sababu:

1. Dhamira haijui kila kitu, bali inaenea duara la fikra na ambayo anayaainisha mwanadamu.
2. Mara nyingi mwanadamu mdanganyifu hodari anaweza kudanganya dhamira yake na kuifanyia hila.
3. Na wakati mwingine unadhoofika wito wa dhamira kwa baadhi ya waovu kiasi kwamba haifikii kwenye usikivu wake.

Na hapa inabainika dharura ya uwepo wa mahakama kubwa ya nne ya siku ya Kiyama.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Mwanadamu anahukumiwa katika mahakama ngapi?
2. Ni zipi alama za mahakama ya kwanza na jina lake?
3. Nini sifa za mahakama ya pili?
4. Nini sifa za mahakama ya tatu?
5. Nini sifa na nukta za udhaifu katika mahakama ya dhamira? Zitaje?

# SOMO LA NNE:

**Marejeo yanapodhihirika kuwa ni sehemu ya maumbile:**

Mara nyingi inasemwa, hakika kumjua Mwenyezi Mungu kupo katika maumbile ya mwanadamu, na kama tukitafuta katika uelewa ndani ya mwanadamu tungekuta imani na mafungamano yake na msingi miongoni mwa misingi iliyopo nyuma ya mazingira. Imejengwa kwa elimu na ratiba na lengo la ulimwengu huu, lakini jambo hili halikomei katika mas'ala ya tauhidi, ambapo ni lazima kuwepo misingi yote ya matawi ya dini ya kimsingi katika mas'ala ya kimaumbile, vinginevyo usingepatikana uelewano na kuafikiana baina ya vyombo vya sharia na maumbile – (tazama hayo kwa makini).

Sisi tutakapozirejelea nafsi zetu na tukadurusu undani wetu hakika sisi tutasikia; Hakika maisha hayamaliziki kwa mauti, bali mauti ni dirisha la ulimwengu wenye kubakia.

Ili tufahamu ukweli huu ni lazima kuangalia nukta zifuatazo:

**1. Kuambatana na hali ya kupenda kubakia:**

Ikiwa ni haki kwamba mwanadamu ameumbwa kwa ajili ya kumalizika na kutoweka, hivyo ni lazima aambatane na hali ya kupenda kumalizika, na kwamba aburudike katika mwisho wa umri, kwa mauti. Lakini tunaona kwamba mauti (kwa maana ya kutoweka) sio tu hayakubaliki kwake, bali anakimbia hali hiyo kwa kila uwepo wake. Hakika kukimbia nyuma ya maisha na umri mrefu, na kutafuta utajiri wa ujana, na kusafisha maji ya uhai, yote hayo ni dalili ya ukweli huu.

Hakika uhusiano huu na kupenda hali ya kubakia unaonyesha kwamba sisi tumeumbwa kwa ajili ya kubakia. Kama tungekuwa tumeumbwa kwa ajili ya kumalizika na kutoweka, hivyo kusingekuwa na maana ya upendo na uhusiano huu.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 208 1/13/2017 3:33:28 PM

Hakika aina zote za ashki au upendo au uhusiano uliopo ndani mwetu zinakamilisha uwepo wetu, na vivyo hivyo hakika kupenda kubakia au kutamani kubakia vilevile ni ukamilisho wa uwepo wetu. Msisahau kwamba sisi tunaendeleza utafiti wa marejeo baada ya kukubali kwetu kuwepo Mwenyezi Mungu Mwenye hekima, Mjuzi, Mwenye kutakasika, na sisi tunaitakidi kwamba kila kilichoumbwa katika uwepo wetu hakika ni kulingana na mpangilio wa hesabu makini, hivyo ni lazima hali ya mwanadamu kupenda kubakia iwe ni kulingana na mpangilio wa lengo, nalo ni kuwepo ulimwengu mwingine baada ya ulimwengu huu.

## 2. Kufufuliwa kwa watu wengine:

Kama inavyotaja historia ya binadamu, hakika dini ilikuwepo miongoni mwa watu waliotangulia na tangu zamani, na haya yanaonyesha juu ya itikadi imara aliyokuwa nayo mwanadamu wa zamani juu ya mas'ala ya maisha baada ya mauti.

Hakika athari ambazo amezivumbua mwanadamu wa zamani, na hata mwanadamu wa kabla ya historia na njia ya kujenga makaburi ya wafu, na namna ya kuzika, yote yanaonyesha juu ya ukweli huu, nayo ni kwamba wao walikuwa wanaamini maisha baada ya mauti. Hakika itikadi hii iliyojikita ndani ya mwanadamu haiwezekani kuizingatia kuwa ni mas'ala mepesi au kwamba yalikuwa ya mila au ni matokeo ya kuelezwa.

Hakika sisi tunapokuta itikadi imekita na ipo katika historia katika jamii ya mwanadamu, hakika inaonyesha juu ya kwamba ipo katika maumbile, kwa sababu maumbile ndio peke yake ambayo yanaweza kubakia mbele ya mnyumbuliko wa zama na mwendelezo wa zama na mabadiliko ya kijamii na kifikira, vinginevyo hakika ada na mila zinasahaulika na kumalizika kwa kupita zama.

Hakika kuvaa vazi fulani mara nyingi au kwa kuiga, mazoea haya yanabadilika pamoja na kubadilika mazingira na sehemu au kwa kupita muda. Ama mapenzi ya mama kwa mtoto wake ni utashi wa asili, na hivyo hauwezekani kuondolewa na mabadiliko ya mazingira wala kwa kupita muda na wala hauwezekani kuachwa kwa kusahau. Na mfano wa utashi huu ni dalili juu ya kwamba upo katika maumbile ya mwanadamu.

Maulamaa wanaposema: "Hakika utafiti makini unaonyesha kwamba makundi ya binadamu wa kwanza yalikuwa na madhehebu, kwa sababu walikuwa wanazika maiti zao kwa njia maalum pamoja na vifaa na nyenzo za kazi zao, kwa njia hii na kwa muundo huu walikuwa wanaakisi itikadi yao kwa uwepo wa ulimwengu mwingine."

Na vilevile tunajua kwa sura nzuri kwamba watu wa zamani walikuwa wanakiri uwepo wa maisha baada ya mauti hata kama muundo huo ulikuwa wa makosa, na wanaitakidi kwamba ni maisha mengine yanayofanana na ya dunia hii, na kwamba maiti anahitaji zana zake na nyenzo za kazi yake.

**3. Hakika uwepo wa mahakama ya ndani kwa jina la dhamira ni dalili nyingine juu ya maumbile ya marejeo:**

Na kama tulivyosema mwanzo hakika sote tunahisi kwa uwazi kwamba ndani mwetu kunapatikana mahakama inayohesabu amali zetu, inatulipa kheri katika amali zetu, ambapo tunahisi raha ya ndani na kutuenea furaha kubwa. Haiwezekani kuelezea utamu ambao unapatikana kutokana na hayo kwa kalamu yoyote. Na kuteremsha adhabu hususani kuhusiana na dhambi kubwa, ambapo anahisi mwenye dhambi uchungu wa maisha.

Na mara nyingi inaonekana kwamba watu wengi ambao wamefanya makosa makubwa kama vile kuuwa, na wakakimbia

walirejea wenyewe na kujisalimisha kwenye uadilifu na kisha kujinyonga, na dalili juu ya hilo ni kujinasua kutokana na adhabu ya dhamiri.

Hakika mwanadamu anapoona mahakama hii ya ndani anajiuliza:

"Namna gani inawezekana kiumbe kidogo kubeba mfano wa mahakama hii, wakati ambapo ulimwengu mpana haumiliki mfano wa mahakama hii?" Na hivyo tunaweza kuthibitisha kwa njia ya maumbile itikadi ya kuwepo marejeo kwa kutumia nukta tatu:

**1.** Kwa njia ya kupenda kubakia.

**2.** Kwa njia ya uwepo wa imani kupitia historia ya mwanadamu.

**3.** Kwa njia ya mfano wake mdogo ndani ya mwanadamu.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Namna gani inawezekana kujua mambo yasiyokuwa ya maumbile?

**2.** Kwa dalili gani mwanadamu anapenda kubakia, na namna gani inawezekana hali hiyo kuwa ni dalili juu ya itikadi ya marejeo?

**3.** Je, watu wa zamani walikuwa wanaamini marejeo?

**4.** Namna gani mahakama ya dhamira inatupa thawabu na au kututeremshia adhabu?

**5.** Nini mafungamano au uhusiano baina ya mahakama ya dhamira na mahakama kubwa ya Siku ya Kiyama?

# SOMO LA TANO:

## Utafiti katika mizani ya uadilifu:

Kwa utafiti mfupi katika mpangilio wa ulimwengu wa uwepo na kanuni za viumbe, hakika sisi tutaona kwamba kila sehemu kuna kanuni zinazotawala kila kitu. Na katika mwili wa mwanadamu mpangilio huu unatawala kwa namna ya umakini na ya ajabu. Hakika mabadiliko au kasoro ndogo inasababisha maradhi au mauti.

Mfano katika kiungo cha jicho, moyo, ubongo, unaona kwamba kila kitu kimewekwa katika mahala pake kwa umakini na kwa umbo linalohitajika. Na uadilifu huu na mpangilio huu sio tu upo katika mwili wa mwanadamu bali upo katika ulimwengu wa viumbe vyote.

## Kwa uadilifu zimesimama mbingu na ardhi:

Hakika mamilioni ya mada za Atom ndogo sana yanaweza kubebwa na ncha ya pini. Hivyo fikirieni ni namna gani inapasa muundo wa Atom kuwa makini na uwe umepangiliwa kiasi kwamba uendelee kuishi kwa mamilioni ya miaka.

Hakika hayo ni kwa sababu kuna uadilifu na hesabu makini kabisa katika mpangilio wa elektronati na protonati, na haihitaji chombo chochote, kikubwa au kidogo, kwa mpangilio huu wa ajabu.

## Hiyari na uhuru wa matakwa:

Ukweli ni kwamba mwanadamu anatofautiana tofauti kubwa ya kimsingi na viumbe vya ulimwengu, nayo ni kwamba anamiliki uhuru wa matakwa na hiyari. Kwa nini Mwenyezi Mungu amemuumba huru na akamwachia hiyari katika kufanya analotaka?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 212 1/13/2017 3:33:28 PM

Dalili, hakika yeye kama hakuwa huru asingepita katika njia ya ukamilifu, na sifa hii kubwa inamhakikishia ukamilifu wa kimaanawii na kimaadili. Mfano kama mtu akilazimishwa kuwasaidia wanyonge na kufanya amali za kheri kwa maslahi ya jamii, hakika vitendo hivi vya kheri pamoja na hayo havitamletea mwenye kuvifanya ukamilifu wowote wa kitabia na ubinadamu, lakini ikiwa mtu anafanya moja ya kumi ya kazi ya amali hiyo ya kibinadamu yeye mwenyewe, hakika anapiga hatua kwa hilo kuelekea kwenye ukamilifu wa kitabia na kimaanawi.

Na hivyo hakika sharti la kwanza la ukamilifu wa kimaanawi na kitabia ni kuwepo hiyari na uhuru wa matakwa kwa mwanadamu na sio kulazimisha kama sababu za kimazingira za kulazimika katika ulimwengu. Na ikiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa zawadi hii kubwa kwa mwanadamu, hakika ni kwa lengo hili tukufu.

Lakini neema hii kubwa inafanana na ua la waridi ambalo linamea pembezoni mwa miba, nayo ni watu kutumia uhuru huu na kuuchafua kwa dhulma, ufisadi na makosa. Hakika hakuna kizuizi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuteremsha balaa kwa namna asiyoifikiria mchafuzi huyo, kama kupoozesha mkono wake, kupofuka jicho lake na kukatwa ulimi wake. Ni sahihi kwamba hali hii itamfanya yeyote yule asiutumie uhuru kwa matumizi mabaya, na asielekee kwenye kosa, lakini uchamungu wa namna hii kwa uhakika una pande za kulazimisha na wala hauleti fahari kwa mwanadamu kwa sura yoyote ile, bali ilikuwa ni hofu ya adhabu kali na ya haraka.

Hivyo, ni lazima mwandamu awe huru, na asimame mbele ya mitihani mbalimbali ya Mwenyezi Mungu na abaki amehifadhiwa – isipokuwa katika hali za kipekee – na adhabu ya haraka, ili ibainike thamani ya uwepo wake.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 213 1/13/2017 3:33:28 PM

Lakini inabakia maudhui moja, nayo ni: Ikiwa itabakia hali katika muundo huu na akachagua kila mmoja njia yake, hakika kanuni ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu ambao unafunika ulimwengu itatenguliwa. Na hapa tuna yakini kwamba kuna mahakama kwa ajili ya wanadamu, wote watasimama mbele yake bila ya kubagua, ili wapate malipo ya amali zao katika uadilifu mkuu wa Muumba wa viumbe.

Je, inawezekana kusimama watu mfano wa Namrudi, Firaun, Jankis, Qarun kwa dhulma na ukandamizaji walioufanya muda wote wa umri wao bila ya kuwepo na hesabu wala daftari kwa ajili yao? Je, wanalingana waovu na wachamungu katika kipimo cha uadilifu wa kiungu? Ambapo Qur'ani Tukufu inasema: "Je, tuwafanye Waislamu kama waovu. Namna gani mnahukumu." (Sura al-Qalam: 35 na 36). Na katika sehemu nyingine: "Au tuwajalie wachamungu kama waovu." (Sura Swaad: 28).

Ni sahihi kwamba baadhi ya wenye madhambi watapata malipo ya amali zao katika dunia hii, na ni sahihi kwamba mahakama ya dhamira ni mas'ala muhimu, na ni sahihi kwamba kulipiza kisasi kutamwenea mwanadamu anapodhulumu, anapokosea na kukandamiza. Lakini tukifikiri vizuri hakika sisi tutaona kwamba mambo haya matatu sio ya jumla ili dhalimu na mkosaji apate kwa kiwango cha dhulma yake na kosa lake, kuna wengi ambao wanakimbia kutokana na malipo ya vitendo vyao na adhabu ya dhamira na kisasi cha vitendo vyao viovu au hapati adhabu inayotosha.

Ni lazima kuwepo na mahakama adilifu kwa ajili ya watu mfano wa hawa, ambayo haiachi amali ndogo ya kheri au ya shari bila ya kuhesabiwa, vinginevyo hakika msingi wa uadilifu hautotimia.

Na hivyo hakika kukubali kuwepo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na uadilifu Wake kunalingana na kukubali kuwepo kwa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 214 1/13/2017 3:33:28 PM

Siku ya Kiyama na ulimwengu wa Akhera, na haya mawili haiwezekani kuyatenganisha baina yao.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Namna gani zinasimama mbingu na ardhi kwa uadilifu?
2. Kwa nini mwanadamu amepewa uhuru wa matakwa na hiyari?
3. Nini kitatokea kama watu waovu watapata malipo yao haraka kutokana na vitendo vyao katika dunia hii?
4. Kwa nini malipo ya amali, adhabu ya dhamiri na kulipiza kisasi cha vitendo havizuii kuwepo kwa mahakama ya Siku ya Kiyama?
5. Kuna mafungamano gani baina ya uadilifu wa Mwenyezi Mungu na mas'ala ya marejeo?

## SOMO LA SITA:

**Tumekwishaiona Siku ya Kiyama mara nyingi katika dunia hii:**

Aya za Qur'ani Tukufu zinabainisha kwa uwazi ukweli huu kwamba wapagani na makafiri wengine, sio katika zama za Nabii ﷺ tu, bali hata katika zama zingine pia, walikuwa wanaona kwamba mas'ala ya marejeo na kuhuisha wafu yanaleta mshangao na hofu katika nyoyo za watu, hadi wao walikuwa wanazingatia kuwa hicho ni kichaa na wanawaambia baadhi yao: "Je tuwaonyeshe mtu anayewaambia mtakapochambuliwa mapande mapande mtakuwa katika umbo jipya. Amemzulia Mwenyezi Mungu au ana wazimu." (Sura Sabaa: 7 – 8).



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 215 1/13/2017 3:33:29 PM

Ndio, itikadi ya ulimwengu baada ya mauti na kuhuisha wafu inahesabiwa kuwa ni aina ya kichaa kutokana na ujahili na ukosefu wa fikra, au tuhuma juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kama walivyokuwa wanazingatia kutembea wanyama katika vitu vilivyoganda (barafu) ni aina ya kichaa. Lakini Qur'ani Tukufu imekuja na dalili mbalimbali mbele ya fikra hizo na inawezekana kunufaika nazo watu wa kawaida, na vile vile maulamaa wakubwa, kila mmoja kulingana na uwezo wake.

Pamoja na kwamba ufafanuzi wa hoja zote za Qur'ani katika nyanja hii unahitaji kutunga kitabu maalum, lakini sisi tutaleta baadhi yake hapa:

**1.** Qur'ani Tukufu inawaambia hao: Hakika nyinyi kila siku mnaona katika maisha yenu ya duniani ushahidi wa marejeo, namna gani vitakufa viumbe kisha kuhushwa mara nyingine, je, mnashaka na marejeo baada ya hayo?

وَاللَّهُ الَّذِي أَرْسَلَ الرِّيَاحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَسُقْنَاهُ إِلَىٰ بَلَدٍ مَيِّتٍ فَأَحْيَيْنَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ كَذَٰلِكَ النُّشُورُ

**"Na Mwenyezi Mungu Ndiye anayezituma pepo na ziyatimue mawingu. Nasi tukayafikisha kwenye nchi iliyokufa tukaifufua ardhi baada ya kufa kwake. Ndio kama hivyo kufufuliwa."**
**(Sura al- Fatwir: 9).**

Tuangalie mazingira katika msimu wa kiangazi, kila kitu kinaonyesha mauti, miti haina majani kabisa, maua na matunda, na inabaki imesimama bila ya uhai wala majani yanayochanua, wala ua linalochanua. Kama ambavyo hatuoni maisha yanamea milimani na jangwani.

Na ghafla unakuja msimu wa vuli hali ya hewa inakuwa nzuri, na yanadondoka matone ya mvua ambayo yanaleta



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 216 1/13/2017 3:33:29 PM

uhai. Na ghafla zinaanza harakati katika mazingira yanayodhihirisha majani. Miti inaota majani, maua yanachanua na ndege wanarukaruka juu ya matawi, na (kiyama) kinasimama! Ikiwa uhai haufahamiki baada ya mauti, tusingeona kila mwaka mbele ya macho yetu muonekano huo. Na kama maisha baada ya mauti yangekuwa hayawezekani, au ni kichaa isingejirudia kwenu kama jambo la hisia! Kisha nini tofauti baina ya uhai wa ardhi baada ya ukame na uhai wa mwanadamu baada ya kufa?

**2.** Na wakati mwingine Qur'ani Tukufu inawaongoza hao kwenye mwanzo wa kuumba, na kuwakumbusha uumbaji wa kwanza. Alikuja bedui na kipande cha mfupa ulioharibika kwa Nabii Mtukufu ﷺ na akapaza sauti yake: "Ewe Muhammad nani anaweza kuhuisha mifupa hii iliyobungulika? Niambie nani anaweza?" Huyu bedui alidhani kwamba amekuja na dalili yenye kushinda dhidi ya masa'ala ya marejeo; ikaja Qur'ani Tukufu kwa Nabii Mtukfu ﷺ na kumwamuru: "Sema ataihuisha ambaye aliianzisha mara ya kwanza." (Sura Yaasin: 79).

Nini tofauti baina ya mwanzo wa kuumba na kurudia kuumba?

Na Qur'ani Tukufu inasema hayo katika Aya nyingine, mfano katika sentensi fupi iliyojaa maana nyingi: "Kama tulivyoanza uumbaji wa kwanza tutamrejesha." (Sura al-Anbiyai: 103).

**3.** Na wakati mwingine Mwenyezi Mungu anakumbusha upana wa uumbaji wa mbingu na ardhi na anasema: "Je, aliyeumba mbingu na ardhi ni muweza wa kuumba mfano wao, ndio na Yeye ni muumbaji mkuu. Hakika jambo lake anapotaka kitu hukiambia kuwa na kina kuwa."



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 217 1/13/2017 3:33:29 PM

Hakika wale ambao wanashuku katika mas'ala haya walikuwa ni watu ambao fikra zao hazivuki mazingira ya nyumba zao duni, vinginevyo wangejua kwamba kurejea kwenye uhai ni rahisi zaidi kuliko kuumba, na kwamba kurejeshwa upya uhai kwa uwezo wa muumba wa mbingu na ardhi sio mas'ala magumu.

**4.** Na wakati mwingine inaakisi mbele yao Kiyama na uwezo, anasema: "Ambaye amejalia moto kutokana na mti wa kijani, nanyi mkawa mnauwasha." (Sura Yaasni: 80). Tunapodadisi katika maneno haya ya ajabu ya Qur'ani Tukufu na kupata msaada katika elimu ya kisasa, hakika elimu inatuambia: Tunapochoma ubao wa mti na kupata moto hakika joto hilo ni nguvu, joto na mwanga wa jua. Ulihifadhiwa kwenye mti miaka mingi, wakati ambapo tulikuwa tunaitakidi kwamba nuru na joto la jua limetumika na kumalizika, lakini sisi tunaona leo kwamba mti unakuwa hai kwa mara nyingne, na kuvaa pambo jipya la uhai.

Je, ni vigumu kwa Mwenyezi Mungu ambaye amehifadhi nuru na joto la jua kwa makumi ya miaka katika mti, na kwa punde ametoa yote hayo, je ni vigumu kwake kurejesha maisha upya kutoka kwenye mauti? Vovyote iwavyo tunaona Qur'ani Tukufu namna gani inawajibu wale ambao wanashuku katika marejeo na kuyazingatia kuwa ni kichaa kwa mantiki ya kutoa hoja na uwazi, na inathibitisha marejeo, na tumeshafafanua sehemu ya hayo katika tuliyoyataja.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Kwa nini washirikina wanashangaa mas'ala ya marejeo?

**2.** Namna gani tunashuhudia marejeo katika ulimwengu wa mimea kila mwaka?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 218 1/13/2017 3:33:29 PM

3. Kwa nini Qur'ani Tukufu inaleta Aya za uhai katika kizazi (yaani mimba katika kizazi) kama dalili ya marejeo?
4. Ni kipi Kiyama cha nguvu?
5. Kwa nini Qur'ani Tukufu imetilia mkazo juu ya mti wa kijani?

# SOMO LA SABA:

**Marejeo na falsafa ya kuumba:**

Wengi wanaulizana: Kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuumba?

Na mara nyingi wanakwenda mbali zaidi kuliko hayo: Nini falsafa ya kuumbwa ulimwengu huu mkubwa?

Mkulima anapanda mti kwa ajili ya matunda yake, analima ardhi na anapanda mbegu. Muumba ametuumba kwa lengo gani? Je, Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa anahisi upungufu ili kuondoa upungufu kwa kutuumba sisi? Katika hali hii ni lazima awe ni mwenye kuhitaji, na haya hayaafikiani pamoja na kutokuwahitajia Kwake kwa hadhi Yake, na kwamba Yeye yupo milele na pasipokuwa na mwisho.

Kuna maneno mengi katika kujibu swali hili, lakini inawezekana kufupisha jawabu katika sentensi nyingi na zilizo wazi nazo ni: Hakika ni kosa kubwa kulinganisha sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu na sifa zetu. Sisi viumbe wenye kikomo tunafanya kazi ili kuondoa upungufu, tunasoma ili kuondoa ujinga kwetu, tunafanya kazi ili tupate mali, tunatafuta afya ili tusiugue.

Ama Mwenyezi Mungu Mtukufu Yeye ni uwepo usio na mwisho kwa pande zote. Anapofanya jambo ni lazima tutafute lengo nje ya



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 219 1/13/2017 3:33:29 PM

uwepo Wake mtukufu, hakika Yeye haumbi ili apate faida bali lengo lake ni kuwaneemesha viumbe. Hakika ni jua lenye kuangaza hakuna kuzimika, halihitaji nuru. Yeye anaangaza ili wote wanufaike kwa nuru yake. Na kutoka kwenye dhati Yake yenye kujaa rehema isiyo na kikomo anavisukuma viumbe kuelekea kwenye ukamilifu. Hakika kuumbwa kwetu kutoka katika hali ya kutokuwepo ni hatua kubwa kuelekea kwenye ukamilifu. Kama ambavyo kutuma Manabii na kututeremshia vitabu vya mbinguni na kuainisha kanuni na ratiba, yote hayo ni dalili ya kuelekea kwenye ukamilifu huu.

Hakika dunia hii ni chuo kikubwa na sisi ni wanafunzi wa chuo hiki. Hakika dunia hii ni shamba na sisi ni wakulima wa shamba hili. Hakika dunia hii ni biashara yenye faida na sisi ni wafanyabiashara wake. Hivyo namna gani tunaweza kutokuamini lengo la kuumbwa kwa mwanadamu? Wakati ambapo tukiangalia na kudadisi kwa makini katika viumbe vyote, tutaona kwamba kila kimoja kina lengo.

Katika kiwanda cha mwili wa ajabu, hakika sisi hatumiliki chombo kisicho na lengo, hata kope za macho na upinde uliopo chini ya unyayo! Hivyo namna gani inawezekana dhari (chembe) za uwepo wetu zikawa na lengo wakati ambapo uwepo wetu hauna lengo lolote.

Na tutoke kwenye uwepo wetu, na tuangalie ulimwengu mkubwa, hakika sisi tutaona kila chombo kina lengo, lengo la mionzi ya jua, lengo la mvua, lengo la kuwepo kwa hewa, lakini inawezekana mkusanyiko wa ulimwengu huu uwe bila ya lengo?

Kwa hakika ni kana kwamba kitambaa kikubwa kimewekwa katika kitovu cha ulimwengu huu mpana kinabainisha lengo la mwisho. Wakati mwingine kwa ukubwa wa kitambaa hiki hatuwezi kukiona katika wakati wa mwanzo, na ibara iliyoandikwa juu ya kitambaa nayo ni malezi kamilifu.

Sasa hivi tumekwishajua lengo la kuumbwa kwa kifupi, je, inawezekana maisha yetu mafupi katika dunia hii pamoja na matatizo yake na masaibu yake kuwa ndio lengo la kuumbwa kwetu?

Jaalieni kwamba mimi naishi katika dunia hii miaka miwili najitahidi asubuhi na jioni kwa ajili ya kupata riziki ya kila siku. Narejea jioni nyumbani nimechoka, na matokeo yanakuwa ni kutumia tani kadhaa za chakula na maji katika umri wangu. Kisha baada ya juhudi nyingi najenga nyumba na baada ya hapo naondoka na kuacha dunia hii, je lengo hili linastahiki kuja na kujitahidi na juhudi zote hizi?

Mhandisi anapojenga ghorofa katikati ya jangwa na anachukua muda wa miaka mingi kisha anaweka katika kila ghorofa nyenzo za raha na furaha Akiulizwa juu ya lengo lake anasema: "Hakika lengo langu ni msafiri apite hapa, muda wote wa ghorofa hili ili apumzike humo saa moja", je hatushangai kauli yake na kumwambia: "Hakika kupumzika saa moja haistahiki vitu vyote hivi."

Kwa sababu hii hawaitakidi hawa Siku ya Kiyama na maisha baada ya mauti, bali wanaona maisha ya dunia hii hayana maana. Na haya ndio tunayoyaona sana katika kauli za watu wa mada kwamba maisha ya dunia hii hayana lengo. Hata watu miongoni mwao wanajinyonga kwa sababu wao kama wanavyosema wameshachoka na maisha haya ya kimada yenye kujirudia ambayo hayana lengo.

Hakika kitu ambacho kinayapa maisha maana na lengo na kuyafanya ni ya kiakili na ya hekima, ni kuwa dunia hii na maisha haya ni utangulizi wa ulimwengu mwingine, na kubeba matatizo ya maisha haya na maandalizi ya utangulizi ni kwa ajili ya kunufaika na mwendo wa maisha katika njia ya kudumu.

Tumekwishaleta awali mfano wa kitoto kichanga katika tumbo la mama yake, kikiwa na akili na uerevu wakikiambia: "Hakuna kitu baada ya maisha haya uliyonayo hapa" bila shaka mtoto atapinga

maisha yake na kusema: "Nini maana ya kubakia mfungwa hapa? Kula damu na kubakia nimefungwa miguu miwili hapa kisha hakuna kitu baada ya hapo, nini lengo la muumba kwa kiumbe huyu?" Lakini akipata matumaini kwamba miezi hii ni hatua tu itaondoka haraka, nayo ni utangulizi wa maisha marefu katika dunia, ambayo ndio ulimwengu mpana kuliko mazingira ya mimba. Humo kumejaa utukufu na nuru, humo kuna neema nyingi, hakika wakati huo atapata matumaini kwamba maisha ya mimba yana maana na lengo la kiakili, na kwa hiyo anaweza kuyavumilia, yaani hatua ya mimba.

Qur'ani Tukufu inasema: "Mmeshajua uumbaji wa mwanzo kama mnakumbuka." (Sura al-Waqiah: 62).

**Hitimisho:** Hakika ulimwengu huu kwa kila uwepo wake unapiga kelele kwamba kuna ulimwengu mwingine baada ya ulimwengu huu, vinginevyo maisha yangekuwa ni upuuzi na mchezo na bila kuwa na maana. Sikilizeni inayoyasema Qur'ani Tukufu:

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ

**"Je, mmedhani kuwa tuliwaumba bure na kwamba ninyi Kwetu hamtarudishwa?" (Sura al-Muuminun: 115).** Ni ishara kwamba kama sio marejeo ambayo inayazungumzia Qur'ani Tukufu, ya kurejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ingekuwa kumuumba mwanadamu ni sawa na upuuzi. Matokeo ni kwamba hakika falsafa ya kuumba inasema: Ni lazima kuwepo ulimwengu mwingine baada ya ulimwengu huu.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Kwa nini haiwezekani kulinganisha sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu na sifa za viumbe?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 222 1/13/2017 3:33:29 PM

2. Nini lengo la kuumbwa kwetu?
3. Je, inawezekana kuwa lengo la kuumbwa mwanadamu ni kuishi katika dunia hii?
4. Nini unatufunza ulinganisho wa maisha ya hatua ya mimba pamoja na maisha ya dunia?
5. Namna gani Qur'ani Tukufu inatoa hoja katika kuumbwa ulimwengu huu juu ya kuwepo Akhera?

# SOMO LA NANE:

**Kubakia roho ni dalili ya Siku ya Kiyama:**

Hajui yeyote tangu alipofikiria mwanadamu kuwepo kwa roho, lakini inawezakana kusema: Hakika mwanadamu tangu mwanzo alikuwa anapata tofauti kati yake na wanyama, kati yake na mawe, mbao, mlima hadi na jangwa.

Yeye alikwishaona hali ya ndoto, vilevile hali ya mauti, hakika alikuwa anahisi bila ya kutokea mabadiliko katika mwili na mada, anapatwa na mabadiliko makubwa katika hali ya usingizi na mauti, na hapa amefahamu kwamba kuna asili nyingine anayoibeba isiyokuwa mwili.

Na alikuwa anaona vilevile kwamba kuna tofauti baina yake na wanyama, yeye anamiliki katika harakati zake uhuru, matakwa na hiyari, wakati ambapo harakati za wanyama za utashi ni za jaala na kutenzwa nguvu. Na alipokuta kwa sura maalum, katika ulimwengu wa ndoto, kwamba viungo vya mwili vimetulia, akahisi kuwa kuna nguvu isiyofahamika inatawala uwepo wake, akaiita roho.

Maulamaa walipoweka msingi wa falsafa wakaijaalia roho kuwa ni mas'ala ya falsafa muhimu sambamba na mas'ala mengine.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 223 1/13/2017 3:33:29 PM

Na baada ya hapo wakawa wanatoa rai zao kuhusu maudhui kiasi kwamba baadhi wamesema hakika maulamaa wa Kiislamu wametaja rai na nadharia elfu moja takriban kuhusu uhalisia wa roho na mas'ala mengine yanayoambatana nayo. Na mazungumzo kuhusu maudhui haya marefu, na jawabu la swali hili ni maudhui muhimu nayo ni: "Je, roho ni mada au si mada? Na kwa maneno mengine je, iko huru au ni katika umahususi wa fizikia na kemia ya ubongo na mnyororo wa mishipa?

Baadhi ya wanafalsafa wa kimada wanadhani kwamba roho na asili ya roho ni ya kimada na ni miongoni mwa umahususi wa chembe chembe za ubongo, na mwanadamu anapokufa roho pia inaondoka. Ni sawa kabisa na kama lau sisi tumepiga saa kwa nyundo na kuiteketeza itasimama kufanya kazi.

Mukabala wa hawa kuna kundi la wanafalsafa wa kiungu. Hadi kundi la wanafalsafa wa kimada wanaitakidi kwamba roho haitokufa kwa kufa mwili, bali hakika itaendelea kuiishi. Na kuna dalili nyingi za kuthibitisha mas'ala haya, yaani asili ya roho, uhuru wake na kubakia kwake. Na dalili hizi ni ngumu kiasi fulani, sisi tutaelezea katika mazungumzo yetu kwa muhtasari na kufafanua dalili hizi kwa ibara rahisi na nyepesi kwa vijana wetu watukufu:

### 1. Haiwezekani kuweka ulimwengu mkubwa katika mazingira madogo:

Jaalieni kwamba nyinyi mmekaa ufukweni mwa bahari kubwa na pembezoni mwake kuna majabali marefu, na mawimbi makubwa yanagonga mawe ya ufukweni kisha yanarejea na hasira baharini. Hakika mawe makubwa chini ya jabali yanaashiria urefu wa kilele cha mlima ambapo unafunikwa na mbingu ya bluu, kama ambavyo hutanuka katika bahari na usiku unadhihiri ukubwa kwa uwazi wa maana yake.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 224 1/13/2017 3:33:29 PM

Tunaangalia kwa muda mandhari haya, kisha tunafumba macho yetu na kuchora tuliyoyaona katika akili zetu kwa ukubwa huo. Hakuna shaka kwamba picha hii ya kiakili, ya ukubwa huo inahitajia sehemu isiyowezekana kuenea katika chembe za ubongo mdogo, vinginevyo hakika ni lazima kuchora picha kubwa katika nukta ndogo, haya wakati ambapo sisi tunahisi picha hiyo iliyochorwa kwa ukubwa wake ndani ya akili yetu.

Hakika hii inaonyesha kwamba sisi tunamiliki asili nyingine isiyokuwa mwili na chembe chembe za ubongo ambazo zinaweza kuchora picha yoyote, vyovyote itakavyokuwa kubwa na kwa kipimo chochote kile ndani yake. Na hakuna shaka kwamba asili hii ni lazima iwe nyuma ya ulimwengu wa mada, kwa sababu sisi hatuoni mfano wa haya katika ulimwengu wa kimada.

## 2. Sifa dhahiri ya roho:

Hakika sisi tunahisi sifa nyingi za kifizikia na kikemia ndani ya uwepo wetu. Harakati za moyo na tumbo, ni sifa ya kifizikia, lakini cheche za mate na majimaji ya tumbo juu ya chakula ni vitendea kazi vya kikemia. Hakika mfano wa vitendea kazi hivi ni vingi katika miili yetu. Na ikiwa roho na fikra ni za kimada, na ni miongoni mwa sifa na umahususi wa kikemia wa chembechembe za ubongo, hivyo kwa nini kunapatikana tofauti kubwa kati yake na umahususi uliobakia wa miili yetu.

Hakika fikra na roho zinaunganisha kati yetu na ulimwengu na zinatufahamisha yanayozunguka pembezoni mwetu. Ama umahususi wa mate ya kikemia na majimaji ya tumbo na harakati za kifizikia za jicho, ulimi na moyo hazina hali hizo.

Na kwa maneno mengine, hakika sisi tunahisi kwa sura nzuri kwamba uwepo wetu unafungamana na ulimwengu uliopo nje yetu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 225 1/13/2017 3:33:29 PM

na sisi tunajua mas'ala yake. Na sasa hivi linakuja swali: Je, ulimwengu uliopo nje yetu unapenya ndani yetu? Bila shaka hapana, hivyo nini uhalisia wa mas'ala? Hakika sura inakuja mbele yetu na sisi kwa kufaidika na umahususi wa dhahiri ya roho tunaangalia ulimwengu wa nje, na sifa hii haipatikani katika dhahiri yoyote ya kifizikia au kikemia katika miili yetu.

Na kwa maneno mengine vilevile, kuna haja ya dharura ili tufahamu vilivyopo nje yetu, dhahiri kwa macho yetu. Na maarifa haya hayafungamani na chembechembe za ubongo. Hakika chembechembe za ubongo zinaweza tu kuathirika kwa nje sawa kabisa na chembechembe nyingine za mwili.

Hakika tofauti hii inaonyesha kwamba kuna uhalisia mwingine usiokuwa mabadiliko ya kifizikia na kikemia katika mwili, unaotupa elimu nje ya uwepo wetu, na uhalisia huu si kingine isipokuwa ni roho ambayo iko juu ya mada na umahususi wa mada.

### 3. Dalili za majaribio ya asili na uhuru wa roho:

Kwa bahati nzuri hakika maulamaa wameweza kwa njia ya elimu na tajriba, kuthibitisha asili ya uhuru wa roho na kuelekeza jawabu lenye kushinda kwa wale ambao wanakanusha uhuru wa roho na wanaizingatia kuwa ni katika umahususi wa mada.

**1.** Ndoto za usingizi wa sumaku ni moja ya zile dalili hai ambazo zimethibitisha hayo ndani ya majaribio mengi, na wengi wameziona, na ambaye hajaziona tunamfafanulia kwa muhtasari wenye faida: "Baadhi ya watu kwa njia mbalimbali za kielimu kutoka kwa wengine, wanazama katika usingizi, anayefanya hayo anaitwa kwa jina la (mtendaji) wakati ambapo mtu anayezama katika usingizi anaitwa (*mediom*), yaani kwa njia ya kutamkishwa na kuzamishwa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 226 1/13/2017 3:33:29 PM

katika fikra na kwa nguvu ya mkodoo wa jicho na mfano wa hayo. Mtu anazama katika usingi mzito ambao si kama usingizi wa kawaida, bali ni usingizi ambao inawezekana kupitia usingizi huo kufanya mafungamano pamoja naye na kuzungumza naye na kuchukua jawabu kutoka kwake.

Na katika hali hiyo roho inamchukua hadi sehemu mbalimbali na wakati mwingine zinakuja habari mpya, na wakati mwingine mwanadamu anapata maarifa ambayo asingeyapata katika hali ya kawaida. Na wakati mwingine anazungumza kwa lugha isiyokuwa lugha yake ya kuzaliwa, na hakuwa anaijua kabla ya hapo. Na anaweza kutatua mas'ala magumu ya hesabu katika hali hiyo. Na wakati mwingine anaandika katika ubao uliowekwa katika sanduku lililofungwa kwa umakini.

Kama ambavyo roho zinaweza kudhihiri kwa njia ya marohani yenye kuangaza na vivuli katika vikao hivyo, na tumeshafafanua hayo katika kitabu *Audatul- Aruwaahi*.

**2.** Mafungamano na roho, baada ya mauti kuna alama nyingine juu asili na uhuru wa roho. Sasa hivi kunapatikana jumuiya za kiroho katika sehemu zote za ulimwengu, na kulingana na kauli ya mwanachuoni wa kimisri maarufu kwa jina la Farid Wajidiy, ni kwamba kunapatika zaidi ya majarida na magazeti mia tatu kutoka katika jumuiya hizo katika ulimwengu. Zinashiriki shakhisiya maarufu katika vikao vyake ambavyo humo zinahudhuria roho, na yanafanyika mambo yaliyo kinyume na ada (kawaida).

Na pamoja na kwamba kuna Manasibi wanaodai kujua mas'ala ya mafungamano na roho, pamoja na ujahili wao katika hayo na kwa lengo la kuwahadaa watu, wanakwenda mbio kupata mali, lakini hayo hayazuii kukubali uhalisia wa roho ambao wanautambua



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 227 1/13/2017 3:33:29 PM

wahakiki wakubwa, na vilevile mas'ala ya uwezekano wa kuwasiliana na roho. Mambo yote haya ni dalili juu ya asili, uhuru wa roho na kubakia kwake baada ya mauti na hatua yenye kuathiri kuelekea kwenye marejeo na maisha baada ya mauti.

3. Hakika ndoto ambazo tunaziona ni muonekano unaoonekana mbele yetu katika usingizi, na wakati mwingine unaondoa pazia juu ya matukio ya mustakabali na mas'ala yenye kufichikana, ambapo hatuwezi kusema kwamba tukio hilo ni katika mlango wa bahati mbaya, na hii ni dalili nyingine juu ya asili na uhuru wa roho.

Mara nyingi wameshasikia watu katika maisha yao kuhusu mifano ya ndoto za kweli na namna gani rafiki fulani amekwishaona ndoto na ikatimia akiwa macho kama alivyoiona, ambapo inaonyesha kwamba roho ya mwanadamu ina mafungamano na ulimwengu mwingine katika hali ya usingizi, na kuona matukio ya mustakabali.

Hakika mkusanyiko wa mambo haya unaonyesha kwa namna ya wazi kwamba roho sio mada na haina sifa za ubongo wa kifizikia na kikemia, bali ni uhalisia uliopo nyuma ya mazingira, haumaliziki wala hauondoki kwa mauti ya mwili, na jambo hili linaandaa njia ya kuthibitisha mas'ala ya marejeo na ulimwengu wa baada ya mauti.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Nini tofauti katika mas'ala ya roho kati ya wanafalsafa wa kiungu na kundi la watu wa mada.
2. Nini makusudio ya kutokuingia kitu kikubwa ndani ya kidogo, jambo ambalo ni katika dalili za asili ya roho.
3. Unajua nini kuhusu usingizi wa sumaku?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 228 1/13/2017 3:33:29 PM

**4.** Nini makusudio ya mawasiliano na roho?

**5.** Namna gani ndoto za kweli zinakuwa ni dalili ya asili na uhuru wa roho?

## SOMO LA TISA:

### Marejeo ya mwili na roho:

Miongoni mwa mas'ala yanayoulizwa katika utafiti wa miadi na marejeo ni swali hili: Je, marejeo yana upande wa kiroho peke yake? Au ni mwili wa mwanadamu utarudi katika ulimwengu wa akhera, yaani kwa mwili wake na roho yake ambavyo anavimiliki katika dunia, lakini kwa kiwango bora zaidi ili aanze maisha mapya?

Baadhi ya wanafalsafa wa zamani walikuwa wanaitakidi kwamba marejeo ni kwa roho, na walizingatia mwili kuwa ni umbo linapatikana pamoja na mwandamu katika dunia hii tu, na baada ya mauti halihitajiki kwake, hivyo atauacha na kuharakisha kwenda kwenye ulimwengu wa roho.

Lakini maulamaa wakubwa wa Kiislamu na wengi kati ya wanafalsafa wanaitakidi kwamba marejeo yana pande mbili, roho na mwili. Ni sahihi kwamba mwili unabadilika na kuwa udongo na kumalizika, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Muweza na Mjuzi wa chembe chembe zote za udongo atakapozikusanya siku ya Kiyama, na atazivalisha vazi mpya, na hiyo inaitwa marejeo ya mwili, kwa sababu wao hawashuku katika kurejea roho. Hakika mazungumzo hapa ni kurejea mwili vile vile, na kwa sababu hiyo yameitwa kwa jina hilo.

Kwa hali yoyote ile hakika Aya zote za Qur'ani ambazo zinazungumzia kuhusu marejeo – nazo ni nyingi – pia zinategemea marejeo ya kimwili.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 229 1/13/2017 3:33:29 PM

**Ushahidi wa marejeo ya kimwili katika Qur'ani Tukufu:**

Tumekwishasoma mwanzo namna gani alikuja bedui na kipande cha mfupa kwa Mtukufu Nabii ﷺ na akauliza: Nani anaweza kuhuisha mifupa hii? Mtume ﷺ akamjibu kwa amri kutoka Mwenyezi Mungu Mtukufu:

قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ مِنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنْتُمْ مِنْهُ تُوقِدُونَ

**"Sema: Ataihuisha aliyeiumba mara ya kwanza. Na Yeye ni mjuzi wa kila uumbaji. Yeye ambaye aliwajaalia moto kutokana na mti wa kijani nyinyi mkawa mnauwasha." (Suratu Yasin: 79 na 80).**

Na katika sehemu nyingine anasema: "Na itapulizwa parapanda mara wanatoka makaburini wakikimbilia kwa Mola Wao." (Sura Yaasin: 51). Na "Macho yao yatainama; watatoka makaburini kama kwamba wao ni nzige waliotawanyika." (Sura Al-Qamar: 7). Na sisi tunajua kwamba kaburi ni makazi ya miili ambayo inageuka kuwa udongo na sio sehemu ya roho.

Kwa hakika mshangao wa wakanushaji wa marejeo unajikita katika kauli yao: Tutakapokuwa udongo na kupeperushwa na upepo; namna gani tutarejea mara nyingine kwenye uhai? "Na wakasema je, tukipotelea katika ardhi sisi tutarejea katika umbo jipya?" (surat Sajidah: 10).

Na Qur'ani tukufu inawajibu: "Je hawajaona namna gani Mwenyezi Mungu anaanzisha kiumbe kisha anakirejesha, hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi." (Sura Al-Ankabuti: 19).

Waarabu wa kijahiliya walikuwa wanasema; Kama ilivyobainisha hayo Qur'ani Tukufu katika Sura al-Muuminina: 35: "Je, anawaahidi kwamba nyinyi mtakapokufa na mkawa mchanga na



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 230 1/13/2017 3:33:29 PM

mifupa kwamba nyinyi mtatolewa." Hakika Aya hizi za Qur'ani na nyinginezo zinabainisha kwa uwazi kwamba Mtukufu Mtume ﷺ daima alikuwa anazungumzia kuhusu marejeo ya kimwili, na kwa sababu hiyo washrikina wakijahilia wanashangaa, na kwa hivyo tunaona Qur'ani Tukufu inataja mifano ya marejeo ya kimwili katika ulimwengu wa mimea na mfano wa hayo ambayo yanaonekana kwa jicho la hao, na kushuhudia uumbaji wa kwanza na uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kwa ajili hii haiwezekani Mwislamu vyovyote yatakavyokuwa maarifa yake katika Qur'ani Tukufu kushuku marejeo ya kimwili, kukanusha marejeo ya kimwili katika upande wa mtazamo wa Qur'ani ni sawa na kukanusha msingi wa marejeo.

**Ushahidi wa kiakili:**

Kwa kuongezea katika hayo akili inasema: Hakika roho na mwili ni vitu viwili visivyotengana. Pamoja na uhuru wa kila kimoja lakini vinafungamana pamoja, na vinakuwa pamoja na ni katika jambo la kawaida vitu hivyo viwili kuhitajiana ili kuendelea maisha yenye kudumu.

Na vikitengana kwa muda mfupi katika hatua ya Barzakh (kaburi), kitenganishi baina ya dunia na akhera, hakika jambo hili haliwezi kuwa ni la daima. Kama ambavyo mwili bila ya roho ni mpungufu, hakika roho bila ya mwili ni pungufu pia. Hakika roho ni kiongozi na mtendaji wa harakati, na mwili ni chombo kinachokubali amri na kwa hiyo haiwezekani kwa chochote miongoni mwao kutokuwa na haja na kingine. Isipokuwa ni kwamba roho Siku ya Kiyama itachukua nafasi tukufu na kwa kiasi kilekile ni lazima mwili ukamilike, na haya ni wajibu yawe, yaani hakika mwili Siku ya Kiyama utakuwa umeepukana na upungufu na kasoro.



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 231 1/13/2017 3:33:29 PM

Kwa hakika mwili na roho vinapatikana pamoja na kila kimoja kinamkamilisha mwingine. Na marejeo hayawezekani kufanyika kwa upande wa kiroho tu au upande wa kimwili tu. Kwa maneno mengine, hakika utafiti wa kuumbwa mwili na roho na mafungamano baina yao ni dalili ya wazi kwamba marejeo yatatimia kwa vyote viwili pamoja.

Na katika upande mwingine hakika kanuni ya uadilifu inasema: Hakika marejeo yatakuwa kwa viwili hivyo, ambapo mwanadamu akifanya kheri anakuwa amefanya kwa mwili wake na roho yake, na amali ya shari inakuwa vivyo hivyo, na kwa sababu hii adhabu na thawabu inakuwa kwa vyote viwili kwa pamoja. Na ikiwa itaupata mwili bila ya roho au roho bila ya mwili, katika hali hii haitakuwa imetekelezwa kanuni ya uadilifu abadani.

**Maswali kuhusu marejeo ya kimwili:**

Katika nyanja hii maulamaa wameuliza maswali magumu na kwa kukamilisha utafiti ni lazima kuuliza baadhi ya mas'ala haya:

1. Kulingana na uhakiki wa maulamaa wa mazingira, hakika mwili wa mwanadamu unakabiliwa na mabadiliko katika umri wake, na inafanana kabisa na birika la kuogelea ambalo yanaingia humo maji kutoka upande na kutoka kidogo kidogo katika upande mwingine. Na ni kawaida baada ya muda maji ya birika kubadilika kabisa. Jambo hili linaweza kuupata mwili wa mwanadamu baada ya miaka saba mara moja na hivyo hakika sisi tunabadilika mara nyingi katika umri wetu. Na sasa linaulizwa swali: ni mwili upi kati ya miili hii itarudi tena? Jawabu: Tunasema ni mwili wa mwisho, nayo ni kama tulivyosoma katika Aya zilizotangulia kwamba Mwenyezi Mungu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 232 1/13/2017 3:33:29 PM

Mtukufu atarejesha uhai upya kwenye mifupa iliyobungulika, na maana ya maneno haya ni kwamba mwili wa mwisho ndio ambao utarudi, na vilevile hakika kufufuka katika makaburi maana yake ni kurejea mwili wa mwisho.

Ama nukta muhimu hapa ni kwamba mwili wa mwisho utahifadhiwa kwa athari na sifa za miili yote ambayo ilikuwa kwa mwanadamu muda wote wa umri wake. Kwa maneno mengine: Hakika mwili ambao unamaliza na kuondoka kidogo kidogo zitahama sifa zake zote ambazo alikuwa anazimiliki na kuhamia katika mwili wa mwisho. Na hivyo hakika mwili wa mwisho ndio utakaorithi sifa zote za mwili wa mwanzo na unaweza kulingana na kanuni adilifu kupata thawabu na adhabu.

**2.** Baadhi wanasema: Tunapobadilika na kuwa udongo na chembe zetu zinakuwa sehemu ya mimea na matunda, na matokeo yake zinakuwa ni sehemu ya mtu mwingine, nini taklifu Siku ya Kiyama? (Hii ndio inayoitwa falfasa ya elimu ya mantiki) Inafanana na (mlaji na kilicholiwa).

Pamoja na kwamba jawabu la swali hili ni pana lakini sisi tunajitahidi kufupisha kadiri iwezekanavyo.

Tunasema katika jawabu hili: Hapana shaka kwamba chembechembe za mwili wa mwanadamu ambaye amekuwa udongo zimeingia katika mwili wa mtu mwingine, hivyo ni lazima zirejee kwenye mwili wa kwanza (aya tulizozitaja ni ushahidi uliowazi). Tatizo ambalo linadhihiri katika hali hii ni kwamba mwili wa pili utabakia pungufu.

Lakini ni wajibu tuseme: Hakika hautabakia pungufu, bali utakuwa mdogo, kwa sababu chembechembe zimegawanywa sehemu zote za mwili, na ikichukuliwa kutoka kwayo hakika hilo litatimia kwa

kiwango kilekile kutoka katika sehemu zote za mwili, na kwa hivyo utadhoofika na kuwa mdogo.

Hivyo hakika mwili wa kwanza hautomalizika wala mwili wa pili hautamalizika, kitu pekee kitakachotokea ni mwili wa pili kuwa mdogo, na hii haitasababisha tatizo lolote, kwa sababu sisi tunajua kwamba Siku ya Kiyama itakamilika miili ya wanadamu, na kuondoka kasoro zote, sawa kabisa na kukua kwa mtoto, au kama majeruhi ambaye linapona jeraha lake, hivyo shakhisiya yake haitobadilika. Hakika miili pungufu na midogo Siku ya Kiyama itakamilika katika ulimwengu wa ukamilifu. Na hivyo hakutabakia tatizo.

## TAFAKARI NA UJIBU:

1. Je, maisha ya mwanadamu Siku ya Kiyama yanafanana na maisha yake katika dunia?
2. Je, tunaweza kujua kwa sura ya uhakika thawabu na adhabu za Siku ya Kiyama katika dunia hii?
3. Je, neema za peponi na adhabu ya motoni zina upande wa kimwili tu?
4. Nini makusudio ya umbo la vitendo, namna gani Qur'ani Tukufu inatoa dalili juu ya hayo?
5. Utamjibu nini mwenye kutilia shaka itikadi ya maumbo ya matendo katika utafiti wa Marejeo?

## SOMO LA KUMI:

### Pepo na moto na umbo la vitendo:

Ni wengi ambao wanauliza: Je, ulimwengu wa baada ya mauti unafanana na huu mkubwa au kuna tofauti baina yao? Je, neema zake,



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 234 1/13/2017 3:33:29 PM

adhabu yake, mpangilio wake na kanuni zake zinafanana na zilizopo katika ulimwengu huu?

Jawabu ni wajibu kusema wazi: Tunao ushahidi mwingi unaonyesha juu ya hali ya tofauti kubwa baina ya ulimwengu huu na ulimwengu huo mwingine, kwa kiasi kwamba ambayo tunayajua kuhusu Siku ya Kiyama, katika ulimwengu huu yanafanana na mazigazira yanayoonekana kwa mbali.

Ni bora kunufaika na mfano wa kichanga tumboni. Kama ambavyo kuna tofauti baina ya ulimwengu wa mimba na dunia hii, vilevile tofauti kati ya dunia hii au kati ya ulimwengu huu na ulimwengu huo mwingine au zaidi. Kama mtoto katika ulimwengu wa mimba angekuwa anamiliki akili na werevu na akataka kufikiria kuhusu dunia ya nje ya kizazi, yaani mbingu, ardhi, jua, mwezi, nyota milima, mapori na bahari, kwa hakika hatoweza.

Hakika mtoto anayekuwa katika ulimwengu wa mimba na hakuona isipokuwa mazingira finyu ndani ya tumbo la mama, hakika jua, mwezi, bahari, mawimbi na tufani, upepo, maua, uzuri wa ulimwengu huu hauna maana kwake, na kama tukijaalia kwamba mtu amemsemesha nje ya tumbo la mama hakika hatofahamu kitu.

Hakika tofauti ya ufinyu wa ulimwengu huu pamoja na upana wa ulimwengu mwingine ni kwa kiasi hiki au zaidi. Na kwa hiyo hakika sisi hatuwezi kujua neema zilizopo peponi au ulimwengu huo mwingine. Na kwa sababu hiyo tunasoma katika hadithi: "Humo kuna mambo ambayo jicho halijaona, wala sikio halijasikia, wala moyo wa mwanadamu haujafikiria."

Na Qur'ani Tukufu inaakisi maana hii ambapo inasema:

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أُخْفِيَ لَهُمْ مِنْ قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 235 1/13/2017 3:33:29 PM

**"Nafsi yoyote haijui waliyofichawa katika yanayoburudisha macho; ni malipo kwa yale waliyokuwa wakiyatenda." (Sura Sajidah; 32:17).**

Hakika mifumo ambayo inahukumu ulimwengu huo mwingine ina tofauti kubwa pamoja na iliyopo katika ulimwengu huu, mfano: Mashahidi katika mahakama ya Kiyama juu ya vitendo vya mwanadamu ni mikono yake, miguu yake, ngozi yake na mwili wake, bali hata ardhi ambayo amefanya kosa au wema juu yake:

الْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰ أَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَا أَيْدِيهِمْ وَتَشْهَدُ أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ

**"Leo tunaviziba vinywa vyao, na iseme Nasi mikono yao, na itoe ushahidi miguu yao kwa waliyokuwa wakiyachuma." (Sura Yaasin; 36:65).**

وَقَالُوا لِجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدْتُمْ عَلَيْنَا ۖ قَالُوا أَنْطَقَنَا اللَّهُ الَّذِي أَنْطَقَ كُلَّ شَيْءٍ

**"Na wataziambia ngozi zao: Kwa nini mmetushuhudilia? Zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu ambaye ametamkisha kila kitu….." (Sura Fuswilat; 41:21).**

Bila shaka kufikiria hayo ilikuwa vigumu wakati fulani, lakini kwa maendeleo ya elimu katika kurekodi matukio na sauti sio jambo la mshangao tena.

Hakika pamoja na ugumu huo, tunaona kivuli cha neema za ulimwengu mwingine, na hatuwezi kujua upana na umuhimu wa sifa hizo, isipokuwa hakika sisi tunajua kwamba neema za ulimwengu huo mwingine na vile vile adhabu yake zina upande wa kimwili na upande wa kiroho, kwa sababu marejeo yana pande mbili. Ndio ni wajibu kuwe na adhabu na thawabu, yaani kama anavyosema katika upande wa kimada na kimwili:

وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 236 1/13/2017 3:33:29 PM

ۖكُلَّمَا رُزِقُوا مِنْهَا مِنْ ثَمَرَةٍ رِزْقًا ۙ قَالُوا هَٰذَا الَّذِي رُزِقْنَا مِنْ قَبْلُ ۖ وَأُتُوا بِهِ مُتَشَابِهًا ۖ وَلَهُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُطَهَّرَةٌ ۖ وَهُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

**"Na wabashirie ambao wameamini na wakafanya vitendo vizuri, kwamba watapata mabustani ambayo hupita mito chini yake. Kila mara watakapopewa matunda humo kuwa riziki, watasema: 'Haya ndiyo yale tuliyopewa mwanzo' kwani wataletewa hali ya kuwa yamefanana. Na humo watapata wake waliotakaswa; nao watakaa milele humo." (Sura al-Baqarah; 2:25).**

Na anasema kuhusu neema za kimaanawi:

وَرِضْوَانٌ مِنَ اللَّهِ أَكْبَرُ ۚ

**"Na radhi za Mwenyezi Mungu ni kubwa zaidi." (Sura Tawba; 9:72).**

Ndio, hakika watu wa peponi wanahisi utamu na furaha ambayo hailinganishwi na kitu, wanapohisi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu yuko radhi nao na ameshakubali amali zao.

Ama kuhusu watu wa motoni, hakika wao kwa kuongezea katika adhabu ya kimwili na moto watakabiliana na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kutokuwa radhi nao, nayo ni hali mbaya zaidi kuliko adhabu!

## Umbo la vitendo:

Inafahamika kutokana na Aya nyingi kwamba vitendo vyetu vitarejea katika uhai Siku ya Kiyama na kudhihirika kwetu kwa maumbo mbalimbali. Muhimu zaidi ni kwamba adhabu na thawabu zitaonyesha vitendo hivi.

Dhulma itatuzunguka kama wingu jeusi kama ilivyokuja katika hadithi ya Nabii ﷺ: Dhulma ni giza Siku ya Kiyama.

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا ۖ وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيرًا

**"Hakika wale wanaokula mali ya yatima kwa dhulma, hapana shaka wanakula moto matumboni mwao; na wataingia katika moto uwakao." (Suratun-Nisa; 4:10).**

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَىٰ نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ

**"Siku utakapowaona waumini wanaume na waumini wanawake, nuru yao inakwenda mbele yao na kuume kwao….." (Sura al- Hadid; 57:12).**

Hakika wala riba ambao wanaharibu uwiano wa jamii kiuchumi kwa vitendo vyao vyenye kufedhehesha, wao ni kama wagonjwa waliopatwa na mauti, ambao wanakwenda mbio kusimama kwa nyayo zao lakini wao wanaanguka kwa kutoweza kuhifadhi uwiano wao, na kwa sababu hii wanasimama na kuanguka.

Na mali waliyoikusanya watawala na wakailimbikiza, na hawakulipa kwayo haki za wanyonge itakuwa mnyororo mzito katika shingo zao, kiasi hawatoweza kutembea.

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخَلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَهُمْ ۖ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَهُمْ ۖ سَيُطَوَّقُونَ مَا بَخِلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ

**"Na wasidhanie kabisa wale ambao wanafanyia ubakhili vile alivyowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila Zake kuwa ni bora kwao, bali ni shari kwao. Watatiwa mandakozi ya hivyo walivyofanyia ubakhili Siku ya Kiyama….." (Sura Aal Imran; 3:180).**

Vivyo hivyo kwa vitendo vingine kila kimoja kwa sura inayofaa.

Sisi tunajua kwamba elimu leo inasema kwamba hakuna kitu katika ulimwengu kitakachoondoka, nguvu na maada zitabadilika kwa



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 238 1/13/2017 3:33:30 PM

umbo na sura, bila ya kuondoka, na vitendo vyetu havitoki katika kanuni hii, navyo vitabaki milele, pamoja na kwamba maumbo yake yatabadilika.

Qur'ani Tukufu inasema katika Aya fupi inayotikisa hisia ya Kiyama: "Na watakuta waliyoyafanya yapo hadhiri." (Sura Kahfi: 49). Kwa hakika anayoyachuma mwanadamu ni vitendo vitakavyokuwa mbele yake, hivyo katika mwisho wa Aya hii Qur'ani Tukufu inaongeza: "Na Mola Wako hamdhulumu yeyote."

Na tunasoma katika sehemu nyingine katika Qur'ani Tukufu kuhusu Siku ya Kiyama:

يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا لِيُرَوْا أَعْمَالَهُمْ فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

**"Siku hiyo watu watatoka kwa mtawanyiko ili wakaonyeshwe vitendo vyao! Basi anayetenda chembe ya wema atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!" (Sura Zilzala: 6 - 8).**

Je, mnaona? Hakika inasema nyinyi mtaona vitendo hivyo, vilevile.

Na kwa kuangalia ukweli huu, nayo ni kwamba vitendo vyetu vidogo au vikubwa, vyema au vibaya, vitabakia thabiti na vimehifadhiwa katika ulimwengu huu na havitofutwa na vitakuwa pamoja nasi Siku ya Kiyama. Na tahadhari hii ni kwa wote ili wawe ni wenye kutahadhari katika amali zao na waelekee upande wa kheri kwa ukweli na uaminifu.

Na ajabu ni kwamba imetimia kuvumbua vyombo vinavyoweza kuelezea haya mas'ala katika dunia hii. Ameandika mmoja wa Maulamaa anasema:



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 239 1/13/2017 3:33:30 PM

Inawezakana sasa hivi kusikiliza sauti ya mawimbi ya sauti ya watengeneza chombo cha Misri waliotengeza kabla ya miaka elfu mbili, ambapo chombo cha kabla ya miaka elfu mbili kinapatikana katika makumbosho ya Misri, ambapo watengenezaji hao walitengeneza chombo cha umbo la duara ambacho kimerekodi sauti za wafanyakazi wa chombo hicho, ambapo leo imewezekana kuhuisha mawimbi hayo ya sauti ambapo tunayasikiliza.

Vyovyote iwavyo ni kwamba yameshajibiwa maswali ambayo yameulizwa kuhusu mas'ala ya marejeo, kudumu milele, thawabu na adhabu katika Qur'ani Tukufu, ikiwa ni pamoja na maumbo ya vitendo ambayo yanaonyesha kwamba vitendo vyovyote vitakavyokuwa, sawa viwe vibaya au vyema, huacha athari juu yetu na athari hii inabakia daima.

## TAFAKARI NA UJIBU:

**1.** Je, maisha ya mwanadamu Siku ya Kiyama yanafanana na maisha yake katika dunia hii?

**2.** Je, tunaweza kuona adhabu na thawabu katika dunia hii?

**3.** Je, neema za pepo na adhabu ya Jahanam zina pande za kimwili?

**4.** Nini makusudio ya maumbo ya amali, na namna gani Qur'ani Tukufu inaonyesha hilo?

**5.** Utamjibu nini mwenye kutilia shaka itikadi ya maumbo ya matendo katika utafiti wa Marejeo?



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 240 1/13/2017 3:33:30 PM

# OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
   ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia

26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 242 1/13/2017 3:33:30 PM

57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 243 1/13/2017 3:33:30 PM

88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 244 1/13/2017 3:33:30 PM

119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l’Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni

150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 246 1/13/2017 3:33:30 PM

181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi



12_16_Misingi_13_January_2017.indd 247 1/13/2017 3:33:30 PM

212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha– Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli

241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU
242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhia
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitoa Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukosoaji na Usahihishaji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo (Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi